**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 24 Julai, 2007**

*(Mkutano ulianza saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA – (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka uliopita, pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 272

**Hitaji la Mhandisi – Muleba**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mhandisi yeyote ni mtaalam mahiri wa fani aliyohitimu na kwa kuwa mhandisi wa ujenzi Wilayani Muleba, aliondolewa madaraka na kushushwa cheo kutokana na sakata la kuhujumu ujenzi wa daraja la Kishara na kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu hatua hiyo ichukuliwe.

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni jambo la dharura kuipatia Muleba Mhandisi mwingine ili kazi na miradi mingine inayoendelea isiathirike zaidi?

(b) Je, ni kwa nini mtaalam anayehujumu fedha za Serikali asirudishe fedha alizohujumu badala ya kushushwa cheo tu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:- Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Kishara katika Mto Ngono lipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 na 2005/2006 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 53 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, ambalo ni kiungo muhimu katika barabara ya kutoka Katoke mpaka Nyawaibaga. Daraja lililotarajiwa kujengwa ni aina ya *Bailey Bridge.* Daraja hili kwa mujibu wa usanifu wa awali lilipaswa kuwa na nguzo tatu (mbili pembeni na moja katikati. Katika mkutano wa nne tarehe 3 Agosti, 2006 wakati najibu swali la namba 335 nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba uwezo wa aliyekuwa Mhandisi wa Wilaya ya Muleba, kusimamia ujenzi wa Daraja hilo ulikuwa mdogo na ndiyo maana Halmashauri ililazimika kumtumia Mhandisi wa Mkoa. Pia, nilieza kuwa mhandisi huyo alisimamishwa kazi kuanzia tarehe 28 Februari, 2006 kutokana na kushindwa majukumu yake ipasavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Muleba wakati ikisubiri kupatiwa Mhandisi mwingine, Halmashauri iliajiri Mhandisi wa muda mwenye sifa ambaye aliendelea kusaidia katika usimamizi wa miradi ya ujenzi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia ofisi yangu tayari imekwishaipatia Halmashauri ya Wilaya Mhandisi mwenye sifa ambaye amekwisharipoti na kuanza kazi katika kituo chake cha kazi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la swali namba 335 nililiarifu pia Bunge lako Tukufu, kuwa kulikuwa na mapungufu ya kiufundi kwenye usanifu wa daraja ambapo awali makisio ya ujenzi wa kuta hayakujumuisha gharama za nondo zitakazotumika. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa mgogoro kati ya Halmashauri ya Muleba na Mkandarasi husika ambaye ni *Mbago Enterprise*. Kwa sasa mkandarasi aliyepewa kufanya kazi hii amefungua kesi katika Mahakama ya Wilaya ya Bukoba akidai malipo ya *retention* kiasi cha shilingi milioni 1.55.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mgogoro wa daraja la Kishara upo Mahakama na kulingana na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, hakuna

hatua zaidi inayoweza kuchukuliwa dhidi ya Mhandisi mpaka Mahakama itoe hukumu juu ya mgogoro huu.

Na. 273

**Upatikanaji wa Mafao ya Wastaafu**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa ni vema mwajiri kuwa na rekodi za waajiriwa wao na kwa kuwa waajiriwa hawana taarifa ya kustaafu miezi 6 kabla ya tarehe ya kustaafu:-

(a) Je, ni sababu gani zinazochelewesha wastaafu kupata mafao wanayostahili mara tu wanapostaafu?

(b) Ili kuondoa tatizo la watumishi wanaostaafu kucheleweshwa malipo. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuna haja ya Bunge kutunga sheria itakayowaamuru waajiri wanaochelewesha kulipa waajiriwa wanaostaafu, walipe mafao hayo pamoja na riba kwa muda aliokaa na pesa za wastaafu?

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu umeonyesha kuwa malipo ya pensheni yanacheleweshwa pamoja na mambo mengine na kukosekana kwa nyaraka muhimu kwenye majalada ya wastaafu. Kumbukumbu hizo ni pamoja na barua ya kuajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni, barua ya kuthibitishwa kazini na barua za kupandishwa cheo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haiafiki pendekezo la kutunga sheria itakayoamuru waajiri wanaochelewesha kulipa mafao ya wastaafu walipe mafao hayo pamoja na riba kwa muda waliokaa na pesa za mstaafu kwa sababu zifuatazo:-

(i) Sheria inawataka waajiri na waajiriwa kutunza kumbukumbu za utumishi. Hivyo ni wajibu wa watumishi pia kutunza kumbukumbu zinazohusu utumishi wao.

(ii) Kwa mujibu wa Kanuni f. 48 ya Kanuni za kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 1994, mtumishi anao wajibu wa kutoa taarifa ya kustaafu katika kipindi cha miezi sita kabla ya kustaafu.

(iii) Matatizo haya yanawahusu kwa kiwango kikubwa watumishi waliostaafu kabla ya kuundwa kwa mfuko wa pensheni ya watumishi wa umma *(Public Service Pension Fund (PSPF).* Wale wanaostaafu chini ya masharti ya mfuko huu, usumbufu

umepungua kwa kiasi kikubwa kwa kuwa taarifa zao sasa zimewekwa katika mtandao wa kompyuta. Kadri mifumo inayozidi kuboreshwa matatizo mengi yatazidi kupungua.

(iv) Pale ambapo kuna sababu za msingi watumishi na waajiri wanashauriwa kufuata masharti yaliyomo katika kifungu cha 27 cha sheria za pensheni kwa watumishi wa umma namba 2 ya mwaka 1999 ambacho kinampa Mheshimiwa Rais, mamlaka ya kusamehe kipengele chochote kusudi watumishi husika waweze kulipwa pensheni.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sasa matatizo ya wastaafu yamepungua:-

(a) Je, anajua kwamba hata pale nyuma ya jengo la Wizara ya Fedha, Waziri anadondoka chini kwa kusimama kwenye mistari wakitaka namba, huko ndiko kusaidia? (*Makofi*)

(b) Je, anafahamu kwamba pale kwenye mahesabu mashine za kompyuta zilikuwa zimeharibika kwa muda wa karibu miezi miwili na wao wako pale huko ndiko kusaidia wastaafu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba kwa sasa hivi wanaopata matatizo makubwa ni wale waliostaafu kabla ya kuanzishwa kwa huu Mfuko wa Watumishi wa Umma (*PSPF*). Lakini kwa ambao wanastaafu sasa hivi kwa kiasi kikubwa matatizo hayo yamepungua.

Kwa swali lake la pili analosema kwamba *computer* imeharibika hayo ni matatizo ya muda na sidhani kama yenyewe kweli tunaweza tukayatungia sheria. Kuharabika kwa *computer* ni suala la kawaida lakini linashughulikiwa kila mara linapojitokeza. (*Makofi*)

Na. 274

**Mafao ya Viongozi wa Kitaifa**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Je, mafao ya viongozi wa kitaifa waliostaafu kama Marais na Mawaziri Wakuu yanatolewa kwa kuzingatia hali halisi ya gharama za sasa?

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya viongozi wastaafu hulipwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, mafao ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa yamekuwa yakibadilika kwa kuzingatia mazingira yaliyokuwepo wakati viongozi hao wanastaafu. Hivyo Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanaostaafu hivi sasa hulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya

Hitimisho la Utumishi wa Kisiasa Na. 3 ya mwaka 1999, kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 13 ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi, kwa Viongozi wa Kisiasa na. 3 ya mwaka 1999 ilianza kutumika tarehe 1 Novemba, 1999. Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanaohusika na mafao ya sheria hiyo ni wale waliostaafu kwa mujibu wa sheria hiyo. Viongozi waliostaafu kabla ya sheria hiyo wanaendelea kulipwa mafao yao kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa Na. 2 ya mwaka 1986.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hadhi na heshimiwa waliyonayo viongozi wetu wastaafu katika jamii, Kitaifa, Serikali na hali halisi ya gharama za maisha ilivyo hivi sasa Serikali, imeanza mchakato wa kuifanyia marekebisho sheria ya mafao ya hitimisho la kazi la la utumishi wa kisiasa Na. 3 ya mwaka 1999 ili kuwianisha mafao yanayolipwa viongozi wastaafu wa kitaifa. Kwa kuangalia mabadiliko ya sheria zinazohusu mafao ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa Wastaafu kuanzia mwaka 1986 na juhudi zinazoendelea hizi sasa utaona kuwa Serikali inajitahidi kuboresha mafao ya viongozi wetu wastaafu ili yatolewe kwa kuzingatia mabadiliko ya gharama za maisha na uwezo wa Serikali.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Sasa anaweza kututhibitishia kwamba mafao yanayotajwa katika sheria Na. 2, Na. 3 yataporekebishwa yatawahusu viongozi wote na haki kwa usawa kwa wale wa zamani na wa sasa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni yetu ni kuhakikisha kwamba viongozi wote wanalipwa kwa usawa, waliostaafu kabla ya sheria hii ya mwaka 1999. Lakini kwa kuwa hiyo sheria itapita hapa nadhani na wenyewe Waheshimiwa Wabunge, wanayo nafasi ya kutusaidia kuipitisha hiyo sheria kama vile ambavyo tunakusudia. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wako viongozi ambao wamestaafu pande zote mbili za nchi yetu kwenye Jamhuri ya Muungano na kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Je, mafao yao wanalipwa sehemu zote mbili au ni sehemu moja tu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida mtumishi hawezi kupokea mishahara miwili na wala mstaafu hawezi kupokea pensheni mbili. Kinachotakiwa ni kwamba anachagua na ile sheria inaangalia kama amestaafu katika maeneo yote mawili ni wapi anaweza kwenda au wakati mwingine unachagua wapi ni kuzuri kuliko kwingine. (*Makofi*)

Na. 275

**Viwango vya Matumizi ya Maji Majumbani**

**MHE. BINILITH S. MAHENGE (K.n.y. MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, viwango vya matumizi ya maji majumbani yaani (*Domestic Water Standards)* viliandaliwa kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita na viwango hivyo vimepitwa na wakati vikilinganishwa na viwango vya Kimataifa:-

(a) Je, ni athari gani zinatokana na kutumia viwango hivyo hafifu?

(b) Je, ni lini viwango hivyo vitapitiwa upya ili kuviboresha?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani au kunywa ni suala muhimu hasa kutokana na uhusiano wake na afya za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu kutoka sehemu mbalimbali duniani unaonyesha kwamba ni muhimu kuweka utaratibu wa kuzuia athari hizi kuanzia kwenye vyanzo vya maji hadi kwa watumiaji maji majumbani. Viwango vya ubora wa maji pamoja na sheria husika ndiyo njia kuu ya kusimamia ubora wa maji na kuhakikisha viwango vinavyokubalika. Hivyo, tangu mwaka 1982 Shirika la Afya Duniani lilisitisha dhana ya viwango vya Kimataifa na kuanzisha miongozo ya Kimataifa. Shirika la Afya duniani hutayarisha na kutoa miongozo ya kimataifa ya kimataifa mbalimbali duniani kama msingi wa kutayarisha sheria na viwango vya kitaifa vya ubora wa maji. Matumizi ya miongozo, huzingatia hali halisi ya kijamii, utamaduni, mazingira na uchumi katika nchi husika. Miongozo hii inalenga kusaidia wataalam wa maji, afya, wanasheria, wanasiasa na washauri wao katika kutayarisha miongozo ya kitaifa..

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, athari zinatokana na maji ya kunywa husababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo vijidudu ambukizi ambavyo vinasema (*infectious agents),* kemikali za sumu, *(toxic chemicals* na mionzi *(radiological hazards).* Athari hutokea tu iwapo vipimo vya viwango vinavyokubalika havikufuatwa au vimezidi. Athari hizi zikiwemo pamoja na matatizo ya kiafya ya binadamu pamoja na kuchafua rangi ya maji, pia kutia harufu kwenye maji na pia kuharibu mabomba na vifaa mbalimbali vinavyotumika.

(b) Viwango vya ubora wa maji vilivyopo havijapitwa na wakati na vinaendana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Kwa kufuata miongozo ya Shirika la Afya Duniani utayarishaji wa viwango hivi ukizingatia kulinda afya za wananchi wetu ambapo

wataalamu mbalimbali walishiriki katika kuandaa viwango hivi wakiwemo madaktari. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya viwango vya ubora wa maji nchini, chini ya usimamizi wa Shirika la Viwango nchini (*TBS*) vimekamilisha kazi ya kupitia upya viwango vya zamani na kuongeza vile ambavyo havikuwekwa hapo awali kutokana na mazingira ya wakati ule na uwezo mdogo wa kiuchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Viwango nchini linaendelea na kazi ya kupitia viwango ambavyo bado vinahitaji marekebisho.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ili kuweza kusimamia viwango hivyo lazima kuwe na watalaam na ambapo kuna wataalam Wahandisi wa Maji na ma-*technician* wa maji. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akalihakikishia Bunge hili kwamba Chuo cha Maji, kilichokuwa kinatoa ma-*technician* bado kinaendelea kutoa hayo mafunzo na kama hakitoi anapata wapi ma-*technician* wa kwenda kusimamia hivyo viwango? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Ni kweli kwamba Wizara yangu ina Chuo cha Maji. Katika Chuo cha Maji, somo kuhusu viwango vya maji na mambo ya maabara za maji ni somo mojawapo muhimu na linaendelea kufundishwa hadi sasa na watalaam wa namna hiyo tunao.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ubora wa maji ni lazima hasa kwa maji ambayo wanatumia wananchi kwa kunywa. Je, Wizara inatumia utaratibu gani katika yale maji yanatengwa ya maporomoko yanayokwenda moja kwa moja kwa wanywaji na hasa maji ya Chanzo cha Manga kule Mpanda, Wizara inasema nini kuhusu ubora wa maji hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba maji yote ambayo yanatumika hapa nchini na yale ambayo yametokana na vibali vya Wizara ya Maji, maji hayo yanapimwa. Isipokuwa napenda kutoa wito kwamba kwa maji yale yote wananchi ambao wanatoa moja kwa moja kwenye vyanzo na kutumia natoa wito kwamba washirikiane na Wizara ya Maji ili kuhakikisha kwamba Mkemia wao wa Mkoa anapeleka sampuli ili yaweze kupimwa kabla ya kutumiwa. (*Makofi*)

Lakini juu ya hiyo napenda kusema ya kwamba maji yote tunayotumia naomba kutoa wito kwamba pia yachemshwe. Hilo ni jambo muhimu sana kwa sababu maji yanapotoka kwenye chanzo yanaweza yakawa salama lakini njia yanayopitia yanaweza yakakumbana na athari mbalimbali na mambo mbalimbali, kuingia humo hadi yanapomfikia mnywaji yanakuwa siyo salama. Hata maji ya bomba pia kwa sababu yanatoka ni salama na yamepimwa, lakini njia yanayopitia wakati mwingine bomba linaweza likawa limetoboka baadhi ya vidudu vya aina mbalimbali vinaweza kuingia au wakati mwingine bomba linaweza likawa kule mwishoni vyombo vinavyotumika kuchotea siyo salama. Kwa hiyo, natoa wito kwamba maji lazima yachemshwe. (*Makofi*)

Na. 276

**Kasoro katika Baadhi ya Sehemu ya Maumbile ya Mwanaume**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni ukweli uliodhahiri kwamba Mungu alipomuumba mwanadamu alitofautisha kati ya mwanamke na mwanaume na moja kati ya maumbile yanayotofautisha jinsi hizo kwa wanaume ni kwa kuota ndevu na sharubu.

(a) Je, ni madini gani yamekosekana mwilini mwa wanaume ambao hawakuota kabisa ndevu, sharubu hata nyusi?

(b) Je, kuna dawa yoyote ambayo inaweza kutumiwa na wanaume waliokosa maumbile hayo ili waweze kuyapata?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna tofauti nyingi za kimaumbile kati ya mwanaume na mwanamke kama vile kuota ndevu na sharubu. Sababu zinazoleta tofauti hizi ni nyingi, mojawapo ikiwa ni homoni katika miili yetu. Homoni zinazohusika katika swali hili ni *androgens*, ambazo ni homoni za kiume, na *estrogens*, ambazo ni homoni za kike. Kila binadamu anazo homoni aina zote mbili; *androgen* zinapokuwa nyingi kuliko *estrogen* mtu anakuwa na maumbile ya kiume, k.m. kuota ndevu na sharubu na kuwa na sauti nene, n.k. Aidha, *Estrogen* zinapokuwa nyingi kuliko *androgen* maumbile yanakuwa ya kike, kwa mfano kuota matiti, maumbile ya makalio na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo viini vya urithi yaani jenetiki vinatuamulia vile vile masuala mbalimbali yakiwemo ndevu, upara, mvi ambapo homoni huwa kichocheo tu. Ndiyo maana utakuta watu wa ukoo fulani, kwa ujumla, wana ndevu nyingi, ukoo mwingine hawana.

(b) Kimsingi hakuna dawa ya kukuza au kuotesha nywele za usoni kama vile ndevu sharubu na hata nyusi. (*Makofi*)

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri sasa kwa hawa akina mama ambao wanatoa sauti nzito kama mama yangu Maria Ibeshi Hewa tunawasaidia vipi? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Hauwezi kujibu swali hilo kwa sababu kwani yeye ana shida? Hana shida, kwanza yeye ndiyo sawa sawa kabisa. (*Kicheko*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli binadamu tuna maumbile tofauti hasa ametaja suala la nywele, kuna wengine tuna nywele za kipilipili na kuna wengine wana nywele za singa. Lakini wale ambao wengi tulio na nywele za kipilipili sasa hivi kuna *modification* tunapeleka vichwa vyetu kwenye mashine zinabadilika zinatoka zimelainika na hasa akina mama.

Je, hizi mashine hazitakuwa kuwa na madhara mimi nina wasiwasi zinaweza kuwa zinaathiri ubongo baada ya miaka 20 tukajikuta wa akina mama wengi wanasema maneno ya ajabu au wakawa vichaa? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jaribu kujibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna watu wengine wana nywele za kipilipili na nywele za singa kama alivyosema na kwamba anadai hasa akina mama wanakwenda *saloon* na kuweka dawa ambazo zinafanya nywele zao kuwa laini.

Lakini nataka niseme hata kuna wanaume pia wanaweka dawa siyo akina mama peke yao. Kama akina mama na akina baba ambao wanatumia dawa za kulainisha kama ilivyo dawa nyingine kuna madhara yake. Kwa hiyo, mimi ningewaomba wachukue tahadhari kuweza kuona kwamba dawa yoyote ile kama nilivyozungumza katika swali nililojibu jana zina madhara ya muda mfupi na muda mrefu. Kwa hiyo, kila mmoja awe na tahadhari ili aweze kuwa salama kama dawa nyingine zozote zile.

**NAIBU SPIKA:** Naambiwa Chilolo anataka kuuliza swali lingine la nyongeza. Haroub amemwandikia kwamba Chilolo ndiyo aulize swali la nyongeza.

Na. 277

**Tabia ya Wajawazito Kula Udongo**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA (K.n.y. MHE. JAMES P. MUSALIKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa iko tabia kwa baadhi ya akina mama wajawazito ya kula udongo, maarufu kwa jina la vipemba:-

(a) Je, tabia hiyo imeanza lini na wapi ilianzia?

(b) Je, kuna madhara gani na faida gani kiafya inayotokana na ulaji wa udongo huo?

(c) Kama kuna faida yoyote. Je, Serikali iko tayari kuwahamasisha wanaume pia waanze kula vipemba hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Udongo unaoitwa pemba ni udongo ambao mara nyingi huwa wa rangi nyekundu unaoliwa na kinamama hasa wale wajawazito. Uchunguzi unaonyesha kwamba kina mama wanaokula udongo huu mara nyingi pia hukutwa wana upungufu wa damu mwilini.

Damu hutengenezwa mwilini kwa kutumia madini ya chuma *(iron).* Binadamu huyapata madini haya kwenye vyakula hasa vile vyenye asili ya wanyama, matunda na mboga za majani. Ujauzito huongeza kwa kiasi kikubwa mahitaji ya madini ya chuma mwilini. Hivyo basi, ulaji duni wakati wa ujauzito hupelekea kupungua kwa madini ya chuma mwilini na kusababisha upungufu wa damu. Hali hii huwafanya wanawake wajawazito kupata hisia kali na hamu kubwa ya kupata madini chuma na hii ndiyo sababu baadhi yao hula udongo ambao una madini chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina taarifa rasmi kuhusu wakati na mahali ambapo tabia hii ya kula udongo kwa baadhi ya kina mama wajawazito ilianza.

(b) Udongo huu hauna faida yoyote kiafya. Badala yake matumizi ya udongo huu yana madhara kadhaa yafuatayo:- Kwanza, udongo sio kitu laini kinachoweza kupita kwa usalama kwenye njia ya chakula mwilini. Hivyo ulaji wa udongo waweza kusababisha mikwaruzo, michubuko na kupata majeraha ya ndani kwenye utumbo.

Pili, udongo unaweza kukwama kwenye kidole tumbo *(appendix)* na kusababisha ugonjwa wenye homa na maumivu makali unaojulikana kama *appendicitis.* Tiba yake mara nyingi ni upasuaji. Tatu, udongo una uchafu wa kila aina vikiwemo vijidudu vya bakteria na mayai ya minyoo. Hivyo kuutumia kama chakula ni hatari kwa afya ya mtumiaji. Kwa maneno mengine mtu anayekula udongo haambulii chochote katika nia yake ya kutaka kupata madini chuma. Badala yake ni madhara ambayo nimekwishayataja hapo awali.

(c) Kama nilivyojibu kwenye kipengele (b) hapo juu pemba ama udongo mwingine wowote ule hauna faida yoyote ya kiafya mwilini. Kwa sababu hiyo, Serikali haiwezi kuhamasisha jamii ikiwa ni pamoja na wanaume kuutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kutoa wito kwa kina mama wajawazito kuhudhuria kwenye kliniki ya Mama na Mtoto ili waweze kupatiwa vidonge vya madini ya chuma na dawa nyingine kwa ajili ya kuongeza damu badala ya kula udongo.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba pemba hii anayokula mama wajawazito inapunguza damu mwilini na aina hii ya pemba inatengenezwa sana. Serikali sasa haioni haja ya kuhakikisha kwamba angalau wanapunguza utengenezaji wa pemba hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nirekebishe, sijasema kwamba pemba inapunguza damu mwilini, nimesema pemba haina faida yoyote mwilini. Baada ya kufanya marekebisho hayo ningependa kusema kwamba ni kweli kwamba haya mapemba yanauzwa katika masoko. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba kwanza napenda niwaambie wale wanaouza pemba kwamba wanawafanya akina mama wawe na hisia kwamba kweli wanaweza kurekebisha upungufu wa damu yao.

Kwa hiyo, kwa kweli mimi ningependa kuwashauri wananchi kwamba hasa akina mama wajawazito kwamba unapojisikia una hamu ya kula pemba ujihisi kabisa kwamba wewe una upungufu wa madini chuma. Kwa maana hiyo uende kliniki ya Mama na Mtoto ili uweze kushauriwa vinginevyo badala ya kwenda sokoni na kununua pemba ambayo haitakusaidia badala yake itakuletea matatizo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ametueleza wazi kwamba udongo huu hauna faida yoyote mwilini na kwa kuwa udongo huu umeenea sana na unauzwa kila pembe hapa nchini na kwa kuwa udongo huu unapochukuliwa na unatengenezwa ili uje uuzwe unaharibu mazingira.

Je, sasa Wizara haioni umuhimu wa kupiga marufuku kabisa kuuza udongo huu kwa sababu hauna faida yoyote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya awali nimesema udongo huu hauna maana. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu wale wote wanaouza mapemba ili kuwashawishi akina mama kuweza kula kwa sababu kama kutibu afya zao mara moja waache kuuza pemba hili halina faida lakini badala yake inasababisha mama aache kwenda kliniki na kwenda kupata ushauri ambao utamfaa.

Kwa hiyo, naliarifu Bunge lako hili Tukufu kusema kwamba na nyinyi akina mama mnaokula pemba marufuku msile pemba nendeni hospitalini ili muweze kupata maelezo kutoka kwa wataalam. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata. Maana mapemba sasa yameshafutwa.

Na. 278

**Soko la Nje la Mazao**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe inazalisha kwa wingi mazao ya chakula hasa maharage na ndizi na kwa kuwa soko la ndani humpunja mkulima kiasi cha kushindwa kurudisha gharama za uzalishaji:-

(a) Je, Serikali inao mpango wowote wa kutafuta soko la nje la mazao ya ndizi na maharage?

(b) Kama mpango huo upo. Je, ni lini soko hilo litapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Karagwe huzalisha kwa wingi mazao ya chakula yakiwemo maharage na ndizi ambapo kiasi kikubwa cha mazao hayo huuzwa katika soko la ndani pamoja na nchi za kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na nchi nyingine za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Mbunge ya kutaka kuona wakulima wa Karagwe wanauza mazao hayo katika masoko ya nje bado hatuna uhakika kama uzalishaji wa mazao haya unakidhi mahitaji ya masoko hayo. Changamoto za kujibu ni pamoja na ubora wa juu wa mazao yanayozalishwa, aina ya ndizi na maharage hayo kama ndiyo yanayotakiwa katika nchi hizo, kama kuna miundombinu ya kusafirisha na kuhifadhi mazao yanayoharibika haraka kama ndizi, na yanayoliwa haraka na wadudu kama maharage pamoja na uzalishaji mdogo usiokidhi mahitaji ya masoko ya kimataifa. Kwa hiyo, ili kukidhi mahitasji ya soko la nje, ni muhimu kwa sasa kuweka msisitizo kwanza katika kuelewa mahitaji ya kila soko kwa maana ya wingi na ubora na kisha kuhamasisha wazalishaji kuzingatia zaidi mahitaji ya soko kwa maana ya aina ya zao/bidhaa, kiasi kinachohitajika, ufungashaji *(packaging)* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imefanya utafiti na kubaini kuwa mazao ya ndizi na maharage yanayozalishwa Wilayani Karagwe yana soko katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi nyingine jirani. Kwa mfano, taarifa ya bei ya zao la maharage katika eneo la Afrika Mashariki na Kati kwa mwezi Mei 2007 inaonyesha kuwa bei ya maharage kwa gunia la kilo mia moja mjini Bukoba ilikuwa shilingi 52,500 ikilinganishwa na shilingi 70,625 jijini Mwanza, shilingi 49,792 Jijini Kigali, shilingi 65,152 Jijini Nairobi, shilingi 70,912 Jijini Kampala na shilingi 66,304 Jijini Dar es Salaam. Kutokana na utafiti huo ni dhahiri kuwa majiji ya Kampala na Mwanza yalikuwa masoko yenye bei za juu kwa zao la maharage katika kipindi hicho na hivyo kuweza kuwa soko muhimu kwa zao la maharage yanayozalishwa Mkoani Kagera.

Kutokana na hali hiyo Serikali inaamini kwamba mazao ya maharage na ndizi kutoka Kagera yanaweza kuwa shindani katika soko la ndani na katika nchi jirani ili mradi tu wazalishaji na wafanyabiashara wanazingatia vigezo vyote muhimu vinavyohitajika katika soko.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge, awape wafanya biashara wa Karagwe na Mkoa wa Kagera kwa ujumla, habari hizi njema ili wachangamkie masoko hayo. Wizara yangu iko tayari kuendelea kushirikiana nao hadi wafanikiwe nia yao hiyo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumwuliza Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba kuna masoko katika nchi za jirani lakini vile vile atakubaliana nami kwamba ingekuwa ni jukumu la Wizara kuiandikia na kutoa miongozo kwa mikoa ili uzalishaji wa mazao haya yanaweza kuuzwa nje kama ndizi na matunda mengine yakatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa na kuweza kuuzwa huko na nchi nyingine kama Arabuni?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni wajibu wa Wizara kutaarifu Mikoa juu ya viwango na wingi wa mazao yanayohitajika katika masoko mbalimbali na ndiyo maana haya nimeeleza kwamba Wizara yangu imeshaanza kufanya tafiti mbalimbali hasa huu nilioueleza hapa sasa hivi nia yake ni kuona kama mazao haya yanaweza yakauzwa katika viwango gani na katika nchi gani. Kwa hiyo, Wizara iko tayari kuhakikisha kwamba jukumu hilo kwa kutaarifu Mikoa litafanyika. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa fursa na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo tu. Kwa kuwa suala la uzalishaji wa mazao haya ya ndizi, maharage na mengine hayako Karagwe tu, sehemu kama za Tukufu, Pemba na sehemu nyingine yapo. Uzoefu unaonyesha ni kuwa ukisafiri nayo kienyeji yale mazao watu walioko sehemu za nje wanahitaji sana. Je, Serikali inasaidiaje, kwanza kujua hicho kiwango cha uzalishaji wa ndizi kwa mfano Tukufu, Pemba, Kagera na mahali kwingine ni kiwango gani. Lakini pili wanasaidiaje basi kupata hilo soko na angalau ile nidhamu ya kuja kuhifadhi yale mazao yenyewe kwa sababu watu wanakata ndizi kienyeji tu, Wizara inasaidiaje jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kueleza hapa changamoto ambazo tunakabiliano nazo kuzijibu ikiwa ni pamoja na hilo la kuhakikisha kwamba tunakuwa na uhakika wa kuyasafirisha mazao haya ili yaweze yakafika huko yanakohitajika kwa usalama zaidi. Kwa hiyo, suala tu ya kwamba watu wa nje wanapokuwa hapa wanachangamkia bidhaa zetu hapa. hiyo tu haitoshi kwa kweli, kinachotakiwa zaidi ni kuhakikisha kwamba miundombinu yetu inaweza ikakidhi haja hiyo ya kuwafikia huko waliko. Kwa hiyo, ni jitihada za changamoto tulizonazo ambazo tunazifanyia kazi.

Na. 279

**Unywaji wa gongo**

**MHE. OMAR S. KWAANGW' (K.n.y. MHE. DAMAS P. NAKEI)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu nchini unywaji wa pombe haramu ya gongo umekuwa ukipigiwa kelele bila mafanikio:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, ni aibu kushindwa kutokomeza kabisa pombe haramu ya gongo?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa, katika jimbo la Babati Vijijini katika Kata ya Bashnet, Madunga na kadhalika. Watu wengi wanakufa kutokana na ulevi huo; na kwamba, katika maeneo hayo, wao wenyewe kwa wenyewe wanajuana ni nani atakufa baada ya mwingine kwa jinsi walivyochoshwa na gongo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali siku zote imekuwa inapiga vita utengenezaji, uuzaji na utumiaji wa pombe haramu ya gongo. Serikali katika kukabiliana na uhalifu huo imekuwa inafanya misako, upekuzi wa majumbani na maeneo mengine ya vilabu vya pombe za kienyeji, minadani pamoja na upekuzi wa vyombo vya usafiri ambavyo wakati mwingine hutumika kusafirisha pombe hiyo haramu ya gongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2006 katika Wilaya ya Babati, jeshi la polisi kwa kushirikiana na walinzi wa mgambo, viongozi wa vijiji, kata, tarafa na wananchi lilifanikiwa kukamata lita 2,826 za pombe ya gongo, mitambo ya kutengeneza pombe hiyo 26, malighafi ya kutengeneza pombe hiyo lita 60,000 na kufanikiwa kuwakamata watu 122, kati yao wakiwa wanaume 57 na wanawake 35. Watu wote hao walifikishwa Mahakamani na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa na nyingine kutolewa uamuzi. Aidha, katika kipindi cha Januari, 2007 hadi Juni, 2007 Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata lita 2,457 za pombe ya gongo, mitambo ya kutengeneza pombe 23 na watuhumiwa 84 kukamatwa. Kesi zilizofunguliwa Mahakamani ni 84, kesi zilizopata mafanikio ni 57. Mapipa 69 ya malighafi yalikamatwa na kuharibiwa yakiwa na ujazo wa lita 13,800.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri jitihada zote hizo zilizochukuliwa na Serikali siyo dalili za kushindwa kupambana na pombe haramu ya gongo bali ni hatua za mafanikio.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Kata ya Bushneti, Madunga na kadhalika kuna dalili za wazi za watu kuathirika na pombe ya gongo licha ya kufanya misako ili kutokomeza uhalifu huu. Napenda kutoa wito kwa viongozi wa Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa kuandaa kampeni kabambe ya kuelimisha wananchi wa Wilaya ya Babati Vijijini ili wajiepushe na utengenezaji na unywaji wa pombe hiyo haramu, kwani ni mbaya kwa afya zao. *(Makofi)*

Aidha, jeshi la polisi litaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na unywaji wa pombe hiyo na kuwaomba wananchi wema kushirikiana na vyombo vya dola katika kuwafichua wale wote wanaojihusisha na pombe haramu.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi katika swali hilo. Lakini nina swali moja la nyongeza. Hivi Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuliambia Bunge hili katika idadi ya waliokamatwa ambao wanahusika na utengenezaji au unywaji wa gongo ni askari wangapi wa polisi wamo katika wanywaji na wapikaji wa gongo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Hapana hilo swali, atajuaje wangapi polisi jamani. *(Kicheko)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa unywaji haramu wa pombe ya gongo umeshamiri sana maeneo ya mengi na jeshi la polisi wanafanya jitihada kubwa sana ya kukamata na kuwapeleka Mahakamani wanywaji na wauzaji. Je, Serikali inafahamu kwamba polisi wakati wanapeleka vidhibiti Mahakamani huwa si kiasi chote cha gongo kilichokamatwa ndiyo wanachopeleka Mahakamani? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haifahamu kwamba vidhibiti vinavyopelekwa Mahakamani vinapelekwa vilivyo na kasoro. Serikali inaamini kwamba askari wetu ni waadilifu na ni waaminifu na wanafanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu na Sheria za nchi. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniruhusu. Kwa kuwa kuna nchi ambazo zimesharuhusu wananchi wake kunywa gongo na kwa kuwa hao hawaziki watu wao kila siku na kwa kuwa kuna ugumu na polisi wana kazi nyingi kuliko kushughulikia gongo, Serikali haioni kwamba ni wakati sasa wa kuruhusu wananchi wakanywa gongo kama Uganda na Malawi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika swali la msingi kwamba unywaji wa gongo unaleta madhara kwa afya za binadamu. Kwa hivyo, kwa kuwa Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi inapenda sana wananchi wake haiko tayari kuruhusu watu wanywe gongo. *(Makofi)*

Na. 280

**Ubovu wa barabara ya Mpanga – Taweta**

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH (K.n.y. MHE. CASTOR R. LIGALLAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mpanga hadi Taweta Wilayani Kilombero iko chini ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na barabara hiyo haijapigwa greda tangu mwaka 1994 ilipomalizika kujengwa kwa msaada wa Serikali ya Uswisi na kwa kuwa, wananchi wa Vijiji vya Taweta na Tanganyika ni wakulima wakubwa wa machungwa na mpunga:-

Je, ni lini *TANROADS* itatengeneza barabara hiyo ili wananchi wawahi msimu ujao kuuza mazao yao:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallam, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Morogoro imefanya matengenezo ya barabara ya Mpanga hadi Taweta ambayo yalianza mwaka 2005/2006 kama ifuatavyo:-

(a) Kusafisha eneo la barabara *(bush clearance)* lenye urefu wa kilometa 36 kwa kutumia tingatinga na kazi imekamilika.

(b) Kuumba upya na kushindilia sehemu ya barabara yenye urefu wa kilometa 16 kwa kutumia greda na shindilia *(roller)* na kazi imekamilika.

(c) Kuchepusha sehemu ya barabara kwa kutumia tingatinga *(dozer)* na kazi imekamilika.

(d) Matengenezo makubwa *(major repair)* katika daraja la Mnyera na kazi imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kwa sasa inapitika pamoja na kuwa sehemu ambayo haikuumbwa na kushindiliwa, ina matatizo kidogo. Sehemu hii itaumbwa na kushindiliwa katika mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali moja la nyongeza. Hii barabara ambayo wenzetu wamesaidia kujenga upande wa Kilombero ni muhimu sana kuunganisha na Mkoa wa Iringa yaani Wilaya ya Njombe. Sasa amefika Taweta na Njombe Iringa wamefika Madeke na kuacha kaeneo kakilomita kama 20 hivi kwa hivyo kufanya barabara hizi zisiwe na faida kumbe kama wangeunganisha

hapa wangeunganisha Mkoa wa Ruvuma, Iringa na Morogoro. Je, Wizara haioni umuhimu wa kuunganisha hii sehemu ya Taweta na Madeke ili ndoto hizo na kazi hiyo muliofanya nzuri iweze kuwa na maana zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuunganisha mikoa yetu ni jambo ambalo ni zuri kwa sababu linachochea Maendeleo ya kiuchumi. Na ni kweli kwamba kama barabara hiyo ingeunganishwa kati ya Taweta kwenda Madeke kwenye Wilaya ya Njombe ingeleta manufaa.

Lakini kwa sasa kipande hicho ambacho kutokea Taweta bado haijawa chini ya *TANROADS* kama ambavyo imeombwa kwenye Bunge hili kama barabara hiyo itaunganishwa na ikawa chini ya *TANROADS* basi tutaiboresha, kwa sasa bado ni barabara ya Wilaya.

Na. 281

**Kiwanja cha Ndege Nambarashani**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER (K.n.y. MHE. KAIKA S. TELELE)** aliuliza:-

Kwa kuwa kampuni ya uwindaji ya *OBC (Orttello Business Corporation)* ilijenga kiwanja kikubwa cha ndege katika kitalu chake cha uwindaji huko Mambarashani karibu kabisa na *corridor* ya wanyama wanaotoka katika mbuga ya Serengeti na kwa kuwa, ndege kubwa za kubeba mizigo mizito na magari makubwa hutua na kuondoka katika uwanja huo:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa mtikisiko, kelele, ngurumo na milio ya ndege hizo kubwa imesababisha wanyama kuhamia katika makazi ya watu na kusababisha madhara kwa binadamu na mali zao ikiwa ni pamoja na mifugo na mashamba?

(b) Je, ni sababu zipo za msingi zilizosababisha kampuni hiyo iache kutumia uwanja wake wa awali ulioko Wasso karibu na makao makuu ya Wilaya na kwenda kujenga uwanja mwingine porini tena kwenye *corridor* ya wanyama, kuna siri gani huko?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning’o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu kuwa kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, viwanda, utalii, usafirishaji karibu na mbuga za wanyama kunaweza kusababisha mitikisiko, kelele, ngurumo na milio ya ndege kubwa

na hivyo kusababisha wanyama kuhama eneo moja kwenda eneo jingine na wakati mwingine kwenda katika makazi ya watu na kutishia usalama wa maisha yao.

Hii ndiyo maana kabla mwekezaji yeyote kuruhusiwa kujenga kiwanja cha ndege katika hifadhi zetu ni lazima apate kwanza kibali kutoka katika mamlaka inayohusika na hifadhi hiyo. Mamlaka hiyo hutoa ruhusa baada ya kujihakikishia kuwa ujenzi huo hauna madhara yeyote kwa viumbe wanaoishi katika hifadhi husika.

Aidha, mamlaka hudhibiti aina ya ndege zinazotua na kuruka kwenye viwanja vilivyopo kwenye mbuga za wanyama pamoja na aina ya magari ili kuhakikisha kwamba hazisababishi wanyama kuhama kutoka mbugani kwenda sehemu nyingine hususan kwenye makazi ya watu na kusababisha madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Wanyamapori ina viwanja ambavyo viko kwenye *corridor* za wanyama kama vile Serengeti na Seronera ambavyo vimekuwa vikitumika kwa muda mrefu na hakuna matukio yeyote ya wanyama kuhamia kwenye makazi au wanyama kukimbia kwani ndege zinazotua mara nyingi ni ndogo na hazina mitikisiko au kelele za kusababisha wanyama kuhama.

Aidha, kupitia mawasiliano na Idara ya Wanyamapori chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii tumearifiwa kuwa hakuna matukio ya kuhama kwa wanyama ambayo yameathibitishwa kutokana na miungurumo au kelele za ndege. Hata hivyo, ndege zenyewe hutua hapo mara chache sana na kwa kawaida, wanyama huhama *(animal migration)* wakati wa mvua – yaani kati ya miezi ya Agosti na Desemba kila mwaka. Lakini pamoja na uhamaji huo, hakuna tukio lolote lililowahi kutokea la wanyama kuhamia kwenye makazi ya watu na kuleta uharibifu.

Mheshimiwa Spika, sababu za msingi zilizosababisha kampuni ya *Orttello Business Corporation* iache kutumia kiwanja chake cha awali kiitwacho Wasso kilichopo karibu na makao makuu ya Wilaya na kwenda kujenga kiwanja kingine porini ni kutokana na umbali kati ya kiwanja cha Wasso ambacho pana urefu wa kilomita zipatazo 84 hadi sehemu kilipo kitalu chake cha uwindaji. Kujengwa kwa kiwanja cha Kichochoroni, kunawezesha ndege kutua karibu na kitalu cha Kampuni. Kumbukumbu zetu zinaonyesha kwamba ujenzi wa kiwanja ulipata idhini za mamlaka zote kuanzia Serikali ya Kijiji, Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine za kuhamisha kiwanja ni kampuni kutaka kuimarisha usalama wa ndege wakati wa kutua na kuruka kwani kiwanja cha Wasso kimezungukwa na milima ambayo pia kuhatarisha usalama wa ndege na abiria.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kampuni hii imeacha kiwanja hiki cha Wasso. Je, Serikali haiwezi ikachukua kiwanja hiki na kukiendeleza ili wananchi na Serikali wa Loliondo waweze kukitumia? Swali la pili, kwa kuwa *corridor* mara nyingi sana wananchi wanang'ang'ania kuishi kwenye *corridor* au kulitumia hilo

*corridor* lakini Sheria hairuhusu. Je, wanaporuhusiwa hii kampuni kuweka kiwanja cha ndege si itasababisha wananchi kuona kwamba matumizi ya *corridor* inawezekana hata kwao hasa kwa mifugo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimwambie Mheshimiwa Laizer kwamba kwa sasa Serikali haina nia ya kukichukua kiwanja cha Wasso lakini kama yuko mwekezaji ambaye angependa kuendeleza kiwanja cha Wasso basi anakaribishwa kwa mikono miwili.

Hivi sasa Mheshimiwa Naibu Spika, tuna viwanja 63 ambavyo hivi sasa vinatupa taabu. Lakini nadhani kama atatokezea mwekezaji ambaye anataka aendeleze Wasso basi sisi kama Wizara tutampa ushirikiano unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *corridor* kilipo kiwanja cha Kibarashani sasa hivi sio *corridor* ya kupitia wanyama. Kwa maana hiyo, hatuoni kwamba kuna matatizo yoyote ya masuala ya ndege kutua katika eneo lile.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, hivi viwanja ambavyo wanajenga wenye vitalu vinakuwa ni viwanja ambavyo wanatumia wao wenyewe binafsi ama hata wananchi wanaruhusiwa kutua huko na ndege zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi viwanja vinavyojengwa ni viwanja vya watu binafsi kwa matumizi yao. Nadhani kama kuna mtu anataka kutua pale mkiwasiliana na mwenye kiwanja sidhani kama kutakuwa ni tatizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtutura, si nilikuona au nimekosea? Siyo Mtutura, ulikuwa umesimama. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umeisha. Kwa hiyo, tunaendelea na matangazo.

Kwanza matangazo kuhusu wageni. Tunao wageni wa Mheshimiwa Capt. Chiligati, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ambao ni Mama Hana Atilia kutoka Finland. Halafu kuna Ndugu Lyamuya wa Shirika la Msingi, *Friendship Association.* Halafu pia tuna wageni wa Mheshimiwa Joyce Machimu, ni Bwana Isack Msanifu, yeye ni Mdau wa Chama cha Wafanyabiashara wa ng'ambo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu kuna wanafunzi wa shule ya msingi ya Uhuru ya Mkoani Dodoma na walimu wao, naomba wasimame wote, haya karibu watoto. Halafu tuna wanafunzi wengine wa shule ya *Basic Modern of Dar es Salaam,* wasimame wote na viongozi wao, karibu sana. *(Makofi)*

Halafu tuna matangazo ya kazi, sasa huyu ni Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma kwa Wabunge kwamba anaomba tutawatangazie Waheshimiwa Wabunge, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe anawaalika Wabunge wote kwenye Maonyesho ya Machapisho mbalimbali ya chuo chake, kwenye uwanja wa tafrija katika viwanja vyetu vya Bunge.

Halafu tuna matangazo mengine Mheshimiwa Kimiti, Mwenyekiti wa Chama cha Idadi ya Watu na Maendeleo, anawatangazia wanachama wake kwamba saa saba mchana kutakuwa na mkutano kwenye ukumbi wa Pius Msekwa. Halafu kuna Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anawatangazia wajumbe wake kwamba Kamati yao itakutana leo saa tano asubuhi, chumba 231, katika jengo la Utawala.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala, anawatangazia wajumbe wake kwamba kutakuwa na mkutano saa tano hii kwenye chumba 133. Nadhani tumemaliza matangazo, Katibu tuendelee na shughuli nyingine.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi Kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Maendeleo ya Mifugo

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa inayohusu Wizara yangu iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo na Ardhi, lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendelo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maelezo juu ya hali ya maendeleo ya sekta ya mifugo nchini, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya bajeti hii. Kamati ilitoa ushauri, maoni na maagizo kwa Wizara yangu ambayo yamezingatiwa katika kuandaa bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu itazingatia na kutekeleza ushauri, mapendekezo na maoni yatakayotolewa na Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu.Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa umahiri wake katika kuliongoza Taifa letu na kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo; naahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa nitasimamia kwa uwezo wangu maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Hayati Juma Jamaldin Akukweti pamoja na watumishi aliokuwa nao wakati wa ajali ya ndege; na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Vijana (CCM) Hayati Amina Chifupa Mpakanjia, vifo vya viongozi wa Chama cha Ushirika cha Nyaza, Marehemu Steven Kazi, Hezron Ndono, na William Kasubi, Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Nachukua fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Tunduru, Umoja wa Vijana (CCM) na Taifa kwa ujumla kwa misiba hii mikubwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza baadhi ya wabunge wenzetu kwa kupewa dhamana ya uongozi katika nyadhifa za uwaziri na unaibu waziri. Nawapongeza Mhe. Bernard Kamillius Membe, Mbunge wa Mtama kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Mhe. Dr. Batilda Salha Burian, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nachukua fursa hii kuwapongeza wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Yusufu Rajab Makamba kwa kuteuliwa kuwa Mbunge; Mheshimiwa Mtutura Abdalla Mtutura kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tunduru; na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dr. Aman Walid Kabourou, Mhe. Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba, Mheshimiwa Septuu Nasoro, Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortunatus Lwanyatika Masha. Ninawatakia mafanikio katika jukumu lao la kuimarisha Jumuiya yetu ya Afrika ya Mashariki.Mwaka huu nchi yetu imepata heshima ya kipekee kwa kupewa nafasi za uongozi katika asasi za Kimataifa. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha Rose Mtengeti Migiro aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dr. William Shija ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola na Balozi Liberatta Mulamula kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mtendaji wa kwanza wa Sekretariati ya Ukanda wa Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Edward Ngoyai Lowassa**,** Mbunge wa Monduli kwa

hotuba yake nzuri ya bajeti ambayo imeelezea mafanikio, changamoto zilizojitokeza pamoja na maelekezo ya kazi za Serikali kwa mwaka 2007/2008. Pia, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kwa hotuba zao nzuri ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, naomba kuwashukuru Waheshimiwa wabunge wote waliochangia masuala ya maendeleo ya Sekta ya Mifugo kupitia hotuba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo hapa nchini ni kati ya sekta zinazoweza kuchangia zaidi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA. Rasilimali kubwa ya mifugo iliyopo ikiendelezwa na kutumika vizuri itachangia zaidi kwenye kukuza uchumi wa Taifa na kupunguza umaskini kwa kuwa takriban kila kaya ina mifugo (ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, bata, wanyamapori wafugwao na wanyama wengine), hususan maeneo ya vijijini. Nchi yetu inakadiriwa kuwa na ng'ombe milioni 18.8, mbuzi milioni 13.5, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.37 na kuku wa asili milioni 33 na wa kisasa milioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo huchangia nguvu kazi na mbolea ya samadi kwenye kilimo, nishati, ajira, ni chanzo cha mapato na uhakika wa chakula pamoja na shughuli nyingine za kijamii. Pia, matumizi ya mifugo na mazao ya mifugo yanayozalishwa hapa nchini huokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuyaagiza kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, kama nchi yetu isingekuwa na mifugo inakadiriwa kuwa kati ya shilingi trilioni 11 na 15 zingehitajika kwa mwaka kuagiza mazao ya mifugo; sekta hii pia hutoa ajira na mahitaji mengine kwa watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa mwanzoni mwa mwaka huu, ulaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo umepungua kutoka wastani wa kilo 11 kwa mtu kwa mwaka mwaka jana hadi kilo 10.5 mwaka huu. Hata hivyo, ulaji wa nyama ya kuku na nguruwe uliongezeka katika kipindi hicho. Aidha, unywaji wa maziwa kwa mtu kwa mwaka ulipungua kutoka lita 40 hadi 39.

Ulaji wa mayai umebakia kuwa mayai 64 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na mwaka jana. Viwango hivi bado viko chini sana ikilinganishwa na vinavyopendekezwa na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005; Maagizo ya Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005; Maagizo ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara ya Maendeleo ya Mifugo tarehe 18 Januari, 2006 na MKUKUTA. Maelekezo hayo yameingizwa katika Mpango Mkakati wa Wizara kipindi cha mwaka 2007 – 2010 (*Medium Term Strategic Plan - MTSP*) pamoja na Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti ya Serikali (*Medium Term Expenditure Framework - MTEF*) kwa kipindi cha 2006/2007 hadi 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kuu la Sekta ya Mifugo ni kuongeza na kuboresha uzalishaji wa mifugo na mazao yake ili kuinua kipato cha wafugaji nchini. Katika mwaka 2006/2007 utekelezaji ulizingatia maeneo yafuatayo:-

(i) Kudhibiti magonjwa ya mifugo, kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mazao bora ya mifugo na pembejeo ili kuchangia uhakika wa chakula na kuinua viwango vya lishe ya jamii;

(ii) Kuongeza uzalishaji, usindikaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake ili kuongeza kipato na kuinua viwango vya maisha vijijini;

(iii) Kuhamasisha uzalishaji na uuzaji nje wa mifugo na mazao yake ili kuongeza pato la fedha za kigeni kwa Taifa;

(iv) Kubuni na kusambaza teknolojia sahihi ambazo zitaongeza tija katika matumizi ya ardhi na nguvu kazi;

(v) Kuendeleza matumizi ya uwiano na endelevu ya nyanda za malisho ikiwa ni pamoja na ardhi, maji na uoto wa asili;

(vi) Kuwaendeleza wataalamu wa Sekta ya Mifugo ili wawe na uwezo na morali ya kufanya kazi kwa lengo la kuongeza tija; na

(vii) Kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha utoaji wa huduma nzuri, sahihi na endelevu katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 yamekuwepo matukio muhimu yaliyowagusa wananchi katika maeneo mbalimbali, Sekta ya Mifugo na Taifa kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuhamisha wafugaji na mifugo yao kutoka Ihefu lilianza mwezi Septemba, 2006 na ilitarajiwa kuwa ng'ombe 303,254 wangehamia katika wilaya za Chunya, Kisarawe, Rufiji, Lindi Vijijini, Kilwa na Nachingwea. Hadi kufikia mwezi Juni 2007, takriban ng'ombe 218,000 walikuwa wamehamia katika wilaya za Chunya 100,000, Kisarawe 8,000, Rufiji 65,636, Lindi Vijijini 4,958 na Kilwa 18,000.

Aidha, jumla ya ng'ombe 4,000 walihamishiwa katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Kilosa. Jumla ya ng'ombe 17,406 walihamishiwa katika mikoa ya Dodoma, Rukwa, Ruvuma, Singida na Tabora. Zoezi hili lilifanyika ili kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira, Ardhi na Vyanzo vya Maji. Tathmini ya zoezi hili imefanywa na Tume iliyoteuliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Aprili 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulitokea nchini kuanzia mwezi Februari 2007 katika wilaya za Ngorongoro na Monduli. Hadi kufikia Mei 2007, ugonjwa huo uliripotiwa katika vijiji 130 vya wilaya 42 za mikoa 11 ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Singida,

Tabora na Tanga (Kiambatanisho Na. 2). Hadi tarehe 30 Juni, 2007, ng'ombe 15,726, mbuzi 19,199 na kondoo 11,085 walitupa mimba; na ng'ombe 16,973 mbuzi 20,913 na kondoo 12,124 walikufa (Kiambatanisho Na. 3). Ugonjwa huu uliathiri sana ulaji wa nyama, unywaji wa maziwa na biashara ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa, Serikali ilitoa Shilingi 4,798,675,000 kwa ajili ya kununua na kutoa chanjo, vifaa vya kuimarisha maabara na ufuatiliaji wa matukio. Jumla ya dozi milioni 5.5 kati ya lengo la dozi milioni 10 zimenunuliwa na kusambazwa katika wilaya 51 nchini. Aidha, Serikali imeandaa mpango wa miaka mitatu wa kukabiliana na ugonjwa huo unaohitaji kiasi cha dola za Kimarekani milioni 12.3. Mpango huo umepelekwa kwa wahisani mbalimbali kuombewa fedha na hadi sasa, mashirika ya Umoja wa Mataifa *(FAO* na *UNICEF)* yametoa dola za Kimarekani milioni 1.0 kwa ajili ya kutekeleza sehemu ya mpango huo. Hadi mwezi Juni 2007, jumla ya ng'ombe 1,553,379, mbuzi 892,619 na kondoo 319,613 wamechanjwa na zoezi la uchanjaji linaendelea katika mikoa ya Singida, Tabora, Dodoma, Arusha, Morogoro, Iringa, Kilimanjaro, Tanga na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi umeonyesha kuwa katika maeneo kame ambako asilimia kubwa ya mifugo hupatikana, ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever - RVF*) hutokea na kurudia kila baada ya miaka 5 hadi 15, panapokuwepo na mvua nyingi inayoambatana na mafuriko. Takwimu za mvua au kumbukumbu sahihi za hesabu zinazotokana na msongamano wa mawingu baridi (*Cold Cloud Density*) zinazopatikana kwa kutumia picha za satelaiti zinazotolewa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini zitatumika kama nyenzo za kutabiri milipuko ya ugonjwa huo na kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(Office Internationale des Epizooties - OIE)* ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege mpaka sasa umetokea katika nchi 55 zikiwemo tisa (9) za Afrika ambazo ni Burkina Faso, Cameroon, Cote d'Ivoire, Djibouti, Ghana, Misri, Niger, Nigeria na Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali iliendelea kujenga uwezo wa kutambua na kufuatilia ugonjwa huo, kupiga marufuku uingizaji wa kuku na mazao yake kutoka nchi zilizoathirika na uchukuaji wa sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa maabara. Aidha, sampuli za ndege pori, kuku, bata na kanga 9,290 zilifanyiwa uchunguzi katika Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke kwa kushirikiana na maabara za nje ya nchi na hadi sasa ugonjwa huo haujathibitika kuwepo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano wa Wadau wa Sekta ya Mifugo nchini ulifanyika tarehe 3 Oktoba 2006 mjini Dodoma. Mkutano huo ulijadili nafasi ya Sekta ya Mifugo katika uchumi wa dunia na katika kuinua pato la Taifa na kumwondolea mfugaji umaskini; uhamaji wa wafugaji; utengaji wa maeneo ya ufugaji; na matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya ufugaji endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkutano huo ulifunguliwa na Waziri Mkuu Mhe. Edward Ngoyai Lowassa kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baadhi ya masuala muhimu yaliyoazimiwa ni pamoja na; kukamilisha Sera ya Taifa ya Mifugo, kufanya Sensa kamili ya mifugo, kutoa elimu kwa wafugaji na kujenga miundombinu. Aidha, maazimio mengine ni kutenga na kumilikisha maeneo ya ufugaji, kutunga sheria ya kusimamia maeneo ya malisho, kuimarisha masoko ya mifugo, kuwawezesha wafugaji kifedha, kudhibiti magonjwa ya mifugo, kushirikisha sekta binafsi katika kuendeleza sekta, kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO),* ranchi ndogo na taasisi za Wizara. Baadhi ya maazimio hayo yametekelezwa na mengine yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, wataalam wa Wizara yangu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza na sekta binafsi walikutana Arusha tarehe 1 na 2 Desemba 2006 kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa majukumu, kubadilishana uzoefu, kuweka mikakati ya kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi katika Sekta ya Mifugo. Aidha, makongamano ya Vyama vya Wataalam wa Tiba *(Tanzania Veterinary Association (TVA)*, Uzalishaji wa Mifugo *(Tanzania Society of Animal Production (TSAP)* na Chama cha Wanawake Wataalam wa Kilimo na Mazingira (*Tanzania Association of Women Leaders in Agriculture and Environment-TAWLAE*) yalifanyika kwa madhumuni ya kujadili matokeo ya tafiti za teknolojia mpya, kubadilishana uzoefu, kujadili maslahi ya wataalam na uboreshaji wa utoaji huduma katika Sekta ya Mifugo. Wizara yangu inayafanyia kazi maazimio ya makongamano hayo ili yaweze kusaidia katika kuboresha maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilishiriki katika kuandaa, kuonesha na kuadhimisha sikukuu ya wakulima Nane Nane ambayo kitaifa ilifanyika katika viwanja vya Themi-Arusha kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti 2006. Maonyesho hayo yalipata heshima kubwa ya kutembelewa na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yalihitimishwa na Mhe. Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kaulimbiu ya maonesho hayo ilikuwa *Tokomeza Njaa na Umaskini kwa Kuzingatia Kilimo, Ufugaji Endelevu na Kuhifadhi Mazingira”.*

Nachukua nafasi hii kuwashukuru viongozi wote, wadau mbalimbali na wananchi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kushiriki na kufanikisha maadhimisho hayo. Aidha, nawashukuru wananchi na viongozi walioadhimisha maonyesho hayo katika kanda mbalimbali. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itashiriki katika kuandaa maadhimisho hayo ambayo kitaifa yatafanyika tena viwanja vya Themi-Arusha. Kaulimbiu ya maonyesho hayo ni “ Punguza umaskini kwa kuzingatia kanuni za kilimo, ufugaji, ushirika na hifadhi ya mazingira”.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Juni kila mwaka wadau wa maziwa huadhimisha Wiki ya Unywaji Maziwa duniani kote. Lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha unywaji wa maziwa ili kupanua soko la ndani na kuinua viwango vya utumiaji wa maziwa na mazao yake. Katika mwaka 2006/2007, Wiki ya Unywaji Maziwa iliadhimishwa kitaifa mkoani Mbeya kuanzia tarehe 31 Mei hadi 3 Juni 2007.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa:- "Kunywa maziwa kwa afya yako; Maziwa yaliyosindikwa ni salama; yasiyosindikwa yachemshwe kwanza".

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani hufanyika duniani kote tarehe 16 Oktoba kila mwaka. Wizara yangu ilishiriki katika maadhimisho hayo yaliyofanyika kitaifa mjini Morogoro kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzalisha chakula cha kutosha na kuwa na lishe bora. Kaulimbiu ilikuwa "*Wekeza Katika Kilimo kwa Uhakika wa Chakula "*.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya veterinari huadhimishwa na nchi nyingi duniani tarehe 29 Aprili kila mwaka kwa lengo la kutangaza mchango wa taaluma ya veterinari katika ustawi wa wanyama. Maadhimisho ya mwaka huu yalihusisha pia uzinduzi wa ofisi ya Chama cha Kulinda Wanyama Duniani *(World Society for Protection of Animals - WSPA)* tawi la Afrika hapa nchini. Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa *"Tambua Anuai Katika Taaluma"*.Kwa ujumla, matukio yote niliyoyaelezea hapo juu yametoa changamoto, msukumo na mchango mkubwa katika kuboresha maendeleo ya Sekta ya Mifugo. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuyafanyia kazi maazimio yaliyotokana na matukio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba niwasilishe Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007.
Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007. Sera na Sheria za Mifugo, mwaka jana Wizara yangu ililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa rasimu ya Sera ya Taifa ya Mifugo imewasilishwa Serikalini ili kupitishwa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Sera hiyo imepitishwa na Serikali mwezi Desemba, 2006 na hivyo Wizara yangu sasa itakuwa na mwongozo sahihi wa kusimamia Sekta ya Mifugo ipasavyo. Sera hiyo imechapishwa katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili na imesambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kuhuisha na kuandaa mapendekezo ya sheria mbalimbali pamoja na kuandaa kanuni na miongozo inayohusu Sekta ya Mifugo. Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 (*The Meat Industry Act No. 10, 2006*) iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mnamo mwezi Novemba 2006 imeanza kutumika mwezi Mei 2007 kwa Gazeti la Serikali Toleo Na. 19 (88) la tarehe 11 Mei, 2007. Aidha, rasimu ya Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Act) na* Sheria ya Biashara ya Ngozi (*The Hide and Skins Trade Act*) zimeendelea kuandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni sita (6) chini ya Sheria ya Magonjwa ya Mifugo (*Animal Diseases Act No. 17, 2003*) zimekamilishwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali Toleo Na. 4 (88) la tarehe 26 Januari, 2007 na ziko tayari kwa matumizi. Aidha, kanuni moja (1) chini ya Sheria ya Maziwa (*Dairy Industry Act No. 8, 2004*) imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakadiriwa kuwa nchi yetu ina rasilimali ya ardhi ya malisho ya takriban hekta milioni 60 zenye uwezo wa kulisha uniti za mifugo *(Livestock Units)* milioni 20. Hata hivyo, ni hekta milioni 40 zinazotumika kwa malisho na hekta milioni 20 zilizobaki ni vichaka na ardhi iliyopumzishwa. Pamoja na ukubwa wake, eneo

hilo halikidhi mahitaji ya malisho ya mifugo kutokana na kuwepo kwa mbung'o, uhaba wa maji, uhaba wa nyenzo na teknolojia katika kuzalisha na kuhifadhi malisho. Matatizo haya yamekuwa ni chanzo cha uhamaji holela wa wafugaji wa asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara yangu imeendelea kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya kuainisha, kutenga na kumilikisha maeneo kwa wafugaji na kuhakikisha yanaendelezwa. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya hekta 706,783 kati ya hekta takriban 1,894,700 zilizokuwa zimeainishwa, zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika vijiji 135 vya Halmashauri za Wilaya za Chunya (hekta 448,977), Kisarawe (hekta 28,579), Lindi Vijijini (hekta 76,800), Kilwa (hekta 10,733), Nachingwea (hekta 41,577), Makete (hekta 823), Mbarali (hekta 28,101), Morogoro (hekta 9,871), Chamwino (hekta 9,176) na Rufiji (hekta 52,146).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuharakisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya ufugaji, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilitoa mafunzo na vitendea kazi kwa wataalamu 18 wa Halmashauri za Bagamoyo, Bukombe, Kilindi, Kishapu, Manyoni, Mvomero, Namtumbo, Nkasi, Kilwa na Urambo kwa lengo la kuwawezesha kuandaa mipango ya matumizi endelevu ya ardhi ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji kwa ajili ya Mifugo, maeneo mengi nchini yanakabiliwa na uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo, na hivyo, kusababisha wafugaji kuhamahama ili kutafuta maji. Katika jitihada za kutatua tatizo hilo, Wizara yangu ilichangia uchimbaji na ukarabati wa malambo 13 katika Wilaya 8 za Lindi (2), Nachingwea (2), Kilwa (2), Longido (2), Maswa (2), Misungwi (1), Bariadi (1) na Chunya (1). Pia, ilichangia ujenzi wa mabwawa mawili ya Kishapu na Mwanga. Aidha, Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani *(Distrct Agriculture Development Plans* (*DADPs)* imechangia uchimbaji wa malambo 33 katika mikoa 13 na mradi Shirikishi wa Kuendeleza Kilimo na Uwezeshaji (*Participartory Agriculture Development Project (PADEP*) umechangia uchimbaji wa malambo 57 na visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbegu za Malisho na Hei, ili kuhakikisha wafugaji wanapata mbegu bora za malisho za aina mbalimbali, Wizara yangu iliendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu ya Langwira (Mbeya) na Vikuge (Pwani). Aidha, mashamba mapya sita (6) ya mbegu yalianzishwa katika Taasisi za Serikali za Mivumoni na Buhuri (Tanga), Kizota na Kongwa (Dodoma), Mabuki (Mwanza) na Sao Hill (Iringa) kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mbegu za malisho. Pia, mashamba sita (6) ya sekta binafsi yameanzishwa kwa madhumuni hayo. Katika mwaka 2006/2007 takriban tani 26 za mbegu bora za malisho na marobota 306,000 ya hei yalizalishwa na kuuzwa na taasisi za Serikali na sekta binafsi. Kati ya hizo, sekta binafsi ilizalisha tani 15 za mbegu na marobota 90,000 ya hei.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa malisho unaendelea kufanyika katika vituo 5 vya utafiti kwa kusia mbegu bora za nyasi, mikunde na miti malisho kwa lengo la kutathmini uwingi na ubora wa malisho. Aidha, hifadhi ya malisho (*forage conservation*) ilijaribiwa ili kukidhi mahitaji hususan wakati wa kiangazi. Jumla ya hekta 117 za malisho zilihusika katika mikoa ya Dodoma, Mbeya, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika,  Vyakula vya Mifugo Vilivyosindikwa, vyakula vilivyosindikwa ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija ya mifugo. Sekta binafsi imeendelea kusindika na kuuza vyakula hivyo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kusimamia ubora wa vyakula vilivyosindikwa kwa kuchukua sampuli na kuhamasisha umuhimu wa kusindika vyakula vyenye viwango vinavyokubalika. Aidha, tathmini ya viinilishe vya mchanganyiko wa vyakula vilivyosindikwa inaendelea. Uzalishaji wa vyakula vya mifugo uliongezeka kutoka tani 559,000 mwaka 2005/2006 hadi 606,566 mwaka 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Asilimia 90 ya vyakula hivyo vilikuwa vya kuku. Uzalishaji huo ni sawa na asilimia 93.3 ya mahitaji ya takriban tani 650,000 za vyakula vya mifugo nchini.

Mazao ya Mifugo na Masoko  Uzalishaji na Usindikaji wa Maziwa  katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imeendelea kuimarisha mashamba ya mfano ya kuzalisha mitamba ya Nangaramo, Ngerengere, Sao Hill, Mabuki na Kitulo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mitamba bora ya ng'ombe wa maziwa. Jumla ya ng'ombe wazazi 230 aina ya *boran* walinunuliwa kwa ajili ya mashamba ya Mabuki (85), Nangaramo (85) na Sao Hill (60).

Mheshimiwa Naibu Spika,  Wizara kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali yakiwemo *Heifer Project Tanzania (HPT)* na *Southern Highlands Livestock Development Association (SHILDA)* imesambaza mitamba 6,721 ya ng'ombe wa maziwa kwa wazalisha wadogo. Kati ya hiyo, 1,516 waliuzwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali na Ranchi za Taifa. Aidha, jumla ya mbuzi wa maziwa 1,202 walisambazwa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Usambazaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa uliofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali ulifanyika chini ya mpango wa "Kopa ng'ombe/mbuzi, lipa ng'ombe/mbuzi". Kwa sasa mahitaji ya Taifa ya mitamba ni takriban 8,000 kwa mwaka ukilinganisha na 6,721 iliyozalishwa na kusambazwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika,  asilimia tatu ya ng'ombe waliopo nchini ni chotara wa maziwa na hutoa kati ya lita 2,500 hadi 3,000 za maziwa kwa mwaka. Kiasi kikubwa cha ng'ombe hao kinatokana na uhamilishaji ambao hutumika kama njia mojawapo ya kuongeza ubora wa mifugo. Ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora kwa ajili ya uhamilishaji, Wizara yangu imeimarisha Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji *Usa River Arusha* kwa kukarabati mtambo wa kutengeneza hewa baridi ya naitrojeni itumikayo kuhifadhi mbegu za uhamilishaji pamoja na kununua hadubini (*microscope*) maalum ya kubaini ubora wa mbegu. Aidha, Wizara imenunua mtambo mpya wa kuzalisha hewa baridi ya naitrojeni kwa ajili ya kituo cha Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika,  uzalishaji wa mbegu za uhamilishaji uliongezeka kutoka dozi 51,230 mwaka 2005/2006 hadi 58,500 mwaka 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 14.2. Vile vile,  ng'ombe waliohamilishwa waliongezeka kutoka 46,530 mwaka 2005/2006 hadi 50,500 mwaka 2006/2007 ikiwa ni ongezeko la asilimia  8.5.

Aidha, wataalam 70 kutoka Halmashauri mbalimbali walipatiwa mafunzo ili kuboresha na kuongeza utoaji huduma ya uhamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa iliendelea kuratibu uzalishaji, usindikaji na uhamasishaji wa unywaji maziwa nchini. Ilikadiriwa kuwa uzalishaji wa maziwa ungeongezeka kutoka lita bilioni 1.41 mwaka 2005/2006 hadi lita bilioni 1.43 mwaka 2006/2007. Hata hivyo, kutokana na Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa uzalishaji ulifikia lita bilioni 1.42.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa na Chama cha Wasindikaji wa Maziwa *(TAMPA)* imefanya tathmini ya kubaini maeneo yenye maziwa mengi ili kuweza kuanzisha mfumo wa kukusanya, kuhifadhi na kusindika maziwa. Tathmini hiyo imefanyika kati ya mwezi Machi na Aprili 2007 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Manyara, Mbeya, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida na Tanga na kubaini kuwa maeneo hayo yanazalisha maziwa mengi isipokuwa hakuna mfumo mzuri na miundombinu kwa ajili ya ukusanyaji na usindikaji wa maziwa hayo. Aidha, tathmini imebaini kuwa viwanda 24 vikubwa na vya kati vina uwezo wa kusindika lita 496,000 na viwanda vidogo 11 vina uwezo wa kusindika lita 11,000 kwa siku. Kwa sasa, viwanda hivyo vinasindika lita 56,580 kwa siku, sawa na asilimia 11.2 ya uwezo. Usindikaji wa maziwa hapa nchini unakabiliwa na matatizo ya uzalishaji mdogo hasa wakati wa kiangazi, gharama kubwa za usindikaji na ulaji mdogo wa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti kuhusu uchanganyaji wa damu ya kigeni *(cross breeding)* na ile ya ng’ombe wa asili katika mazingira ya uchungaji huria kwa ajili ya kuboresha kiwango cha kuzaa (*calving rate*) na kupunguza muda kati ya mzao na mwingine (*calving interval* ) uliendelea katika vituo vya utafiti wa mifugo vya Tanga, Uyole na Mpwapwa. Matokeo ya awali katika kundi la ng’ombe wa maziwa yanaonyesha kuwa kiwango cha kuzaa kimeongezeka kutoka asilimia 40 na kufikia asilimia 55 na muda kati ya mzao mmoja na mwingine kushuka kutoka miezi 24 hadi 20. Vile vile, vifo vya ndama vimepungua kutoka asilimia 40 hadi 30. Aidha, uzalishaji wa maziwa kutoka ng’ombe wa asili umeongezeka kutoka wastani wa nusu lita hadi lita 2.5 vyote vikiwa na uhusiano wa karibu na lishe ya wanyama na kiwango cha damu ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji na Usindikaji wa Nyama, asilimia 97 ya ng’ombe waliopo nchini ni wa asili ambao ni chanzo kikuu cha nyama. Vyanzo vingine vya nyama ni mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Kutokana na Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa, uzalishaji wa nyama ulipungua kwa asilimia 9.3 kutoka tani 388,294 mwaka 2005/2006 hadi tani 370,566 mwaka 2006/2007. Kati ya tani hizo, nyama ya ng’ombe ni tani 180,629, mbuzi/kondoo 80,936, nguruwe 31,721 na nyama ya kuku 77,280 kama inavyoonyeshwa hapa chini. Ili kukidhi mahitaji ya soko, uzalishaji wa nyama unaendelea kuboreshwa kupitia mfumo wa unenepeshaji (feedlot) katika mashamba mbalimbali yakiwemo *Glienshils Ranch* na *Mtibwa Feedlot* (Morogoro), *Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries (SAAFI),* ranchi za Manyara na Mzeri na wafugaji wadogo katika mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga. Katika mwaka 2006/2007, takriban ng’ombe 26,400 walinenepeshwa kupitia mfumo huo. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa nyama kupitia mfumo huo kwa wafugaji wadogo kwa kutumia mbinu shirikishi ya shamba darasa (*Farmer Field School (FFS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za uzalishaji nyama zimeendelezwa pia na Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* ambapo kwa sasa ranchi zake (Kiambatanisho Na. 7a) zina jumla ya ng'ombe 39,883. Katika mwaka 2006/2007, *NARCO* iliuza jumla ya ng'ombe 9,553 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 kati ya lengo la kuuza ng'ombe 10,414 na kununua ng'ombe 950 wenye thamani ya shilingi milioni 166 kati ya lengo la ng'ombe 2,377 kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi. Lengo halikuweza kufikiwa kutokana na Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulioathiri biashara ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilisha zoezi la kugawanya hekta 294,188 za *NARCO* katika ranchi ndogo 125 zenye ukubwa wa kati ya hekta 2,000 na 4,000, zoezi la kutoa hati miliki kwa ranchi ndogo hizo limeanza kutekelezwa. Hadi sasa, utoaji wa hati miliki umekamilika kwa ranchi za Mzeri, Misenyi, Kitengule na Mkata. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya wawekezaji wameanza kuwekeza katika ranchi hizo na tayari kuna ng'ombe zaidi ya 25,000.

Napenda kuwapongeza wawekezaji wote walioitikia mwito wa Serikali wa kuanzisha ranchi ndogo ili kuboresha ufugaji nchini. Ranchi za *NARCO* pamoja na ranchi ndogo zikiendelezwa zitaweza kufuga jumla ya ng'ombe 183,700. Vile vile, kuimarishwa kwa ranchi hizo kutawezesha wafugaji wadogo kupata mbegu bora za mifugo, huduma za ufugaji, ushauri na soko kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** sambamba na uzalishaji wa nyama ulioendelea katika ranchi hizo, Wizara yangu iliendelea kufanya utafiti wa uzalishaji nyama bora. Madhumuni ya utafiti huo ni kuongeza uzito wa ng'ombe wa asili kutoka wastani wa sasa wa kilo 250 hadi kufikia kilo 450 katika umri wa miaka minne katika mazingira ya mfugaji. Utafiti huo ulihusisha kuchagua (*selection*) na kuchanganya damu za kigeni na zile za asili. Matokeo ya awali katika Wilaya za Bagamoyo, Handeni, Longido, Monduli na Mpwapwa yameonyesha kuwa ng'ombe hao wamefikisha kilo 400 katika umri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mbuzi na kondoo, katika mwaka 2006/2007, utafiti umeendelea katika vituo vya Tanga, West Kilimanjaro, Kongwa, Naliendele na Mpwapwa. Utafiti huo ulilenga kuongeza uzito kutoka wastani wa kilo 25 za sasa kufikia kilo 45 katika umri wa miaka miwili kwa kuboresha mabanda na lishe. Matokeo ya awali ya utafiti huo yameonyesha kuongezeka kwa uzito kutoka kilo 25 hadi 30 katika umri huo. Aidha, vifo vya vitoto vya mbuzi vimepungua kutoka asilimia 50 hadi 30. Idadi ya mbuzi aina ya *Malya* katika Vituo vya utafiti wa mifugo kwa ajili ya kusambaza vijijini imefikia 637 na kati yake, madume bora 53 yalisambazwa katika wilaya za Dodoma, Iramba, Kondoa, Kongwa, Manyoni na Mpwapwa kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, chambuzi za koo *(breed characterazation)* za mifugo ya asili zimeendelea kufanyika kwa ng'ombe aina ya *Iringa Red* (Iringa Vijijini na Kilolo)*, Ufipa* (Sumbawanga Vijijini na Nkasi) na *Ankole* (Geita); na mbuzi aina ya *Newala, Pare na Ujiji* na kwa kuku wa asili aina ya *Kuchi, Bukini, Kinyavu/Sasamala, Kiduchu/Kikwekwe na Kishingo*. Matokeo ya awali yanaonyesha

kuwa, kuna tofauti kubwa kati ya koo mbalimbali za mifugo ya asili katika stahimili ya magonjwa, ukubwa wa umbo, uzito, uzalishaji wa nyama na mayai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhifadhi koo asili za mifugo hii, Wizara yangu imenunua na kuhifadhi vituoni ng'ombe 64 aina ya *Ufipa* (Uyole), 12 aina ya *Ankole* (Mabuki); mbuzi 150 aina ya *Upare* na kondoo 100 aina ya *Red Maasai* (West Kilimanjaro), mbuzi 150 aina ya *Newala* na kuku 200 wa asili (Naliendele).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, utafiti wa ng'ombe aina ya Mpwapwa uliendelea katika Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na vijiji vya Mtumba (Dodoma Vijijini), Chipogolo (Mpwapwa), Ititi (Singida Vijijini) na Iguguno (Iramba). Idadi ya ng'ombe hao pamoja na chotara wao wameongezeka kutoka 979 hadi 1,060 ambapo madume bora 50 yamesambazwa vijijini katika wilaya ya Iramba ili kuinua kiwango cha uzalishaji wa ng'ombe wa asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, utafiti unaolenga kuboresha nguruwe wa asili umeendelea kufanyika katika kaya 75 za Wilaya ya Sumbawanga Vijijini. Tathmini imeonyesha kuwa katika mazingira ya wafugaji, nguruwe wa asili huzaa wastani wa watoto saba kwa mzao na kati yao ni wanne tu wanaofikia umri wa kuachishwa kunyonya. Aidha, uzito wakati wa kuzaliwa ni kilo 0.9 na uzito wakati wa kuachishwa kunyonya ni wastani wa kilo 10.8 katika hali ya mazingira ya vijijini. Uzito wakati wa kuchinja ni wastani wa kilo 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wadogo walioko vijijini na mijini wameendelea kutegemea ufugaji wa kuku kama chanzo kimojawapo cha mapato na lishe. Hata hivyo, ufugaji huo umeendelea kuathirika kutokana na ugonjwa wa mdondo ambao husababisha vifo vya kuku wengi kwa wakati mmoja. Katika mwaka 2006/2007, vifaranga milioni 28.7 vya kuku wa kisasa vilizalishwa nchini ikilinganishwa na vifaranga milioni 26.8 vilivyozalishwa mwaka 2005/2006. Aidha, vifaranga 782,550 viliingizwa nchini ikilinganishwa na vifaranga milioni 2.1 vilivyoingizwa katika kipindi hicho. Vile vile, mayai ya kutotoa vifaranga milioni 3.1 yaliingizwa nchini mwaka 2006/2007 ikilinganishwa na mayai milioni 8.4 mwaka 2005/2006. Kushuka kwa idadi ya vifaranga na mayai yaliyoingizwa nchini kulitokana na zuio kwa hofu ya tishio la Mafua Makali ya Ndege. Pia, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai bilioni 2.15 mwaka 2005/2006 hadi bilioni 2.23 mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 4 (Jedwali Na. 1).

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa kuku ulilenga kuongeza uzito wa kuku wa asili kufikia kilo 2 wakati wa kuchinjwa katika kipindi cha mwaka mmoja ikilinganishwa na robo tatu ya kilo; uzito wa yai kuwa gramu 100 ikilinganishwa na gramu 45 za sasa. Mojawapo ya njia za kufikia lengo hili ilikuwa ni kutumia majogoo bora kwenye kuku wa asili pamoja na mazingira yaliyoboreshwa. Tathmini ya ubora wa kuku chotara katika mazingira ya vijijini yaliyoboreshwa imefanyika katika vijiji 30 vya wilaya za Bagamoyo, Korogwe, Muheza, Pangani na Tanga mjini. Matokeo ya awali yanaonyesha kuwa, kuku chotara wakilishwa vyakula vya ziada wanataga kati ya mayai 60 hadi 70

kwa mwaka ikilinganishwa na mayai 40 yanayotagwa na kuku wa asili wanaofugwa kwenye mazingira hayo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Biashara ya Mifugo na Mazao Yake, Wizara yangu imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji katika biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi kwa kuhamasisha wafanyabiashara ya mifugo na nyama kutumia fursa ya soko la nyama la Uarabuni na la Jumuiya ya Ulaya *(EU).* Aidha, Wizara inaendeleza mpango wake wa kuanzisha maeneo huru ya magonjwa ya mifugo na kukamilisha uanzishwaji wa Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilifanya tathmini ya mashamba 35 ya serikali na watu binafsi kwa lengo la kuyasajili katika Rejesta ya Taifa ya Kumbukumbu za Mifugo.

Aidha, watalaamu wa mifugo 250, wafugaji 300, wafanyabiashara ya mifugo 80 na wamiliki wa viwanda vitano vya kusindika mazao ya mifugo walielimishwa na kuhamasishwa kuhusu mfumo huo. Vile vile, ujenzi wa viwanda vya kusindika nyama vya *Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries (SAAFI)* na *Tanzania Meat Pride* cha Morogoro ulikamilika na viwanda hivyo vimeanza kufanya kazi.

Pia, tathmini ya hali halisi ya viwanda vya kusindika nyama imefanyika katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Shinyanga. Serikali imekubali kubinafsishwa kwa Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kwa Kampuni ya *Triple "S" Beef Limited* na kuuza asilimia 51 ya thamani ya mali za machinjio ya kisasa, Dodoma kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited (NICO).* Taratibu za mikataba ya mauzo zinaendelea. Ni matumaini yangu kuwa, kuanzishwa na kubinafsishwa kwa viwanda hivyo kutahamasisha na kuongeza uzalishaji wa nyama na mazao yake kwa ajili ya soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, mauzo ya mifugo na mazao yake yaliyouzwa nje ya nchi yaliliingizia Taifa jumla ya shilingi bilioni 17.3. Pamoja na mauzo hayo, kumekuwepo na uagizaji wa mifugo na mazao yake kutoka nje ya nchi ambayo yaligharimu kiasi cha shilingi bilioni 6.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mauzo hayo, jumla ya ng'ombe 2,542 na mbuzi 1,852 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.03 waliuzwa Comoro, Kuwait, Falme za Kiarabu (Dubai), Oman na Burundi ikilinganishwa na ng'ombe 1,706 na mbuzi 800 wenye thamani shilingi milioni 675.9 waliouzwa mwaka 2005/2006. Pia, tani 92 za nyama ya mbuzi, kondoo na ng'ombe zenye thamani ya shilingi milioni 352 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 3.5 zenye thamani ya shilingi milioni 6.8 zilizouzwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la ngozi limeendelea kuwa zao kuu la mifugo linaloliingizia Taifa fedha za kigeni. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 1.98, mbuzi milioni 1.52 na kondoo milioni 1.2 vyenye

thamani ya shilingi bilioni 8.7 vilikusanywa. Aidha, jumla ya vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 1.7, mbuzi milioni 1.05 na kondoo 925,530 vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.2 viliuzwa nje ya nchi katika kipindi hicho ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 7.5 mwaka 2005/2006. Ongezeko hilo kubwa linatokana na kuongezeka kwa ubora na uuzaji wa ngozi zilizosindikwa (*semi-processed*) nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha zao la ngozi, Wizara yangu imetoa mafunzo kwa wachinjaji, wachunaji na wataalam 441 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Shinyanga, Dodoma na Arusha. Aidha, wakaguzi 80 wa nyama na ngozi kutoka Halmashauri 16 katika mikoa sita walipatiwa mafunzo yaliyogharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Kuendeleza Mazao ya Kilimo (*Common Fund for Commodities (CFC)*. Kutokana na mafunzo na uhamasishaji unaoendelea, kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa ngozi (*recovery rate*) kutoka asilimia 50 hadi 75 na ubora umeongezeka kama ifuatavyo:- Grade 1 kutoka asilimia 10 hadi 25 na *Grade II* kutoka asilimia 30 hadi 35. Vivyo hivyo, *Grade III* imepungua kutoka asilimia 45 hadi 35 na *Grade IV* kutoka asilimia 15 hadi 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (*Livestock Development Fund)* ulioanzishwa mwaka 2003/2004 kutokana na makusanyo ya ushuru wa asilimia 20 ya mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi, hadi kufikia mwezi Juni, 2007 umekusanya jumla ya shilingi bilioni 4.1. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mfuko huo utaanza kutumika rasmi mwaka huu wa fedha ili kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo na Viwanda vya Ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea na juhudi za kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo hasa yale ya mlipuko yenye kuleta madhara na hasara kwa wafugaji na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Aidha, magonjwa mengine ambayo madhara yake sio makubwa kiuchumi yaliendelea kudhibitiwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magonjwa ya Mlipuko, Wizara imeendelea kufuatilia ugonjwa wa Sotoka katika Kanda za Ziwa na Kaskazini ambapo sampuli za damu 2,842 za ng'ombe, 1,186 za mbuzi na kondoo na 18 za wanyama pori zilipimwa na kuthibitisha kwamba nchi yetu haina maambukizi ya ugonjwa huo. Aidha, Wizara iliwasilisha maombi tarehe 25 Septemba 2006 ya kutambuliwa na Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni (*OIE*) kuwa huru na virusi vya ugonjwa wa Sotoka. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mwezi Mei 2007, Shirika hilo lilikubali maombi yetu na hivyo kutoa cheti kwa nchi yetu kutambuliwa kutokuwa na virusi vya ugonjwa wa Sotoka. Kupatikana kwa cheti hicho, kunaondoa kipingamizi cha kufanya biashara ya mifugo na mazao yake kimataifa, kinachotokana na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (*CBPP*) uliendelea kudhibitiwa chini ya mpango wa *Roll Back Vaccination* katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Vile vile, chanjo dhidi ya ugonjwa huo ilifanyika katika mikoa mingine iliyothibitika kuwa na matukio. Katika mwaka 2006/2007, Serikali imenunua dozi milioni 3.2 za chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Shirika la Kilimo na

Chakula Duniani *(FAO)* lilitoa dozi milioni 1.0 kwa ajili ya kampeni dhidi ya ugonjwa huo. Hadi Juni 2007, jumla ya ng'ombe milioni 2.5 wamechanjwa na uchanjaji unaendelea. Tathmini imeonyesha kupungua kwa kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo, ambapo matukio katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yamepungua kutoka 147 mwaka 2002 hadi mawili mwaka 2006. Aidha, vifo vya ng'ombe kutokana na ugonjwa huo nchini vimepungua kutoka 1,533 hadi 90 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa Ugonjwa wa Miguu na Midomo umeendelea kufanywa na sekta binafsi kwa kushirikiana na Wizara. Katika mwaka 2006/2007, kulikuwa na matukio ya ugonjwa huo katika wilaya 44 za mikoa yote isipokuwa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambapo ng'ombe 8,506 waliugua na 172 walikufa. Wizara yangu iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kuagiza na kusambaza dawa ya chanjo ya ugonjwa huo ambapo dozi 240,000 zilinunuliwa na kutumika katika mikoa ya Mwanza, Iringa, Arusha, Morogoro, Dar es Salaam na Pwani. Katika mwaka 2006/2007, kulikuwa na matukio ya Ugonjwa wa Mapele-ngozi (*Lumpy Skin Disease*) katika wilaya 38 za mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Tabora na Tanga. Jumla ya ng'ombe 23,010 waliugua ugonjwa huo na kati ya hao 1,490 walikufa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzuia usafirishaji wa mifugo, kutoa chanjo kwa ng'ombe 1,244 na kutibu mifugo iliyoathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kudhibiti ugonjwa wa mdondo kwa kutumia chanjo inayostahimili joto (I-2) kwenye kuku wa asili. Uzalishaji wa chanjo ya mdondo uliongezeka kutoka dozi milioni 6.8 mwaka 2005/2006 hadi milioni 14.5 mwaka 2006/2007. Chanjo hiyo ilisambazwa kwa wafugaji kupitia Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Kanda na sekta binafsi. Vifo vya kuku viliendelea kupungua kutoka asilimia 90 hadi tano katika maeneo ilikotumika chanjo hiyo kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magonjwa Yanayoenezwa na Wadudu, magonjwa yanayoenezwa na kupe, hususan ugonjwa wa Ndigana Kali, ni moja ya matatizo makubwa yanayochangia kupunguza uzalishaji wa mifugo na mazao yake. Ili kudhibiti magonjwa hayo, katika mwaka 2006/2007, Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) na mipango mingine ilitoa shilingi milioni 362.7 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majosho 66.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na gharama kubwa za dawa za kuogesha mifugo, Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua dawa hizo ambazo wafugaji wanauziwa kwa asilimia 60 ya bei ya soko. Kampuni 8 ziliingia mkataba wa kuagiza na kusambaza lita 126,000 za dawa hizo katika mikoa 18 nchini (Kiambatanisho Na. 12). Aidha, dozi 120,000 za chanjo ya Ndigana Kali zilitolewa na FAO ambazo zilitumika kuchanja ng'ombe 117,184 katika mikoa 12 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakadiriwa kuwa asilimia 40 ya hekta milioni 60 za ardhi inayofaa kwa ufugaji nchini zina mbung'o na hivyo kuathiri ufugaji katika maeneo hayo. Katika mwaka 2006/2007, tathmini kwa ajili ya maandalizi ya kutekeleza Kampeni

ya Kutokomeza Mbung'o na Nagana Barani Afrika *(Pan African Tsetse and Trypanosomosis Eradication Campaign - PATTEC)* inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ilifanyika katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza na Tabora. Aidha, wataalamu 15 kutoka Halmashauri za Wilaya za Iringa Vijijini, Karatu, Kibaha, Kiteto, Kyela, Mbeya Vijijini, Mbulu, Mvomero, Newala, Ngorongoro, Simanjiro, Singida Vijijini, Temeke, Tunduru na Uyui walipatiwa mafunzo ya kudhibiti mbung'o na ugonjwa wa nagana. Vilevile, vipeperushi 2,500 na vijitabu 3,500 vya udhibiti mbung'o na nagana vilichapishwa na kusambazwa kwa wafugaji na shule za msingi katika mikoa ya Arusha, Kagera, Shinyanga na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kufanya utafiti kuhusu Ugonjwa wa Nagana ambapo mbung'o 900 walichunguzwa katika mbuga ya Tarangire na 5,859 katika mbuga ya Serengeti. Matokeo ya awali ya utafiti huo yameonyesha kuwa asilimia tatu ya mbung'o kutoka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na asilimia sita katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti walikuwa na vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa nagana. Vile vile, Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Nagana - Tanga iliendelea na ufugaji wa mbung'o wa aina mbalimbali kwa lengo la kutumia teknolojia ya madume ya mbung'o waliohasiwa ili kutokomeza mbung'o. Aina na idadi ya mbung'o waliofugwa kwa mwaka 2006/2007 ilikuwa *Glossina pallidipes* (3,000), *G. austeni* (55,445), *G. brevipalpis* (600) *na G. morsitans centralis* (1,700).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Magonjwa ya Mifugo Yanayoambukiza Binadamu (Zoonoses), Wizara yangu imenunua na kusambaza dozi 100,000 za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kwenye wilaya 39 zilizotoa taarifa za matukio ya ugonjwa huo na uchanjaji unatekelezwa na Halmashauri husika. Kutokana na ukubwa wa tatizo katika baadhi ya wilaya, Wizara yangu haikuweza kupeleka chanjo hiyo katika wilaya 90 kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, jumla ya ng'ombe 2,228 walichunguzwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba ambapo ng'ombe 103 sawa na asilimia 4.6 waligundulika kuwa na ugonjwa huo na hatua za kuudhibiti zilichukuliwa. Jumla ya dozi 5,000 ziliingizwa nchini na sekta binafsi na ng'ombe 3,500 walichanjwa. Aidha, utafiti wa chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba *(S19)* uliendelea katika Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke ambapo mchakato wa kutengeneza chanjo hiyo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti na uzalishaji wa chanjo ya Kimeta uliendelea katika Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke. Katika mwaka 2006/2007, kulikuwa na matukio 21 ya ugonjwa wa Kimeta katika wilaya za Hai (10), Monduli (2), Rombo (2) na tukio moja moja kwa wilaya za Bariadi, Kinondoni, Ludewa, Moshi Vijijini, Mpwapwa, Ngorongoro, na Singida Vijijini. Aidha, jumla ya dozi za majaribio 13,000 za chanjo ya Kimeta zilizalishwa katika Maabara hiyo na dozi 5,000 ziliingizwa nchini na sekta binafsi ambapo ng'ombe 4,402 walichanjwa. Vile vile, tathmini ya ubora wake imeonyesha kuwa chanjo hiyo inafaa kudhibiti ugonjwa huo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utoaji Huduma za Mifugo katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilifanya ukaguzi wa mifugo na mazao yake yaliyoingizwa na yaliyotoka nje ya nchi kwa lengo la kudhibiti usambaaji wa magonjwa ya mifugo. Ukaguzi ulifanyika kwa ng'ombe 2,542, mbuzi 1,852, nyama tani 92 na ngozi vipande milioni 3.68 vilivyouzwa nje. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwa vifaranga 782,550, mayai milioni 3.1, nyama tani 659, maziwa yaliyosindikwa tani 2,410 na bidhaa za maziwa tani 127 zilizoingizwa nchini. Pia, jumla ya ng'ombe 348,336, mbuzi 210,506, kondoo 60,677 na nguruwe 29,263 waliochinjwa kwa ajili ya matumizi ya ndani walikaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Baraza la Veterinari ina jukumu la kusimamia utoaji huduma za afya ya mifugo kwa lengo la kuhakiki viwango na ubora wa huduma hizo. Katika mwaka 2006/2007, madaktari wa mifugo 36 walisajiliwa na wataalamu wasaidizi 217 waliorodheshwa na kuandikishwa. Aidha, vituo 37 vya huduma za afya ya mifugo vilisajiliwa, vituo 43 vilikaguliwa na watoa huduma 135 walikaguliwa sifa zao katika Manispaa za Arusha, Kinondoni, Morogoro na Dodoma, Wilaya ya Handeni na Majiji ya Mbeya na Tanga. Matokeo yalionyesha kuwa vituo 22 havikukidhi viwango na watoa huduma 48 hawakuwa na sifa na hivyo kuagizwa kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kulingana na Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003. Pia, miongozo mitatu kuhusu madawa muhimu ya mifugo, vifaa-tiba vya mifugo na kuanzisha na kuendesha vituo vya karantini ya mifugo iliandaliwa na itasambazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo katika Sekta ya Mifugokatika mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha na kuwaelimisha wafugaji mbinu bora za uzalishaji, usindikaji wa mazao ya mifugo na upatikanaji wa masoko. Jumla ya wafugaji 20,440 walipatiwa mafunzo juu ya ufugaji bora na wa kibiashara ikilinganishwa na lengo la kufundisha wafugaji 20,000.

Mafunzo hayo yalitolewa kwa wafugaji wakufunzi 1,173 katika wilaya za Babati (42), Kahama (50), Karagwe (350), Kasulu (51), Kibaha (50), Misungwi (78), Monduli (50), Mpwapwa (46), Musoma (34), Nachingwea (23), Newala (21), Njombe (50), Nzega (40), Shinyanga (102), Simanjiro (50), Singida (46), Sumbawanga (47) na Tarime (43). Wafugaji wakufunzi kwa kushirikiana na maafisa ugani walitoa mafunzo kwa wafugaji 12,065 katika maeneo yao. Aidha, mafunzo hayo yalitolewa kwa wafugaji 902 katika vyuo vya mafunzo na mashamba ya mifugo na mafunzo nje ya darasa yalitolewa katika wilaya za Kilombero (2,140), Mvomero (960), Morogoro (1,360) na Kilosa (1,840).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, wataalam tisa wa mifugo kutoka Halmashauri nane za Chamwino, Kongwa, Meatu, Misungwi, Morogoro Vijijini, Mvomero, Ngorongoro na Nyamagana walipata mafunzo kwa ajili ya kuanzisha mashamba darasa katika Halmashauri zao. Mashamba darasa tisa kuhusu ufugaji bora yameanzishwa katika wilaya hizo. Aidha, nakala 13,200 za vijitabu, 152,100 za vipeperushi na mabango 30,700 za mada mbalimbali ziliandaliwa na kusambazwa kwa walengwa. Pia, vipindi 52 vya redio na 12 vya televisheni vilitayarishwa na kurushwa hewani. Vilevile, taarifa na makala 60 yalitolewa kwenye vyombo vya habari kuhusu matukio muhimu ya sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya taaluma ya mifugo katika ngazi ya astashahada na stashahada yaliendelea kutolewa katika vyuo vya mafunzo ya mifugo. Katika mwaka 2006/2007, wanafunzi 765 walisajiliwa na kati ya hao, 190 wanafadhiliwa na Serikali na 575 sawa na asilimia 75 wanajigharamia. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wataalamu 50 kuhusu uendelezaji wa njia za asili za hifadhi ya malisho na matumzi bora ya mabaki ya mazao ya kilimo; 241 kuhusu mbinu za kukabiliana na milipuko ya magonjwa; na 85 kuhusu ukaguzi wa maadili chini ya Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003. Vile vile, mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 17 na ya muda mfupi kwa watumishi 25 yalitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uimarishaji wa Miundombinu ya Sekta ya Mifugo, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imeendelea kuboresha miundombinu ya masoko ya mifugo ya Lumecha (Songea), Buhigwe (Kasulu), Kasesya (Sumbawanga) na Mbuyuni (Chunya). Aidha, katika mnada wa Kizota (Dodoma), Wizara yangu imejenga bucha, maeneo ya kupumzikia wateja na ya kuchomea nyama kwa lengo la kuufanya uwe na hadhi ya kituo cha biashara ya mifugo. Pia, Wizara imeanzisha mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo *(Livestock Information Network Knowledge System - LINKS)* katika minada 14 ya Pugu (Ilala), Mhunze (Kishapu), Meserani (Monduli), Weruweru (Hai), Ulemo (Singida), Korogwe, Lugodalutali (Mufindi), Mkongeni (Mvomero), Kizota (Dodoma Manispaa), Igunga (Igunga), Nasa (Magu), Kiabakari (Tarime), Kiliamatundu (Sumbawanga Vijijini) na Mbuyuni (Chunya) ambayo hutoa taarifa za bei na aina ya mifugo iliyouzwa kwa madaraja kwa kutumia ujumbe wa simu. Mathalani, taarifa za mnada wa Kizota zinapatikana kwa kuandika ujumbe *mk r dom* na kutuma kwenye namba *0787441555*. Vile vile, taarifa za *LINKS* zinapatikana katika mtandao wa *http://www.lmistz.net* na pia kupitia tovuti ya wizara *http://www.mifugo.go.tz* ambayo imeendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Taasisi na Vituo vya Utafiti wa Mifugo, Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo, Mashamba ya Kuzalisha Mitamba, Mashamba ya Kuzalisha Mbegu bora za Malisho, Kituo cha Uhamilishaji cha *NAIC - Usa River* na Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya kanda viliimarishwa kwa kukarabati miundombinu mbalimbali ikiwemo majengo, maabara na kuvipatia vitendea kazi.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa maabara na kufunga mitambo katika Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke kwa matumizi ya teknolojia za kisasa, *molecular biological techniques* kwa uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo yakiwemo Homa ya Bonde la Ufa, Mafua Makali ya Ndege na Ugonjwa wa Miguu na Midomo. Vilevile, vituo vya ukaguzi wa mifugo na mazao yake vya Marendego (Kilwa) kwa ajili ya kutoa huduma kwa mifugo inayohamia mikoa ya kusini na Kwala (Pwani) kwa mifugo inayosafirishwa nje ya nchi viliimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Mtambuka, Wizara yangu ina jumla ya watumishi 1,255 kati ya hao 266 ni wanawake na 989 ni wanaume. Mahitaji halisi ni watumishi 2,265. Kati ya waajiriwa, 665 ni wataalam wa mifugo na 590 ni watumishi wa

kada nyingine. Katika mwaka 2006/2007, Wizara imeajiri watumishi wanane na kukamilisha taratibu za kuajiri watumishi wengine 99, kuthibitisha kazini 20 na kupandisha vyeo 179. Aidha, taratibu za ajira katika utumishi wa umma, upandishwaji vyeo, matumizi ya raslimali, mafunzo na michezo zimeendelea kuzingatia misingi ya usawa na jinsia. Aidha, Dawati la Jinsia limeendelea kuimarishwa kwa kuunda Kamati yenye wajumbe kutoka kila idara na mafunzo yalitolewa kwa Mratibu wa dawati hilo. *(Makofi)*

Pia, Wizara imelipa jumla ya shilingi milioni 434 zikiwa ni malimbikizo ya marekebisho ya mishahara (*arrears*) kwa watumishi wake 243. Vile vile, Wizara yangu imehuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) ili kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu kwa watumishi wake na wadau wa Sekta ya Mifugo kuhusu taratibu, kanuni, na maadili ya utendaji katika utumishi wa umma ili kuboresha utoaji huduma na kuziba mianya ya rushwa. Aidha, Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa umeendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kutangaza nafasi za kazi na zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Mkakati wa kudhibiti UKIMWI sehemu ya kazi umetekelezwa kwa kuunda Kamati ya Uendeshaji ya UKIMWI pamoja na Sekretarieti yake. Aidha, dawati la kudhibiti UKIMWI limeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi ikiwamo kompyuta, luninga na vifaa vya ofisi. Pia, jumla ya makasha 411 ya kondom yalinunuliwa na kusambazwa kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara kwa mwaka 2007/2008 yamezingatia Mpango Mkakati wa Wizara kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 - 2009/2010 ambayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2010:-

(i) Patakuwepo na mifugo bora na mazao yake yanayokidhi mahitaji na viwango vya soko la ndani na nje;

(ii) Uwekezaji katika Sekta ya Mifugo uwe umeongezeka kwa asilimia 15;

(iii) Elimu kuhusu ufugaji wa kisasa iwe imetolewa kwa wafugaji na kuleta mabadiliko kwa asilimia 50 kutoka hali halisi iliyopo sasa;

(iv) Mifumo yote ya ufugaji iwe imeboreshwa na huduma za ugani ziwe zimeongezeka kwa asilimia 50 kutoka hali halisi iliyopo sasa;

(v) Magonjwa yote ya mifugo yenye athari kubwa za kiuchumi yawe yamedhibitiwa au kutokomezwa nchini;

(vi) Kuwepo na ukusanyaji, utunzaji, usambazaji na matumizi ya takwimu sahihi za mifugo pamoja na matokeo ya tafiti mbalimbali kwa wadau wa Sekta ya Mifugo;

(vii) Kuwepo na mfumo thabiti wa elimu, habari na mawasiliano kwa Wizara nzima;

(viii) Watumishi wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo wawe wamehamasika na kujikinga dhidi ya UKIMWI na magonjwa nyemelezi; na

(ix) Usimamizi wa rasilimali za Wizara uwe umeimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itatekeleza malengo niliyoyataja hapo juu kwa kuzingatia Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, MKUKUTA, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Dira ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Sera na Sheria za Sekta ya Mifugo, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itakamilisha kuandaa Mkakati wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo na kuandaa mpango wa utekelezaji. Mpango huo utakuwa ni sehemu ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini *(Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* iliyozinduliwa mwezi Julai 2006, Dodoma. Aidha, Wizara yangu itaendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera hiyo kupitia matukio muhimu ya Wizara, kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itakamilisha maandalizi ya sheria na kuandaa kanuni nyingine za sheria zilizopitishwa na zitakazopitishwa. Sheria hizo ni pamoja na:-

(i) Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Act);*

(ii) Sheria ya Biashara ya Ngozi (*The Hide and Skins Trade Act*);

(iii) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo (*The Grazing Land and Animal Feed Resources Act*);

(iv) Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo *(The National Livestock Research Institute Act);*

(v) Sheria ya kuanzishwa Maabara Kuu ya Mifugo *(The Central Veterinary Laboratory Act);*

(vi) Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo (*The Livestock Identification, Registration and Traceability Act*); na

(vii) Kanuni tatu (3) chini ya Sheria ya Veterinari (*Veterinary Act No. 16, 2003*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahitaji ya Ardhi, Malisho, Maji na Miundombinu kwa Mifugokatika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri katika kuhamasisha matumizi bora ya ardhi ya ufugaji iliyotengwa na kupimwa kiasi cha hekta 706,783 katika Halmashauri za Wilaya za Chamwino, Chunya, Kilwa, Kisarawe, Lindi Vijijini, Makete, Mbarali, Morogoro, Nachingwea na Rufiji. Aidha, Wizara itafuatilia

mwenendo wa hali ya malisho ili kutoa taarifa za tahadhari kwa wafugaji. Pia, mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho yataimarishwa ili yaweze kuzalisha tani 40 za mbegu na marobota 300,000 ya hei.

Vile vile, utafiti wa malisho ya aina mbalimbali yanayoweza kuboresha nyanda za malisho hasa wakati wa kiangazi utafanyika kwa kushirikisha wafugaji na kufanya utambuzi wa jinsi ya kujikinga na majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itakamilisha na kusambaza miongozo ya ujenzi wa malambo, uvunaji wa maji na matumizi ya maeneo ya malisho katika halmashauri za wilaya. Pia, Wizara kwa kushirikiana na halmashauri za Wilaya itafanya uchunguzi wa maeneo mapya ya ujenzi wa malambo katika Wilaya za Lindi, Nachingwea, Kilwa, Kisarawe, Rufiji, Chunya, Kishapu, Maswa na Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inasimamia miundombinu mbalimbali inayohusika na masoko ya mifugo na mazao yake, huduma za mifugo, utafiti na mafunzo. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itakarabati minada ya mifugo ya mipakani ya Buhigwe (Kigoma) na Kasesya (Rukwa) na kujenga mnada wa Kishili (Mwanza) na vituo vya kupakilia na kupakulia mifugo katika minada hiyo. Pia, mnada wa Mbuyuni (Mbeya) utakamilishwa.

Aidha, Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke, Maabara ya Utafiti wa Ndorobo, vituo vya utafiti wa mifugo, vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo na Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo vitaimarishwa ili viweze kutekeleza majukumu yake. Vile vile, minada na vituo vya kupumzikia mifugo katika mikoa saba ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo *(Livestock Information Network Knowledge System - LINKS)* vitaunganishwa. Vituo hivyo ni Babati (Manyara), Buhigwe (Kigoma), Kwala (Pwani), Masasi (Mtwara), Ngongo (Lindi), Lumecha (Ruvuma) na Rukole (Kagera).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Miundombinu kwa Mifugo iliyotoka Ihefu, ili kukabiliana na ukosefu wa miundombinu katika maeneo inakohamia mifugo kutoka bonde la Ihefu, hususan katika kukabiliana na magonjwa yaenezwayo na kupe, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008, kupitia *DADPs* itachangia katika ujenzi wa majosho 15 katika wilaya za Chunya (2), Nachingwea (2), Kilwa (3), Lindi (2), Mbarali (2), Kisarawe (2) na Rufiji (2). Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri kupitia *DADPs* itajenga minada ya awali ya Kitomanga (Lindi), Mbwemkuru na Nangurukuru (Kilwa), Umwekusini/Ikwiriri na Chumbi (Rufiji) ili kuwapatia soko la mifugo wafugaji waliohamia katika maeneo ya Wilaya hizo. Vile vile, malambo yatajengwa katika vijiji vya Mji Mwema na Mnyangala (Lindi), Somanga, Nangurukuru na Kiranjeranje (Kilwa).

Mheshimiwa Naibu Spika, Msingi wa Biashara ya Nje ya Mifugo na Mazao Yake, katika kuchangia kujenga msingi wa biashara ya nje ya mifugo na mazao yake; Wizara yangu inatarajia kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uboreshaji wa Urari wa Biashara Sekta ya Mifugo inao uwezo wa kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi wa Taifa, hasa urari wa biashara *(positive balance of payment*) kama tukifanya ubunifu sahihi.

Ili kufikia azma hiyo, Wizara imeandaa Programu ya Kuwezesha Upatikanaji wa Mifugo Bora na Mazao yake (*Supply-Side Improvement Program)* ambayo itachangia zaidi kwenye urari wa biashara. Katika programu hiyo, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* inatarajiwa kuuza mifugo (ng'ombe, mbuzi na kondoo) kwa makampuni ya hapa nchini yenye uzoefu wa kusafirisha nyama nje. Baadhi ya makampuni hayo tayari yana makubaliano na hoteli za kitalii hapa nchini ya kuwauzia tani 2½ za nyama kila wiki. Aidha, makampuni mengine yana makubaliano ya kuuza nyama kwenye migodi na maduka makubwa (*supermarkets*).

Vile vile, *NARCO* kwa kushirikiana na sekta binafsi itaanza kujenga machinjio mapya ya Ruvu (Kibaha), Bunda, Magu, Themi (Arumeru), Kyaka (Misenyi) na kukamilisha ujenzi wa machinjio ya Mbeya. Matangazo ya kupata wabia yamekwishatolewa kwenye magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, machinjio za kisasa na viwanda vya nyama vilivyoko Dodoma, Morogoro *(Tanzania Pride Meat),* Sumbawanga (SAAFI) na machinjio za kuku zilizopo Bagamoyo *(Mkuza Chicks)* na Dar es Salaam (Interchick) sasa zina uwezo wa kuzalisha nyama katika viwango vya ubora wa kimataifa. Kutokana na fursa hizi, hoteli za kitalii, migodi na maduka makubwa sasa yameanza kununua nyama humu nchini badala ya kuagiza kutoka nje. Mpango huu unatarajia kunusuru dola za Kimarekani milioni 2.5 kwa mwaka, kiasi ambacho kilikuwa kikitumika kuagiza nyama nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine zinazotarajiwa kupatikana kutokana na mpango huu ni pamoja na:-

(i) Kuinua kipato cha mfugaji mmoja mmoja kwa kuwa soko la nyama sasa litakuwa la uhakika;

(ii) Kumpatia mfugaji soko la uhakika kupitia mfumo unganishi wa "Ufugaji asili - Unenepeshaji ng'ombe - Uchinjaji na Uuzaji nyama nje";

(iii) Sekta ya Mifugo kuchangia katika kuimarisha Sekta ya Utalii nchini; na

(iv) Kampuni ya *NARCO* kuendeshwa kibiashara, kuboresha ufugaji wa asili na kuleta mageuzi katika Sekta ya Mifugo nchini.

Mkakati wa Kuboresha Mazao ya Mifugo kwa Kiwango cha Kimataifa, pamoja na jitihada nilizozitaja hapo juu, mazao ya mifugo bado yanakabiliwa na changamoto ya ubora na viwango vinavyokubalika kimataifa kwenye masoko makubwa kama Jumuiya ya Ulaya *(EU).*

Ili kukabiliana na hali hii, Wizara yangu kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Mifugo inashirikiana na wadau wa sekta kwa mfano, Bodi ya Maziwa, Bodi ya Nyama, Chama

cha Wafanyabiashara ya Ngozi *(LAT),* Vyuo Vikuu, watafiti na wafugaji kuandaa mkakati wa pamoja wa kuzalisha kibiashara na hatimaye kuuza kwenye masoko ya nje. Utekelezaji wa mkakati huo ambao unatarajiwa kuchukua miaka 15 hadi 20 kuanzia sasa, utaleta mageuzi ya haraka katika Sekta ya Mifugo nchini. Kwa kuanzia mkakati huo utatekelezwa na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini *(ASDP)* na fedha iliyoko kwenye Mfuko wa Kuendeleza Mifugo (*Livestock Development Fund)* ambao utaanza kutumika mwaka 2007/2008.

Mageuzi ya kuzalisha kibiashara na hatimaye kuuza kwenye masoko ya nje yanaweza kutekelezeka. Kwa mfano, miaka 20 iliyopita Brazil ilitekeleza mpango wa kubadilisha aina za koo za mifugo na kuzalisha kibiashara na hivi sasa, ni kati ya nchi zinazotawala soko la dunia kwa mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo na Kuandaa Maeneo Yasiyokuwa na Magonjwa *(Disease Free Zones),* aina nyingine ya kikwazo cha biashara ya mifugo na mazao yake nje ni kukosekana kwa maeneo huru ya magonjwa ya mifugo kama vile Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Homa ya Bonde la Ufa, Homa ya Mapafu, Mapele-Ngozi, Mdondo, Homa ya Nguruwe na kadhalika.

Aidha, ili kuzalisha mazao yanayokidhi mahitaji ya masoko yenye masharti mahsusi ya kiafya (*stringent sanitary and phytosanitary conditions*) baadhi ya wawekezaji wamekuwa wakiomba kupatiwa hati ya kuwa huru na magonjwa (*disease free certification).* Masharti hayo ni pamoja na kuwa na uzio wa asili au wa kutengeneza, usalama dhidi ya visababishi vya magonjwa (*bio-security*), utambulisho wa wanyama, kutokuwepo kwa visababishi vya magonjwa yaliyoainishwa na kuwa na utaratibu wa kufuatilia mwenendo wa magonjwa.

Ili kukidhi mahitaji haya kwa mujibu wa kanuni za OIE, Wizara itahakikisha kwamba utaratibu unaokubalika katika kudhibiti magonjwa yanayoathiri biashara ya nje ya mifugo unatekelezwa na kuendelezwa. Hili litatekelezwa kwa Serikali kuwezesha Halmashauri zenye maeneo ya uwekezaji wa mifugo kwa ajili ya biashara ya nje kudhibiti magonjwa yanayoathiri biashara ya mifugo na mazao yake, kwa kushirikiana na wafugaji wanaozunguka maeneo hayo. Aidha, Wizara itahimiza uogeshaji wa lazima wa mifugo (*compulsory dipping*) katika maeneo hayo.

Uboreshaji huu wa mazao ya mifugo kwa kiwango cha Kimataifa utaongeza tija ya Sekta ya Mifugo na kuchangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Vile vile, Wizara yangu itaendelea kutoa ruzuku kwa madawa ya kuogesha mifugo, kufanya savei na kufuatilia ikolojia ya kupe na usugu wa kupe kwa dawa za kuogeshea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zilizofanywa na Wizara yangu kutokomeza ugonjwa wa Sotoka na kuifanya nchi yetu kutambuliwa kimataifa kuwa huru na ugonjwa huo, zitaendelezwa kwa magonjwa mengine ili kuingia katika masoko ya nje. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikina na Halmashauri na wadau wengine itaendelea na jitihada za kupunguza hatari ya kutokea magonjwa na kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo hususan yale ya mlipuko yenye kuleta hasara kwa wafugaji,

madhara kwa walaji na uchumi wa Taifa. Ili kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya ng'ombe *(CBPP),* Wizara itanunua dozi milioni tano za chanjo kuendelea kutekeleza mpango wa "*Roll Back Vaccination*". Pia, Serikali kwa kushirikiana na nchi nyingine za Jumuia ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika *(SADC)* itaanza kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendela kufuatilia mwenendo wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa na kutoa chanjo katika maeneo yaliyoathirika. Kuhusu tishio la Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege, Serikali itaendelea kudhibiti uingizaji wa kuku na mazao yake kutoka nje ya nchi, kufuatilia mienendo ya ndege pori na kujenga uwezo wa tahadhari kwa lengo la kuutambua na kuukabili mapema. Vile vile, Wizara itazalisha dozi milioni 15 za chanjo ya Ugonjwa wa Mdondo (I-2) na kufanya tathmini ya matumizi ya chanjo hiyo kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kufanya uchunguzi wa mtawanyiko wa mbung'o pamoja na kutoa elimu ya mbinu shirikishi za udhibiti wa mbung'o katika mikoa yenye matukio ya magonjwa ya Nagana na Malale ya Kigoma, Kagera, Tabora, Rukwa, Lindi na Mbeya (Chunya). Pia, kituo cha utafiti wa mifugo na udhibiti wa mbung'o kitaanzishwa mkoani Kigoma kwa lengo la kuimarisha huduma za mifugo katika mikoa hiyo.

Kituo hiki kitaendesha shughuli zake kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa hiyo. Aidha, utekelezaji wa Kampeni ya Kutokomeza Mbung'o na Nagana Barani Afrika *(PATTEC)* unategemewa kuanza mwaka huu. Vile vile, Wizara itaendeleza matumizi ya teknolojia sahihi za kudhibiti kupe na mbung'o na magonjwa yanayoenezwa na wadudu hao ikiwa ni pamoja na kutumia madume yaliyohasiwa (*Sterile Insect Technique*), mitego na chambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa ikiwa ni pamoja na kununua na kusambaza chanjo dozi 50,000. Aidha, ng'ombe 5,000 watachunguzwa dhidi ya ugonjwa wa Kutupa Mimba na utafiti wa chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba (S19) kwa majaribio utaendelea. Vile vile, dozi milioni mbili za chanjo ya Kimeta zitazalishwa. Pia, Wizara itaimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa *'molecular biological techniques'* katika uchunguzi wa magonjwa ya mifugo na kuchunguza, kutathmini na kuhamasisha matumizi ya elimu asilia katika tiba ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, katika taratibu za biashara ya kimataifa, hasa ya mazao ya chakula, mlaji ana haki ya kujua chanzo cha chakula anachokula bila kujali kinatoka nchi gani. Ukosefu wa mfumo wa kutambua chanzo cha mazao ya chakula hapa nchini, ni moja ya sababu zinazofanya mazao ya mifugo ya Tanzania kushindwa kupenya kwenye soko la kimataifa. Ili kukabiliana na changamoto hii, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendeleza mpango wake wa kuhakikisha kuwa mifugo yote, hususan ng'ombe inatambuliwa,

kuandikishwa na kufuatiliwa ili kuhakiki ubora wa mifugo kuanzia kule inakofugiwa. Uhakiki huo utatoa msukumo kwa wafugaji kuboresha mifugo yao.

Katika kutekeleza mpango huo, mifugo yote hususan ng'ombe kwa kuanzia, itatakiwa kuvikwa hereni maalum. Aidha, mifugo yote itakayouzwa minadani ni ambayo itakayokuwa imeandikishwa kwenye Rejista ya Taifa ya Takwimu za Mifugo nchini. Utambuzi huu utasaidia kujua ng'ombe husika aliyeuzwa mnadani na kuchinjwa kwenye machinjio alikula chakula cha aina gani na ametunzwa namna gani kiafya ili kuwaondolea wasiwasi walaji wa ndani na wale wa soko la Kimataifa. Kwa kutumia mfumo huu, Wizara itasajili mashamba ya mifugo 100 na wafugaji 5,000 wakiwemo wa asili, kutambua ng'ombe 20,000 na kuanzisha Rejista ya Taifa ya Takwimu za Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji na Uendelezaji wa Mazao ya Mifugo, Maziwa, ili kuongeza uzalishaji wa maziwa pamoja na ulaji wake, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika maziwa, kubaini maeneo yenye maziwa mengi, uundwaji wa vikundi vya kukusanya na kusindika na kuimarisha Bodi ya Maziwa. Inakadiriwa kuwa lita bilioni 1.5 za maziwa zitazalishwa mwaka huu. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mifugo kwa kuyapatia vitendea kazi na kuyanunulia mifugo wazazi wakiwemo ng'ombe 400 na mbuzi 80. Aidha, mitamba 1,800 itazalishwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali na Ranchi za Taifa na kusambazwa kwa wafugaji kwa bei nafuu (ruzuku) ikilinganishwa na bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupanua soko la maziwa hapa nchini, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine katika mwaka 2007/2008 itaendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa pamoja na kutekeleza Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni (*School Milk Programme*) katika wilaya za Arusha, Hai, Moshi Vijijini, Tanga na Njombe.

Kwa sasa, Mpango huo unaotekelezwa katika shule 39 unafadhiliwa na wazazi, wasindikaji wadogo, *Fukeni Dairy Company Ltd, Peach Software Company Ltd, Tanga Fresh, Panges Omnus* na Shirika la Maendeleo la Italia – *CEFA.* Aidha, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* limeahidi kututafutia wafadhili zaidi watakaosaidia kupanua mpango huo katika wilaya nyingine nchini kwa lengo la kuwanufaisha wanafunzi 840,000 kutoka 12,985 wanaonufaika kwa sasa. Kutokana na Mpango huo kiasi cha lita milioni 43.7 za maziwa zitanyweka shuleni ikilinganishwa na lita 337, 610 zinazonyweka kwa sasa.

Aidha, Mpango huo unalenga kuboresha afya za watoto, kuongeza mahudhurio shuleni, kujenga utamaduni wa kunywa maziwa, kupanua wigo wa soko la maziwa na kuongeza ajira. Kwa kutambua umuhimu wa maziwa kwa watoto, nchi za *SADC* huadhimisha Siku ya Unywaji Maziwa Shuleni wiki ya mwisho ya mwezi Septemba kila mwaka. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau itafanya maadhimisho hayo kitaifa tarehe 26 Septemba, 2007 mjini Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendeleza tafiti mbalimbali zinazolenga kuongeza uzalishaji wa maziwa ya ng'ombe wa asili kutoka wastani wa nusu lita hadi lita 4 kwa siku. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji na vituo vya kutolea huduma za uhamilishaji vya kanda vya Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam na Dodoma ili kupanua huduma ya uhamilishaji nchini. Dozi 60,000 za mbegu bora zitazalishwa na kuuzwa kwa bei nafuu (ruzuku) na ng'ombe 52,000 wanatarajiwa kuhamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyama, katika mwaka 2007/2008, inakadiriwa kuwa tani 416,829 za nyama zitazalishwa. Aidha, Bodi ya Nyama itaanzishwa kama inavyoainishwa kwenye Sheria ya Nyama ya Mwaka 2006 kwa lengo la kusimamia sekta ndogo ya nyama.

Pia, ranchi za Kongwa na Ruvu zitaendelea kuimarishwa na kuendelezwa ili kuongeza uzalishaji. Wizara yangu itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji katika biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi kwa kuhamasisha wafanyabiashara ya mifugo na nyama kutumia fursa ya soko la nyama la Uarabuni na la Jumuiya ya Ulaya *(EU).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, uzalishaji wa mayai na vifaranga unatarajiwa kuwa bilioni 2.4 na milioni 34 sawia. Wizara yangu itaendeleza utafiti wa kuku wa asili (*Kuchi, Bukini, Kinyavu/Sasamala, Kiduchu/Kikwekwe na Kishingo*) katika mazingira yaliyoboreshwa ili kuongeza tija na uzalishaji wa kuku wa asili vijijini. Ngozi, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itatekeleza Mkakati wa Kuendeleza Zao la Ngozi nchini kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo. Utekelezaji wa mkakati huo pamoja na mambo mengine unalenga kuongeza ubora na ukusanyaji wa ngozi. Katika kipindi hicho, inakadiriwa kuwa vipande milioni 2.3 vya ngozi za ng'ombe, milioni 1.7 vya mbuzi na milioni 1.4 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 10.5 vitakusanywa. Vile vile, vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 2.0, mbuzi milioni 1.5 na kondoo milioni 1.2 vyenye thamani ya shilingi bilioni 18.0 vinatarajiwa kuuzwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Huduma, Mifugo na Mazao yake, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Baraza la Veterinari ili liweze kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kukagua na kusajili asilimia 100 ya wataalam wahitimu wa afya ya Mifugo na vituo vya kutolea huduma. Aidha, Wizara itaboresha mfumo wa mawasiliano wa Baraza la Veterinari, kuandaa miongozo na viwango vya kusimamia wataalamu wa afya ya mifugo, kutoa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma na ujasiriamali kwa wataalamu 100 wa mifugo pamoja na wale wa Sekta binafsi. Vile vile, Baraza litakagua mitaala ya mafunzo ya mifugo na kuhamasisha ushirikishwaji wa sekta binafsi kupitia vyama vya kitaaluma katika kutoa huduma bora za afya ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kufanya ukaguzi wa mifugo na mazao yake yatakayoingizwa na kutoka nje ya nchi kwa lengo la kudhibiti usambaaji wa magonjwa ya mifugo. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na

kukarabati na kuimarisha vituo 30 vya ukaguzi vya mipakani; kukarabati na kuimarisha miundombinu na vifaa katika maeneo 15 ya kupumzikia na ya karantini kwa mifugo; kuimarisha huduma za udhibiti na ukaguzi kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa nyama na ngozi 200 na wakaguzi 60 wa mazao ya mifugo kwenye Halmashauri. Aidha, itashirikiana na TFDA kusimamia matumizi ya pembejeo za mifugo, ubora na usalama wa mazao ya mifugo na kuelimisha jamii kuhusu viwango na usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Ugani na Mafunzo, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na sekta binafsi, itaendelea kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji juu ya matumizi ya teknolojia sahihi na mbinu bora za ufugaji. Kwa sasa, wapo wataalam wa ugani wa mifugo 2,581 ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam 16,050 kulingana na lengo la Serikali la kuwa na mtaalam wa ugani wa mifugo katika ngazi ya Kata na kijiji. Ili kukidhi mahitaji hayo, Serikali itajaza nafasi hizo kwa awamu na kwa mwaka huu itaajiri wataalam 1,250 watakaotokana na wahitimu waliopo katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu itaandaa na kusambaza vijitabu 13,000, vipeperushi 152,000, mabango 30,000 na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya televisheni kuhusu ufugaji bora. Vile vile, wafugaji 21,000 wataelimishwa juu ya ufugaji bora na kuanzisha mashamba darasa 10 ya mfano katika wilaya za Hai (2), Same (2), Arumeru (2), Karatu (1), Korogwe (2) na Handeni (1) pamoja na kuimarisha yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaandaa mitaala kwenye mfumo wa moduli na kusimamia utekelezaji kufuatana na matakwa ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Pia, Wizara itagharamia mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 300 waliopo kazini na 1,000 watarajali. Aidha, wadau mbalimbali wataendelezwa kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo wakiwemo wataalam 90 kuhusu kuendeleza njia za asili za kuhifadhi malisho kama vile *ngitiri* na *ololili;* wakaguzi 80 wa vyakula vya mifugo ili kudhibiti ubora wa vyakula; na wataalam 75 wa uhamilishaji kutoka Serikali za Mitaa, mashamba ya serikali na ya binafsi. Pia, wadau 200 wakiwemo wachinjaji, wakataji nyama, wachunaji, wawambaji na wakaguzi wa ngozi wataelimishwa ili kuendelea kuboresha zao la ngozi.

Masuala ya Mtambuka, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaajiri watumishi 283 wakiwemo wakufunzi wa mifugo 72 wa vyuo vya mifugo watakaotoa mafunzo maalum kwa maafisa ugani ili kupunguza pengo lililopo. Aidha, Wizara itaendelea kuzingatia sheria na miongozo ya ajira katika utumishi wa umma, manunuzi na ugavi ili kuleta uwazi katika utoaji huduma na kuziba/kuzuia mianya ya rushwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa. Vile vile, Wizara itaendelea kuboresha mahusiano kazini, kuendesha mafunzo na kuandaa viashiria muhimu vya jinsia ili kuweza kufuatilia na kupima mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya athari za UKIMWI katika Wizara na taasisi zake, kutoa mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kupambana na kuzuia maambukizi mapya.

Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kupima UKIMWI kwa hiari na kuelimisha walioambukizwa kuishi kwa matumaini, kuondoa unyanyapaa na kusambaza kondomu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Shukurani, hotuba yangu haitakuwa imekamilika kama sitawashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada mikubwa ya kifedha, vifaa na kiufundi kutoka nchi wahisani, mashirika mbalimbali, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za fedha. Aidha, mafanikio hayo yametokana na hamasa na ushirikiano wa wananchi hasa wafugaji wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kupitia Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzishukuru Serikali za nchi za Australia, Austria, Denmark, Japan, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Ireland, Marekani, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Italia.

Aidha, napenda kutoa shukrani kwa mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IFAD, CFC, UNICEF* na *IAEA.* Pia napenda kutoa shukrani kwa taasisi za kifedha za kimataifa ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japani (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID), Taasisi ya Raslimali za Wanyama la Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Norway (NORAD).

Aidha, nachukua nafasi hii kuyashukuru Mashirika ya kidini ikiwa ni pamoja na Kanisa Katoliki Tanzania *(TEC)* na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania *(KKKT),* pamoja na Taasisi nyingine za hiari za *Vet Aid, OXFAM* na *Wellcome Trust* za Uingereza, Austro-*Project, Heifer Project Tanzania (HPT)*, *World Vision, FARM Africa, Land 'O' Lakes, Bangladesh Rural Advancement Commitee (BRAC), Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA)* na *International Livestock Research Institute (ILRI)* na wote wale ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara yangu. Naomba kwa dhati kabisa na kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote na kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuendeleza Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa

Shinyanga Mjini kwa msaada na ushauri wake wa karibu katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Dr. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu Dr. Jonas Melewas, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi Ya Fedha Kwa Mwaka 2007/2008, ili Wizara yangu iweze kutekeleza na kufikia malengo yaliyokusudiwa, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara yangu inaomba kutumia jumla ya shilingi 22,397,516,000.00. Kati ya kiasi hiki, shilingi 12,621,516,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 9,776,000,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 6,931,332,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengine (OC) na shilingi 5,690,184,000.00 ni kwa ajili ya mishahara *(PE).* Vilevile, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi 1,424,000,000.00 ni fedha za hapa na shilingi 8,352,000,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono sasa nitamwita Msemaji wa Wizara hii kutoka kwenye Kamati Mheshimiwa Kidawa, tunaomba wale watakaokuwa wanatakiwa kusema wawe wanasogea mbele kwa sababu muda tunaotumia ni mwingi.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 81 (1) Toleo la 2004 na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka uliopita 2006/2007 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba yake na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wanawake wote wa

Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa juhudi zao kubwa za kujiletea maendeleo yao kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati natumia fursa hii kutoa pole kwa wazazi, ndugu na jamaa wote wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Aidha Kamati inatoa pole kwa ndugu na jamaa wa aliyekuwa Meneja wa Kampuni ya Mkuza *Chick* Marehemu Max Mambali aliyefariki hivi karibuni. Vile vile Kamati inatoa mkono wa pole kwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed kwa kufiwa na mama yake, Mungu aziweke roho za marehemu wote hao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ilikutana Dar es salaam tarehe 01 Juni 2007 ili kuchambua na kutathimini utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka uliopita, pamoja na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Ili kutekeleza kazi hiyo, Kamati ilizingatia mambo/utaratibu ufuatao:-

(i) Kupitia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati iliyochambua Bajeti ya mwaka uliopita (2006/2007).

(ii) Kuchambua utekelezaji wa malengo ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

(iii) Kuchambua na kupitia kazi zilizopangwa kufanyika mwaka huu wa fedha 2007/2008 pamoja na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya mifugo ni moja kati ya sekta ambazo ikiwekewa taratibu nzuri za ufugaji na kwa kutolewa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji bora, inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini wa kipato kwa Watanzania walio wengi na hasa kwa jamii ya wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2006/2007, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati ilitoa maoni na ushauri kadhaa ambapo ilipendekeza yazingatiwe na kutekelezwa kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza tija katika Sekta ya Mifugo. Aidha, yamekuwepo mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka uliopita wa 2006/2007. Baadhi ya mafaniko hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Serikali ilifanikiwa kupitisha, kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala za Sera ya Taifa ya Mifugo. Aidha, Wizara imekamilisha kazi ya kutafsiri Sera hiyo katika lugha ya Kiswahili.

(ii) Rasimu ya Sheria mpya ya Ustawi wa Wanyama (*Animal Welfare Act*) na rasimu ya Sheria ya maeneo ya malisho na vyakula vya wanyama (*Grazing Land and Animal Feed Resources Act*) imekamilika na ipo katika mchakato wa kupelekwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Kadhalika rasimu za Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa mifugo (*National Livestock Research Institute Act*) na Sheria ya Utambuzi, Usajili, na

Ufuatiliaji (*Livestock Identification, Registration and Traceability Act*) zipo katika hatua mbalimbali za kitaalamu kwa lengo la kuziboresha.

(iii) Kuendelea na mchakato wa ubinafsishaji wa machinjio ya Dodoma na kiwanda cha kusindika nyama cha Shinyanga ambapo tathimini ya hali halisi ya viwanda vya kusindika nyama katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Shinyanga imefanyika. Aidha, Serikali imeridhia ubinafsishaji wa kiwanda cha nyama cha Shinyanga kwa Kampuni ya *Triple "S" Beef Limited.* Pia, Serikali imeridhia kuuza asilimia 51 ya mali za machinjio ya Dodoma kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited (NICO)*.

(iv) Ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa takwimu mbalimbali za mifugo kwa wadau kwa nia ya kuboresha sekta hiyo.

(v) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo (*DADP's*) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), pamoja na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika.

(vi) Kuratibu na kufuatilia miradi ya maendeleo inayofadhiliwa kwa misaada na mikopo kutoka kwa wahisani na taasisi zingine za fedha.

(vii) Wizara imeendelea kufanya utafiti wa magonjwa ya mifugo katika maabara kuu ya mifugo – Temeke na taasisi ya utafiti wa Ndorobo na Malale (*tsetse* na *Trypanosomosis Research Institute – TTRI*), Tanga yakiwemo Homa ya Mafua Makali ya Ndege na Homa ya Bonde la Ufa.

Aidha, sampuli za ndege 3,438 zilifanyiwa uchunguzi katika maabara hiyo kwa kushirikiana na *OVI* – Afrika kusini na Chuo Kikuu cha Minesota Marekani na kudhihirisha kuwa ugonjwa wa Homa ya Mafua Makali ya Ndege haujaingia nchini.

(viii) Utafiti wa ng'ombe wa maziwa kwa ajili ya kuongeza kiwango cha kuzaa (*calving rate*) na kupunguza muda wa mzao (*calving interval*) unaendelea katika vituo vya utafiti wa mifugo vya Tanga, Uyole na Mpwapwa ambapo matokeo ya awali katika kundi la ng'ombe wa maziwa nchini yanaonyesha kuwa kiwango cha mzao umeongezeka kutoka miezi 24 hadi 30.

(ix) Utafiti unaolenga kuboresha ufugaji wa asili wa mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku umefanyika katika Wilaya mbalimbali za mikoa ya Tanga, Dodoma, Mbeya, Pwani, Mtwara n.k. Matokeo yameonyesha kuongezeka kwa uzalishaji na kupungua kwa vifo vya mifugo hiyo.

(x) Kutayarisha muongozo na utoaji wa huduma za ugani na kusambazwa kwa wadau wote ili kupata maoni yao. Lengo la muongozo huo ni kusaidia kuratibu utoaji wa huduma za ugani katika Halmashauri na sekta binafsi.

(xi) Kuendelea na elimu kwa Umma kwa njia ya mashamba darasa kuhusu ufugaji wa ng'ombe, mbuzi wa nyama na kuku; kutayarisha vijitabu, vipeperushi na mabango

kuhusu uzalishaji bora wa mifugo, usindikaji, malisho, masoko n.k. na kusambaza kwa wadau.

(xii) Kuendelea na ukarabati na ujenzi wa majosho kupitia mipango ya maendeleo ya Wilaya (*DADPs*) na wadau wengine. Jumla ya shilingi 314,749,000.00 zimetumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna changamoto, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu, Kamati pia ilibaini changamoto kadhaa zinazoikabili Wizara ya Maendeleo ya Mifugo katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Uhaba wa fedha za ndani unaoikabili Wizara, umesababisha baadhi ya miradi ya maendeleo kutotekelezwa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei 2007 kati ya Shs.8,214,662,000.00/= za fedha za nje, ni Shs.1,151,993,225.00/= sawa na asilimia 14 tu zilikuwa zimepatikana.

(ii) Gharama kubwa za pembejeo za mifugo ambazo ni pamoja na dawa za kuogeshea mifugo. Hali hii imesababisha wafugaji wengi kushindwa kumudu gharama hizo na hivyo kusababisha uzalishaji uwe na tija ndogo.

(iii) Wafugaji wengi kuwa na mifugo ya asili ambayo ina kosaafu ndogo na hivyo kutokuwa na tija kubwa na kushindwa kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa.

(iv) Kutokuwepo kwa Taasisi za mikopo zinazokopesha wafugaji na masharti magumu yanayowekwa na vyombo vya fedha vilivyopo, hivyo kusababisha wafugaji kukosa fursa ya kukopa.

(v) Biashara ya mifugo imeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ambao umesababisha vifo vingi vya mifugo. Aidha, kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo na tishio la ugonjwa wa mafua makali ya ndege vimeathiri kwa kiasi kikubwa biashara ya mifugo nchini.

(vi) Mchango wa mifugo katika pato la Taifa haukuwa wa kuridhisha sana kutokana na uhaba wa viwanda vya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mifugo na ukosefu wa masoko na uduni wa miundombinu.

(vii) Kutokamilisha zoezi la kutenga maeneo maalumu ya wafugaji kumesababisha wafugaji kuhamahama na hivyo kuleta uharibifu wa mazingira, kusambaza magonjwa ya mifugo na kusababisha migogoro baina yao na wakulima.

(viii) Mpango wa kuwahamisha wafugaji kutoka katika bonde la Ihefu ilikuwa ni nia njema ya Serikali. Hata hivyo Serikali haikuweza kukalimilisha zoezi la kuboresha miundombinu kama majosho, mabwawa na huduma za jamii katika sehemu ambazo wafugaji walikuwa wamehamishiwa.

(ix) Tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo ya asili kama mbuzi, bata, kuku, kondoo na nyuki imefanya sekta hii ishindwe kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Mifugo inakuwa endelevu na yenye kuleta tija. Baadhi ya shughuli hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kukamilisha mkakati wa kutekeleza Sera ya Taifa ya mifugo (2006) na kuandaa Programu ya utekelezaji.

(ii) Kuendeleza huduma za afya ya mifugo kwa kuimarisha idara ya huduma za mifugo na Sekretarieti ya Baraza la Veterinari kwa kuwapatia vitendea kazi, ruzuku ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya madawa ya kuogesha mifugo na uchanjaji wa ng'ombe kuzuia ugonjwa wa homa ya mapafu.

(iii) Kukarabati na kuendeleza Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa ili kutekeleza majukumu yake. Aidha, kushiriki katika tafiti za mienendo na udhibiti wa magonjwa ya mifugo hasa yale ya mlipuko yanayosababishwa na virusi, bacteria na vimelea vingine itazingatiwa.

(iv) Kuimarisha huduma za ugani kupitia kitengo cha elimu kwa wafugaji (*FEPU*) na kusambaza Teknolojia mpya kwa wadau.

(v) Kuendeleza mifumo ya ufugaji wa asili kwa njia ya mafunzo, miongozo, sheria n.k kwa wafugaji husika kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

(vi) Kutekeleza mikakati na mipango ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (*CBPP*), Homa ya Bonde la Ufa (*RVF*), na kukamilisha maandalizi ya mikakati ya kudhibiti magonjwa ya Miguu na Midomo (*FMD*), kichaa cha Mbwa, mapele ya ngozi kwa ng'ombe (*LSD*) na Mdondo (*NCD*).

(vii) Kuimarisha Idara ya Mifugo kwa kuipatia vitendea kazi pamoja na kuendelea kuiwezesha Bodi ya Maziwa na kuanzisha Bodi ya Nyama ili ziweze kusimamia eneo hilo ipasavyo.

(viii) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuziba mianya ya rushwa katika sekta ya Mifugo kwa kuzingatia mkakati wa Taifa wa kupambana na Rushwa (*National Ant-Corruption Strategic Plan –NACSP*).

(ix) Kutoa taarifa ya hesabu za mapato na matumizi ya Wizara kwa Kamati ya Fedha za Umma na kuwapatia wahasibu Mafunzo ya uhasibu na matumizi ya kompyuta katika kutekeleza majukumu yao.

(x) Kuendelea kutoa elimu kwa watumishi kupima UKIMWI na kuhamasisha kupima UKIMWI kwa hiari ili kujua afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008, baada ya kueleza kwa kifupi mafanikio na changamoto zinazoikabili Wizara katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka uliopita 2006/2007 na matarajio ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2007/2008, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Rais – Mazingira iendelee na zoezi la kutenga maeneo ya wafugaji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya vijiji Na.5 ya mwaka 1999. Hii itasaidia kuepusha migogoro baina ya wafugaji na wakulima katika maeneo mbalimbali hapa nchini na hivyo kuleta tija katika ufugaji. Utaratibu huu utasaidia wafugaji waweze kuwa na hatimiliki na hivyo kuwa na dhamana ya kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.

(ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi kubwa katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali ya mifugo. Pamoja na juhudi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi na utekelezaji kwa kuihusisha TAMISEMI ili kuleta ufanisi zaidi. Aidha, jitihada za ukarabati wa majosho yaliyopo, uende sambamba na ujenzi wa majosho mapya. *(Makofi)*

Pia Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kukabiliana na tatizo la mlipuko wa ugonjwa wa Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever*) kuanzia mwezi Februari 2007 katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za makusudi ili kuboresha maabara kuu ya mifugo kwa kuipatia vifaa vya kisasa kwa ajili ya utambuzi wa magonjwa na kuwapatia watumishi mafunzo ya kukabiliana na magonjwa hayo ya mlipuko.

(iii) Kamati pia inaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuwapatia wafugaji mafunzo juu ya ufugaji bora, usindikaji wa mazao ya mifugo, malisho bora na udhibiti wa magonjwa ya mifugo.

Aidha Kamati inaishauri Serikali kuongeza mafunzo ya ugani ili kuboresha hali ya mifugo kupitia njia mbalimbali kama vipindi vya redio, elimu mashuleni na wataalamu kuwatembelea wafugaji katika makazi yao vijijini. Pia Serikali iwafadhili wanafunzi zaidi katika vyuo vya Mafunzo ya Mifugo, ili kupata wataalamu wengi zaidi katika sekta ya Mifugo nchini.

(iv) Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuhakikisha kwamba wafugaji wanapata maeneo mazuri ya malisho. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ihamasishe watu binafsi na makampuni kuwekeza katika malisho ya mifugo. Msisitizo uwekwe katika uanzishwaji wa mashamba makubwa ya malisho ya mifugo katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

(v) Serikali ichukue hatua za makusudi kutenganisha majukumu ya Bwana Shamba na Bwana Mifugo ili kuleta ufanisi na uwajibikaji kwa mujibu wa fani na masharti ya

kazi zao. Aidha, Serikali ifanye juhudi ili kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta ya mifugo kwenye Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

(vi) Serikali iendelee kufuatilia na kusimamia kwa karibu zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka eneo la Ihefu na kuhakikisha huduma zote muhimu zinatolewa katika maeneo mapya waliyohamia.

(vii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, juu ya umuhimu wa kula nyama na kunywa maziwa kwa ajili ya afya zao, na kuhamasisha wananchi kuongeza kiwango cha matumizi ya mazao hayo yatokanayo na mifugo. Kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*), kiwango kinachopendekezwa ni lita 200 za maziwa na kilo 50 – 60 za nyama kwa mtu 1 kwa mwaka. Kwa Tanzania inakadiriwa kuwa mtu 1 anakunywa lita 39 za maziwa na kilo 10.3 za nyama kwa mwaka kiwango amabacho ni cha chini sana. *(Makofi)*

(viii) Serikali ihamasishe ujenzi wa machinjio ya kisasa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika Mikoa yenye mifugo mingi. Aidha, Serikali isimamie ipasavyo ubora wa mabucha ya nyama kote nchini ili kulinda afya za walaji.

(ix) Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wafugaji ili waweze kutumia mifugo yao kuboresha maisha na kuchangia katika pato la Taifa (wingi wa mifugo waliyonayo uende sambamba na ubora wa maisha ya wafugaji na mifugo yenyewe).

(x) Tunaipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku za madawa ya mifugo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya na kuboresha utaratibu mzima wa kusambaza ruzuku za madawa ili ziweze kuwafikia walengwa kama ilivyokusudiwa.

(xi) Kutokana na kasi ya maambukizi ya UKIMWI katika jamii ya Watanzania hususan wafugaji, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu juu athari za UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2007/2008, kama nilivyokwisha eleza hapo awali, Kamati ilipata nafasi ya kupokea na kuchambua Bajeti ya Wizara. Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo alieleza kwa kina mpango wa Wizara wa kuwa na sekta ya mifugo inayokua kulingana na viwango vya Kimataifa ambayo ni endelevu kiuchumi, kijamii na kimazingira. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia kukua kwa ufugaji wa kisasa, uzalishaji wa mazao ya mifugo na utoaji wa huduma bora kwa kushirikiana na wadau wa sekta ili kuwa na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata maelezo hayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, na baada ya kupata majibu ya hoja mbalimbali za wajumbe wa Kamati, pia kupokea maoni na ushauri, Kamati iliridhika na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Kamati inaliomba Bunge lako tukufu lijadili na kukubali kupitisha Bajeti ya fungu 99 - Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kama ifuatavyo:- Shilingi bilioni ishirini na mbili, milioni mia tatu tisini na saba, mia tano kumi na sita elfu (22,397,516,000/=). Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia sita ishirini na moja na mia tano kumi na sita elfu (12,621,516,000/=) ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni tisa na mia saba sabini na sita elfu (9,776,000,000/=) ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, baada ya kusema hayo napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ambao maoni, ushauri na mapendekezo yao katika Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo yamewezesha taarifa hii kuwasilishwa mbele ya Bunge hili Tukufu. Wabunge hao ni Mheshimiwa Gideon A. Cheyo Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Kidawa Saleh ambaye ni Makamu Mwenyekiti. Aidha Wajumbe wa Kamati ni Mheshimiwa Maida H. Abdallah, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Mwadin A. Jecha, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama Mheshimiwa Joyce M. Machimu, Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omar, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mheshimiwa Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo Mheshimiwa Antony Diallo, Mbunge na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mbunge kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Kamati. Nawapongeza pia Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Jonas N. Melewas pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii pamoja na Ofisi yako hasa katibu wa Bunge Ndugu Damian S.L. Foka na wasaidizi wake kwa ushirikiano wao mzuri wanaoutoa kwa Kamati na Katibu wa Kamati hii Ndugu Frank K. Mbumi kwa kuratibu shughuli za Kamati hii ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, na kwa niaba ya Kamati napenda kutamka kuwa naunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika awali ya yote nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye kupasa kushukuriwa ambaye ni Rahimu, Mwenye nguvu mwenye ukarimu na Mwingi wa hekima Ambaye ametupa uhai

na afya njema siku ya leo tukaweza kukutana kutekeleza wajibu wetu tuliokabidhiwa na wananchi kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika nikushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b) na (c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuchukuwa nafasi hii kukishukuru chama changu cha *CUF* kwa kuniteuwa na hatimae kuchaguliwa kuwa Mbunge. Aidha napenda kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Wete kwa kuendelea kuniunga mkono kutekeleza yale waliyonituma. Nawaahidi kwa uwezo atakaonipa Mwenyezi Mungu nitawatumikia vyema na kwa juhudi zangu zote, na sitowaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa yanayonipelekea kuifanya kazi zangu kwa wepesi na kwa ufanisi zaidi. Bila ya kuwasahau wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwa uswahiba na urafiki tulionao unaonifanya kujiona ni miongoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukuwa fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza, kutuelekeza na kutusimamia vyema katika shughuli zetu za kila siku. Ufanisi mkubwa unaoonekana katika Kambi yetu ni kutokana na Uongozi wao mahiri. Napenda kuwapa pole familia ya hayati Amina Chifupa na kadhalika Bunge lako kwa kuondokewa na Mpendwa wetu. Mungu ampe malazi mema. Amina.

Kuhusu hali halisi ya mifugo nchini, takriban asilimia 99% ya mifugo hapa nchini inamilikiwa na kutunzwa kienyeji. Kwa bahati mbaya mifugo yetu ya asili uzalishaji wao ni mdogo. Mathalan, kiwango cha kuzaa *(calving rate)* ni chini ya asilimia 40%; muda wa mzao *(calving interval)* ni miezi 18 – 24, na hivyo kuzaa ndama 4 – 5 katika uhai wao. Vifo vya ndama ni zaidi ya asilimia 25%. Aidha uzalishaji wa maziwa uko chini ya lita 500 kwa mwaka. Matokeo ya haya yote yamesababisha ukuaji wa *National herd* kubaki katika kiwango cha asilimia 0.02%.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 1% iliyosalia ni mifugo inayofugwa katika mashamba makubwa kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na maziwa. Kiwango cha kuzaa kwa ng'ombe hawa ni asilimia 80%, muda wa mzao ni miezi 10 na huzaa ndama 9 katika uhai wao. Aidha matokeo ya vifo ni chini ya asilimia 10%. Pamoja na rasilimali kubwa ya mifugo tuliyonayo, takriban zaidi ya asilimia 63% ya wafugaji wetu bado ni masikini. Hii ni changamoto kubwa, inatupasa tukae na kutafakari nini la kufanya kuondokana na hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/07 ukuaji wa Sekta ya Mifugo ulishuka kwa asilimia 1.2, kutoka 5.2% hadi kufikia 4.0%. Kushuka huku kwa

asilimia 1.2 si jambo dogo, athari zake katika Sekta kuu ya Kilimo na uchumi wa nchi kwa ujumla ni kubwa.Matatizo yanayoikabili sekta ya mifugo nchini, Sekta ya Mifugo imekabiliwa na matatizo mengi yanayokwaza maendeleo yake. Miongoni mwa matatizo hayo ni pamoja na tatizo la kuyafikia masoko na kukosekana taarifa za masoko *(limited access to market outlets and market information)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida wafugaji nchini mwetu huwa hawazalishi kwa sababu ya kibiashara. Mara nyingi huzalisha kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, hutafuta soko pale tu wanapokuwa na ziada. Wanapokosa kuuza hiyo ziada huwa ni sababu ya kupunguza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa muda mrefu haijawekeza ipasavyo katika kukuza masoko, kadhalika upatikanaji wa taarifa za masoko ya mifugo na mazao yake. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa juhudi ya kuongeza uzalishaji. Ipo haja basi kwa Serikali kuongeza juhudi za makusudi kuwashajiisha wafugaji kuzalisha zaidi ili kuuza katika masoko. Juhudi hizo zinaweza kuzaa matunda iwapo tu utunzaji wa mifugo, kukuza masoko, upatikanaji wa taarifa za masoko na usindikaji wa mazao ya mifugo utaendelezwa. Kwa mfano, soko la maziwa na mazao yatokanayo na maziwa linaweza kuongezeka iwapo vitaanzishwa vikundi vya wafugaji, pamoja na kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kusindika maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano na uchukuzi, hali ya mawasiliano na uchukuzi hapa nchini bado haijakuwa ya kuridhisha sana. Sehemu nyingi hazifikiki hasa nyakati za mvua kutokana na ubovu au ukosefu wa barabara. Hali hii inaathiri juhudi katika kuendeleza ufugaji hasa vijijini, matokeo yake ni kudumaa uchumi katika kaya, na kwa hivyo basi, mawasiliano na uchukuzi ni sekta muhimu sana katika kuendeleza ufugaji na kukuza uchumi, kutokana na kuamsha ari ya uzalishaji na kufungua masoko ya mazao hayo.

Kuhusu usindikaji wa mazao ya mifugo, usindikaji wa mazao ya mifugo hasa maziwa na nyama unaongeza thamani ya mazao hayo na hivyo mahitaji kwa mlaji huongezeka na hatimae kupanuka uzalishaji. Kwa bahati mbaya hapa nchini viwanda vingi vya kusindika maziwa vilivyokuwa vinaendeshwa na Serikali vimekufa. Hali hii ilitokana na utaratibu mbaya ulokuwepo kwamba Serikali ndiyo pekee iliyokuwa inasimamia na kuendesha viwanda vya maziwa nchini. Kwa upande mwengine viwanda vya kusindika nyama navyo ni vichache, hali inayopelekea kukwaza biashara ya nyama na bidhaa zitokanazo na nyama nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kubinafsisha machinjio ya Dodoma na kiwanda cha kusindika nyama cha Shinyanga ni hatua muhimu katika kukuza biashara ya nyama na bidhaa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukuwa nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua hii. Aidha niishauri Serikali kwamba ichukuwe hatua za makusudi na kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhamasisha ujenzi wa machinjio ya kisasa katika

Halmashauri zao. Hatua hii itapoenda sambamba na kusimamia ipasavyo mabucha kote nchini sio tu kutaongeza thamani ya nyama bali pia kulinda afya ya mlaji.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, nilisema kwamba kwa muda mrefu sasa tumekuwa na tatizo la kwamba tafiti nyingi zinazofanywa kuhusu mifugo hazijaelekezwa ipasavyo kutatua matatizo ya mfugaji. Aidha , ugani nao kutokana na udhaifu wake umeshindwa kubadilisha hali ya ufugaji nchini na badala yake wafugaji wanaendelea kufuga kwa mtindo ule ule wa kale jambo ambalo linadumaza uzalishaji. Aidha , uhusiano baina ya Utafiti na Ugani bado umeendelea kuwa mdogo mno kiasi ambacho matokeo ya tafiti zinazolenga kukwamua matatizo ya mfugaji hayawafikii walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu ya *ASDP,* Serikali kwa mwaka huu imepanga kuajiri maafisa ugani 2500 ili kuziba pengo la uchache wa wagani hao katika Halmashauri mbalimbali. Aidha, inapasa tuzingatie kwamba kuongeza idadi ya wagani ni lazima kuendane sambamba na: (i)kuoanisha na kuimarisha mahusiano baina ya Utafiti, Mafunzo, Ugani na Mfugaji; (ii)kuimarisha miundombinu, ikiwemo nyumba za kuishi, usafiri na vifaa mbalimbali kwa ajili ya shughuli za ugani; (iii) kuwaimarisha kielimu watafiti, wakufunzi wa Vyuo vya Mifugo, wagani na Wafugaji wenyewe; (iv)kutenganisha shughuli za ugani baina ya mabwanashamba na mabwanamifugo ili kuleta ufanisi na uwajibikaji kwa mujibu wa fani zao; (v)kuviimarisha vyuo vya mifugo nchini, kwa kuvipatia nyenzo na wataalam wa kutosha; (vi)kuviimarisha Vituo vya Utafiti nchini kwa kuvipatia nyenzo na wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upatikanaji wa maji na malisho limekuwa kwa kiasi kikubwa linaathiri mwenendo mzima wa ufugaji hapa nchini. Kutokana na hali hii wafugaji wanalazimika kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kufuata maji na malisho pale yanapopatikana. Kadhalika sehemu kubwa ya nyanda zilizokuwa zinatumika kwa kuchungia mifugo zimekuwa zinavamiwa na kutumika kwa matumizi mengine kama hifadhi za wanyama pori, machimbo ya madini na kadhalika. Katika hali kama hii wafugaji hulazimika kuhama kutafuta maeneo mengine ya kulisha mifugo yao. Kutokana na kuhamahama huko kwa wafugaji, na kwa sababu hakuna utaratibu maalumu ulioandaliwa katika uhamaji huo ndiko wakati mwingine kunakopelekea mazingira kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba njia mahususi ya kupunguza ufugaji wa kuhamahama ni kuongeza maeneo yanayotumika kwa malisho; Wafugaji wapatiwe ardhi ya kutosha na kupewa hati ya kumiliki maeneo hayo; kujenga mabwawa na malambo yanayoweza kuhifadhi kiasi kikubwa cha maji. Aidha, majosho ya kutosha yajengwe na yale yaliyoharibika yafanyiwe ukarabati wa kutosha.

Kadhalika utaratibu wa kufuga kwa pamoja mifugo ya kawaida, wanyama pori na utalii (*livestock, wildlife and tourism integrations*) katika eneo moja unasaidia kuongeza kipato kwa jamii. Miradi hii imebuniwa na kufadhiliwa na Shirika la *African Wildlife Foundation (AWF).*

Mradi huu umeanzishwa Kenya na umeleta faida kubwa. Hapa Tanzania mradi huu umeanza katika shamba la ng'ombe la Manyara *(Manyara Ranch)*. Wananchi wa maeneo hayo wameanza kufaidika na mradi huo, ukiwemo ujenzi wa shule ya msingi bweni, kukuza shughuli za utalii, kusaidia miradi ya kijamii, tiba ya mifugo, hifadhi ya ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika nichukue nafasi hii kulipongeza shirika hili la *AWF* hapa Tanzania, na hasa Mkurugenzi wake Dr. Kahurananga pamoja na wafanyakazi wote kwa juhudi kubwa wanazochukuwa kuhakikisha kuwa nchi yetu nayo inafaidika kwa kiasi kikubwa na mpango huu muhimu. Aidha, niiombe Serikali nayo itoe mashirikiano makubwa kwa shirika hili ili mradi huu uweze kuenea sehemu nyingi za nchi yetu likiwemo shamba la ng'ombe la *West* Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, wafugaji katika Bonde la Ihefu inasemekana wamekuwepo kwa zaidi ya miaka 35 iliyopita. Hifadhi ya Ihefu ilitangazwa mnamo mwaka 1998, kiasi cha miaka 9 sasa. Tangazo hilo ndilo lilipelekea kuanza kwa mchakato wa kuwahamisha wafugaji kwa kile kinachodaiwa kuwa wafugaji hao wanasababisha uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali za kisayansi ukiwemo ule wa Machibya na Mduma 2005 zimeonyesha kuwa kilimo cha umwagiliaji pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa ndivyo vilivyohusishwa na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo. Kwa ujumla mifugo katika bonde hilo imekuwa ikipungua kutoka 513,600 mwaka 1984 na kufikia 366,000 mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Aprili 2006 baadhi ya vyombo vya habari vilitoa taarifa ya kuwepo Ihefu mifugo milioni 1.8, hiki pia kilikuwa ni miongoni mwa vigezo vilivyotumika kuwahamisha wafugaji kutoka katika Bonde la Ihefu.

Kambi ya Upinzani ina wasiwasi iwapo palithibitishwa kuwepo idadi hii ya mifugo. Kwa kifupi tu ni kwamba zoezi la kuhamisha wafugaji kutoka Ihefu lilianza mwezi Septemba, 2006 ambapo kiasi cha ng,ombe 235,000 walitakiwa kuondoka na kuhamia wilaya za Chunya, Kisarawe, Rufiji, Lindi Kilwa na Nachingwea. Zoezi hili lilikuwa ni Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina pingamizi juu ya Mkakati huu, na tunaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ili kunusuru mazingira ya Bonde la Ihefu. Isipokuwa hoja yetu kubwa tunaielekeza katika hatua za utekelezaji wa zoezi lenyewe.

Kambi yetu ina taarifa kwamba zoezi zima lilikumbwa na mapungufu mengi. Ni dhahiri kwamba yapo matatizo kadhaa yaliwakuta wafugaji hawa katika mchakato mzima wa kuhamishwa kwao:

(i) Muda wa awali ambao Serikali ilitoa kwa wafugaji kuhama ulikuwa Oktoba, 2006 hadi Mei, 2007. Lakini kabla ya wakati huo kuanza wafugaji walianza kuhamishwa kwa nguvu. Tamko la kuhamishwa kwa nguvu lilitolewa mwezi Machi, 2006.

(ii)Kuhamishwa wafugaji hao kuliambatana na ahadi ya kupatiwa maeneo katika wilaya zilizoteuliwa, maeneo ambayo yangekuwa na miundombinu muhimu kama vile majosho, malambo na malisho ya kutosha.

Bahati mbaya miundombinu waliyoahidiwa haikuwepo, jambo ambalo linonyesha kulikuwa na habari za kupotosha juu ya kuwepo kwa miundombinu hiyo. Hali hii iliwaathiri sana wafugaji kulikopelekea kupoteza mifugo mingi kutokana na machofu na maradhi.

(iii)Wafugaji walitozwa faini ya shilingi elfu kumi kila mfugo kwa kisingizio cha kuharibu mazingira. Utitiri huu wa faini umetunisha mfuko wa Serikali kwa zaidi ya shilingi milioni 800.

(iv)Kulikuwepo na uporaji mkubwa wa mali za wafugaji. Katika vijiji ambavyo wafugaji walipangiwa kuhamia, Serikali za Vijiji ziliwatoza wafugaji hao gharama za kuhamia kati ya shilingi 25,000/= na 300,000/= kabla ya kupangiwa maeneo watayokaa na wao na mifugo yao.

(v) Kutokuwepo kwa huduma za mifugo wakati wa kusafirisha na pale wanapofikia.

(vi) Katika utekelezaji wa zoezi hili kumesababisha kusambaratika kwa familia za wafugaji, baba anahama na mifugo lakini mama na watoto wanabaki nyuma. Hii inathibitisha ile dhana ya kwamba hapakuwa na maandalizi ya kutosha.

(vii)Kutokana na kusambaratika kwa familia, kumeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa elimu na huduma nyingine za kijamii kwa watoto wa wafugaji hao.

(viii)Maandalizi na upimaji wa ardhi katika vijiji kwa ajili ya kupokea wafugaji hao haukuwa umepiga hatua, ni vijiji vichache sana ndivyo ambavyo zoezi la upimaji kwa ajili ya matumizi ya ardhi ulifanyika.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa kubainika kwa mapungufu haya ulifanywa na Mashirika yasiyo ya kiserikali ya *PINGOs Forum*, Haki Ardhi na Kituo cha Sheria na Haki za Binadam.

Utafiti huu ulibaini ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika zoezi zima la kuhamisha wafugaji kutoka Ihefu kwenda wilaya za Lindi na Kilwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo hayo yaliyojitokeza, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua zifuatazo:

(i)Serikali ifanye tathmini ya upotevu wa mali za wafugaji waliohamishwa kutoka Mbarali kwenda mikoa ya Kusini, na kufidia hasara walizozipata wafugaji hao;

(ii)Wafugaji warudishiwe fedha walizotozwa kama faini ya uharibifu wa mazingira, kwa kuwa kwamba uharibifu huo haukufanywa na wafugaji pekee;

(iii)Serikali ianzishe mjadala wa Kitaifa utakaowashirikisha wafugaji na wadau wengine kujadili juu ya mustakbali wa ufugaji wa asili Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais baada ya kusikia kilio cha wafugaji na wananchi kwa jumla ameunda Tume ya Jaji Chande kuchunguza juu ya kudhia hii. Na kwa kuwa Tume hii imemaliza kazi na kuwasilisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuyaweka bayana kwa wananchi matokeo ya uchunguzi huo.

Aidha, mapendekezo ya Tume yachukuliwe hatua mapema iwezekanavyo ili kuondoa ile dhana ya muda mrefu ya kuwa mapendekezo ya Tume zilizoundwa awali mara nyingi huwa hakuna utekelezaji wowote unaofanywa, au utekelezaji wake huwa ni wa kusuasua na hivyo kuwakatisha tamaa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukosefu (*Genetic Makeup*), awali katika hotuba yangu nimeeleza jinsi mifugo yetu ilivyo na ukosaafu duni katika sifa za uzalishaji. Juhudi zimekuwa zinafanyika kuboresha kiwango cha ukosefu huo ili kukuza viwango vya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa njia pekee inayotumika hapa Tanzania kuboresha ukosefu wa ng’ombe wetu wa kienyeji ni kupandisha kwa kutumia madume bora au mbegu za kigeni. Lakini ni lazima tukiri kwamba njia hii pamoja na kwamba ni rahisi kulinganisha na nyingine inachukua muda mrefu sana kufikia malengo. Aidha, huduma hii haiwafikii wafugaji wengi kutokana na matatizo ya usafiri, zana na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri katika randama yake aliyowasilisha kwenye Kamati ya Kilimo na Ardhi jijini Dar es Salaam, ambako aliiambia Kamati kwamba Wizara yake ina mpango wa kuanzisha matumizi ya Teknolojia ya viini tete (*Multiple Ovulation Embryo Transfer - MOET).* Hii ni njia moja nyepesi na ya haraka katika kuongeza idadi ya ng’ombe wenye ubora wa uzalishaji. Kwa kuwa teknolojia hii ni ghali na inahitaji vifaa na utaalamu wa hali ya juu, Serikali inatueleza nini kuhusu maandalizi ya awali yanayopelekea kutumika kwa teknolojia hii hapa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, mifugo yetu inakabiliwa na maradhi mbalimbali ambayo husababisha vifo na kupungua kwa uzalishaji. Maradhi kama homa ya mapafu *(CBPP)*, Ndigana kali *(ECF)*, Ndigana baridi *(Anaplasmosis)*, Maji moyo *(Heart water)*, Mkojo mwekundu *(Babesiosis)*, Nagana *(Trypanosomiasis)*, miguu na midomo *(FMD)*, homa ya

nguruwe *(African Swine Fever)* na kadhalika yamekuwa ni kikwazo katika kukuza uzalishaji wa mifugo katika mikoa mingi nchini.

Kadhalika yapo maradhi ambayo yanaambukiza binadamu yakiwemo pia Kimeta *(Anthrax)*, Kichaa cha mbwa *(Rabies)*, Ugonjwa wa kutupa mimba *(Brucellosis)* na Kifua kikuu cha ng'ombe *(Bovine tuberculosis).*

Serikali imekuwa ikichukua juhudi kukabiliana na maradhi hayo. Njia mbalimbali zimekuwa zikitumika zikiwemo kudunga chanjo, kudhibiti mbung'o, kutoa ruzuku kwa madawa ya kukogesha mifugo, kudhibiti mienendo ya mifugo kutoka sehemu moja kwenda nyengine na kadhalika. Kutokana na juhudi hizo maradhi mengi yameweza kudhibitiwa. Na kwa hivyo, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa juhudi yake hiyo.

Mheshimiwa Spika inatupasa sasa tujiulize, hivi ni kwa nini miaka mingi tumekuwa tukijitahidi na kutumia fedha nyingi kudhibiti magonjwa ya mifugo bila ya mafanikio ya kutosha. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa Serikali katika kukabiliana na changamoto hii, tunaona ipo haja sasa kwa Serikali kuchukua hatua zifuatazo:

1. Wadau wanaoagiza madawa ya mifugo kutoka nje wasamehewe ushuru kuwezesha madawa hayo kuingia kwa wingi nchini na hatimaye bei itashuka ili wafugaji wamudu kuyanunua. Ushuru huu unaweza kujirudia *(recovered)* kwenye masoko wanayouza bidhaa za mifugo.

2. Serikali ihakikishe kwamba madawa yanayoagizwa na kuingizwa nchini yana ubora unaostahiki. Aidha, maduka yanayouza madawa yawe yanakaguliwa mara kwa mara kuhakikisha hakuna madawa yanayouzwa ambayo yamepitwa na wakati au yenye viwango duni.

3. Ruzuku kwa madawa hasa ya kukogeshea na chanjo muhimu za kudhibiti magonjwa ya mlipuko itolewe ya kutosha na kuhakikisha madawa na chanzo vinawafikia wafugaji tena kwa wakati.

4. Maabara Kuu ya Mifugo *(CVL)*, ikarabatiwe, iimarishwe kufikia kiwango cha kimataifa na kupatiwa vifaa na vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa ili iweze kufanya kazi katika ufanisi wa hali ya juu. Aidha, maabara nyingine za utafiti/uchunguzi wa maradhi ya mifugo ziimarishwe ikiwa ni pamoja na miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, katika mwezi wa Februari nchi yetu ilikumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa *(Rift Valley Fever)* . Ugonjwa huu ulizikumba wilaya za Monduli (Arusha) na Ngorongoro mkoani Manyara. Aidha, iliripotiwa kuwa hadi kufikia tarehe 20 Mei, 2007 ugonjwa huo ulisambaa takriban katika vijiji 72, katika wilaya 29 za mikoa 9 ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kupambana na maradhi haya zikiwemo, kudhibiti mienendo ya mifugo kutoka sehemu moja kwenda nyingine,

kupiga marufuku ulaji wa nyama hasa zile sehemu zilizoathirika na kununua chanjo na kuzisambaza katika wilaya 33 na mashamba ya serikali na ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Ingawa upatikanaji wa chanjo ulichelewa sana, hali iliyosababisha ugonjwa huu kuenea kwa kasi, hatuna budi kuipongeza serikali kwa hatua madhubuti ilizochukua kukabiliana nao.

Kambi ya Upinzani hata hivyo, inaitaka Serikali kuwa makini na kufanya tafiti za kutosha ili kujua mienendo halisi ya maradhi ya milipuko ambayo huwa inajirejea kila baada ya muda fulani, ili hatua za tahadhari zichukuliwe mapema iwezekanavyo kabla athari yake haijawa kubwa.

Athari za mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa zilikuwa kubwa kwa binadamu na mifugo. Kwa mujibu wa takwimu tulizonazo homa hii imesababisha vifo vya watu 134 nchini kote tangu ulipoibuka miezi sita iliyopita.

Mheshimiwa Spika, idadi ya mifugo iliyokufa kutokana na ugonjwa huo ilifikia 50,000 na inakisiwa mifugo 46,000 imetupiwa mamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza rasmi kwamba kuanzia sasa watu wanaweza kula nyama kwa kuwa ni salama. Ni matumaini yetu kwamba Serikali imefanya utafiti wa kina na kujiridhisha kuwa kwa sasa ugonjwa huo umetoweka. Vinginevyo, ama kinyume cha hayo tutakuwa tunahatarisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, awali katika hotuba yangu nilisema kwamba katika mwaka wa fedha 2006/07 ukuaji wa sekta ya Mifugo ulishuka kwa 1.2%. Kwa mujibu wa kitabu kinachoelezea Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2006, Serikali inaeleza kuwa sababu kuu ya kuporomoka kwa ukuaji wa sekta ya Mifugo nchini ni kuwa sekta hii imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukame ambao ulisababisha upungufu mkubwa wa malisho na vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba katika hotuba yangu ya mwaka jana (2006/07) nilibainisha wazi kwamba idadi ya mabwawa na malambo yaliyopo nchini hayatoshelezi uhifadhi wa maji ya kutosha katika kupunguza makali ya ukame na kuepukana na uchungaji wa kuhamahama. Nikasisitiza umuhimu wa ujenzi wa mabwawa na malambo makubwa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya mifugo. Shauri hili lingetekelezwa kikamilifu athari ya ukame isingelikuwa kubwa kiasi hichi.

Mheshimiwa Spika, mnyama kama ilivyo kwa binadamu, anahitaji chakula kilicho bora na maji safi na salama. Ni makosa makubwa kudhania kwamba wanyama wanaweza kuishi vizuri na kuzalisha katika viwango vilivyo bora kwa kuokota okota malisho na kukosa maji yaliyo bora na salama.

Mheshimiwa Spika, malisho ya mifugo kwenye nyanda na mbuga yanategemea sana mvua na hali ya hewa iliyopo na hivyo uzalishaji unaathirika kulingana na hali ya

hewa. Kipindi kilichopita tumeona jinsi gani ukosefu wa mvua ulivyoathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo.

Kama ulivyo uzalishaji wa mazao ya chakula kwa binadamu, kuna baadhi ya maeneo yalikuwa na uhaba mkubwa wa chakula na maeneo mengine yalikuwa na ziada. Wafugaji walichukua hatua ya kuhamisha mifugo yao na kuipeleka sehemu zenye malisho na maji. Kitendo hiki kimelaumiwa sana na baadhi ya watu na hasa wakulima wa mazao na wanamazingira.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya kuchangia hoja ya Waziri mwaka jana Kambi ya Upinzani ilitoa hoja kuitaka Serikali kuchukua juhudi maalumu kuhakikisha kwamba sensa ya mifugo *(complete enumeration)* inafanywa haraka iezekanavyo.

Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja hiyo aliliambia Bunge lako tukufu kwamba Serikali inafanya juhudi kuwasiliana na Wahisani ili kupata fedha za kufanya sensa kwa kuzingatia kuwa gharama zinazohitajika ni kubwa sana. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze ni hatua gani Wizara imefikia katika upatikanaji wa fedha hizo ili sensa ya Mifugo ifanyike haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekusudia kuendesha mafunzo mbalimbali kwa watafiti, wagani, wafugaji na wadau wengine. Miongoni mwa mafunzo hayo nị:Uchinjaji na ukataji wa nyamạ;Uchunaji; Uwambaji na Ukaguzi wa ngozị;Ufugaji bora na Usindikaji wa mazao ya mifugo;Uzalishaji na matumizi bora ya malisho.

Mheshimiwa Spika mwaka jana Wizara ilitoa mafunzo kwa wachinjaji, wachunaji na wataalam 441 katika mikoa mbalimbali nchini. Kwa kuzingatia umuhimu wa zao la ngozi hapa nchini idadi hii ya wakurufunzi ni ndogo mno. Serikali inapaswa kuongeza idadi hiyo ili hatimaye ubora wa ngozi uongezeke lakini pia na kuongezeka ukusanyaji wa vipande vya ngozi.

Mheshimiwa Spika, nichukuwe nafasi hii kutoa shukurani za dhati kwa wake zangu, Bi Asha Mohammed Haji na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, watoto wetu na familia yangu kwa ujumla kwa kunipa moyo na kuniunga mkono kwa muda wote, nikifanya shughuli zangu za kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mhe. Antony Diallo, (Mb.), na Naibu Waziri Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa (Mb., kwa mashirikiano mazuri wanayonipa.

Aidha, nimpongeze Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamurunda, Naibu Katibu Mkuu , Dr. Jonas Malewas pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kusukuma mbele maendeleo ya Mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kusoma vizuri. Sasa nitawaita wafuatao kwa muda tulionao asubuhi hii tunaweza kupata takriban wachangiaji sita mpaka saba lakini kama watu wakipunguza punguza muda basi wanaweza kupatikana saba.

Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mheshimiwa George Malima Lubaleje, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini , Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na tukifanikiwa sana, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, wengine labda mchana.Tunaendelea na Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, leo ndiyo siku yako kueleza watu mambo yote.

**MHE DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninashukuru sana Waziri kwa kutoa mada nzuri na kundi lake lote la ufundi lililotayarisha ripoti hii nzuri ambayo na mimi nikiwa kama mmoja wa wajumbe wa Kamati ya ile ambayo imesomwa hapo mbele nilikuwepo na nikaipitisha na nikaiafiki.

Lakini pamoja na hayo ninataka kuzungumzia mambo machache ambayo mimi mwenyewe binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Kilwa Kaskazini wamenituma niweze kusema japokuwa hayakusemwa katika mambo ya kundi la upinzani au kundi la Kamati yetu. Kitu cha kwanza, nilipokuwa Wizara ya Maji tulikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitufundisha neno moja alisema kwamba mmejifunza nini? Swali hilo lilitokea wakati lilipoungua moto jumba letu la ofisi. Alisema mmejifunza nini? Yaani tumejifunza nini kutokana na matatizo hayo. Sasa hilo swali kwa kweli liko kwenye kichwa changu na naliuliza tena leo, tumejifunza nini kutokana na kuhamisha wanyama kutoka Ihefu kuwaleta Kilwa au Lindi au Mikoa mingine ya Kusini? Halafu kabla ya hapo ndiyo tuweze kuhamisha vitu vyetu.

Sasa vitu vilivyotekea kwenye Jimbo langu hasa la Kilwa Kaskazini, kwanza, wale tunaowaita wafugaji, sisi kwetu au wananchi wangu wanasema kwamba siyo wafugaji, wale wanaitwa wachungaji, hawafugi bali wanachunga. Halafu kitu cha pili wanapokuja kwa sababu wanaingilia Jimbo langu la Kilwa Kaskazini pale Malendego wanachukuliwa na malori au wanatembezwa kwa miguu na mimi mwenyewe japo sina macho lakini nilikuwa nawasikia wakiniambia watu kwamba hao wanapata mia tatu, mia sita au hata elfu moja, wananiambia lakini ukweli wa mambo kule utayarishwaji ulikuwa bado kabisa.

Nilimshukuru Dr. Charles Ogesa Mlingwa alikuja kwetu akaona pale Malendego josho letu lilivyokuwa limejengwa chini ya kiwango na akakemea na ninashukuru kwamba kwa sababu wakati ule mimi sikuwepo lakini kwenye *RCC* mtu mmoja aliyeongoza pale kidogo amfukuze kazi, lakini tumjalie Mwenyezi Mungu yule mtu hakufukuzwa kazi. Hata hivyo, kuna mfereji mmoja yaani mpasuko kwenye lile josho ambalo kusema kweli hawaoshi. Halafu nimemsikia Mheshimiwa Waziri Anthony Mwandu Diallo anasema kwamba tumeshajenga mabwawa katika Wilaya ya Kilwa. Mimi labda kwa sababu sioni, lakini sijaona bwawa lililojengwa na Wizara hii pale Malendego ambapo tuliahidiwa na mpaka sasa hivi kila saa ninapigiwa simu naambiwa bwawa halijajengwa hadi leo.

Kwa hiyo, naomba kama kuna mpango huo uliopo basi tafadhali muufanye haraka ili na mimi 2010 nionekane hapa, tusilete matatizo ambayo yananipata mimi kama Dr. Samson Ferdinand Mpanda ya kutokupelekwa Cuba kama alivyoagiza mwenyewe Rais wa nchi yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, na kubakia mpaka leo niko hapa nikiwa bado kipofu. Naomba sana mambo haya yafanyike haraka na wananchi wangu waishi kwa amani.

Pili, ninataka kuzungumza kwamba sisi watu wa Pwani kusema kweli ni watu wastaarabu, nizungumze ukweli. Sisi hatuna mambo ya ugomvi, sisi tunajua ugomvi uliotokea kule Kilosa watu walipigana wafugaji na wakulima lakini kwetu sisi hamjasikia hicho kitu kutokea, hii haimaanishi kwamba kwetu sisi mashamba yetu hayaliwi. Si kweli kwani mashamba yetu yanaliwa lakini kwa sababu tunaiamini Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi na Uongozi mkubwa na mzuri wa Wizara, tunajua kwamba siku moja *alhamdulilahi* Mwenyezi Mungu atatuona au Wizara itatuona na sisi tutaweza kupata majosho mazuri kama Dr. Charles Ogesa Mlingwa alivyoahidi japokuwa haijafanyika mpaka leo. Mabwawa yatajengwa na eneo la kulishia hao ambao mimi nawaita wachungaji litahifadhiwa.

Halafu jambo la mwisho, kwa kuwa mimi ni mmoja katika Kamati ile ya Mifugo na Ardhi, sitasema sana, lakini nataka kuzungumzia kuhusu mbung'o. Mbung'o kusema kweli wapo tena wa kutisha. Ukienda kwenye Kata yangu ya Miguruwe halafu unakwenda mpaka kule Zinga kuna mbuga za wanyama, yaani kuna *Selous* katika Kata ya Miguruwe. Kuna wanyamapori, kusema kweli mbung'o ndiyo tatizo letu kubwa, sijamsikia wala sijamwona mtu yeyote mtaalamu wa mbung'o kuja kuzuia wale mbung'o ili wasiweze kuwashambulia wanyama. Na sasa tunaletewa Ng'ombe! Hiyo ni hatari kubwa kwani wanaweza wakapata maafa makubwa na mimi binafsi nilikwishawahi kuzungumza kwenye *RCC* kuhusu suala hilo. Lakini waliniambia kwamba maneno haya nenda kasemee Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa naongea na wananchi wangu wa pale Maradego na sehemu zingine walisema kwamba wao watakunywa maji na ng'ombe. Sasa kwa kuwa Waziri Mkuu alikuwa Waziri wangu wakati huo na Katibu Mkuu naye alikuwepo kwenye Wizara hiyo, anajua kabisa mambo yanayotokea. Sisi tulikuwa tunaomba maji ya watu na maji ya wanyama yatenganishwe na tupewe malambo au mabwawa yanayotufaa katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugomvi kati ya wakulima na wafugaji sisi hatutaki. Hupendelei kupigana na wafugaji wanaokuja, tunataka kuwa watu wasamaria wema kama ilivyokuwa desturi yetu katika maisha, sisi ni watu wakarimu tunamkaribisha kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia tena kimoja kwamba kuondolewa kwa wale wafugaji kutoka Hefya, kutoka sehemu zingine kama Monduli, Shinyanga kuja kwetu sisi hatupingi kabisa, tunawakaribisha. Maana yake zamani mimi nilipokuwa kijana mdogo nasoma shule ya msingi nilikuwa nikimwona ng'ombe nakimbia. Lakini sasa hivi mimi namshika mkia ng'ombe, nashukuru sana. Kwa hiyo, na mimi nimejifunza vitu vingi. Lakini kama hawatatuwekea miundombinu inayofanana na ufugaji naona balaa litaanza na wananchi wangu wataanza kuleta vurugu tena tuanze tena mambo mengi ambayo hayahusiani na itikadi za wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu ndugu zangu kuna Vyama vya Upinzani vikubwa. Kimojawapo, samahani nitakitaja tu ni CUF. Wale wanaangalia kila dosari ndogo ya matatizo, wanaweza kutuangusha watu wa Chama cha Mapinduzi. Sasa msipofanya vitu hivyo haraka ndugu zangu tutakwenda na maji. Mwaka 2010 hamtaniona mimi hapa. Kwa kuwa ugonjwa wa macho ndiyo hivyo kama mnavyoniona na *Cuba* huko ndiyo ninasikia kwenye Redio tu, basi itakuwa ndiyo *Asaalam Aleikhum*! Kwa hiyo, bila kupoteza muda nasema kwamba tuweke miundombinu mizuri ili haya mambo tuliyoyazungumza hapa yafanywe kwa haraka na kwa wakati na ufanisi. Halafu na mimi *Alhamdulilahi* nitakwenda kuwaeleza wananchi wangu kwamba wawe watulivu Wizara inawaangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vinginevyo sijui itakuwa namna gani. Maana yake simu ninazopigiwa zinatisha na ninaogopa. Kwa hiyo, nitakuja kuomba kwenu. Nikija kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu sijui kama yupo, maana yake sioni kwa sababu macho ni mabovu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, yupo mwakilishi wake na Serikali yote inasikia!

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama hayupo basi salamu hizi zimfikie kwamba jamani wasipotufanyia mambo yetu yakaenda haraka kule wale wanyama watakula mahindi na wanavamia visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpanda muda wako umekwisha. Usiwe unasema hadharani kwamba una matatizo. Sasa nitamwita Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Felister Bura ,ajiandae na Mheshimiwa Salim Hemed pia ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Kwanza, ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, nina mambo machache tu ya kuzungumzia. Kwanza kabisa ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu na watalaamu wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri sana ya kuendeleza Sekta hii ya Mifugo. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekwishatembelea mara nyingi Wilaya ya Mpwapwa na wanaendelea kufanya hivyo kwa sababu wanatusaidia wanapofika pale kuweza kurekebisha mambo au kasoro zinazojitokeza au kuweza kukutana na watumishi na kuwasikiliza matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nataka nizungumzie suala la Sekta ya Mifugo, kwamba Tanzania tuna ng'ombe au tuna mifugo mingi. Tuna ng'ombe zaidi ya milioni 18 na sote tunafahamu kwamba ng'ombe ni rasilimali na ng'ombe vilevile wanachangia pato la Taifa, kilimo pamoja na sekta ya mifugo.

Lakini mifugo haiwezi kuchangia pato la Taifa kama haitaboreshwa. Ndiyo maana tuna Vituo vya Utafiti; ndiyo maana tuna wataalamu mbalimbali, lengo letu hasa ni kuwaelimisha wafugaji ili waweze kuboresha au kufuga ufugaji wa kisasa kuliko kuchunga. Maana kuna uchungaji na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa magonjwa kama alivyozungumzia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba ni lazima tuhakikishe kwamba tunadhibiti hayo magonjwa ya mifugo. Ninaishukuru sana Serikali kwa jinsi ilivyolishughulikia tatizo la ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa yaani *Rift Valley Fever*. Kwa kweli kwa Mkoa wa Dodoma lilikuwa ni tatizo kubwa na wananchi walipoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kwamba tatizo hilo limepungua, maana yake kuna wengine wanasema tatizo hilo limekwisha, ugonjwa umekwisha, kwa hiyo, watu wanakula nyama, hakuna haja tena ya kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tatizo hili limepungua, lakini bado ipo haja ya kuendelea kuwaelimisha wananchi kwamba wasile mizoga, wasile nyama ambayo haijakaguliwa na wataalamu.

Kwa sababu mimi nina hakika hata kama ugonjwa umepungua, lakini inawezekana haujaisha kabisa bado unaendelea katika maeneo fulani fulani, labda Mheshimiwa Waziri atatueleza kama kweli hakuna mgonjwa hata mmoja hadi leo. Lakini ombi langu ni kwamba wananchi waendelee kuelimishwa wasile mizoga. Tunaomba Wizara hii kwa sababu kuna vijiji vingi havina wataalamu wa kukagua nyama ipeleke wataalamu huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu ni kwamba watu wanakula nyama ambayo haijakaguliwa, ni lazima nyama ikaguliwe. Wakaguzi lazima wawe wamepata mafunzo siyo *deep attendant* anakuwa *meat inspector* haiwezekani. Kila kazi ina maadili yake, haiwezekani kabisa. Maana yake zamani ilikuwa *deep attendant* ndiyo anakagua nyama.

Sasa kuna *procedure* za *meat inspection*, haiwezekani kila mtu anakagua tu. Lazima mtu unapokagua ujue unakagua tatizo gani. Hivi kweli *deep attendant* anaweza

kujua maradhi yote ya mifugo, haiwezekani! Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kama inawezekana wataalamu wapelekwe katika vijiji vyetu ili waweze kusaidia pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu udhibiti wa magonjwa na ufugaji wa kisasa. Lakini vilevile iko haja ya kuhakikisha kwamba wananchi wanakula nyama ambayo imekaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni huduma ya mifugo na hayo magonjwa niliyosema ya kuambukiza mifugo. Kinga ni bora kuliko tiba. Kuna wadudu ambao wanaambukiza magonjwa mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kitu cha aibu kwamba ng'ombe anakufa eti kwa sababu hajaogeshwa. Maana yake kuna magonjwa yale ya kupe, sasa ukimwogesha ng'ombe au ukiwaogesha mifugo wale kupe wanakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi tuna tatizo kubwa sana la majosho karibu nchi nzima. Majosho mengi hayafanyi kazi na kila mwaka tunaiomba Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kwamba majosho yote yanafanyiwa ukarabati. Mbona tumeweza kujenga shule za sekondari kwa muda mfupi. Kwa nini Serikali isitenge fedha tukakarabati majosho yale yote ili tuondokane na tatizo hilo. Nitaomba kupata maelezo kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ufinyu wa bajeti hauwezi kwisha leo au kesho, unaendelea tu, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni mkakati gani ambao umewekwa wa kuhakikisha kwamba majosho yote yanakarabatiwa ili tuweze kuogesha mifugo yetu. Ni aibu kwa kweli ng'ombe anakufa eti kwa sababu hajaogeshwa. Ugonjwa wa kupe ni ugonjwa ambao tunaweza kuuzuia kwa sababu ni ugonjwa ambao unatoka kwenye mifugo na kwenda kwa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni huduma ya mifugo hasa kuhusu malambo na mabwawa. Huwezi kuboresha mifugo kama nilivyosema kama huna majosho. Kama hakuna bwawa la kunyweshea mifugo, madawa ya chanjo ni ghali, madawa ya tiba ni ghali, haiwezekani. Kwa sababu wafugaji wengi hawawezi kununua madawa hayo kwa sababu yana bei kubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba bei ya madawa inapungua ili wafugaji wengi waweze kununua madawa na kuweza kuhudumia mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la mabwawa ni muhimu sana. Lazima tuhakikishie kwamba tunakuwa na mabwawa ya kutosha ili tuweze kunyweshea mifugo yetu isianze kuhangaika na kuzunguka kutafuta maji. Inawezekana wafugaji wengine wanazunguka katika nchi nzima kwa sababu ya kutafuta malisho na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nizungumzie Taasisi ya Utafiti wa Mifugo pale Mpwapwa. Kwanza, napenda nimshukuru Waziri, kilikuwa ni Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, sasa ni Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Lakini unapobadilisha au unapokipandisha hadhi Kituo kikawa Taasisi lazima mambo mengi

yaweze kuboreshwa. Kwanza, lazima kuhakikisha kwamba Kituo kile kinapangiwa bajeti ya kutosha, kiwe na watafiti wengi na wa kutosha, kiwe na vitendea kazi na kukarabati yale majengo. Haiwezekani tukakiacha kama kilivyokuwa, lazima kufanyike ukarabati wa kutosha ufanyike, kuwe na watafiti wa mifugo wa kutosha pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kuwe na mabadiliko angalau watu wakija waseme kwamba hii ni Taasisi ya Utafiti wa Mifugo. Kwa hiyo, naomba kupata maelezo Serikali imeweka mikakati gani kuhakikisha kwamba Taasisi hiyo inaboreshwa. Lakini Taasisi hiyo pamoja na kwamba imeanzishwa bado haijaanzishwa kisheria. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni lini sheria hiyo itakuja Bungeni ili ipitishwe na Bunge ili Taasisi hiyo iweze kuanza kufanya kazi rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda niwapongeze sana watumishi wote wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa cha Mpwapwa pamoja na Chuo cha Mafunzo. Tunaomba Vituo vyote viboreshwe, viimarishwe, viongezewe vitendea kazi na maslahi ya watumishi wa maeneo hayo yaboreshwe. Pamoja na kuhakikisha kwamba Vituo vyote vya Utafiti katika nchi hii vinaimarishwa, vinaboreshwa na pamoja na kupewa vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo machache. Lakini napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote. Nawaomba waviangalie Vituo vyangu vya Mpwapwa kwa jicho la huruma, vitengewe bajeti ya kutosha. Kwa sababu tegemeo kubwa tukifuga kisasa tutaongeza pato la Taifa na likiongeza hali ya uchumi wetu itakuwa nzuri, na ikiwa nzuri tutaboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana kwa kunipa dakika tano. Sasa ninamwita Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo. Lakini kabla sijaanza kuchangia nimpongeze Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri ambayo tunaendelea kuiona wakifanya katika Sekta hii ya Mifugo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naomba nikukatishe kidogo. Naona kwa sababu Bunge limepanywa niwataje Waheshimiwa Wabunge watakaofuatia. Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Juma Killimbah watafikia mchana huu. Tafadhali endelea!

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapa pole wafiwa wote hasa familia ya aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa marehemu Amina Chifupa kwa msiba mzito walioupata kwa kufiwa na mpendwa wao na sisi mpendwa wetu. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kusahau kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa iliyofanya kwa kupambana na ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa katika nchi yetu hasa katika Mkoa wa Dodoma. Sisi tuliathirika zaidi kuliko mikoa mingine na Serikali ilifanya jitihada kubwa sana katika kuleta madawa ya kuogesha mifugo, kuchaja mifugo na mpaka mwisho sasa hali imekuwa nzuri, na ninaendelea kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kwamba wale nyama ya kuchoma na ya kuchemsha bila matatizo yoyote kwa sababu ugonjwa umetokomezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kunukuu maelezo machache kutoka katika Kitabu cha Hotuba cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 5 amesema hivi, ninanukuu: "Sekta ya Mifugo hapa nchini ni kati ya Sekta zinazoweza kuchangia zaidi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA." Rasilimali kubwa ya mifugo iliyopo ikiendelezwa na kutumika vizuri itachangia zaidi kwenye kukuza uchumi wa Taifa na kupunguza umaskini kwa kuwa takriban kila kaya ina mifugo." Mwisho wa kunukuu. Kwa nini nimesoma eneo hilo. Nimeona kwamba Serikali bado haijaweka mikakati mahususi katika kuendeleza Sekta ya Mifugo. Mifugo ina mazao mengi. Naomba niyataje, mifugo ina maziwa, nyama, mayai, mifupa ni chakula cha kuku, ngozi tunatumia kutengenezea viatu na mabegi na kadhalika. Lakini ukiangalia katika sekta ya mifugo bado wafugaji wanahangaika. Wafugaji hawajapata uhakika wa mazao hayo. Wafugaji bado wanadhulumiwa katika kuuza mazao yao kama maziwa, kama ngozi, kama mayai kwa sababu hawana msimamizi. Mazao ya kilimo kama korosho, pamba, tumbaku, kahawa yana bodi. Bodi hiyo inatetea bei ya mazao hayo inaposhuka. Lakini mifugo haina mtetezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfugaji anapopeleka mazao yake katika mnada, mazao yake hayauzwi kwa kupima kilo, ng'ombe hauzwi kwa kupima kilo, wala mbuzi, wala kondoo. Wanategemea unene wa ng'ombe, unene wa mbuzi, uzuri wa kondoo, lakini hauzwi kwa kupima kilo. Sasa tunategemea kwamba huyo mfugaji atatoka katika hali yake ya uduni lini? Kwa sababu katika nchi yetu hatuna viwanda vya kusindika nyama, hatuna viwanda vya kusindika maziwa, hatuna Sekta inayosimamia vizuri ngozi ya mifugo. Kwa hiyo, mfugaji anafuga akitegemea kuuza mnadani tu kwa walaji wa nyama na kwa wasafirishaji wa mifugo hiyo nje. Lakini tungekuwa na viwanda vya mazao ya mifugo, naamini kabisa wafugaji wetu maisha yao yangebadilika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona katika Mkoa wetu wa Dodoma, tangu tumejengewa kiwanda cha kisasa cha kukata nyama, hatuna kiwanda cha kusindika nyama sisi. Tuna kiwanda cha kisasa hapo mnadani cha kukata nyama, lakini kiwanda kile kingekuwa na kiwanda jirani cha kusindika nyama, wafugaji wa Dodoma wangebadilika na wangefuga kwa hali iliyo tofauti na wanavyofuga sasa. Kwa sababu ng'ombe mmoja kwa mfugaji sasa anawezekana akawa na kilo 60. Kwa sababu akipeleka ng'ombe yule mnadani anategemea kumuuza tu kwa kumwangalia kwa

macho. Lakini tungekuwa na mahali pa kuwauza mifugo yetu kwa kupima kwa kilo ingekuwa vizuri, wanapelekwa kiwandani, wanauzwa kwa kupimwa kwa kilo, wengi wangefuga mifugo kwa hali ya kisasa wakitegemea kupata fedha ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata viwanda vya usindakaji wa maziwa sisi Dodoma ni wafugaji wazuri sana na Mkoa wa Mwanza ni wafugaji wazuri sana, Mkoa wa Shinyanga ni wafugaji wazuri sana, Arusha ni wafugaji wazuri sana, Mkoa wa Manyara ni wafugaji wazuri sana. Maziwa katika mikoa ya mpakani yanaenda nje ya nchi, wale wenzetu wanachukua maziwa kutoka kwenye nchi yetu tena wanayanunua kwa bei ndogo sana. Wanapelekwa kwao wanasindika, wakiyaleta nchini kwetu maziwa yaliyokwisindikwa wanatuuzia kwa bei ya juu sana. Kwa nini Serikali isitafute namna ya kuwekeza katika viwanda angalau ijenge viwanda na kutafuta wawekezaji ambao watafanya kazi ya kusindika maziwa na kusindika nyama ili wafugaji wapate soko la uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka zamani tulikuwa na viwanda vya maziwa. Akinamama vijijini walikuwa na Vituo vya kuuzia maziwa; akinamama wa vijijini walikuwa wanatoka ndani huko vijijini wanakwenda kwenye Vituo vya kuuzia maziwa na mwisho wa mwezi wanakuwa na uhakika wa kupata fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya nyumbani. Vituo hivyo siku hizi hakuna na kwa sababu hakuna viwanda vya kusindika maziwa. Kuna tatizo gani la kuwekeza katika viwanda vya kusindika nyama na viwanda vya kusindika maziwa? Nimesoma katika katibu cha hotuba cha Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Ukurasa wa 46 Malengo na Mipango ya Wizara. Mimi nilitegemea kwamba katika Malengo na Mipango ya Wizara wanalenga kuwavutia wawekezaji katika maeneo yenye mifugo mingi kama Dodoma wawekeze na wajenge viwanda vya kusindika nyama na kusindika maziwa. Wananchi wa Dodoma bado ninarudia kusema kwamba siyo maskini, wana mifugo ni mingi sana, lakini mazao yanayotokana na mifugo hiyo wayauze wapi? Wanangoja kuuza mazao ya mifugo yao kwa wafanyabiashara wa kawaida ambapo wengi wanainunua kwa bei ndogo. Sasa nilitegemea kuwa Waziri angeonyesha kwamba kuna mkakati wowote, ama wa kuhamasisha wawekezaji wajenge viwanda vya mazao ya mifugo katika Mikoa yenye wafugaji wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika ukurasa wa 46 hilo halikuzungumzwa. Ni mwaka gani Serikali itaweka mikakati ya kujenga viwanda hivyo katika nchi yetu? Je, sisi tusafirishe ng'ombe tusisindike? Ni lini tutasindika nyama na ni lini tutasindika maziwa? Tunategemea maziwa kutoka Afrika Kusini, tunagemea maziwa kutoka Zimbabwe na Kenya wakati wale siyo wafugaji kama sisi tulivyo wafugaji. Mimi nadhani Tanzania kama sikukosei ni kati ya zile nchi 10 zenye mifugo mingi na mifugo mizuri, lakini hatuna viwanda. Kama nilivyonukuu katika katibu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwamba Sekta ya Mifugo ikisimamiwa vizuri itachangia kwa kiasi kikubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu. Tunaiacha kwa nini Sekta ya Mifugo isichangie kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Watakapojenga viwanda katika maeneo yenye mifugo, tutaongeza ajira. Sioni sababu ya kusubiri *SACCOS* tu iongeze ajira kwa wananchi wakati kuna sekta nzuri ambayo inaweza ikaongeza ajira kwa vijana na kwa wanawake kama Sekta ya Mifugo. Tutakapokuwa na viwanda hivyo

wengi watapata kazi na wengi watauza mazao yanayotokana na mifugo na tutainua uchumi wa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 49, amesema atajenga mnada Mwanza na mnada Mbeya. Lakini katika minada hiyo nitahadharishe kwamba wananchi wasiendelee kunyonywa kwa kuuza mifugo kwa kutazama kwa macho. Mifugo hiyo iuzwe kwa kupimia kwa kilo kama mazao mengine ya kilimo. Niungane na Mheshimiwa George Malima Lubeleje kusema kwamba majosho tuliyonayo katika Mkoa wetu wa Dodoma hayatoshelezi mahitaji ya wafugaji. Tuna ng'ombe wengi, tuna mbuzi wengi, tuna kondoo wa kutosha, punda na wanyama wengineo, lakini hatuna majosho ya kutosha kwa mahitaji ya wafugaji. Sikuona katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri ni wapi wanategemea kuongeza majosho na mabwawa katika Mkoa wa Dodoma. Ninaomba sasa Serikali ione umuhimu wa kuongeza majosho katika maeneo yenye wafugaji wengi. Huduma ya ugani pia haitoshelezi katika Mkoa wa Dodoma, Afisa Kilimo ndiye Afisa Mifugo. Kwa nini hao Maafisa wa Wizara wasifanye kazi kwa kufuatana na taaluma zao? Tangu lini Bwana Kilimo akawa Bwana Mifugo?

Ninaomba Wizara hii iangalie namna ya kutenganisha sekta hizo mbili. Bwana Mifugo awe Bwana mifugo na Bibi mifugo awe Bibi Mifugo na Bwana Kilimo awe Bwana Kilimo.Wafugaji wanashindwa kupata ushauri mzuri kutoka kwa Maafisa Ugani kwa sababu wengine hawana hiyo taaluma. Kwa sababu wakishafanya kazi kwenye Idara hiyo kwa muda mrefu basi wanachukuliwa kwamba wana utaalamu huo. Hawana utaalamu huo. Wachukuliwe wale wenye utaalamu na wale ambao wataajiriwa na Wizara hii basi wakasambazwe katika maeneo ya vijijini na wananchi wapate huduma nzuri kutokana na ushauri utakaotolewa na hao Maafisa Ugani.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika Wizara hii. Kwanza, nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inaonyesha mwelekeo mzima na mipango mizuri katika Wizara hii. Tuna uhakika kutokana na mipango hiyo, basi Sekta hii ya Mifugo inaweza kukua kwa asilimia 10 kama yalivyo malengo yetu katika Ilani yetu. Kwanza, nasikitika sana kuona kwamba Wizara hii nyeti ambayo ni sambamba na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika nayo pia inaajiri asilimia 80 ya Watanzania, lakini katika mgawanyo wa rasilimali ya pato la Taifa imepewa asilimia 1 tu ya bajeti nzima ya Taifa. Sasa nilikuwa nashindwa kuelewa ni kwa nini pia Sekta hii muhimu haikupewa muhimu ule ule kama iliyopewa Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii kwetu sisi wanawake naweza kusema inaajiri i karibu wanawake asilimia 95. Kila mwanamke mbali na kufanya kazi za kiofisi lakini lazima anajishughulisha na ufugaji. Aidha, ufugaji mkubwa au ufugaji mdogo mdogo hasa wa kuku akiwa nyumbani na kujipatia kipato, lakini sekta hii imepewa asilimia moja tu ya bajeti nzima ya Taifa. Nikienda katika idadi ya ng'ombe kwa kufuata sensa

iliyofanyika mwaka 1984 kwamba inasemekana Tanzania tunao mifugo karibu 18,000,000 na ukiangalia hiyo 18,000,000 ubora bado ni duni sana, lakini nchi yetu ni nchi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi katika Afrika ukiachia nchi ya kwanza Ethiopia na ya pili Sudani, lakini nchi yetu Tanzania ni nchi ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nashauri pamoja na kwamba tunao ng'ombe wengi sana lakini ng'ombe wetu wanaonekana ni duni hawana afya ya kutosha. Kwa hiyo, kama tunavyoweka mikakati kabambe katika Wizara ya Kilimo vilevile sekta hii inahitaji mikakati kabambe ya kuweza kuwafanya ng'ombe wetu waonekane bora.

Nilikuwa nashauri hapa katika suala zima la malisho zipo mbegu kwa ajili ya malisho bora. Tunaweza tukatafuta mbegu kwa ajili ya majani kama *lukina* au *elephant grasses* tukaweza kuwapatia wakulima wetu wakaweza kutengeneza mashamba madogo madogo na kupanda zile mbegu na kuweza kuwalisha wale mifugo baada ya kutegemea majani pori. Ng'ombe wetu wanakula majani pori na hivyo wanaonekana sio ng'ombe bora.

Nikija kwenye suala zima kwamba tuna ng'ombe wengi sana lakini kitu cha kusitikitisha ni kwamba hatujafikiria zaidi kuwekeza kwenye suala zima la viwanda kwa ajili ya k u-*process* yale mazao ya mifugo kama maziwa, nyama na ngozi vilevile. Hatuna viwanda vingi vya kutosha, hii inapelekea kuwakatisha tamaa wakulima na kuona kwamba sekta hii sio muhimu na haiwezi kuwapatia kipato cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu Mheshimiwa Bura ameiongelea kwa kirefu sana kwamba Wizara ni lazima sasa iweke mikakati ya kutafuta wafadhili ili waweze kuwekeza katika sekta nzima ya viwanda ili basi wale wafugaji wetu waweze kujua ni wapi wanaweza kuuza maziwa yao na ni wapi wanaweza kuuza nyama yao na ni wapi wanaweza kuuza ngozi zao. Ukiangalia kwenye *supermarket* zetu inasikitisha sana, tunasema kwamba sisi ni nchi ya tatu kuwa na mifugo mingi katika nchi ya Afrika lakini *supermarket* zetu zimejaa maziwa kutoka Botswana, Zimbabwe, *South Africa*, hii sio sawa. Ukiangalia maziwa kutoka nchini kwetu ni asilimia 4 tu. Kwa hiyo, naiomba Wizara ifanye mkakati mzima wa kuwekeza katika viwanda ili basi tunapokuwa tunakwenda kwenye hizo *Supermarket* ni vizuri tukawa tunanunua maziwa kutoka kwenye nchi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna hii tabia sijui Wizara itaikabili vipi. Watanzania wengi mbali na kwamba ni wafugaji lakini hawana utaratibu, hawana tabia ya kunywa maziwa. Unakuta familia ina mifugo mingi, ng'ombe karibu 1,000 lakini wanakamua yale maziwa, wanakwenda kuuza wenyewe, wanabakia wanakunywa labda chai ya rangi, watoto wanapikiwa uji bila ya kuwekewa maziwa. Hii pia inasababisha sio tu familia kuwa na afya duni lakini wale watoto wanaokua kama wangeweza kuwekewa maziwa yao basi wangeweza kukua vizuri. Kwa hiyo, naomba Wizara ijaribu kuhamasisha familia katika suala zima la utumiaji wa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mtaalamu wa mifugo, nimesimama hapa nikiwa na jambo moja muhimu sana ambalo huwa najiuliza sijui Wizara huwa inaona au

vipi. Ukiangalia kwenye bucha zetu za nyama, nazungumzia bucha zetu zilizoko Kariakoo, kwa kweli mimi binafsi nikipita kwenye zile bucha huwa nasikitika sana. Utakuta nyama nyingi pale hazifai kabisa kuuzwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu, lakini nyama zile ziko pale zinaning'inia na watu wanapiga debe, unakuta kilo inashuka mpaka shilingi 1,200 na watu kwa ule urahisi wanakimbilia wanakwenda kununua nyama zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri *Meat Inspector* wapo na wote wananisikia leo hii. Kwa kweli mimi naona kitu kama rushwa hivi inakuwa inatokea wale *Meat Inspectors* wanapokwenda kule kwenye machinjio unakuta ng'ombe pale anapelekwa. Lakini yule ng'ombe ni mgonjwa labda ana *TB* lakini amepelekwa pale kwenye yale machinjio na amepitishwa na yule *Meat Inspector* anatoka pale ile nyama ina *TB* moja kwa moja kwenye bucha.

Kwa sisi ambao ni wataalamu ambao tumesomea hiyo kazi ukiiangalia tu ile nyama pale buchani unajua kabisa nyama hii ina *TB* na haifai kuuzwa kwa binadamu, lakini nyama zile zinauzwa. Matokeo yake kesi za *TB* zimezidi sana lakini kesi hizi nyingi ukiangalia zinatoka pia kwenye hizi kesi za wanyama. Mtu ananunua nyama ile yenye *TB* anapeleka nyumbani, hapiki vizuri, anakula naye anapata *TB*. Kwa hiyo, naomba *Meat Inspectors* wote wafanye kazi yao vizuri kabisa inavyotakikana wasiweke sana rushwa au pesa mbele na kuangamiza Watanzania wengi kwa magonjwa ambayo yanatokana na nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile pia napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada nzima iliyochukua kutokana na huu ugonjwa uliotokea wa *Rift Valley Fever.* Nawapongeza sana, kwa kweli Serikali imejitahidi sana. Lakini basi nilikuwa najiuliza kitu kimoja ambacho kilikuwa kinanichanganya sana. Yapo magonjwa mengine pia ambayo yana dalili zile zile kama za *Rift Valley Fever* sasa sijui kama Serikali wameliona hilo. Upo ugonjwa wa *Anthrax* ambao unasababishwa na virusi na Watanzania wafugaji wengi sana wanakufa kwa sababu ya ugonjwa huo.

Napenda leo katika majumuisho basi Serikali inifafanulie wanawezaje, kama hii *Rift Valley Fever* tu wanachukua *samples* na kuzipeleka Nairobi, je, huu ugonjwa ambao tuko nao siku nyingi na unaua kwa haraka zaidi na dalili zake ni kama zile zile za *Rift Valley Fever* Serikali inakabiliana nao vipi? Sijui Serikali inawezaje kutenganisha magonjwa haya mawili na kuona kwamba ugonjwa huu wa *Rift Valley Fever* ndio unatakiwa kupewa mkazo mkubwa wa kuangaliwa na sio huu mwingine wa *Anthrax.* Naomba wakati wa majumuisho nipewe taarifa kamili kuhusiana na ugonjwa huu mwingine wa *Anthrax.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine napenda kusisitiza hizi Maabara zetu za mifugo zilizoko kwenye *centres* zetu, naomba zipatiwe vifaa muhimu kabisa ambavyo vinahitajika, yaani tunatakiwa tuwe *standbye*
sio tunasubiri yanapotokea magonjwa ya milipuko basi tunaanza kukimbilia nchi za jirani. Ni lazima tuwe *standbye* wakati wowote tuweke vifaa vyote vinavyotakikana na

tuwe tayari kwamba unapotokea ugonjwa wowote basi tuweze kupima *samples* zetu pale pale kwenye maabara zetu na si kukimbilia nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo mwenzangu Mheshimiwa Bura amelizungumzia ni kuhusu hawa *extension officers*. Kwanza napenda tu niwapongeze kwa kazi ngumu wanazofanya, watu hawa wanafanya kazi chini ya sekta mbili. Wanafanya kazi sekta ya kilimo na vilevile sekta ya mifugo. Ni dhahiri kabisa ukiangalia sekta hizi mbili ni nyeti. Sasa ni dhahiri kabisa sekta moja itadorora kama inavyoonekana sekta ya mifugo kudorora. Sasa hii imedorora kutokana na kwamba imeunganishwa sana na sekta ya kilimo kuonekana kwamba sekta ya kilimo ndiyo ime-*dominate* zaidi na hata hao watu wanaosomea mifugo wakishapelekwa kufanya kazi za kilimo basi wanajikuta wamebobea kule kwenye kilimo na kusahau kabisa sekta nzima ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama alivyosema mwenzangu naomba sekta hizi mbili zitenganishwe, hizi ni sekta mbili tofauti. Mtaalamu wa Mifugo hawezi kuwa yule yule akawa mtaalamu wa kilimo au mtaalamu wa kilimo hawezi akawa mtaalamu wa mifugo kwa sababu mambo kule ni tofauti. Magonjwa ya mimea ni tofauti na magonjwa ya mifugo, sasa unapomweka mtu mmoja ana fani ya mifugo unamweka ndiyo huyo huyo wa kilimo, huyo huyo awe wa mifugo inakuwa vigumu sana katika kuleta ufanisi wake mzima wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umenisalia, mengi yameongelewa na Mheshimiwa Bura, kwa hiyo, sio vizuri sana kurudia kile alichokisema mwenzangu, ila napenda tu kuweke msisitizo. Narudia tena kusema kuwa hawa *Meat Inspectors* wanaoruhusu nyama zinauzwa ambazo hazifai kuuzwa, naomba wachukuliwe hatua kwa sababu magonjwa mengi ya mifugo ndiyo yale yale yanayoambukiza pia binadamu kwa kupitia nyama hiyo hiyo kama haijapikwa vizuri. Kwa hiyo, naomba Mabwana Mifugo wote na Mabibi Afya na Mabwana Afya waweze kusaidiana kupekua hizi bucha waweze kuangalia je, zile nyama zinazouzwa kule zinafaa kuuzwa na kama hazifai kuuzwa basi wajaribu kumchukulia hatua yule *Meat Inspector* wa lile eneo ili kuweza kuwanusuru watu na magonjwa mengi ambayo yanajitokeza. Ahsanteni sana na ninaitakia Wizara kila kheri katika kuhakikisha kwamba sekta hii ya mifugo tutashirikiana nao bega kwa beba kuhakikisha kwamba sekta hii inakua. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

**NAIBU SPIKA**: Kwa hiyo unaunga mkono?

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mifugo. Ningependa kusema kwamba Wizara hii ni muhimu sana kwangu kwa sababu mimi mwenyewe ni mfugaji na ningependa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii nawapongeza sana. Jambo lingine napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne. Mimi nilifurahi sana Wizara hii ilipotengwa kuwa Wizara peke yake bila kuungana na Kilimo au Maji. Kwa sababu wakati ule ilikuwa kidogo Maji ndiyo inatambulika zaidi au Kilimo ndiyo inatambulika zaidi na sasa ni Wizara peke yake. Lakini ningeomba Serikali itambue Wizara hii kwamba sio Wizara ndogo ya kuipa fedha kidogo kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka wafugaji wafuge vizuri na mifugo iboreshwe ni lazima kuwa na majosho katika maeneo yote ya wafugaji. Pesa iko wapi hapa ya kuweka majosho katika maeneo mengine, maeneo ya wafugaji. Ukiweka majosho wafugaji hawatahama tena kuacha majosho kwa sababu wakihama, wakiacha majosho mifugo itakufa kwa hiyo lazima watarudi pale kuogesha. Sasa hakuna fedha za majosho, hata mabwawa, mabwawa 18 nchi nzima ndiyo unasema mabwawa, hakuna mabwawa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kusema kwamba Serikali itambue kwamba mifugo ni rasilimali kama rasilimali nyingine iliyoko katika nchi hii. Lakini hatukutambua, mimi niko mpakani na nasema kila siku Kenya wanachukua pato kubwa sana la Tanzania kwa mifugo. Sisi tunategemea Kiwanda cha Kenya, *Kenya Meat Commission*, asilimia 60 ya mifugo inayochinjwa pale nasema kila siku inatoka Tanzania. Kenya ndiyo inauza nyama nyingi nchi za nje, ndiyo inauza ngozi nyingi sana, lakini mifugo inatoka Tanzania. Hivi tunakubali kila siku uchumi wetu uende Kenya? Nimeshangaa sana kuona kwamba hakuna hata Kiwanda kimoja kilichowekwa kwa sababu nilitegemea kwenye bajeti hii tungeambiwa kwamba kuna kiwanda kinajengwa Arusha au Mwanza au Shinyanga sio machinjio, machinjio yanawasaidia walaji wa hapo hapo, walaji wa hapa Dodoma wanasaidiwa na machinjio yaliyopo Dodoma, lakini kama ni biashara ni viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia suala la ardhi ya wafugaji. Bado wafugaji katika nchi hii ni wakimbizi, wanafukuzwa na wakulima. Inaonekana kwamba mkulima ni muhumu akija akiweka shamba la eka mia moja, atahamishwa mfugaji aliyekutwa pale aachwe mkulima. Ningependa kusema kwamba itambuliwe ardhi ya wafugaji kwa sababu mnaona kwamba ni ardhi ambayo haina matumizi, ina matumizi kwao. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba ardhi ya wafugaji itambuliwe na wapewe hatimiliki. Jambo lingine ningependa kulisemea kwamba mbung'o wamechukua eneo kubwa sana katika nchi hii kwa sababu kuna mapori ambayo yanafaa kwa ufugaji lakini wafugaji hawawezi kuhamia kwa sababu ya mbung'o. Ningeomba Serikali itafute namna ya kuwaangamiza mbung'o ili maeneo hayo yatumike. Ni mapori ambayo hayatumiki kwa ajili ya mbung'o. Sasa ningependa kusema kwamba Serikali itafute namna ya kuua hao mbung'o kwa sababu inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye masoko. Niliona katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri kwamba kuna masoko ya Uarabuni au ya nje. Ningependa kusema kwamba na sisi tuanze kutumia haya masoko. Lakini hizi ranchi kama Kongwa Ranchi , ni aibu ranchi zetu tukatumia kama wachungaji. Mnatusema sisi

ni wachungaji sio wafugaji, tunasema hata hizi ranchi kama Kongwa na wapi nao wamekuwa wachungaji kama sisi. Hivi ranchi ambayo ina mifugo 7,000 lakini inajitosheleza tu kwa kulipa watu mishahara na kununua madawa ya mifugo iliyoko pale basi hakuna kitu kingine, hakuna pato lingine linaloiletea Taifa? Hivi hawa ng'ombe walioko Kongwa hapa wana tofauti gani na mifugo wa kwangu walioko nyumbani kama hawazalishi, hawaleti pato lolote hapa nchini?

Mnatuambia sisi tuuze mifugo nyinyi mnakusanya ng'ombe hapa Kongwa, yanakuwa mamilioni na mamilioni hamuuzi! Hivi kwa nini hamkuuza hawa waliopo hapa Kongwa? Mnasema wafugaji wapunguze mifugo ranchi zenu zimejaa mifugo mingi sana na wala hawazalishi. Ningependa kusema kwamba mtuonyeshe mfano, sasa haya masoko muanze kuuza nyama za Kongwa ifahamike Tanzania inauza nyama kutoka Kongwa katika nchi fulani na sisi wafugaji wengine tuige. Nashangaa kuona maelfu ya mifugo lakini inatosheleza tu kulipa mishahara ya watu pale. Kama haiwezekani basi hiyo ranchi igawanywe wapewe wananchi wa Kongwa wanaozunguka kwenye hiyo ranchi kwa sababu haina faida inayoiletea Taifa, inawasaidia wale wanaofanya kazi pale pamoja na ranchi zingine zilizopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni madawa ya mifugo. Nilisema wakati mmoja kwamba kuna kampuni 8 walipewa fedha za ruzuku lakini hizo kampuni hatuzifahamu kwamba ni zipi. Nasikia kuna Mhindi mmoja amepewa ukanda wa Kaskazini ambaye hatumfahamu jina wala sura. Amepewa shilingi 440,000,000 kwa ajili ya ruzuku ya madawa. Mimi ni mfugaji sijawahi kununua dawa ya huyo Mhindi aliyepewa kwa upande wa Kaskazini. Sasa ningependa kuuliza. hizo Kampuni wamepitisha wapi hizo fedha? Kwa sababu tungependa kuona kwamba dawa hii inapunguzwa, ruzuku ya Serikali ingetusaidia. Ningependa sasa muanze utaratibu mzuri ili tujue maduka hayo kama ni Arusha, Moshi au wapi, tujue kwamba kuna madawa ya ruzuku yaliyopo katika duka fulani na anayeuza tumtambue huyo mtu mliyempa, bahati mbaya sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la ranchi ya *West* Kilimanjaro. Mimi tangu nilipokuja hapa Bungeni kila ninapochangia Wizara hii nataka hii Ranchi ya *West* Kilimanjaro. Ranchi hii ilikuwa ya Serikali zamani lakini sasa hakuna mifugo waliopo au mifugo waliopo ni wachache. Wananchi wapo kwenye hiyo ranchi na tunatambua kwamba ni ranchi ya Serikali ya zamani lakini wananchi wameingia pale miaka 30 iliyopita, wamejenga nyumba za kudumu, wana mashamba. Naomba Serikali iende kuwaangalia na kuwapa maeneo hayo waliyojenga nyumba za kuishi, hiyo ardhi wanayoitumia ihalalishwe, eneo lingine mnaweza kutumia kuwapa wawekezaji, kama ni wawekezaji lakini naomba wananchi watambuliwe zaidi ya wawekezaji. Tusiseme tuwaogope wawekezaji kuliko wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la wafugaji waliohamishwa Ihefu. Serikali ilitoa fedha nyingi sana kwa ajili ya kuwahamisha hawa wafugaji. Leo nataka kuuliza, hivi hizi fedha zilizochangwa kwa nini hawakupewa wale wafugaji kununua hata dawa ya kuwasaidia wanaposafiri. Hakuna hata wazee wakongwe na akinamama wajawazito na watoto wadogo, kwa nini hawakusafirishwa kwa magari waende kule

wanakokwenda. Hivi hizi fedha zimetolewa kwa ajili ya askari wa kuhamisha hawa watu; zimetolewa kwa ajili ya kulipa tu *night* haikupaswa kuwasaidia hawa wafugaji.?

Mzee mkongwe ambaye anatembea kwa kutumia fimbo anasafiri mwezi mmoja hivi tuna hakika hao wamefika wote salama. Serikali imetoa fedha, *TANAPA* imetoa, Ngorongoro imetoa, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori umetoa lakini hakuna senti iliyowasaidia wafugaji, hata madawa ya mifugo.

Naomba mtuambie kwamba kwa nini hizo fedha hazikutumika kwa ajili ya kuwasaidia wale wafugaji ambao walipatwa na mmetoa kwa ajili ya kuwahamisha? Sio kuwahumiza tu pamoja na kuwasaidia hao watu waliohama. Labda niachie hapo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mbegu bora. Tuna kituo cha Tengeru pale. Kituo cha Tengeru kina mbegu bora zaidi hata kushinda Kenya. Tengeru unamkuta dume lenye kilo 1,300 au 1,400, hakuna kituo kingine chenye madume bora kama hawa wa Tengeru. Lakini mbegu zilizoko pale hazijasambazwa kwa wafugaji.

Ningeomba sasa Wizara yako itumie hicho Kitengo kilichoko Tengeru tupate mbegu bora. Wala hii haijatangazwa, wafugaji hawajui wangejua wangeweza hata kuleta kutoka Shinyanga au Mwanza kwenda kuchukua mbegu pale.

Sasa tumeboresha hicho chuo, wanafuga vizuri, wataalamu wazuri, lakini wamebaki wamefungiwa pale hata wananchi wa Tanzania hawajui kwamba kuna mbegu bora hapa. Ningependa kusema hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni elimu kwa wafugaji. Naomba elimu ya wafugaji itolewe tusiwe tunapiga kelele hapa tu Bungeni, tuna wataalamu wa kutosha, naomba wataalamu hao wasambazwe kila Mkoa waende kutoa elimu. Naunga mkono hoja.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu kwa hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mifugo iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mifugo kwa hotuba nzuri aliyoitoa asubuhi hii ya leo. Kwa kweli ilikuwa ni nzuri sana. Mifugo ya Tanzania kama kuna mgodi tulionao mkubwa wa dhahabu basi ni mifugo ya Tanzania. Lakini kwa bahati mbaya sana hatujahangaika namna ya kuchimba mgodi huu. Kama tukiamua leo tufanye mageuzi makubwa katika sekta ya mifugo basi kama kuna sekta itachangia kwenye uchumi wa nchi itakuwa ni mifugo.

Mimi sikubali, tunasema kuna MKUKUTA, haya ni maneno tu tuyapeleke sasa kwenye vitendo. Kuna mambo yakifanyika hata usipotumia neno MKUKUTA tuna hakika mifugo ya nchi hii itakua na ziko *statistics* duniani ambazo zinaonyesha kwamba kuna nchi zimeendelea kwa kutegemea mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sensa ya mwaka 1988 iliyofanyika Tanzania, ilisema tuna mifugo 19,000,000, lakini naamini mpaka leo tukisema tunafanya sensa mifugo ya nchi hii sasa ni zaidi ya 25,000,000. Lakini ipo tu ili mradi siku zinakwisha ndiyo maana ukiangalia bajeti ya Wizara unaona kabisa kwamba sio kitu *serious* ndiyo maana tunakipa fedha kidogo.

Mimi kuna mambo ya kwanza kabisa nashauri tuyafanye ili kuhakikisha kuwa tunaanza kutekeleza mageuzi katika mifugo. Cha kwanza lazima tui-*map* Tanzania ili tuweze kujua *suitable area for livestock* kwamba tui-*map* nchi yetu yote, watu wa kilimo wamefanya na mifugo tunaweza tujue mifugo yetu tunaiweka wapi.

Ukishamaliza ku-*map* nchi yetu sasa *demarcate* mifugo hii itakuwa wapi ambako kuna ardhi nzuri na nyasi. Tukishamaliza sasa tuanze kufikiria namna ya kuongeza ile *pasture* kwa maana ya majani tuyaongeze viwango. Tukishatoka hapo sasa tunaanza kufikiria *quality* ya mifugo zile *hybrid* zetu. Sasa tuweke *investment* kuweza kuongeza *hybrid* zetu ili tuweze kupeleka kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mifugo ya nchi hii iwe na maana kuna mambo ya msingi lazima tuyafanye. Pamoja na kuwa tumekuwa *demarcate* nchi yetu, tumejua tutafuga wapi, tumepata *hybrid* zetu, tukishafika hapo peke yake haitoshi, lazima tuondoke hapo. Nchi yetu Rais alisema tunataka mpaka 2010 tuwe tumetengeneza ajira milioni moja.

Mimi nasema kama kweli tukiamua mifugo peke yake inaweza ika-*produce* zaidi ya shilingi milioni moja kwa miaka mitano, mifugo peke yake. Ni suala tu la kuamua tufanye mageuzi ya mifugo na mageuzi haya yanakuja kwa njia ngapi? Kwanza, kuna wafugaji lakini pia kuna watu wa katikati. Watu wa kati kati hawa ndiyo wafanyabiashara wenye *lunch* ndogo ndogo. Lakini tukishatoka hapo lazima tuanzishe, ama *a private company* ambayo itakuwa ni *Meat Commission* au *Quality National Abattoir*. Vyovyote utakavyoita ile *National Abattoir* kazi yake ni moja tu, ni kuchinja ng'ombe na kutafuta masoko duniani.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema tukitegemea kwamba masoko ya dunia wata-*access* akina Mzindakaya sio kweli, hawawezi! Maana unaweza ukaenda unapewa *quarter* katika *EU market* unatakiwa upeleke nyama labda umechinja kila mwezi ng'ombe 3000. Nani anaweza akachinja hapa ng'ombe 3000 aweze ku-*access* hiyo *market*. Kwa hiyo, lazima tuanze kutengeneza kwamba iwepo *Meat Commission* ambayo Botswana wamefanya ambapo ukienda katika ule Mji wa *Robase* wa Botswana , wametumia watu waliotoka *Tanganyika Parkers*. Leo Botswana wana milioni tatu, lakini ng'ombe wanachangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi wa nchi yao. Sisi tuna milioni karibu 20 bado hawachangii vya kutosha.

Sasa tukishaanzisha *Abattoir* watu wale wa *Abattoir* ni rahisi, wata-*access finance,* tena sio kutoka Serikalini tunawapa *long term bonds*. Mabenki yote yanatoa *long term bonds,* wata-*access* zile pesa, watakuwa na zile pesa zao. Wamekaa pale,

wameshajenga mashine kubwa ya kuchinja ng'ombe na zile *products* zao waweze kuzipeleka nje ya nchi. Wanaokwenda kuwauzia ng'ombe ni hao watu wa katikati wenye vi-*ranch* vidogo vidogo. Hawa wenye *ranch* ndogo ndogo wakishakuwa na *ranch* kubwa wataanzisha kitu kinaitwa *feed roads*. *Concept* ya *feed roads* ilianza mwaka 1920 huko Marekani Australia wakaichukua mwaka 1950 na kweli wakafanya mageuzi makubwa katika *Beef Industry*.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukishatoka hapo hawa watu wa katikati watafanya kazi ya kuwa-*fatten* wale ng'ombe kwenye hivyo *vi-ranch* vyao watakuwa na hizo *feed roads,* unamwingiza ngombe ana maji, ana kila kitu. Kwa hiyo, akishakuwa na *quality* fulani ndiyo anakwenda kwenye *Meat Commission* kuuza. Akifika pale anakabidhiwa *cheque* yake, akirudi anakwenda kwa wafugaji wa kawaida wanamuuzia yule mtu wa katikati. Umetengeneza *employment* ya watu wa tatu kwa kuuza ng'ombe huyu mmoja. Hizi ni hesabu tu, lakini mimi sioni *integrated planning* ya kutumia mifugo, mimi siioni hapa! Tutawalaumu bure hawa, lazima kuwe na *political will* kama tunataka tufanye mageuzi katika mifugo na mtashangaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika lakini nchi hii kuna mambo yanasikitisha sana. Mwaka 2000 Marekani kulikuwepo na Mkutano wa *The Remark of the President of USA* katika *Cattle Industry Animal Conversion* , ilifanyika *Colorado* mwaka 2000. Wanasema Marekani mwaka 2000 walipata 1.3 *trillion dollars* kutoka kwenye *beef industry. Beef industry* imeajiri watu milioni 24 Marekani. Mwaka 2003/2004 Australia wali-*export* wakapata 3.9 *trillion dollars* kutokana na *beef industry*. Haya si kwamba wao Mungu aliwajalia wao tu, tunayaweza haya tukiamua, Mungu ametupa ardhi nzuri, ametupa mvua, ametupa mifugo tunataka nini tena! Tunacho-*lack* hapa ni *leadership*. Hebu tuweke *leadership* tu-*harness* hii *potential*, tutakwenda mbali. Lakini kuna mambo, nchi hii wakati fulani ukijiuliza unasema tunalo tatizo. Wakati tuna-*privatize* Tanganyika *Parkers* naomba niliseme hili, Kampuni ya *Food Cop* na *Sebeco* ya *Holland* walikuja wamekaa hapa wakafanya *feasibility study,* kwa miaka miwili walitaka kufanya mageuzi makubwa katika *beef industry*. Wakaweka mikataba mpaka na *BMW* kwamba watakuwa wana-*provide leather*.

Lakini yakatokea ya kutoa, tukaona Tanganyika *Parkers* tumpe mtu mmoja anaitwa Adamjee ataendeleza. Hakuna mifugo iliyoendelea na leo anataka kujenga shule. Kweli *we must revisit our decisions.* Hatuwezi kwenda namna hii. Hatuwezi tukawa tunasema nchi yetu hatuna pesa kila siku tunakwenda kuomba, hela tunazo, hela ni mifugo yetu. Wamasai hawa ukiwaonyesha soko akiwa na ng'ombe 400 ukimwambia uza 100 atawauza. Wasukuma wale akiwa na ng'ombe 1000 ukamwambia hapa uza ng'ombe 200 atawauza. Kwa sababu watazaliana kesho na mtu huyu utakuwa umemwondolea umaskini, ataweza kulipia shule, ataweza kulipia afya, ataweza kusomesha watoto wake, ataweza kujenga nyumba bora. Lakini yote haya tunahitaji kufanya maamuzi ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *statistics* za dunia kwenye hili soko la nyama unajiuliza tatizo letu ni nini? Kwa hiyo, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri kabisa kabisa tusaidie, uweke *integrated planning* ya kutumia mazao ya ng'ombe wetu.

Sisi tutakuunga mkono, anzisha *Meat Commission* na *Meat Commission* hiyo ukishawaweka wale watu waambie jamani mimi hata hela Serikalini siwaombei, nendeni mka-*access* mikopo kwenye mabenki. Watajenga hizo *abattoirs* kubwa, wakishajenga watu wa katikati wapo wengi wenye vi-*ranch* vidogo vidogo. Vi-*ranch* hivyo watakwenda kuuza.

Mheshimiwa Laizer, amesema pale anasema Kongwa hapa wana mang'ombe yamekaa pale hawana pa kuyauza. Leo hawa watu kama Mzindakaya kazi yao si kujenga viwanda wao wafanye kazi ya kununua ng'ombe kwa watu wadogo wadogo wakishawafikisha kwenye ranch zao wakuze ngombe zao wakauze kwenye *National Abattoir* wale ndiyo wachinje wapeleke ku-*access* masoko ya ndani, masoko ya Afrika na Duniani. Kodi itaongezeka, pesa za nje zitaongezeka, ajira itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema katika hili hakuna muujiza, ni kufanya maamuzi. Kwa hiyo, kazi ya Serikali iwe kuhakikisha wafugaji wetu wanapata mbegu bora, wanapewa elimu ya kutosha ili na wao wakishafika hapo waseme kwa hakika mahali pa kuuza ng'ombe wao. Hiyo elimu yao wataielewa. Lakini leo ukimwendea Mmasai hata ukimpa elimu namna gani wakati hata akitaka kuuza kesho ng'ombe hajui anawauza wapi, bado haitusaidii. Kwa hiyo, *this is a chain. Chain* hii lazima ianze, kwamba kazi ya Serikali iwe kupeleka hiyo elimu wananchi wetu wapate mbegu bora na tui-*map* nchi hii kama walivyofanya watu wa kilimo tujue wapi tunaweza kufuga na tutaondokana na haya mambo ya Ihefu. Haya mambo yalitokea Ihefu ni kwa sababu hatujajua watu wachunge wapi na wapi wasichunge, ndiyo sababu. (*Makofi*)

Tukishatoka huko sasa wale *middle class*, wafanyabiashara hawa kazi yao ni moja tu hata *esteems* tuwape ili wao wafanye hizo kazi. Waanzishe *feed roads,* wakishaanzisha watanenepesha ng'ombe wetu, wakishawanenepesha wanawapa kuuza. Hakuna atakayeacha kwenda kwenye hiyo biashara, hakuna na kweli mafanikio ya Wizara hii ndipo tutakapoyaona. Lakini bila ya hivyo itakuwepo Wizara tutamaliza miaka mitano ukisema *beef industry* imekuwa hatuoni ilivyokuwa, tunaongelea habari ya bilioni 17. Bilioni 17 kwenye ng'ombe? Tunapaswa kuingiza. Mimi ungeniambia dola bilioni 17 angalau ningeelewa, shilingi bilioni 17 sio za kujivunia kwa ng'ombe tulionao katika nchi hii, sio kabisa wa kujivunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namwomba Waziri wakati ana *sum up* jioni atuambie mkakati wa kuweza kutumia maendeleo haya ya mifugo tuyaone ya kweli. Mimi naamini Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais alivyoamua kuunda Wizara ya Maendeleo ya Mifugo alikuwa anatamani kuona *beef industry* inakua. Naamini ndiyo ilikuwa nia yake, sitaki kuamini kwamba alianzisha Wizara hii lakini bado baada ya miaka mitano tusione mageuzi makubwa katika *industry* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono.(*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu wa leo. Awali ya yote nami nichukue

fursa hii nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Anton Diallo na Naibu Wake, Mheshimiwa Charles Mlingwa pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara kwa maandalizi mazuri na kazi nzuri kwa ajili ya bajeti ya mwaka huu wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji waliopita wamezungumzia kwa kina sana juu ya umuhimu wa sekta hii ya mifugo. Hii ni sekta muhimu sana kwa wananchi wetu hasa wanaoishi vijijini. Watanzania walio wengi wanaoishi vijijini hususan katika Jimbo langu na Mikoa ya Kati na Mikoa ya Magharibi, Kaskazini, Kusini wanaitegemea sana, baada ya kilimo wanategemea mifugo. Ni dhahiri kabisa wananchi ukiachilia kilimo kinachofuatia ni mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi leo hii sana sana nitazungumzia kuhusiana na suala la Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 -2010 juu ya Sekta ya Mifugo. Ilani yatu ya Chama cha Mapinduzi ilisema nini na ili tuoanishe na kitabu hiki cha Bajeti cha Wizara. Kwa ridhaa yako nitaomba ninukuu sehemu hii ya juu kabisa ya ukurasa wa 29 inayosema hivi:

"Pamoja na kwamba Tanzania ina mifugo mingi sana, mchango wa mifugo kwenye uchumi wa Taifa ni mdogo kwa lengo la kuendeleza sekta ya mifugo ili ichangie zaidi ukuaji wa uchumi wa taifa na kuwaongezea kipato wafugaji. Serikali za CCM zitaendelea kwa msisitizo zaidi lengo la kuzingatia ubora kuliko wingi pekee katika ufugaji. Ili kufikia lengo hilo hatua zifuatazo zitachukuliwa katika kipindi cha 2005/2010..."

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote tunayoyazungumza majawabu yake ndiyo tulikuwa tunahitaji sasa au mipango ya Wizara iyapate kutokana na hiki kitabu cha Ilani ya Uchaguzi. Mambo yote ya kumwendeleza mfugaji yanayohusiana na ufugaji bora, mambo yote yanayohusiana katika sekta hii yote yametajwa katika kibabu hiki cha Ilani ya uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikiliza Mheshimiwa Waziri na nimekipitia kitabu chake cha Bajeti ya mwaka huu. Yaliyosheheni katika kitabu hiki pamoja na kueleza mikakati kidogo lakini kwa sababu labda tuendane na hiki kitabu cha Ilani naona mambo mengi yameguswa ambayo pengine hayo yote yangepata majawabu kama tukifuata kitabu hiki ambacho kinazungumzia masuala mengi.

Masuala ya *RVF*, mafua ya ndege, maazimisho ya shughuli za wafugaji, mikutano na mambo mbalimbali. Lakini masuala yaliyo muhimu ambayo yanaendeleza sekta hii ya mifugo, naona yamechukua nafasi ndogo sana. Yako masuala mengi yaliyotajwa mazuri kutoka (a) mpaka (k), yote yamegusa maeneo nyeti sana ambayo yalikuwa yanamwendeleza mfugaji. Lakini kama nilivyoeleza ni kwamba naona Mheshimiwa Waziri hakuweza kuifuata kwa umakini Ilani na ninaamini tungefuata haya yote tunayolalamikia yasingeweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudi nizungumzie katika Jimbo langu la Uchaguzi, na hii nazungumzia hasa kuguswa kwa sababu na yale yale yaliyozungumzwa kutokana

na Ilani. Eneo la jimbo langu kwa ukubwa wake linachukua eneo kubwa sana la wafugaji na eneo hili limechukua katika Kata zote zile kama Kata ya Shelui, Mtoa, Mtenkente, Urugu, Ndago, Kaselya Mbelekese na unakuja Kata ya Tulia pamoja na Kidalu, zote kuna wafugaji wengi sana.

Lakini kwa hali ya sasa kwa sababu leo hatujamtengea, tunazungumza mkulima unamkuta analima lakini tayari ipo migogoro kuhusiana na wafugaji na wakulima katika maeneo haya. Migogoro hii ipo kwa sababu leo hata tukija tukiuliza tunaambiwa kwamba ukiwaeleza watu kwamba Wizara hii tunaweza tukaeleza vizuri lakini tukaambiwa kwamba mambo yote siku hizi tumeyapeleka yapo TAMISEMI. Lakini hata wao wenyewe Halmashauri hawana nguvu ya kuweza kuhimili migogoro iliyopo katika maeneo mbalimbali si tu katika Jimbo langu tu lakini naamini hata katika maeneo mengine yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho anieleze maeneo haya niliyoyataja atasaidia vipi ili wale wafugaji watengewe maeneo ya malisho na ili waondokane na vurugu za kugombana na wakulima, jambo ambalo litasaidia sana na watafanya shughuli zao kwa uhakika na hakutakuwa na mwingiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya ukarabati wa majosho. Kwa kweli kama nilivyoeleza kwamba sekta hii imetupwa mkono sana. Tunaomba ng'ombe, mbuzi au kondoo pamoja na mambo yote ya kupata malisho bora lakini anahitaji kwenda kuogeshwa kwa muda fulani. Wakati ule nakumbuka ilikuwa ni miezi mitatu mitatu lakini sasa ng'ombe wanaweza wakapita muda wote hawapati kwenda kuogeshwa kwenye majosho kwa sababu hakuna majosho. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu anieleze katika maeneo hayo ambayo ni muhimu sana kwamba Wizara hii ya Mifugo inafikiriaje kuwapelekea wale wafugaji wapate majosho na wafugaji wako tayari kwamba wapo wanafuga lakini wanahitaji majosho na majosho hayapatikani.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uhaba wa malambo, nimeeleza kwamba Mikoa yetu na hasa Mkoa wa Singida ni mkame sana na tunategemea mvua za kubahatisha lakini hatuna jinsi nyingine, ni kutegemea yale maji ya Mungu ili nayo yaendelee kuwa hai. Vinginevyo tunafikia wakati kwamba ng'ombe wanafika kiangazi wakati maji yakipungua basi na ng'ombe nao wanaanza kupoteza maisha. Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo langu wanategemea shughuli hii mbadala, shughuli ya mifugo kwa sababu mifugo tunategemea kwa shughuli mbalimbali. Tunapoambiwa michango ya ujenzi wa shule wananchi wanauza mifugo, wanapeleka hela kwenda kujenga shule, wanapoambiwa kuchangia ujenzi wa zahanati wanauza wanachangia. Sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu anihakikishie kama maeneo haya yote niliyoyataja hatujawa na lambo. Nimeona hapa amezungumzia Ulemo na amezungumzia na sehemu nyingine huko, lakini naomba sana hayo maeneo mengine niliyoyataja nayo yaweze kupatiwa malambo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumizie juu ya minada. Minada wenzangu wamelalamika sana na wamesema pengine zao hili la mifugo hasa ng'ombe wanapokwenda kule mnadani basi wathaminishwe kutokana na zile kilo zake alizonazo ng'ombe. Lakini wakati tukingoja labda hayo yatakapofikia mimi Jimboni kwangu tulikuwa na minada ambayo ilikuwa inafanya kazi vizuri sana pamoja na hawa wachuuzi walikuja kwa wakati na wakanunua ng'ombe. Walisaidia sana kuweza kumrahisishia mwananchi kuweza kupeleka ng'ombe wake; anajua siku ya mnada ni tarehe fulani akipeleka mfugo wake anakwenda kupata fedha na kutatua matatizo yake. Nina minada ambayo ilijengwa, mimi mwenyewe nazaliwa niliikuta ile minada lakini hadi hivi sasa haijafanyiwa ukarabati. Mnada kama wa Kiele, mnada wa Igumo ambao ndio Kiomboi, mnada wa Kigaa upo Luono, mnada wa Malendi, mnada wa Mgongo, mnada wa Mntekente, mnada wa Urugu na mnada wa Usule na minada hii ilijengwa kwa Kanda na kwamba kila Kanda ilikuwa inakusanya Kata mbili au Kata tatu.

Sasa ili tuwawezeshe wananchi wakati tunangoja pengine itakuja hiyo neema ya Mungu kwamba labda tutafikia wakati tutakapo kuwa na ng'ombe wa kisasa wataokwenda kuuzwa kwa kilo, ninaomba sana Waziri akijibu hoja anieleze kama hii minada wataifanyia ukarabati katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie juu ya viwanda vya usindikaji wa nyama. Kutokana na wingi wa mifugo tuliyonayo hasa kwa Mkoa wa Singida, hapa wenzetu Dodoma wanacho kiwanda cha kuchinjia wanyama, lakini sisi hatuna hata hicho kiwanda, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie masuala haya muhimu sana.

Atuangalie sisi watu wa Singida kwa sababu nayo itarahisisha na itamrahisishia mwananchi na mfugaji wa Singida kwa kuweza kuwa na uhakika kwamba kukiwa na kiwanda hicho pengine hata wanaweza wakachagua na wakaona umuhimu wa kupeleka mazo yao ya mifugo wakayapeleka pale na kuwa na uhakika wa kufanya mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda uliobakia kwa kweli hata ningemtaka msemaji wa haraka sana usingeweza kutosha. Kwa hiyo, jioni tukirudi wafauatao wajiandae: Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman na Mheshimiwa Lucas Selelii, ndiyo watakuwa wasemaji wetu wa jioni kabla hatujawaita watoa hoja.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**Majadiliano Yanaendelea**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge Mchana, nilikuwa nimewataja wafuatao kuwa ndio wachangiaji wetu katika kipindi hiki cha Jioni: Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Mheshimiwa Lucas Selelii. Sasa namwita Mheshimiwa Beatrice.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Hakika nilikuwa nikose Wizara zote kuchangia, lakini hii ingekuwa habari nyingine ningekosa. Aidha, nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Diallo, Mheshimiwa Dr. Mlingwa, Naibu Waziri wake na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, Kilindi ina takriban idadi ya watu 160,000. Kati ya hao, kuna Makabila: Wanguu, Wazigua, Wakamba, Wamasai, Wakaguru na ndugu zetu Wameru, Wachaga na Wapare ambao wamejiunga nasi hivi karibuni. Nimetaja hivyo, kwa sababu nataka kusema kwamba dhana ya kufikiria kwamba wafugaji ni Wamasai tu, Kilindi haipo, wapo na hawa makabila mengine pia ni wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu tuna jumla ya ng'ombe 125,376, tuna mbuzi 84,884, kondoo 20,532, kuku 148,637. Kwa ajili ya muda, nguruwe pia na bata tunao. Kwa hiyo, nataka kusema Kilindi kwa kweli katika suala la ufugaji, tuko mstari wa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali hususan hii Awamu ya Nne ambayo mimi ndio nimeikuta na kufanya nayo kazi kwa karibu, kwa kutambua kwamba iko sekta ya wafugaji. Hii ilidhihirishwa wazi kwa kuandaa semina kubwa ya wadau wa mifugo ambayo ilifanyika hapa Dodoma na mimi niliweza kufika pamoja na wajumbe wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na mafanikio hayo, bado kuna matatizo, ndio maana nimesema sekta hii ni muhimu sana kwangu. Matatizo hayo mimi naona yanaanzia Wizarani kwenyewe. Kwa wale ambao mmepata bahati ya kutembelea Wizara ya Mifugo, tofauti na Wizara zingine, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, nikifika pale Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, ile heka heka na shughuli na watu na harakati, vicheko, ni tofauti. Ile Wizara ukifika tu yaani unajikuta umenyong'onyea. Mazingira tu, utaona tu ng'ombe pale, sijui kuna *hey* kidogo! Yaani hata yale mazingira hayaonyeshi hamasa kwamba hii ni Sekta yenye umuhimu ndani ya nchi yetu. Kwa wale ambao hamjafika, jaribuni kufika, kwa kweli mtaiona hiyo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kinachoshangaza hapa tumepata *RVF*, nyama choma ikapotea, kila mtu alikuwa ananyong'onyea, mabaa yanakosa pesa, kila mtu anataka nyama choma. Wale wanaowezesha ile nyama choma kuwepo, kwa nini hawathaminiwi? Kwa kweli inasikitisha. Mimi ambaye natoka kwenye jamii ya wafugaji, kwa kweli ninaona kabisa tofauti kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilindi ina tatizo la malisho. Tatizo lenyewe ni dogo, lakini naomba niseme muda unavyozidi kwenda tunaliangalia linakua, itakuwa ni habari

tofauti. Tuna wakulima na wafugaji. Kweli tulikuwa na mradi wa *HIA* ambao ulikuwa umetenga maeneo ya malisho na kilimo, nadhani ni Wilaya chache sana ambazo zimepata bahati ya kuwa na mradi wa aina hiyo, mimi nauheshimu. Lakini kwa wakati ule ulikuwa mzuri sana, miaka imebadilika, watoto wamekuwa watu wazima, wajukuu wamekuwa na miji yao, mifugo na maeneo ya kilimo vimeongezeka. Sasa pale ndio unapoona mradi huu kwa sasa hivi kidogo unaleta utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nilikuwa naangalia hii Sera ya Kilimo, nimeikuta kwenye *Pigeon Hole*. Hapa inazungumzia , *Constraints to Livestock Development in* Tanzania. Naomba ninukuu; *"the main cause of a problem of land tenure system, water and pasture resources is lack of proper arrangement to allocate land and give ownership of raising areas according to traditional or legal procedure"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tayari imepitwa na wakati, tayari ile sheria ilikwisharekebishwa, suala hili sasa hivi linashughulikiwa. Kinachoshindikana, wenzetu wa Ardhi wanasema hakuna fedha. Kama kweli tunawapa kipaumbele hawa wafugaji, basi lipewe kipaumbele na hili. Naomba sana haya maeneo yaweze kupimwa kwa sababu kama pale Kilindi naona viongozi wengi wanatangaza ,"watu mtoke huko Kaskazini, nendeni Kilindi kuna ardhi". Ardhi iko wapi? Sisi wenyewe tunanyang'anyana! Nadhani huu upimaji ukifanyika, maeneo haya yakagawanywa kwa utaratibu, nina hakika kabisa kwamba tatizo hili litakuwa limeondoka. Tusingoje liwe baya sana. Waziri Mkuu, anatoka jamii ya wafugaji, na yeye mwenyewe ni mfugaji na anaelewa hili, basi naomba anisikie na aweze kuchukua hatua za haraka ili tusije tukakaribisha mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni ufugaji duni. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alisema katika moja ya hotuba zake, na hapa namnukuu: "unakuta mfugaji kakonda na mfugo wenyewe umekonda". Hii ni kweli kabisa, kutokana na kutumia ufugaji wa kizamani, kule kwetu unakuta mtu ana ng'ombe wengi, lakini anazunguka wakati wote.

Wiki iliyopita nilikuwa natoka Kilindi nikija Bungeni, nikapita hii njia ya kati kati, nikakuta mtu ana mifugo, ana mke na watoto, nadhani zilikuwa familia kama tatu au nne. Wanalala nje porini, wanavyokula havieleweki, walivyovaa havieleweki, baridi watoto wanatetemeka hata shule hawaendi, lakini wana ng'ombe takriban elfu nne na kitu. Sasa jamani huu ufugaji wa kisasa Wizara mnasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tatizo lingine ni elimu duni kwa wafugaji. Ni kweli kabisa mambo mengine tungeweza kuhamasisha wafugaji wakafanya. Kwa mfano, ujenzi wa malambo, majosho na mambo mengine kama hayo. Lakini elimu yao ni duni. Muelewe kwamba mtu anaanza kuchunga akiwa bado mdogo, anaendelea kuchunga, shule haendi, hapati elimu ile ambayo inatakiwa kupatikana hususan naongelea hapa elimu ya ufugaji.

Kuna wafugaji wakubwa na hata humu ndani tumo. Hebu tuondokane na yale mambo ya zamani, maana zamani kiongozi mwadilifu ni yule ambaye ni maskini, yule ambaye amechoka choka, ndio anaonekana, "yule kiongozi safi sana". Hayo yamepitwa

na wakati jamani! Kama tunaweza kuwa na vitu ambavyo tukaonyesha mfano sisi tunaosafiri itasaidia sana, maana unaposafiri unakutana na wengine kwenye njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nampenda sana Rais wa Uganda nilivyokuwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki, ana maranchi kibao, tena ya kila aina na ya kisasa na wala hayaonei aibu. Sasa mimi naomba wale ambao tumo humu ndani na wengine walioko nje, iwe Serikalini au kwenye Sekta binafsi, basi kupunguza ile gharama ya kupata hela za wafadhili kwenda kuwaelimisha wale watu, maana wataalamu hawana hela, hawana vitendea kazi, basi sisi wenyewe tuwe tunaandaa programu ambazo ni za bei nafuu ambazo Halmashauri inaweza ikamudu, ikaleta wafugaji wakajifunza kutoka kwenu kwa sababu nina hakika wengine mmejiweka vizuri katika eneo hilo.

Kwa hiyo, naomba sana hapa tutakapowaelimisha hawa watu ufugaji wa kisasa, ufugaji unaoeleweka, mambo gani yanatakiwa, nina hakika kabisa haya mambo yote ya kulalamikia Serikali, majosho, malambo sijui nin yatakwisha, tutafanya sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni uchache wa maduka ya pembejeo za mifugo. Kwa kweli haya maduka hayapo! Unakuta hata dawa za mifugo hakuna mpaka mtegemee hao maafisa wetu wa Kilimo ambao ndio hao wa Mifugo. Mimi naomba Serikali kama inaweza ikatusaidia, itoe mikopo kwa Sekta binafsi ili waweze kufungua maduka, waweze kutoa huduma hiyo.

Lakini, vilevile Serikali inaweza ikatusaidia kwa kuendelea kutoa hamasa kwa watu wenye uwezo wa kufungua maduka hayo wakiwaeleza umuhimu wao. Kwa kweli mimi Kilindi nikiangalia, sijui labda kwa sababu ndani ndani sana labda sijafika, lakini sijawahi kuona duka la aina hiyo. Sasa hii huduma badala ya kuelemea kwenye Serikali, tupate hawa watu waweze kufanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni ukosefu wa soko la uhakika la mazao haya ya mifugo. Kwa kweli tunayo minada ambayo inazunguka, leo iko kijiji hiki, kesho iko kijiji kile. Lakini ile minada ukiangalia faida ni ndogo sana inayopatikana na haithaminiki wala haimletei yule mfugaji mabadiliko yoyote. Kwa kweli mimi ninaomba Serikali itusaidie kutafuta masoko kama ambavyo inasaidia kwenye sekta nyingine, basi itusaidie kutafuta masoko.

Najua wapo Watanzania, kwa mfano, ndugu yangu Taji Mazala wa hapa Dodoma, wananunua mifugo hata kule kwangu na kadhalika lakini kwa kiwango kidogo sana. Sasa mimi naomba msaidie kutafuta masoko huko nje kama wengine walivyotangulia kusema angalau na sisi tuweze kuona manufaa ya mazao haya ya mifugo.

Wengi wameongea, wameeleza manufaa yake na jinsi ambavyo inachangia kwenye uchumi, lakini pia kwenye mabadiliko ya wananchi wenyewe. Kwa hiyo, mimi naomba sana, ikiwa tunaweza tukatenga maeneo kwa ajili ya wanyamapori, sijui nini,

Ngorongoro, tukatenga haya maeneo ya *hunting blocks*, basi tutenge na maeneo kwenye upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameingia, nilikuwa namwomba kwa kweli asaidie tatizo hili kwa sababu yeye ni jamii ya wafugaji na anaelewa, kwa hiyo, tuweze kuwasaidia watu hawa kwa haraka. Wenyewe wananiambia "mama ile kasi mpya unasema iko wapi?". Lakini naamini kwa kuwa na Waziri Mkuu kama Mheshimiwa Lowassa, mambo yatajipa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niombe majibu ya tofauti leo kutoka kwa Waziri. Jamani haya majibu ya vuteni subira, subira, wananchi wamevuta subira, sasa hivi wanatuona Wabunge waongo hususan mimi naonekana muongo.

Hebu tupate majibu kidogo *concrete*, kwamba hili litafanyika wakati fulani, hili tumefanya, hili tutakusudia kufanya labda katika kipindi fulani. Haya majibu ya wavute subira, tunafanya, tunafanya, 2010 itafika ndugu zangu, zile kura nitazikosa na hakuna litakalokuwa limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa kuhitimisha, nimwombe Waziri na Naibu Waziri, wakipata muda, basi watembelee Kilindi. Wako wafugaji wengi hata kwenye *statistics* sioni sana habari za Kilindi, lakini nawahakikishia wafugaji wengi sana wako Kilindi na karibu asilimia 47 na zaidi ni wafugaji. Kwa hiyo, naomba sana niwakaribishe muweze kutembelea kwa wakati wenu.

Baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba nirejee tena kilio hiki, najua Kilindi mmenisikia, nimeleta habari zenu kama mnanisikiliza, sasa kazi kwa Serikali na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana, naunga mkono hoja. Nashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa fursa ili nichangie kwenye Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo, Wizara muhimu sana. Nianze tu kuwapongeza Waziri na timu yake yote, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine kwa kutuletea hotuba nzuri sana ambayo ina maelezo mengi, *data* nyingi ambazo ukiziangalia unaweza kuhisi kuwa imeandaliwa na watu ambao kweli wamekwenda shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niseme kidogo tu katika masuala ya mifugo. Kwanza, niseme kuwa kuna hoja nyingi tunazowajengea wananchi, lakini sidhani kama tunawaelimisha.

Kwanza, mimi nakubaliana na hoja ambayo wengi wamesema hapa kwamba watu wetu wanachunga, hawafugi kwa sababu mimi siamini kuwa mtu anaweza kufuga ng'ombe 6,000, haiwezekani. Lakini anachunga ng'ombe 6,000 kwa sababu anawaweka

msituni, anaweka watu wawili, hata ukiwaweka, basi inakuwa kazi kubwa kujua kuwa ng'ombe wake ni yupi na yupi. Lakini mtu anayefuga, anawajua ng'ombe wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni ipi? Hoja ni kuwa watu wapunguze kuweka ng'ombe wengi au kuwa na mifugo mingi na badala yake waweke kidogo ambao wataweza kuwamiliki. Sasa tungejiuliza, hivi hii elimu inawafikia?

Mimi sina hakika kuwa wale wafugaji wote walioko kule Ihefu na sehemu zingine za ndani ndani wanapata maarifa haya ambayo yanawafanya wao wabadilike. Kwa sababu ukisema imesemwa Bungeni, kuna watu hawasikilizi Bunge, ukisema umeandika kwenye gazeti, kuna watu hawasomi magazeti. Sasa mimi nafikiri Wizara ingefanya kwa makusudi kabisa pamoja na kuwa ni gharama, lakini wangeandaa timu ikaenda kwenye sehemu za wafugaji, wakafanya utoaji huu wa taaluma. Watu wakielewa, naamini wanaweza kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hata mimi ningejiuliza suala la mbolea hii ya samadi ambayo inatokana na wanyama, hivi Wizara ina takwimu gani kuhakikisha ni kiwango gani cha mbolea hii kinapatikana na kinasaidia vipi katika kurutubisha ardhi yetu tunayotumia katika masuala ya kilimo? Sidhani kama jambo hilo linafanyika. Sasa ikiwa hilo halifanyiki basi nahisi nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa niliulizie au nilisemee ni suala la biashara hii ya nyama. Moja katika kitu ambacho nchi nyingi leo zinaneemeka nacho ni suala la biashara ya nyama. Wanauzwa wanyama wakiwa hai, lakini pia inauzwa nyama yenyewe ambayo inapelekwa. Nchi za Asia kama India na nchi nyingine zinapata soko kubwa tu Uarabuni. Thamani ya mbuzi mmoja Uarabuni ni *riale* za Oman zisizopungua 80 ambazo ukiangalia hapa zinaweza zikanunua mbuzi karibu 20. Sasa inaonekana hatufanyi kazi kubwa katika kuhakikisha kuwa tunapata soko kwa ajili ya wafugaji wetu.

Hii ni kazi ya Wizara kwa sababu mwananchi hawezi akaona umuhimu wa kitu kama hakupata msukumo. Kweli tumeona hatua zinaendelea sasa hivi, watu wanafungua mabucha haya, wanafanya hiyo *packing* ya nyama. Lakini, je, kama Wizara tunachakarika vipi katika kuhakikisha kuwa tuna-*win* masoko ya mahali pengine? Kwa sababu ushindani wa biashara sasa hivi ni mkubwa katika dunia nzima na ubora wa bidhaa ndio unao-*win* soko, siyo kuwa tunapeleka nyama tu, lakini tupeleke nyama ambayo ina kiwango na ili iwe na kiwango, lazima tuisimamie. Sasa hili ni jukumu la Wizara kuhakikisha kuwa wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watafiti wanasema katika nchi yetu tuna ng'ombe milioni 18.5, tuna mbuzi milioni 13.1, tuna kondoo milioni 3.6. Hii ni nchi ya tatu ukiondoa Somalia na Sudan katika Afrika nzima. Sasa kama tuna wanyama hawa wengi, mimi ningependa niulizie kidogo tu au nisemee kidogo biashara hii ya ngozi.

Katika miaka mitatu iliyopita, 2004 - 2006, kila mwaka karibu ngozi milioni 6 zilipatikana na ziliuzwa. Lakini pesa zinazopatikana zinatofautiana sana na wenzetu

wenye kuuza ngozi kama hizo. Kwa mfano, ngozi zote hizo kama ukiziuza katika soko zingeweza kuleta bilioni 50. Lakini zinaleta bilioni 50 kwa sababu ngozi hiyo hiyo ambayo imeandaliwa vizuri inayotoka nchi ya Rwanda inauzwa shilingi 20,000/= kwenye soko.

Ngozi hiyo hiyo ambayo imeandaliwa vizuri inayotoka Sudani inauzwa shilingi 12,000/= kwenye soko na ngozi hiyo hiyo ambayo inatoka Tanzania inauzwa shilingi 8,000/=. Ngozi ya Tanzania inauzwa shilingi 8,000/= kwa sababu ya ukaushaji mbaya, na ukaushaji mbaya unatokea kwa sababu inaonekana hakuna mafunzo maalumu yanayoandaliwa na Wizara kusimamia biashara hii.

Tukiwaachia watu wetu tu, wala hatutafika mbali kwa sababu hulka za watu wetu tunawajua, anaona ngozi, akishaiweka juani, yamekwisha yake yeye. Lakini sidhani kama ni hivyo kwa sababu elimu yoyote ile inahitaji maelekezo, inahitaji usimamizi. Tukisimamia vizuri, mimi naamini tutafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngozi hizo milioni 6 kama zikiuzwa kwa bei inayotakiwa kama zingekuwa *processed* vizuri, tungeweza kupata bilioni 90 badala ya bilioni 50. Nini sababu zake? Utakuta ng'ombe vijijini wanawekwa alama, anapigwa msumari moto kwenye mwili, yaani ile ngozi imeanza kutoboka kwa kuwekwa yeye alama. Sasa ile ngozi ukienda kuikausha kiwandani, ukiivuta kwa ajili ya kuikausha vizuri, inachanika, ikichanika, matokeo yake inashuka thamani. Hata hili basi, maana mimi nahisi ni dogo tu, ni suala la kuwaelimisha tu, badala ya kuweka alama kwenye ngozi, waweke alama kwenye sikio, haitaathirika ngozi, ikisimamiwa vizuri itaweza kuleta tija inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposimama hapa tunailaumu Wizara au tunaisema Wizara, msingi wake ni kuwa tunataka Wizara ichukue juhudi ya kuwasaidia wananchi ili waweze kupata faida. Nilipokuwa nazungumza na wenzangu mchana kama watatu, wanne au watano, Wabunge wakaniuliza, hivi wewe umejaribu kuangalia hata hii *nature* ya viatu tunavyovaa? Ni kweli, viatu vingi tunavyovaa ni vya *plastic*, viatu ambavyo vinafanywa kwa vitu vya ajabu ajabu kutoka nchi nyingine.

Mimi naamini, kulingana na kiwango cha wanyama tulichonacho kama Serikali itajaribu kuwawezesha Watanzania wazawa wakaweza kupata mtaji wa kuanzisha kiwanda cha viatu kimoja tu hapa Tanzania, lakini kikawa kiwanda cha kisasa ambacho kinazalisha viatu, basi neema kubwa watapata Watanzania. Ajira itapatikana kwa wafanyakazi, lakini pia hata *quality* ya viatu itapatikana. Leo ukienda nchi za nje ukinunua viatu, ukiangalia viatu tunavyoweza kununua hapa na ukipewa bei ya viatu kwa wenzetu unaweza ukashangaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda dukani mara moja, nilipata tatizo mguuni, nilikuwa siwezi kuvaa kiatu cha *boot*. Nilikuwa *London* katika mtaa mmoja, nikaenda kuuliza kiatu, niliambiwa bei ya *sandals* pale paundi za Kiingereza 242, hizi ni zaidi ya 600,000 za Tanzania. Sasa huyu ni Mtanzania gani mwenye akili atatoa shilingi 600,000 anunue *sandals*, hawezi! Nikawaambia basi acha iwe itakavyokuwa, lakini mimi sinunui.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yote haya yanaonyesha kuwa kitu kikiwa kizuri, kina thamani. Sisi tuna uzoefu, kule kwetu Zanzibar kulikuwa na kiwanda cha ngozi na viatu kikizalisha viatu vizuri tu. Hapa Tanzania tulikuwa na kiwanda cha Bora, hapa Dodoma palikuwa na tawi la Bora likiuza viatu vizuri.

Ni kweli tunajitoa kwenye biashara kwamba Serikali isifanye, iwawezeshe watu wafanye, kwa sababu ukiwawezesha watu wakafanya maana yake, inayofanya kwa mlango wa nyuma ni ile Serikali kwa ajili ya faida ya watu wake. Lakini pia ikiwa ngozi ukiziuza nje, zinaleta mikwara ya namna fulani, mara bei inanguka, mara hivi…! Ukiweza kuuza ndani, utaweza kupata faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo haya tunayasema kwa lengo la kuwasaidia wananchi ili wafaidike. Mimi naamini hili likitokea, watatokea Wabunge humu humu ndani watashiriki katika mradi huu wa kuwekeza.

Mimi naamini kuwa tukifanya hivyo, Wabunge watatokeza kushiriki katika mradi huo na matokeo yake faida itapatikana kwa Wabunge wenzetu, kwa Watanzania wenzetu na kodi itarudi katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kitu chochote kinachofanyika ndani ya nchi, mwisho wa siku ikiwa unalipa kodi, basi kodi ile inawasaidia wote hata wale waliokuwa hawakufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu maneno yangu ya mwisho ninayopenda kuwambie ni kuwa wafugaji wapewe elimu. Nimekuwa Mbeya, nikakuta mtu amepelekewa askari kundi zima kwenda kukamata ng'ombe wake Ihefu kuwaleta barabarani na walipofika barabarani, akaambiwa awapeleke Lindi au Kilwa.

Kinachofanyika ni kuwa auze ng'ombe, lazima auze ng'ombe. Ng'ombe amuuze kwa bei aliyopangiwa pale isiyopungua shilingi 100,000/=. Wanunuzi wamelala kwenye magari wanasubiri saa nne au tano usiku wanamwambia ,"kama unataka, mimi nitanunua kwa bei ya shilingi 70,000/= au 60,000/=" na amekwishapewa muda wa kukaa pale awaondoe ng'ombe, anauza tu!

Hivi kweli Wizara hamuwezi kuwasaidia hata ule usafiri tu wa wale ng'ombe kutoka kule mlikowahamisha mpaka mnakotaka kuwapeleka? Vitu kama hivi tunaruhusu malalamiko ya watu bure tu na ni kitu tunachokiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa, naomba watu wa Wizara watilie maanani haya na sina maana ya kujibiwa, lakini majibu yangu ninayoyataka, wajibiwe Watanzania kwa vitendo ili faida iliyokusudiwa ipatikane. Nakushukuru sana! *(Makofi)*

**MHE. LUCAS. L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa msemaji wa mwisho. Sekta ya Mifugo ni muhimu sana kwa sababu inatupatia faida nyingi. Inatupatia mbolea, maziwa, ngozi, nyama na vilevile inatupatia fedha. Lakini katika maeneo ya wafugaji kuna kitu kingine ambacho kinaongezeka zaidi ya hayo, nacho ni kukuongezea hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwa wafugaji au mkulima yeyote mfugaji, ana hadhi kubwa kuliko mtu wa kawaida ambaye hawezi kufuga hata kuku. Kwa wenzangu wamasai, mwenye ng'ombe wengi ana sauti zaidi kuliko mtu mwenye ng'ombe wachache.

Kwa hiyo, sekta ya mifugo ni muhimu sana. Mimi inanisikitisha sana Serikali kuendelea kuiita sekta ndogo. Mimi naamini sekta hii tuibadilishe, tuienzi, tuiite sekta pekee ya mifugo. Tukiipa hadhi hiyo, basi tutaiheshimu, na hata mchango wake wa mapato utabadilika na itasaidia hata kuiongezea pesa Wizara hii. Katika Wizara ambazo zimepewa pesa kidogo sana ni Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo wakati inabeba sekta kubwa ya wananchi walio wengi huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ametueleza jinsi mifugo yetu ilivyo mingi. Ng'ombe tunao milioni 18, mbuzi milioni 12, kondoo milioni 3, kuku wengi tu! Ninaamini akiangalia hata wananchi walio wafugaji ni wengi sana kwa sababu mwananchi ambaye anapata mafanikio kwenye kilimo au anapata mafanikio yoyote mahali popote, basi fedha zake huwekeza kwenye mifugo. Kwa hiyo, jambo hili ni la muhimu sana likitiliwa maanani na Serikali katika kuinua pato la wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninapenda kushauri yafuatayo:- Kwanza, Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka sana kuweka mkakati kwa kushirikiana na sekta binafsi kufungua au kujenga Viwanda vya kusindika nyama katika mikoa ile yenye wafugaji. Lazima kila mkoa wenye wafugaji kuwe na kiwanda walau kimoja. Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Rukwa, Rukwa, Singida, Manyara, Arusha, Dodoma, ingestahili kabisa angalau kila mkoa kuwe na kiwanda kimoja cha kusindika nyama. Hii itasaidia kuongeza thamani ya zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mifugo yetu inauzwa kwa bei ya kutazama bei ya mnadani ya kilanguzi. Mfugo kama ng'ombe unasimama pale, wafanyabiashara wanashindana kwa bei ya kumwangalia. Mwenye shilingi 60,000/=, 50,000/= au 10,000/=, yule atakayeshinda ndiye atakayemchukua kama sadaka vile! Ni kwa sababu hatuna viwanda vya uhakika ambavyo vitanunua mifugo yetu kwa kupima. Kwa hiyo, la kwanza viwekwe viwanda ambavyo mifugo yetu itauzwa kwa bei nzuri yenye manufaa kwa wananchi, lakini vilevile itaongeza thamani ya mifugo kwa sababu tutakuwa na nyama ya kusindika ambayo itasafirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Wizara ya Mambo ye Nje, zitafute masoko nje. Tukiwaachia wananchi au sekta binafsi peke yake kutafuta masoko, hawawezi. Serikali inayo mawasiliano ya kutosha kutafuta soko nje kwa kupitia Wizara hizi na kwa kupitia Balozi zetu zilizoko nchi za nje.

Sasa hivi mifugo inayosafirishwa kwenda kwa mfano, *Comoro*, utakuta mfugo kama ng'ombe anasafirishwa aliye mzima. Nadhani kama ingesafirishwa nyama, tungeweza kufanya vizuri zaidi kama wenzetu wa Botswana wanavyofanya. Botswana ni

nchi ndogo, ina mifugo michache. Kama walivyotangulia kusema wengine, Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kuwa na mifugo mingi ikifuatiwa na Ethiopia na Sudani. Lakini Botswana ni ya kumi na mbili kama sijakosea kwa idadi ya mifugo. Lakini inaongoza kwa kusafirisha nyama katika Afrika. Ni kwa sababu wameweza kutafuta soko na wameweza kufungua viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kwa kushirikiana na Halmashauri zetu za Wilaya na kushirikiana na sekta binafsi, kila Wilaya ambayo ina mifugo, kuwe na machinjio ya kisasa. Sasa hivi mifugo yetu inachinjwa kizamani sana. Wakishachinjwa hata kuchunwa, hata kucharangwa, wanacharangwa kizamani sana. Hii inasababisha kukosekana kwa thamani ya kutosha, kukosekana kwa bei nzuri. Katika nchi hii kuna machinjio mazuri ya kisasa manne tu. Nchi yenye mifugo mingi namna hii, machinjio manne tu hayatoshi. Kwa hiyo, kila Halmashauri ishirikiane na sekta binafsi kujenga machinjio ya kisasa ambayo yatakuwa na manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne ningeshauri Wizara ya Mifugo kuzingatia ujenzi wa mabwawa na majosho. Nimeangalia katika kitabu hiki, sijaridhika sana na juu ya juhudi ambazo zitafanywa na Wizara ya Mifugo, kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa na malambo. Katika sekta ya kilimo kuna *ASDP*. Ningeshauri, kwa kutumia *ASDP* pale ambapo tunajenga mabwawa kwa ajili ya kilimo iende sambamba na ujenzi wa malambo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mafanikio yoyote ya kilimo kwa mkulima yeyote anayefanikisha kilimo kizuri cha kisasa ni yule anayetumia trekta, lakini kwa uwezo wetu, ni yule anayetumia jembe la kukokotwa na n'gombe. Kwa hali hiyo, ng'ombe ni mbia mzuri hata kwenye suala la kilimo. Kwa hiyo, ningeshauri ujenzi wa malambo, ujenzi wa mabwawa liwe ni suala la lazima katika maeneo yote ili kuwafanya wafugaji wasihame hame kufuata maji katika maeneo ya mbali, wayapate pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumekuwa na wito wa kujenga zahanati kila kijiji. Sasa sijui zinaitwa zahanati, sijui hospitali, sijui vinaitwa vituo, lakini vijengwe vituo angalau kila kata vya kuhudumia mifugo. Sijui *teminology* gani ambayo inatumika kwa mifugo. Kwa binadamu inaitwa zahanati. Kila kijiji kunakuwa na zahanati. Lakini kwa mifugo na wenyewe wana zahanati yao! Ukiangalia magonjwa yaliyoorodheshwa katika orodha ya Mheshimiwa Waziri, yako mengi kweli! Kuna mafua ya ndege, kuna ndigana, sijui kuna nini, watalaam wa kule vijijini mabwana mifugo kwanza hawatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaofanyakazi kuliko wengine ni hawa mabwana kilimo na wanakwenda kufanyakazi kwa ajili ya mifugo vile vile. Lakini laiti katika maeneo ya mifugo, mikoa ile yenye mifugo mingi, basi kila Kata kungekuwa na zahanati au kliniki ya mifugo ili mifugo iweze kupelekwa kutibiwa kama vile inavyokuwa sisi binadamu. Mnaweza kudhani ni kitu cha kichekesho lakini katika nchi za wenzetu zilizoendelea ni kitu cha kawaida kupeleka mifugo kwenye zahanati au kituo cha afya kwa ajili ya kutibiwa. Kwa hiyo, hili sikuliona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sikuliona kabisa kama kuna mpango huo. Sambamba na mpango huo, ningependa sana

hili liweze kuwepo, kila sehemu ambayo ina mifugo wengi angalau kila Kata kuwe na zahanati au kliniki ya kusaidia kutibia mifugo yetu.

La tano, nilisema wakati wa hotuba ya bajeti kwamba mara nyingi wenzetu wa nje wamekuwa na tabia ya kutufanya sisi kama eneo la kuleta kila kitu. Nikaomba Serikali ipige marufuku uagizaji wa kuku wa kutoka nje. Soko na mifugo tuliyonalo hapa ni mingi ya kutosha. Katika takwimu za Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake amesema kuku wa kienyeji peke yake, na hapa napenda kuwasifu wananchi wa Mikoa ya Singida, Shinyanga na Tabora kwa ufugaji wa kuku wa kienyeji. Ni milioni 30 kuku wa kienyeji peke yake! Kuku wa kisasa ni milioni 20, ukiweka kuku wa kienyeji na kuku wa kisasa unapata takribani kuku milioni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini bado tuendelee kuagiza kuku kutoka nje? Kwa nini Serikali ikubali kuagiza kuku kutoka mbali wakati tungeweza kuyalazimisha maduka makubwa ya humu nchini ya kanunua kuku hawa wa kienyeji? Tungeweza kuinua pato la wananchi wetu na ndiyo mkukuta. Wafugaji wengi wa kuku, mwanaume anaweza akafuga ng’ombe au mbuzi lakini wafugaji wengi wa kuku ni akina mama. Akina mama ndiyo walezi wa familia. Ukitaka kuinua familia unamwinua mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuinua familia unamuinua mwanamke! Tukipata soko zuri la kuku, hawa akina mama tutakuwa tumewasaidia sana kuondokana na matatizo madogo madogo na ingewafaa sana Serikali ikipiga marufuku kabisa. Kwanza kuku wa kienyeji ni watamu, hata kuwaangalia ni wazuri. Lakini hawa kuku wa kizungu wamesinzia, sijui wamechomwa nini, hawafai na ndiyo maana wanaleta matatizo ya magonjwa mbalimbali ambayo hatuyajui tiba zake. Kwa hiyo, naomba hili Serikali itamke bayana.

Katika nchi nyingine Serikali inapenda sana kulinda bidhaa za ndani. Lakini sisi ni wepesi sana kukubali kila kitu! Hata kuku! Hili Mheshimiwa Waziri atamke wazi kwamba kuanzia sasa kuku wa kuagizwa kutoka nje ni marufuku na nitamuunga mkono kabisa Mheshimiwa Waziri katika hili ili wananchi wetu waweze kufuga kuku wa kienyeji ambao ni rahisi kufugika na ni sehemu nzuri sana ya kuwapatia pato lao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongezea lingine katika ushauri juu ya mafunzo kwa bwana mifugo. Bwana mifugo vijijini ni wachache, sisi wote tunatoka katika maeneo ya wafugaji, ni wachache sana. Sijui kuna vyuo vingapi ambavyo vinafundisha mabwana mifugo. Kama kweli tumedhamiria kuinua sekta hii ya mifugo, basi ni vizuri ikaanzisha kwa makusudi mafunzo ili tuwe na mabwana mifugo wa kutosha katika maeneo yote ambayo kuna wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina bahati kubwa sana, Waziri wake anatoka kwenye mifugo, ni mfugaji toka azaliwe, Naibu wake anatoka kwenye mifugo, ni mfugaji toka azaliwe na Waziri Mkuu, ni mfugaji toka azaliwe. Lakini bado mambo hayaendi! Bado fedha ni kidogo. Kwa nini? Hivi kuna nini? Mimi nilidhani Waziri amekuwa wa Mifugo ni mfugaji, Naibu wa Mifugo, Waziri Mkuu wote ni wafugaji, hata

Katibu Mkuu ni mfugaji, nikajua sasa hapa wafugaji tumeokoka. Jamani kwa kweli ni bahati iliyoje, lakini bado hatujaitumia. *(Makofi)*

Lakini hata ukiangalia humu ndani, Wabunge wengi ni wafugaji. Mikoa yote iliyotajwa, mimi nashangaa, hata Tanga kwa ndugu zetu Wazigua nao wanafuga. Nimeshangaa! Kwa hiyo, ni jambo la mtambuka. Kama kweli tutazingatia itatusaidia kwa kweli kuondokana na umaskini wa kipato, kama kweli tutaamua kufunga kwa tija. *(Makofi)*

Kule kwetu kwa wafugaji mfugaji unaitwa Savii, yaani mwenye mifugo mingi anabadilisha hata jina anaitwa Nsavii. Yule ambaye hana mifugo haieleweki anakuwa kama mzaramo tu hivi kwa sababu hana kitu. Lakini mfugaji ana hadhi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa hadhi hii iende sawa sawa hata kwenye Wizara kwa sababu wafugaji wanabadilisha hata jina. Mimi nashangaa hawa akina yahe wanasema tupunguze mifugo, tutapunguza kwa bei hii. Nyie kwa sababu hamfugi, ndiyo maana mnasema tupunguze mifugo. Hamjui thamani ya mifugo! Kama una mifugo mingi maana yake una thamani kubwa katika jamii. Waulize Wamasai, Wasukuma, Wagogo na jamaa zetu wa Mkoa wa Mara, mfugaji una thamani! Kwa hiyo, mnawaambia punguza mifugo! Apeleke wapi? Bei yenyewe Sh. 50,000, Sh. 60,000, mwisho haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nashauri, kwa kweli tuithamini mifugo. Tukishaithamini, basi hata Wizara na yenyewe itaona imethaminika. Kwa kweli hata Wizara ibadilike kwa kupenda kazi yake ambayo imepewa na kuchunga wananchi ambao ni wafugaji wazuri. Kama itabadilika, itawasukuma, hawa wafugaji wetu wataweza kufanya vizuri sana kama hawa wenzetu wa Botswana wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nawatakia kila la kheri wafugaji wenzangu katika kazi nzito hii. Waziri Mkuu, nakuomba utoe agizo leo, kuku wakiagizwa kutoka nje wapigwe marufuku. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunashukuru sana. Wewe mfugaji huwezi kuendelea tu. Sasa tutamwita mfugaji mwingine atoe maelezo yake hapa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri. Nashauri yafuatayo:-

(i) Ili nyama iweze kupata soko zuri lazima Serikali itoe ruzuku ya kutosha kwa wafugaji na viwanda kwa ajili ya *export.* Nchi zilizoendelea zinatoa ruzuku kwa wakulima na wafugaji kwa hiyo kama hatufanyi hivyo hatuwezi kushindana kwenye soko la dunia.

(ii) Naomba Wizara ielewe ugonjwa wa *Rift Valley Fever* umekuwepo Kenya kwa muda mrefu na unalipuka kila mwaka kama *red eyes.* Sasa umeingia Tanzania,

tumepigana nao umepungua ama umeisha. Lazima tuendelee na chanjo na kuhakikisha kuwa ugonjwa unatokomea kabisa. Kenya unarudi kila mwaka tuhakikishe huku Tanzania haurudi.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa kifupi kwa mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiangalia Kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Mifugo nimegundua kwamba Kigoma haifahamiki hata kidogo kama inajihusisha na ufugaji. Lakini napenda nimhakikishie na ufugaji na tunao ng'ombe wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kasulu inao wafugaji wa ng'ombe wapatao 4,000 wakati Wilaya ya Kibondo inao wafugaji wenye ng'ombe zaidi ya 8,000. Kinachosikitisha badala ya kuwapa moyo hawa wafugaji kwa kuwajengea majosho ya mifugo yao, wanahamishwa kwa nguvu kutoka kwenye maeneo waliyozoea na hasa majani. Hawa wafugaji wa Kijiji cha Katoto Wilayani Kasulu na Kunkanda katika Wilaya ya Kibondo, mifugo yao imeanza kufa kutokana na kuhamishiwa kwenye maeneo ambayo majani yake si mazuri kwa wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Serikali kuwa ni kuwatoa wafugaji katika hifadhi ili kutoa mwanya ama kuzuia uharabifu wa mazingira, naiomba Serikali iangalie upya suala hili la wafugaji niliowataja ambao wanaishi pasipo na amani ikiwa ni pamoja na mifugo yao. Kama wanaweza kutengewa eneo walilolizoea kwa maelekezo ya kutokuvuka mpaka kwa eneo mimi nadhani wananchi hao watakuwa wametendewa haki katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Hai naomba mpokee pongezi na shukrani zao kwa kazi nzuri mnazofanya kwa kuanzia kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote hapo Wizarani hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kushauri mambo machache, kwanza dawa za mifugo; nashauri uwepo mpango maalumu wa kuhakikisha ruzuku ya dwa inawafaidisha wafugaji na sio wafanyabiashara.

Pili ni kuhusu majosho na malambo, naomba mje kule kwetu Hai kwa kushirikiana na watendaji wetu ili tuweze kupanga na kujenga majosho na malambo ya kutosheleza kwani idadi ya mifugo imeendelea kuongezeka sana.

Kuhusu masoko ya mazao ya mifugo, kuna kila sababu ya kuweka mipango ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya soko la mazao ya mifugo yaani ngozi, nyama, maziwa na bidhaa nyinginezo zitokanazo na mifugo kwani panapokuwepo na kuanguka kwa bei kuharibu sana hali za maisha ya wakulima, wafugaji hasa ndugu zangu Wamasai.

Tatu ni kuhusu milipuko ya magonjwa, nashuari tujiandae vema na mapema kwa ajili ya magonjwa ya mlipuko kwa maana ya kuwa na maabara zetu wenyewe kwani biashara ni vita hivyo kutegemea nchi zingine tunaweza kupata majibu yenye lengo la kutuharibia biashara nje ya nchi mfano *RVF* lazima tujifunze.

Nne, minada, naomba Wizara kwa kushirikiana na Halmshauri zetu kudhibiti uendeshaji wa minada yetu kwani panaweza kuwepo na udanganyifu mkubwa sana kwa watendaji wasiokuwa waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kufahamu ni nini kinachoendelea kwenye Kiwanda cha Ngozi kule Moshi kupitia Wizara hii pamoja na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwani ni muda mrefu umepita tangu kiwanda kuchukuliwa na mwekezaji ambaye amefanya ghala tu. Nini hatma yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeza na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu iboreshwe kwenye maeneo yaliyotengwa na wafugaji. Kwenye Jimbo la Songwe Wilayani Chunya wafugaji wametengewa maeneo ya Mbangala Juu kwa ufugaji. Maeneo hayo hayana miundombinu muhimu kama vile majosho na malambo ili wafugaji hao wasirejee mabondeni kwenye Ziwa Rukwa nashauri miundombinu husika ijengwe kwenye maeneo ambako wafugaji wamehamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji katika Jimbo la Songwe wapatiwe mafunzo ya ufugaji bora. Bonde la Songwe Wilayani Chunya kuna zaidi ya mifugo/wanyama 250,000 wanaochungwa kuzunguka Ziwa Rukwa. Uchungaji unaofanywa huko ni ule wa jadi. Naishauri Wizara ifanye mipango ya kuendesha mafunzo juu ya ufugaji bora.

Kuhusu ukosefu wa Wagani wa Maendeleo ya Mifugo, kwenye Jimbo la Songwe kuna Afisa mmoja tu anayeshughulikia maendeleo ya mifugo. Jimbo hilo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari za mraba 29,000 ni kubwa mno kwa Afisa mmoja. Nashauri waongezwe maafisa wawili kuhudumia jimbo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendea kazi kwa wagani, Afisa mmoja aliopo kwenye Jimbo la Songwe hana chombo cha kusafiria wakati akishughulikia suala la ufugaji. Nashauri Afisa huyo apatiwe pikipiki itakayomsaidia kutenda kazi yake. Naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa ya kuambukiza ya mifugo kuna Homa ya Bonge la Ufa uliikumba Tanzania na kusababisha vifo vya watu 139 na mifugo 50,000 hadi tarehe 16 Juni, 2007. Mifugo iliyokufa ni 50,000 ambapo wamo ng'ombe, mbuzi ambao ndio asilimia kubwa hivyo baadhi ya wafugaji wadogo wadogo wameathirika sana baada ya mifugo yao kufa hali ambayo imepelekea wafugaji wadogo wadogo kuwa maskini zaidi kuliko ilivyokuwa awali hvyo kwa vile kuna familia wamekufa baba au mama na mifugo yao asilimia kubwa tena wakiwa wafaguaji wadogo wadogo. Je,

Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha familia maskini zilizopoteza ng'ombe au mbuzi kwa vifo vya Homa ya Bonde la Ufa ili waweze kupambana na umaskini uliowakumba kwa homa hiyo ya mlipuko?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu katika nchi yetu kama Dodoma, Shinyanga kuna mifugo mingi, mabwawa na malambo hayatoshelezi katika kukidhi haja ya mifugo hiyo, hivyo Serikali ina mkakati gani wa kuongeza kuchimba mabwawa na malambo ili kukinga au kudhibiti vifo visitokee tena katika maeneo kama haya ya Dodoma na Shinyanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo kama wafugaji wanalazimika kuhama hama kutafuta malisho kwa mifugo yao. Hivyo Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuanzisha mashamba makubwa ya malisho ili kuinusuru mifugo kufa? Mifugo inaongeza ajira kwa wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wazifanyazo siku hadi siku licha ya mazingira ya kazi kuwa magumu kutokana na Bajeti yao kuwa finyu.

Aidha, ninawapongeze wote ambao kwa njia iwayo yote wamechangia katika uandaji wa Bajeti hii. Ni hotuba nzuri yenye kuleta matumaini ya maendeleo katika sekta ya maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa niaba yangu binafsi na wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo naomba nichangie katika maeneo haya yafuatayo:-

Moja, shamba la Mabuki, shamba hili lina muda mrefu sasa. Kusudi la msingi la kuanzishwa shamba hilo ilikuwa pamoja na sababu zingine, ilikuwa kuwabadilisha wafugaji wa maeneo ya jirani ya eneo hilo waweze kuwa wafugaji wa kisasa, waachane na ufugaji wa utaratibu wa uchugaji. Sina uhakika lengo hili limefikiwa kwa kiwango gani. Naipongeza Serikali kupitia shamba hili kufanikiwa kusambaza mitamba wa maziwa 3,863. Je, kati ya hao ni wangapi wamepelekwa Wilayani Kwimba na Misungwi kwa wananchi walio karibu na shamba hilo kila leo?

Pili, ombi langu shamba hilo lipunguzwe ili sehemu moja iendelee na shughuli zilizokusudiwa kwa nguvu zaidi. Maafisa Ugani wanaongezwe na wapewe maeneo ya kusimamia. Kila Afisa Ugani apimwe kwa maendeleo au mafanikio ya kazi yake.

Sehemu ya pili ya sehemu hiyo ikabidhiwe Wizara ya Miundombinu kwa mpango madhubuti wa kujenga Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa. Sababu za kuomba

Kiwanja hicho ni kwa kuwa Mabuki ni katikati ya Mwanza na Shinyanga. Miji hii inakua na ujenzi wa makazi ya watu unaongezeka haraka kutokana na idadi ya watu katika Mikoa hiyo ni kubwa. Ardhi wazi isiyohitajika fidia inazidi kukua. Nafikiri eneo hili likijengwa Kiwanja cha Ndege litasaidia sana kwa Miji hiyo miwili ya Shinyanga na Mwanza hasa kwa kuzingatia kuwa Kiwanja hicho kitakuwa cha manufaa kwa mazao ya mifugo mbalimbali kutokana na shughuli zitakazokuwa zikiendelea hapo mabuki na maeneo yanayozunguka eneo hilo kama Wilaya ya Misungwi, Kwimba, Maswa, Magu na Shinyanga Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuomba Serikali kupitia Wizara hii kama sasa inaweza kuanza kufikiria mpango wa kuwa na machinjio ya kisasa Hungumalwa. Hungumalwa kuna mnada mkubwa sana wa ng'ombe na ni mnada wa miaka mingi. Katika mnada huo kama kutajengwa machinjio ya kisasa, hii itasaidia kuongeza thamani ya ng'ombe wauzwao katika mnada au gulio hilo. Zoezi hili litatoa mafunzo kwa wafugaji umuhimu wa kuboresha mifugo yao. Nitashukuru sana kama Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atatoa maelezo ya haya yafuatayo:-

Moja, kutakuwa na athari zipi kwa malengo ya maendeleo ya mifugo iwapo eneo la Mabuki litamegwa kuacha nafasi ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa kitakachoweza kuhudumia Miji ya Mwanza, Shinyanga, Ngudu, Kwimba, Maswa na Magu pamoja na mbuga ya wanyama ya Serengeti kwa miaka mingi ijayo.

Pili, uwezekano wa kujenga machinjio ya kisasa Hungumalwa ili kuongeza thamani ya mifugo hususan ng'ombe, mbuzi na kadhalika ukizingatia ukweli kuwa Hungumalwa haiko mbali na Kiwanda cha Kusindika cha Shinyanga.

Tatu, uwezekano wa kuboresha huduma zitolewazo Mabuki kwa kufanya utaratibu bora zaidi wa kulifanya shamba hilo kuwa karibu zaidi na wananchi wafugaji wanaozunguka shamba hilo, kwa kuongeza Maafisa Ugani katika maeneo yanayozunguka shamba hilo wakihimizwa ufugaji bora na faida za utumiaji wa nyama na maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pokeeni pongezi kwa jinsi mnavyosimamia Wizara hii na kwa hotuba nzuri ambayo mmewasilisha leo, Mheshimiwa Anthony Diallo na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Pili ni kuhusu utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo. Waziri amesema ng'ombe watakaotambuliwa ni 20,000 na kwamba mifugo itakayouzwa minadani ni ambayo itakuwa imeandikishwa kwenye *register* ya Taifa ya takwimu za mifugo nchini.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii italeta urasimu mkubwa kwa mfugaji anapotaka kuuza ng'ombe wake?

(b) Kwa kuwa uanzishwaji wa Rejista ya Taifa ya Takwimu za Mifugo kunategemea sana utunzaji wa tathmini kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata na Wilaya, je, Wizara imejipanga vipi kuzishirikisha ngazi hizo?

Tatu, kwa kuwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni Wizara pana sana zenye kazi nyingi na maelekezo mengi, kwa nini Serikali bado inasita kuzitenganisha Idara ya Mifugo na Kilimo ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, Mji na Manispaa ili kuleta ufanisi?

Nne, ujenzi wa majosho na malambo, kasi ya ujenzi wa majosho na malambo bado ni mdogo sana, ni lini Serikali itatenga fedha kugharamia yafuatayo:-

(i) Ujenzi wa malambo vijiji vya Bugayabahya Mwandu I , Inonelwa na Mwakalumbi?

(ii) Ujenzi wa majosho vijiji vya Lubiga, Mwabuma na Mwabusahi?

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa inazungumzia jinsi gani wafugaji walivyoathiriwa wakati wa zoezi hili bila kufikiria pia na adha inayowapata wale ambao wako katika maeneo yanayopelekwa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida ieleweke kwamba katika Mikoa na Wilaya iliyoelekezwa mifugo hiyo ina wananchi ambao ni wakulima na hawana uzoefu wa mifugo. Iwapo wafugaji hao watakaa maeneo ambayo hawakupangiwa Serikali itachukua hatua gani?

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja hii. Baada ya hapo napenda kuipongeza sana Wizara kwa kuhamisha wafugaji toka eneo la oefu la Ihefu ili kuokoa mazingira na maji yaliyosababisha ukosefu mkubwa wa umeme mwaka jana. Baadhi ya mifugo hiyo imepelekwa Wilayani Chunya kwenye mbuga ya Shoga - Lualaje. Naiomba sana Wizara ipeleke kwa upendeleo fedha za kutosha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ili waweze kujenga malambo na majosho kwenye mbuga hiyo. Bila kufanya hivyo wafugaji hao watarudi Ihefu kuendelea kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka huu wa 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ya mifugo ni sekta nyeti na muhimu sana nchini mwetu, kwa kuwa nchi yetu ni maarufu kwa ufugaji na ni vema basi sekta hii kupewa kipaumbele ili wananchi wale wasiokuwa na shughuli nyingine mbadala sekta hii ndiyo inayoweza kuwapa mapato kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli na maisha yao kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua Mikoa yote ya nchi yetu inayo jamii ya wafugaji, aidha, ufugaji endelevu ama ufugaji wa asili mifugo inayofugwa iliyo na idadi kubwa kwa wafugaji ni kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, kuku na kadhalika vyote hivi nilivyovitaja vina tija kwa wananchi. Tukianzia ng'ombe, faida zake ni nyingi, ng'ombe anatumika kwa uzalishaji wa chakula (kilimo) na kadhalika kama mboga, maziwa na kutoa mbolea, mafuta na hivyo hivyo kwa mbuzi, kondoo na pengine punda pekee ambaye hutumika kwa kitoweo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa jinsi gani sekta hii haipewi kipaumbele hasa kwa kuwajali wafugaji hasa kwa kutenga fedha za dawa na maeneo ya malisho ili mifugo yao iwe endelevu kama ilivyo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida hasa Jimbo langu la Uchaguzi la Iramba Magharibi linao kwa kiwango kikubwa jamii ya wafugaji maeneo kama ya Kata ya Mtoa, Vijiji vya Msai, Mgela, Tyeme, Mesagi na vile vya Kata ya Mtekente na Urughu vijiji vya Msansao, Ujungu (kwa Mwanamajiku) Msombi Madalawa, Mayanzani, Masimba, Mlandala, Maeneo haya yanayo wafugaji wengi sana.

Matatizo yanayotukabili katika maeneo ni haya yafuatayo; hakuna *Vertenary* (Kituo cha Kitibu mifugo na dawa), hakuna majosho ya kuogeshea mifugo, kuna uhaba wa malambo ya maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo, maeneo ya malisho hayajatengwa hivyo kusababisha misuguano ya mara kwa mara na wakulima na Maafisa Ugani hawatoshi, wanahitajika kwa ushauri wa mara kwa mara kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mifugo hasa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku ni mazao mbadala Jimboni kwangu Iramba Magharibi. Naomba Mheshimiwa Waziri aelekeze mikakati ya kulinda na kuboresha sekta hii muhimu Jimboni kwangu na huduma ya mnada iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri aboresha minada yote ya Jimboni kwangu kwa kujenga yale maboma ya kuhifadhia mifugo siku ya mnada ya Kiele, Igumo, (Kiomboi), Kigaa (Luono) Mgongo (Shelui) Mlekente, Malendi, Urughu na Usue.

Mheshimiwa Naibu Spika, minada hii ni ya siku nyingi sana na ni minada ambayo ilitengwa kwa kanda ili ikusanye wafugaji wote kwa ajili ya wafugaji kuuza mazao yao (mifugo).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kufanya majumuisho anieleze katika mwaka huu wa fedha minada hiyo itakarabatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kituo cha Maksai, Mkulu. Jimboni kwangu Iramba Magharibi kilijengwa kituo cha Maksai katika kijiji cha Mkulu, tangu ujenzi wa kituo hiki kukamilika hadi sasa hakijaanza kufanya kazi, majengo yanaharibika bila fedha iliyowekezwa kufanya kazi. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati akifanya majumuisho anieleze hatma ya kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Kusindika nyama, kwa kuwa sekta hii ni muhimu hasa katika kusaidia kuondoa umaskini, naomba Wizara ihamasishe wawekezaji ili kuja kuanzisha kiwanda cha kusindika nyama Mkoani Singida ili soko la mifugo liongezeke na kutoa fursa ya zao hilo la ng'ombe kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuweza kuhudhuria katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe, Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vizuri. Ufugaji bora pamoja na viwanda vya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mifugo kunaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Hivyo ni vyema kwa Serikali kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji pamoja na kuweka viwanda katika maeneo yenye mifugo mingi ili kuongeza pato la wafugaji na Pato la Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kutenga maeneo maalumu kwa wafugaji halikufanikiwa kama lilivyotegemewa na kusababisha wafugaji kuhama hama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine na kupelekea uharibifu wa mazingira pamoja na usambazaji wa magonjwa mbalimbali ya mifugo. Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hii ili kuondoa migogoro baina ya wafugaji wa wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wengi ambao mapato yao yanatokana na mifugo lakini wanashindwa kuzalisha vizuri na kupata tija inayoridhisha kutokana na gharama kubwa za pembejeo za mifugo ikiwa ni pamoja na dawa za kuogeshea. Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kuwapunguzia gharama kubwa za pembejeo kwa wafugaji ili waweze kuzalisha kwa tija nzuri na kuweza kupata mahitaji yao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kwa Serikali kuhamasisha wananchi kujenga machinjio ya kisasa ili kutoa vyama bora na iliyo salama kwa walaji na kuepukana na magonjwa mbalimbali. Serikali ihamasishe wananchi kuhusu umuhimu wa kunywa maziwa pamoja na kula nyama kwa ajili ya kujenga miili yao na hivyo kuwa na afya bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafugaji huhama hama kwa kutafuta maji kwa ajili ya mifugo yao, ujenzi wa mabwawa na malambo pamoja na majosho ni muhimu sana ili kuwaondoa tatizo hilo. Serikali ihamasishe mifugo ya asili kama vile mbuzi, kuku, bata, nyuki na kadhalika katika kukuza pato lao na la Taifa kwa jumla. Ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa *RVF* uliotokea mapema mwaka huu. Pamoja ni pongezi hizi ninazo hivyo chache zifuatazo:-

Kwanza uchimbaji malambo, mbuga za Manyoni ni miongoni mwa Wilaya zenye mifugo mingi hapa nchini. Moja ya tatizo kubwa la wafugaji ni maji kwa ajili ya mifugo. Hiki ni eneo la Nkome hivyo uchimbaji wa Malambo *(Chorcel Dams)* ni la lazima kabisa. Lakini taarifa ya Waziri inaonyesha mwaka 2006/2007 hakuna lambo hata moja lililochimbwa katika mbuga ya Manyoni. Ombi letu ni kwamba mwaka 2007/08 Wilaya hii nayo iwezeshwe kuchimba malambo kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa ajili ya mifugo. Aidha, yapo malambo ya zamani yalifukiwa na mchanga, ni vema tuanze kufufua malambo hayo kabla ya kuchimba mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na ujenzi wa majosho. Mwaka 2006/2007 Wilaya ya Manyoni ikishirikiana na Wizara hii tulikarabati majosho matano tu bado kuna majosho mengi (zaidi ya 10) yanayohitaji ukarabati na kujenga mengine mapya. Mwaka 2007/2008 tunaomba Wizara hii tushirikiane na Halmashauri yetu kupitia *DADPs* tuendeleze miradi ya kukarabati majosho ambayo hayafanyikazi na pia kujenga mengine mapya ili kupambana na magonjwa ya kupe yanayoangamiza mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho narudia kuipongeza Wizara hii kwa usimamizi wa sekta ya mifugo.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Wilaya ya Dodoma Mjini ni vya wafugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Wafugaji hupata shida sana wakati wa kiangazi kutokana na uhaba wa maji ya mifugo. Suala la uchimbaji wa malambo na mabwawa lazima lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maofisa mifugo ni kata chache za wafugaji ambazo zimepewa maofisa mifugo. Hata hao wachache wana matatizo yafuatayo, kwanza baadhi yao ni maofisa kilimo na siyo watalaamu wa mifugo na pili, wachache waliopo mara nyingi hawakai vijijini wanakohitajika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa nyama ya mifugo inayochinjwa, ni vijiji vichache sana vinavyopata huduma ya watalaamu ya kupima nyama kabla ya matumizi. Hili limechangia kwa kiasi kikubwa kwenye tatizo la ugonjwa wa *Rift Valley Fever*. Wananchi walio wengi vijijini wanakula nyama isiyopimwa siyo kwa kupenda wenyewe bali kutokana na ukosefu wa wataalamu wa kuipima nyama yenyewe. Hii ni hali ya hatari na yanapotokea magonjwa ya mlipuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira duni ya minada ya mifugo, minada mingi haina miundombinu ya kuridhisha. Uchinjaji na uuzaji wa nyama (pamoja na ile ya kuchoma) hufanyika kwenye mazingira duni na yanayohatarisha afya za walaji. Pamoja na minada kuwa ni jukumu la Halmashauri husika ni muhimu kwa Wizara hii kuweka miongozo na vigezo vya kuzingatiwa katika kujenga na kuendesha minadi ya mifugo. Aidha, isimamie kwa karibu utekelezaji wa miongozo hiyo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii. Vile vile napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa hotuba yake nzuri.

Kumekuwepo na uhaba mkubwa wa maafisa wa mifugo wengi katika Wilaya, unakuta anasimamia kilimo na mifugo. Sasa kweli kama tunataka kuendeleza mifugo tutafika? Swali, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha tunapata Afisa Mifugo katika kila Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ng'ombe wa maziwa, pamoja na Serikali kusisitiza wananchi kutumia maziwa lakini bado Serikali haijawasaidia sana wafugaji katika matunzo, vifaa, dawa kwa ajili ya wafugaji hivyo maziwa hayatoshi, cha kushangaza nchi za Uarabuni ni majangwa lakini katika *Supermarket* zetu zimejaa maziwa kutoka huko. Hili ni jambo la aibu!

Swali ni kwa nini hoteli kubwa hapa nchini wanaagiza *fillet stake, sirloin, t/bone stake* na kuku wa kisasa kwa matumizi ya hoteli zao kutoka nje ya nchi? Ukizungumzia ng'ombe tunao, pia kuku tunao, tatizo ni jinsi ya kuwasaidia wafugaji kwenye *quality,* watalaamu wawaelekeze/kufundisha ni vyakula gani vya kuwapa mifugo hiyo ili tuweze ku-*export* kwa wingi na kupata *forex*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfugaji wa asili, sehemu nyingi duniani kwa sasa hivi kuna msisitizo wa kula *organic food*, kwa bahati nzuri Tanzania tumejaliwa sehemu kubwa ya kuweza kufuga kuku wa kienyeji kwa wingi kiasi ambacho tunaweza hata kuuza nje. Mji wetu wa Singida unafahamika kwa kuwa na kuku wengi sana wa kienyeji. Swali je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuwasaidia ufugaji wa Singida uwe wa kisasa na iwe ni sehemu maalumu kwa kupatikana kuku wa kienyeji?

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za pembejeo kama tunavyofahamu wafugaji wengi wa vijijini wanashindwa ku-*afford* hata dawa za kuogeshea mifugo, chanjo na kadhalika. Hii ni changamoto kubwa ili tuweze kuwa na wafugaji na wafugaji wa kisasa Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuweza kuwasaidia hata kwa kupata mikopo yenye riba nafuu ili waweze kununua pembejeo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa samaki, je, imetoa au inawasaidiaje kuhakikisha kuwa mazalio mapya ya samaki? Sababu samaki wanavuliwa tu mfano katika Zziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na kadhalika.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurasa za 9 na 10 za hotuba ya Waziri, ugonjwa wa *Rift Valley Fever (RVF)* umeongelewa kwa undani, naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu mkuu niliouona katika kupambana na *RVF,* ni Serikali kuhangaikia zaidi kuzima moto kuliko kuzuia moto usitokee**.** Nasema hivyo kutokana na jinsi Wizara ilivyopuuzia maombi ya hatua za kuzuia mlipuko wa ugonjwa huo katika maeneo yaliyoonyesha dalili za wazi za kuzika *RVF.* Tarehe 17 Aprili, 2007, Wilaya ya Kyela ilimwandikia barua Katibu Mkuu - TAMISEMI na kunakiliwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, kueleza kuwa kutokana na uchunguzi wa kimaabara wa sampuli za damu zilizochukuliwa Kyela tarehe 21 na 22 Machi, 2007, Wilaya ya Kyela ilikuwa inakabiliwa na hatari ya kuzuka ugonjwa huo wakati wowote ule. Aidha, Kyela ipo katika Bonde la Ufa na inapakana na nchi ya Malawi.

Vilevile, Kyela ilikuwa inakabiliwa na mafuriko na kuandamwa na malaria kutokana na uwepo wa mbu wengi. Kutokana na sababu hizo, Wilaya ikaomba shilingi 12,499,000 tu kwa ajili ya kutoa elimu ya tahadhari kwa wananchi juu ya kuzuka ugonjwa, namna ya kuutambua, jinsi ya kujikinga na kuudhibiti ili usienee ndani na nje ya Wilaya. Katika kutimiza azma hiyo, Wilaya ilidhamiria kutengeneza vipeperushi na mabango na kutoa mafunzo maalumu kwa watumishi wa Serikali kueneza elimu hiyo Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mimi Mbunge wa Kyela kuongea na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Kyela haikupata hata senti tano wala kujibiwa! Tukaendesha zoezi hilo nusu nusu tu kwa kutumia fedha za Halmashauri zilizopangiwa mambo mengine. Huo ni ushahidi tosha kuwa hatutoi kipaumbele katika kuzuia kuliko kutibu**.** Huu ni udhaifu mkubwa unaohitaji kufanyiwa kazi. Naomba nimkabidhi Waziri barua hiyo ya Wilaya ya Kyela. Naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Ni maoni yangu kwamba hotuba hii imeweka mipango madhubuti ambayo imeainisha mkakati na mbinu zilizowekwa ili kukuza maendeleo ya mifugo nchini mwetu. Ni kwa msingi huo naunga mkono hotuba hii.

Naomba kupitia hotuba hii nikumbushie mambo machache ambayo kwa muda mrefu nimekuwa nikiyasemea hapa Bungeni. Kwanza, ni kuhusu ukarabati wa majosho na uanzishaji wa majosho mapya katika Wilaya mpya ya Siha. Asilimia 50 ya wananchi wote wa Siha ni wachungaji/wafungaji hivyo kuendeleza majosho yaliyopo na kujenga mengine mapya ni jambo muhimu sana. Aidha, utoaji wa huduma ya dawa kwa bei nafuu ili wananchi walio wengi waweze kumudu ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hai kabla ya kuhamia Siha tulipata maelekezo ambayo Serikali imekuwa inayarudia mara kwa mara kwamba sekta binafsi iachwe ifanye kazi hiyo ya kukarabati na kujenga majosho mapya na pia kutoa huduma ya dawa jambo ambalo halikuwezekana kabisa. Ipo haja kwa Serikali kutamka wazi wazi kuwa maendeleo ya mifugo yataendelea kuhudumiwa na Halmashauri zinazohusika zikisaidiana na Serikali na wananchi watakiwe kushiriki kwa kuchangia sehemu fulani ya huduma zinazotolewa na Halmashauri/Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili, linahusu wananchi walio jirani na Ranchi zilizopo katika Wilaya ya Siha. Kimsingi hatuna tatizo na ubinafsishaji wa ranchi hizi. Tunalosisitiza na kukumbusha hapa ni kwamba Serikali ione umuhimu wa kutenga maeneo ambayo wananchi wanaopakana na ranchi iliyopo Siha ili kusiwepo na migogoro ambayo ingeweza kuepukwa. Wananchi hawa wanatoka vijiji vya Karansi, Magadini, Lekrimuni, Kandashi Sanya Juu, Gararakua, Mawasililano, Wiri ambavyo kwa sasa viko katika Kata ya Siha Kati.

Aidha, kuna haja ya kuona kwamba eneo la ranchi linapokuwa limegawanywa katika *plots* mbalimbali, wananchi wanatengewa *plots* ambazo haziwaingizi katika ushindani wasioumudu ili nao waweze kushiriki katika uwekezaji kwa njia ambayo ni nafuu. Hii ina maana kwamba kuna umuhimu wa kuwawekea wananchi mazingira ambayo yatawawezesha wananchi kushiriki kumiliki ranchi hizo kwa njia ya ushirika ambao utaleta tija. Sisi wananchi wa Siha tutaendelea kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya mifugo ili tuwe na utaratibu mzuri ambao utashirikisha wadau wote muhimu katika kuweka utaratibu mzuri ambao utaepusha tafrani zisizokuwa na umuhimu wowote ule. Naunga mkono hoja.

**MHE**. **ZAYNAB M. VULU:**Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili kuipongeza Wizara na hasa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa umahiri wao, wakisaidiwa na Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na watendaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ni kiungo muhimu cha uchumi kwa Serikali/nchi yetu. Lakini mpaka sasa bado hatujaweza kuinua kipato cha wafugaji kutokana na kutokuwa na miundombinu iliyo mizuri. Hali hiyo inaweza kuleta kudorora kwa ukuwaji wa sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hoja hiyo, naomba Waziri anipatie ufafanuzi ni lini Wizara itapeleka wataalamu wa kutoa mafunzo kwenye maeneo ambayo ni ya wakulima na hawana asili ya ufugaji? Mbali ya mafunzo, wafugaji hao wamehamishiwa kwenye maeneo ambayo hakukuwa na maandalizi ya kutosha na hatimaye kuleta mgongano na migogoro. Je, hili Serikali imelichukuliaje? Hivi sasa mfano Wilaya ya Kisarawe (Gwata) kuna mgogoro baina ya wakulima na wafugaji na isitoshe wafugaji hao wanaingiza mifugo kwenye maeneo ya vyanzo vya maji ya mto Ruvu ambapo madhara yake kukosekana kwa maji Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipatiwe maelezo ni lini Serikali/Wizara itatoa elimu, kuchimba malambo ya kutosha na kushirikisha wakulima na wafugaji ili kusiwe na migogoro na uharibifu wa mazingira ?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Anthony Diallo na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa kwa jinsi ambavyo wanaendesha Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa jinsi walivyoshughulikia tatizo la ugonjwa wa Bonde la Ufa *(RVF)* na tahadhari zilizochukuliwa. Ninao mchango mdogo lakini naona ni muhimu. Mkoani Ruvuma kuna mtindo wa kuachia wanyama hasa nguruwe kufugwa kwa mtindo wa *free range,* hali ambayo inasambaza sana viroboto. Lakini pia sioni kama kuna utaalamu wowote ambao wafugaji hao wanapewa wala majosho hamna hasa katika eneo la Liuli - Mengo. Naiomba Wizara yako ifuatilie na kuwaelekeza wananchi wetu mbinu nzuri za ufugaji ili kuboresha vipato na maisha.

Pia kuhusiana na maeneo waliyohamia wafugaji, eneo kama Mkoa wa Ruvuma ni mkoa wenye miti mingi mikubwa, hakuna nyasi za kutosha na hivyo kuhitaji wafugaji kutumia eneo kubwa zaidi na kuingia kwenye mashamba ya wenyeji. Nashauri kuwa ni vema yatengwe maeneo maalumu ambayo yanaweza yakakatwa miti na kupanda nyasi kwa ajili ya mifugo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilipoenda Lesotho niliona mbegu za nyasi maalumu kwa ajili ya malisho ya wanyama kama ng'ombe na mbuzi ili kutoa maziwa zaidi. Je, hapa kwetu Tanzania mbegu hizo zinapatikana wapi? Kama hazipo je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na mbegu hizo ili kusaidia ufugaji bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Mkoa wa Ruvuma waliwahi kufaidika na mradi wa kopa ng'ombe, lipa ng'ombe. Ili tuweze kuendeleza mradi huo kwa kuwa wengi wanatuulizia, taratibu za kupata wanyama hao zikoje, naomba tafadhali nifahamishwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na zoezi la uhamishaji wa wafugaji kutoka Bonde la Ihefu wafugaji wengi walipata matatizo mengi kutokana na maandalizi hafifu ya zoezi hilo. Kwa kuwa Tume iliyoundwa kuchunguza matatizo hayo imekamilisha kazi yake, je, Serikali iko tayari kuwapatia Wabunge Taarifa kamili ya Tume hiyo ili kufahamu kikamilifu yaliyotokea wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo ambao ukiachwa uwe siri unachafua jina zuri la Serikali yetu hasa katika maeneo ya ukiukwaji wa haki za binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hali halisi ya wafugaji hao sasa ikoje? Wamepatiwa maeneo mbadala kule walikohamishwa na je, wamepewa miundombinu gani kwa ajili ya ustawi wao na wa mali zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wafugaji hasa wa Kibarbaig wanapata matatizo hayo baada ya maeneo yao ya asili kuchukuliwa na Serikali bila hiari yao na bila kupewa maeneo mbadala yaani maeneo yaliyokuja kuwa *Hanang Wheat Complex* katika Wilaya ya Hangang, na kwa kuwa Mpango wa Taifa wa *Wheat Complex* chini ya *NAFCO* umekufa na maeneo hayo ya zaidi ya ekari 100,000 ya sasa yanabinafsishwa, je, ni kwa nini Serikali isifanye mpango wa makusudi wa kuwarudishia wananchi hao maeneo yao ya asili ili wasiendelee kuwa wakimbizi katika nchi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo haiwezekani kuwarudishia maeneo yao katika maeneo ya Hanang, Serikali sasa iko tayari kuwatengea maeneo mahususi popote pale walipo na kuwawekea miundombinu kama mabwawa (kama yale ya asili mathalani Ziwa Bassotu) katika makazi yao hayo mapya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukuza biashara inayotokana na mazao ya mifugo hasa nyama na ngozi, Serikali haioni kuna umuhimu kuwa na mpango mahususi wa kuwaelimisha wananchi kuingia katika ufugaji wa kitaalamu na kisasa wa mifugo asilia ambao tunao wengi sana na wanaweza kuwa kianzio kizuri kwa Pato la Taifa na la mfugaji mmoja mmoja iwapo *quality* ya mifugo hiyo itaboreshwa na kuwekewa mazingira mazuri ya soko la ndani na nje badala ya kujielekeza kwa ng’ombe wa kisasa tu ambao wafugaji wetu wa kawaida si rahisi kuwapata na kuwatunza. Je, si wakati muafaka sasa Serikali kuwa si tu na mpango lakini ratiba mahususi ya utekelezaji ya kufufua machinjio ya kisasa katika mikoa yote ya wafugaji ili kuondoa adha ya kusafirisha mifugo hai kwa mwendo mrefu ambao ni mateso kwa wanyama lakini pia kwa lengo la kuongeza thamani halisi *(value added)* ya mifugo hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni muda mrefu ndani ya Bunge hili kumetolewa ombi la Serikali kutenganisha nafasi na majukumu ya Bwana Shamba na Bwana Mifugo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi hasa katika eneo la mifugo ambalo kwa muda mrefu linaelekea kufunikwa kabisa na majukumu ya kilimo. Kitu gani kinazuia nia njema ya Mheshimiwa Rais kutenganisha majukumu haya katika ngazi ya Taifa na katika ngazi ya Wilaya tukaendelea kufumbia macho jambo hili? Ninaomba maelezo ya kina kwani hili ni suala la kiutendaji tu na sioni sababu ya msingi kushindwa kulitekeleza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Hivyo basi, yote nitakayochangia nitashukuru kama yatatolewa ufafanuzi na Waziri, Mheshimiwa Anthony M. Diallo au Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, machinjio ya kisasa, nashukuru sana Serikali kwani inahimiza kuwepo machinjio ya kisasa. Vile vile nipongeze juhudi za Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuanzisha ujenzi wa machinjio ya kisasa kwa kuwa ujenzi huu umeshakuwa na muda mrefu, nitafurahi kufahamishwa kuna matatizo gani yanayofanya ujenzi huu uchukue muda mrefu kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ujenzi wa machinjio haya Dar es Salaam, naiomba Serikali ishirikiane na Halmashauri zetu ili tuwe na machinjio ya kisasa Mikoani na Wilayani ili tuepukane na maambukizo yanayotokana na nyama, mfano *RVF*. Machinjio haya, ujenzi wake uende sambamba na mabucha. Naomba zoezi hili endapo Serikali itaafiki, ianze Mikoa ambayo ina mifugo mingi ukiwemo Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji bora wa mifugo, nashukuru Mungu kwani kati ya nchi zilizojaliwa kuwa na mifugo ni pamoja na Tanzania. Vile vile ndani ya Tanzania, Mikoa yenye ng’ombe wengi ni pamoja na Singida. Ni ukweli usiofichika kuwa wananchi wanaofuga mifugo, wanafuga bila taaluma. Hivyo basi, ninaiomba Serikali ihamasishe Mabwana Mifugo kufundisha njia bora ya kufuga mifugo, mfano, kupunguza mifugo kwa kuuza na fedha zinazopatikana kufanyia mambo ya maendeleo, mfano kujenga nyumba bora na kadhalika. Pia kutenga maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya usafiri kwa Mabwana Mifugo, ili Mabwana mifugo na Mabibi Mifugo waweze kufanya kazi nzuri ya kuelimisha wafugaji ili wawe wafugaji bora sio kuwa watumwa wa mifugo, wataalamu hawa hasa wa kata nashauri wapatiwe pikipiki ama baiskeli na Mkuu wa Idara wa Halmashauri apewe gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ina faida nyingi sana, mfano kuuza na kupata fedha, ngozi, maziwa, mifupa, mbolea na kadhalika. Hivyo, ni muhimu wafugaji wawapate elimu ili yote haya yaweze kupata soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ili mifugo yetu isishambuliwe na maradhi ni vyema tuwe na majosho ya uhakika kila kijiji chenye mifugo ili kuogesha mifugo kuzuia isipate maradhi. Kuna majosho mengi yamechakaa na hayatumiki kabisa. Naiomba Serikali ihakikishe majosho yote yanaimarishwa na kupewa dawa za majosho. Vile vile kwa vile vijiji ambavyo havina majosho, sasa nadhani ni wakati muafaka wa kuhakikisha kila kijiji chenye mifugo kina josho, mfano, vijiji vya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo maalumu ya malisho ya mifugo, kwa kuwa wafugaji wamekuwa wakichunga mifugo yao holela yaani bila kuwa na maeneo maalumu, naishauri Serikali ihakikishe kila kijiji kiwe na maeneo maalumu ya kuchungia mifugo. Hii itasaidia mifugo hii isiharibu mashamba ya wakulima ambayo nayo ni muhimu sana na kutokuleta uhasama kati ya wafugaji na wakulima. Nitashukuru endapo

nitapata majibu. Vilevile kuna mbegu za malisho ya mifugo, basi wafugaji wapewe waoteshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malambo ikimbukwe kuwa kuna Mikoa ambayo ina matatizo ya ukame, mfano, Singida, Dodoma, Manyara, Tabora, Shinyanga na kadhalika. Hivyo, ni vyema Serikali itilie umuhimu wa kuwachimbia malambo wafugaji kwa ajili ya kunyweshea mifugo kwani kuna maeneo mengi mifugo husafirishwa mwendo mrefu kufuata maji. Naiomba sana Serikali, maeneo yote yaliyoombewa fedha za kuchimba malambo Mkoani Singida, yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itazame upya namna ya kusafirisha mifugo toka Mikoa ya Bara kwenda Dar es Salaam ukiwemo Mkoa wa Singida. Ninashauri mabehewa ya mifugo kwenye treni ya kutoka Singida kwani usafiri wa malori, mifugo inateseka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhudu kutenganisha wataalamu wa kilimo na mifugo, wataalamu hao ni fani mbili tofauti. Hivyo basi, sasa ni wakati muafaka kuwatenganisha ili Bwana Mifugo aende na fani yake na Bwana Kilimo aende na fani yake ya kilimo. Hii itasaidia watendaji hawa kufanya kazi kwa utalaamu waliosomea. Nipewe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika mazao ya wafugaji ambayo yanakosa soko zuri ni pamoja na ngozi za mifugo yetu, naiomba Serikali iwasaidie wafugaji na wapewwe taaluma pia namna ya kuwamba ngozi ili ziwe na soko. Vile vile nasubiri maelezo.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Anthony Diallo na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Singida Kusini lina majosho machache sana, jambo ambalo nilishawahi kumsikitikia Naibu Waziri na kumuomba anisaidie ili vijiji vyangu navyo vipate majosho ukizingatia kuwa Wilaya ya Singida ni Wilaya ya wafugaji. Napenda kusisitiza ombi langu la kupatiwa majosho ya kutosha pamoja na malambo ili kuwasaidia wafugaji ikiwa ni pamoja na kutatua tatizo la maji kwa wanyama/mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma Serikali ilishaeleza kuwa itatoa ruzuku katika dawa za mifugo kwa maana kwamba Serikali italipia 40% na wananchi kulipia 60%. Napongeza uamuzi huo. Tatizo langu ni utekelezaji wa azma hiyo. Napenda kupata maelezo azma hiyo itakelezwa vipi hasa Singida Vijijini? Mfugaji atumie utaratibu gani ili kupata kununua dawa hizo zenye msaada wa ruzuku ?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Singida inajulikana kuwa inazalisha kuku wengi na watamu ambao wanapendwa sana na soko lake ni kubwa hasa Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Tabora na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mambo matatu, kwanza, *study* ifanywe na Serikali namna ya kuboresha ufugaji wa kuku wa kienyeji Singida na wananchi waelimishwe njia bora ya ufugaji wa kuku hao, pili, Serikali isaidie Wilaya ya Singida kupata wafadhili watakaowekeza katika kuanzisha viwanda vya usindikaji wa nyama ya kuku. Hivi sasa hoteli kubwa za Kimataifa zinafunguliwa nchini na zinahitaji nyama ya kuku kwa wateja wao. Wakati umefika wa kuwa na kiwanda cha nyama ya kuku na machinjio ya kisasa ya kuku. Tunaomba msaada huo na tatu, nashauri Serikali itenganishe nafasi za Ofisa Kilimo na Ofisa Mifugo hasa ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji ili kupata ufanisi wa kazi kwa kuzingatia kilimo na mifugo zimetenganishwa.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu, uzima na kuweza kufika Bungeni nikiwa mzima, *Alhamdullillah.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake ambayo imejaa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu kwenye Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaaliwa kuwa na uchumi mkubwa, moja, ni mifugo. Tuna wanyama wa aina na aina kama vile ng'ombe, kondoo, mbuzi nguruwe na kadhalika. Jitihada ya Serikali ya kuweza kuwapatia mifugo yetu majosho ama chanjo husahaulika mpaka pale wanyama hawa wakumbwe na maradhi ndio uone nguvu za ziada zinatendeka. Mara nyingi wanyama wetu hupata maradhi kutokana na kukosekana kwa mambo kama vile Daktari wa wanyama, majosho, chanjo na kadhalika, hili linaeleweka.  Kwa nini Serikali haifanikishi mahitaji haya ili kunusuru mifugo yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maradhi yanayotokana na wanyama pia humfikia binadamu. Maradhi hayo ni kama kichaa cha mbwa. Maradhi haya ni mabaya sana. Kwa vile mbwa wapo wengi nchini na baadhi ya maeneo mbwa hawa wameenea mitaani na kutembea kiholela, je, Serikali imetoa taaluma gani kwa jamii ili kuwanusuru na gonjwa hilo? Je, Serikali imetoa chanjo kwa mbwa nchini kwa muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni sekta inayoweza kukuza uchumi wa nchi yetu, hivyo ni vyema Serikali/Wizara iikuze ili iwawezeshe wafugaji wetu nchini.  Ni vyema Serikali ipange mikakati madhubuti ya kutoa maeneo ya lishe, maji safi, majosho na pia taaluma kwa wafugaji na kuwekwe mtaalamu katika sekta hii ili kunusuru maradhi ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wawezeshwe ili waweze kuzalisha katika sekta hii kwani bado watu wetu uwezo wao ni mdogo. Kwa kufanya hivyo tunaweza kuzalisha kwa wingi. Kukosekana kwa maziwa ya kutosha ni athari kwa watu wetu kwani maziwa ni lishe bora kwa afya zetu na pia kupatikane masoko. Wafugaji wetu hawana soko la uhakika la kuuzia maziwa, nyama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifungue vyuo ili vitoe taaluma kwa wafugaji kwani hivi sasa wengi wafugaji wetu vijijini ndio wengi na wanafuga mifugo yao kwa njia ya kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuku na bata, wafugaji wetu bado ni maskini. Wenye mifugo hii mara nyingi ni akinamama. Ni vyema Serikali iwawezeshe akinamama ili waweze kukuza miradi yao.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nitoe mchango wangu wa maandishi. Nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa mashirikiano yao katika Wizara, wamefanya kazi nzuri kwa kipindi kifupi cha kuanzishwa kwa Wizara. Hatua hii naiunga mkono pamoja na Bajeti yao kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika suala la sekta nzima ya mifugo. Sekta hii ina uwezo mkubwa wa kuchangia Pato la Taifa iwapo itapewa msukumo mkubwa na kutengewa pesa za kutosha kufanikisha azma yake. Ujenzi wa machinjio uongezwe kwa kusaidiana na wawekezaji ili tuweze kuuza nyama nje ya nchi badala ya kuuza ng’ombe jambo ambalo inaleta hasara na usumbufu wa kusafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji kwa ajili ya mifugo bado ni tatizo, hivyo juhudi ziendelee kufahamu ni maeneo yapi yajengwe mabwawa kwa ajili hiyo. Tunaipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri za uchimbaji wa malambo. Hata hivyo ni vyema kushirikiana na Wizara zingine na kuhakikisha tatizo hilo linaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maabara, tunaiomba sana Wizara iangalie kwa makini Idara hii ya Utafiti. Kazi zilizofanyika mwaka huu hasa katika ugonjwa wa Bonde la Ufa, maabara ya Temeke imefanya kazi nzuri katika mazingira magumu, hivyo ni vyema kuboresha tafiti zetu ili tusiingie gharama zisizo za lazima za kupeleka vipimo nje wakati wataalamu wapo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la ajabu kwa idadi ya ng’ombe waliopo hapa nchini, kuendelea kuagiza nyama nje. Nashauri Serikali ipige marufuku kuagiza nyama nje. Tutumie nyama ya hapa nchini, tuagize tu iwapo watumiaji wa Kitanzania watazidi huduma ya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za ruzuku, naipongeza Serikali kuwafikiria wafugaji na kuwapa dawa za ruzuku kwa 60%. Utaratibu wa kufikisha dawa hizi bado ni tatizo kwa zinaishia kwa wajanja. Hivyo, nashauri taratibu nzuri ziandaliwe ili wahusika wapate mahitaji yao kama watakavyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusisitiza suala la Wizara kufuatilia ukarabati wa majosho katika Halmashauri zetu ili majosho yajengwe na yaliyopo yakarabatiwe. Pia idadi ya watumishi wa Idara ya mifugo ili wataalamu hawa waende vijijini na wasikae

ofisini na ofisi zao ziwe katika maeneo ya wafugaji. Kwa maana ya kuwatembelea ni vyema pikipiki zinunuliwe kuwasaidia usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja!

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mkoa wa Shinyanga kuwa na mifugo mingi sana zaidi ya milioni nne na vile vile kupitia mpango wa *DADPs* katika kuimarisha sekta hii, ukweli ni kwamba imeonekana mafanikio ni kidogo sana. Hii ni kutokana na kuwaachia wananchi wenyewe kuibua miradi hiyo, inaonekana kuwa wananchi hawana uelewa sahihi wa vipi na namna gani ya kuibua miradi ya sekta ya mifugo kama vile majosho, malambo na kadhalika kwa sababu hawana takwimu sahihi ya mradi upi ni muhimu kuibua kwa wakati muafaka.

Hivyo, nashauri Wizara ifikirie kuibua yenyewe moja kwa moja miradi ambayo ni tatizo kwa wafugaji na kuendeleza mifugo kwa mfano, Mkoa wa Shinyanga ng'ombe milioni tatu, lakini ina majosho machache sana. Jimbo la Solwa lina ng'ombe 300,344 na kuna majosho 14 tu na yanayofanya kazi ni mawili tu. Kwa utaalamu sahihi, kila josho moja lihudumie ng'ombe 5,000. Hivyo, katika Jimbo la Solwa tunatakiwa kuwa na majosho 60 ili yaweze kukidhi idadi ya ng'ombe tulionao katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijaribu kuibua yenyewe majosho na kuhakikisha kuwa majosho ya zamani yanafanyiwa ukarabati, naomba kupata majibu wakati Waziri anajibu hoja za wachangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua kiwanda cha nyama Shinyanga ambacho tayari kimebinafsishwa kwa mwekezaji kitaanza shughuli zake na nini mpango wao wa baadae kama vile kiwanda cha ngozi , maziwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wananchi itakuwa lazima waibue miradi badala ya Serikali, basi nitoe ushauri ya kwamba Wizara ijaribu kuwaelimisha wananchi juu ya kuibua miradi hiyo ili iweze kutoa kero ya muda mrefu na kweli imezuia sana ukuaji wa sekta ya mifugo kwani ni vigumu wananchi kuibua miradi iliyo sahihi kwani hawana takwimu sahihi za mifugo au takwimu za matatizo yanayoikabili sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia kwa maandishi. Naunga mkono hoja kwa aslimia mia moja. Asante sana.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Charles O. Mlingwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamrunda na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya. Hii imejionesha jinsi walivyojihusisha kuwatetea wafugaji waliotakiwa kuhamisha mifugo yao kutoka Ihefu kwenda maeneo yaliyopangwa na Serikali. Wizara imekuwa ikitoa maelezo kila wakati, pale ambapo taratibu zimekuwa zikikiukwa. Nawapongeza sana kwa hilo.

Naipongeza Wizara kwa kusimama kidete katika kuhakikisha kuwa, Ugonjwa wa Bonde la Ufa hauenei kwa kasi na kuutokomeza na sasa wananchi wanaendelea na ulaji wa nyama kama kawaida. Elimu iliyotolewa ilikuwa nzuri sana na ilieleweka vizuri kwa wananchi.

Nina maombi yafuatayo: Ranchi ya Usungu Mbarali, naomba kujua ni lini hati miliki zitatolewa kwa sababu tangu *offer* zitolewe kwa waombaji ni zaidi ya miaka mitatu sasa imepita? Kama kuna vikwazo vyovyote ni vizuri vikaelezwa wazi ili kuondoa uvamizi wa maeneo hayo.

Kutokana na ukubwa wa eneo la ufugaji lililopo Mbarali, Wilaya inatakiwa kubaki na mifugo 65,000. Tatizo lililopo ni kujua idadi ya ng'ombe waliopo mpaka sasa, baada ya zoezi na kuhamisha mifugo Ihefu. Ninachoomba kujua ni Mkakati wa Wizara uliopo kusaidia Wilaya katika kujua idadi ya mifugo iliyobaki, kwa sababu mpaka sasa wafugaji wanaishi kwa wasiwasi sana kutokana na kutotengewa ardhi kwa kila mfugaji aliyebaki Wilaya ya Mbarali.

Familia za wafugaji zimesambaratishwa sana kutokana na kuhamishwa kwa nguvu bila utaratibu na usimamizi si mzuri, wazee na watoto wamebaki Mbarali na baadhi ya familia wamehamia maeneo mapya na wamebaki maskini kutokana na kupoteza mifugo mingi au yote. Je, Serikali ina mpango gani katika kusaidia familia za wafugaji hawa, kwa kuwa lengo la Serikali lilikuwa zuri isipokuwa utekelezaji wake haukuwa mzuri? Utekelezaji haukufuata maelekezo ya Serikali.

Wafugaji kutoka Wilaya ya Mbarali ni vizuri wakapimiwa maeneo haraka kwenye maeneo mapya na kupewa elimu ya kufuga mifugo ya kibiashara, ili wasije wakawa ni watu wa kuhamishwa tena watakapovamia maeneo yasiyotakiwa. Pamoja na juhudi za kujenga miundombinu, iende sambamba na ugawaji wa maeneo yao kudumu, ikiwa ni pamoja na kuwajengea shule za bweni.

Kwa kuwa fursa ya wafugaji kukopeshwa na taasisi za fedha ni ndogo sana, Wizara ione jinsi ya kuzishawishi taasisi hizi, zione umuhimu wa kuwakopesha wafugaji walioathirika na kupoteza mifugo yao ili warudishe kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Wizara izingatie sana kupunguza mifugo kwa njia ya kuwatafutia soko la mifugo na kusafirisha mifugo kwa usafiri wa magari badala ya kuchunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi nzuri waliyofanya katika kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa nchini katika kipindi cha Februari hadi Juni, 2007. Pia

ninawapongeza kwa hotuba yao nzuri waliyoitoa leo hapa Bungeni. Ninauga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Serengeti ina mifugo mingi lakini mingi ya mifugo hii inaathiriwa na ukame ambapo inakosa maji na hivyo basi, baadhi ya mifugo hufa kwa ukosefu wa maji. Ukiangalia mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wilaya ya Serengeti haikupewa fedha kwa ajili ya kujenga malambo kuptia *DADPS.* Nashindwa kuelewa ni kwa nini Wilaya ya Serengeti, yenye mifugo mingi, haikupewa fedha za kuchimba malambo na kuacha mifugo mingi inakufa kwa ukosefu wa maji? Naomba majibu ya Waziri ili nijue kama katika bajeti hii ya 2007/2008, Serikali imetenga fedha za kuchimba malambo katika Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mifugo mingi katika Wilaya ya Serengeti, inaathirika sana kwa magonjwa yanayosababishwa na kupe, kwani majosho mengi ya kuogeshea mifugo yameharibika sana. Naomba jibu la Waziri ili nijue Wilaya ya Serengeti imetengewa fedha kiasi gani, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majosho?

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma Mkoa wa Mara ulikuwa na viwanda vingi vya maziwa, lakini sasa viwanda hivyo havifanyi kazi na vimefungwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Wananchi wa Mkoa wa Mara katika kufufua viwanda hivyo, kwani sasa wafugaji wanazalisha maziwa mengi lakini hawana pa kuuzia? Mfano, Wilaya ya Serengeti bei ya maziwa ni Sh. 150 kwa lita na mengi humwagwa kwa kukosa soko. Naomba jibu la Waziri kuhusu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama kazi zilizotekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, utaona kuwa, hakuna kazi hata moja iliyofanyika Mkoa wa Mara katika mwaka wa fedha 2006/2007. Sasa inakuwaje mkoa wenye mifugo mingi kiasi hicho, uachwe kufanyiwa kitu chochote mwaka mzima? Naomba majibu ya Waziri kuwa ni nini kitafnyika Mkoani Mara, hasa Wilayani Serengeti katika bajeti ya 2007/2008?

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, kwa kusaidiwa na Mtendaji wao Mkuu, Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamvunda na Dr. Melewas, ambaye ni mtaalamu mzoefu wa fani hii, kwa kudhibiti magonjwa mengi ya mifugo na hasa *RVF.* Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Mifugo ni bora ikapewa nafasi ya pekee kufafanuliwa kwa Wabunge, wafugaji na wadau wengine muhimu, ili kwa pamoja, iandaliwe *Action Programme*, ambayo itatoa dira ya wapi tunaelekea na kwa kuzingatia pia Ilani ya Uchaguzi, angalau hadi mwaka 2010 tuwe na cha kuelezea kwa wananchi tumefanya kitu gani. Pia kuonesha mpango wa kati na wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie kulipima Shamba la Malonje, ambalo lilitakiwa kugawanywa katika mashamba madogo madogo ya ekari 100 – sawa na *ha.* 40/50. Msaada wa kitaalamu kama ulivyofanyika kwa kugawa mashamba

mengine kama Kalambo, lingepunguza matatizo ya kutegemea uwezo mdogo wa mkoa kwa eneo kubwa kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mkoa wa Rukwa umeathirika sana na upungufu wa miti kutokana na kilimo. Naiomba Wizara ione namna ya kusaidia uanzishwaji wa mitambo ya *biogas* ili angalau kuzuiz athari za jangwa katika Nyanda za Juu Kusini. Matumizi ya zana za kukokotwa na ng'ombe budi zikapewa nafasi ya pekee. Mkoa huu upewe ukuu wa kuratibu kazi hii kwa kanda nzima ya Kusini. Mpango wa Panda Miti Rukwa (PAMIRU), unavyooanishwa na mpango wa kuendeleza wafugaji na wakati huo huo kuhifadhi mazingira, uendelezwe na Wizara itoe kila aina ya msaada wa hali na mali.

Naomba Wizara isaidie Kiwanda cha SAAFI Sumbawanga, kipate soko la uhakika wa nyama na kwa kushirikiana na Wizara nyingine, kipate miundombinu ya kukisaidia kuleta ustawi wa mkoa. Maeneo muhimu kwa kiwanda hiki ni pamoja na barabara ya lami, umeme wa uhakika, uwanja mzuri wa ndege na maji safi na salama. Miradi hii itasaidia sana ufanisi wa mradi kama huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, hivi nini hatma ya wataalamu wetu wa mifugo katika kupewa mikopo ya kuwawezesha kuanzisha makampuni yao ya kutibu mifugo; kuuza madawa na kutoa *extension services* kwa malipo? Je, kwa nini wasitafutiwe maeneo nao wakafuga kisasa ili kazi ya ufugaji isibakie kwa wakulima na wafugaji wasio na utaalamu?

Naunga mkono na kuwaomba wote wanaohusika waendeleze utafiti, mafunzo hasa kwa wafugaji na watoto wao waliomaliza Kidato cha IV na zaidi ya hilo, kutoa motisha ya malupulupu kwa watumishi wa Wizara hii ili madaktari wa mifugo wasipitane sana kwa mishahara na madaktari wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, chini ya Ilani ya CCM ya 2005, aliahidi kuwawezesha wanawake na pia vijana kuwapatia ajira; na kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya wakazi wapatao *4.0ml;* na asilimia kubwa ya wakazi hawa wako katika sekta binafsi, ambayo ni ufugaji wa kuku wa nyama na mayai; na kutokana na idadi kubwa ya wanawake kuitikia wito wa kujiunga na vyama vya akiba na mikopo na idadi hiyo ya wafugaji wengi wao ni wanawake ambao wamestaafu; cha kusikisitisha ni kwamba, wafugaji hawa huchukua miezi 6 – 10 kupata vifaranga kutokana na uwezo mdogo wa makampuni yanayojihusisha na ufugaji wa vifaranga. Mfano, JKT Ruvu, *Kibaha Education Centre*, *Mkuza Chicks* na kadhalika. Wafugaji hawa hawawezi kufuga kwa tija na ikizingatiwa Mkoa wa Dar es Salaam hauna eneo la kilimo, isipokuwa ni ufugaji wa kuku wa nyama na mayai.

Kwa sababu hiyo, naomba Serikali iongezee mtaji makampuni haya, aani JKT Ruvu, *Kibaha Education Centre, Mkuza Chicks* na mengineyo ili yaweze kutoa huduma kwa Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa jirani, yaani Pwani na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia wafugaji hawa wanategemea sana ufugaji wa kuku kama nguzo ya kuendesha maisha yao na kusomesha watoto wao, naiomba sana Serikali inieleze kama katika bajeti hii itaweza kuzisaidia taasisi hizi zinazojihusisha na uanguaji wa vifaranga kwa kuziongezea mtaji?

Serikali iamue kwa haraka kumtafuta mwekezaji wa kujenga kiwanda cha kutengeneza vifungashio vya maziwa *(packaging)*. Hii itaongeza thamani ya bidhaa zetu za mazao ya mifugo na mazao mengine yaliyosindikwa kwa ubora na pia vifungisho vilivyo na ubora wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii na mimi kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Maendeleo ya Mifugo. Kwanza kabisa, ningependa kusema kuwa, wafanyabiashara wanaosafirisha mifugo kwa miguu kutoka mkoa hadi mkoa, wamekuwa wakipitisha mifugo katikati ya barabara.

Hali hii inasababisha uharibifu wa barabara na uchafuzi wa barabara zetu. Naiomba Wizara ijaribu kufutilia suala hili na kuweka msisitizo mkubwa kwa wafanyabishara hawa, wapitishe pembezoni mwa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie tena kwenye eneo la majosho ya mifugo. Ni kweli kuwa tuna tatizo kubwa na majosho ya kuogeshea mifugo katika maeneo mengi nchini hivyo, naiomba Serikali ijaribu kuangalia ni jinsi gani wananchi wanasaidiwa kupata majosho ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kidogo kuhusu dawa za mifugo, kwani dawa hizi zimekuwa ni kidogo sana kiasi kwamba, hazikidhi haja hivyo, naiomba Wizara ijaribu kuongeza dawa kwa ajili ya matibabu ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara kuwa hii mbolea ya mifugo ni nzuri sana ikitumika katika ukulima katika maeneo mbalimbali hivyo, ningeshauri Serikali itoe kauli kuwa kila mwananchi mwenye mifugo, aitumie mbolea yake wakati wa kilimo ili iweze kumtolea mazao bora na yenye kushamiri vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri na yenye mpangilio. Pamoja na pongezi zangu, nitashukuru sana kama Wizara itaangalia maeneo mapya ya kuendeleza mifugo kama Jimbo la Tunduru ambako kuna maeneo mengi na makubwa ya malisho.

Njia rahisi ya kuwasaidia wakulima wasio na mifugo ni kuwasambazia mitamba kwa bei nafuu. Jimbo la Tunduru tunalikaribisha sana wazo hili na tutatoa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo linalonikera sana hapa Dodoma ni vitendo vya ukatili vinavyofanywa kwa kuku na wakazi wa hapa mara zote. Nimeshuhudia kuku wakining'inizwa kichwa chini miguu juu. Mheshimiwa Waziri, naomba kusikia tamko la Serikali kupitia Wizara yako juu ukatili huu wanaofanyiwa kuku hapa Dodoma na sehemu nyingine nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia 100.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri na hotuba nzuri. Naunga mkono hoja hii. Lakini naomba kuchangia mambo kidogo kuhusu kuhamishwa kwa mifugo Kilwa Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwepo na miundombinu kabla ya kuhamishwa mifugo hiyo huko Kusini, pia kuwepo na malambo ya maji, majosho na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hapa Waziri atuhakikishie, kuwepo na miundombinu hii, siioni *budget* iliyotengwa hapa. Vilevile tunaiomba Serikali ifanye Mpango Maalum, Wananchi wa Lindi wapate wataalam wa mifugo wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua kuhusu mifugo kama ng'ombe kutumia kwa kulimia mashamba. Tunaomba Wananchi wa Kilwa, wapatiwe wataalamu wa kuwafundisha kilimo hicho cha kukokota na ng'ombe. Namwomba Mheshimiwa Waziri, sisi Wananchi wa Kilwa tupate mafunzo hayo. Hatupingi kuingizwa kwa mifugo hiyo Mkoani Lindi, lakini tunaomba tamko la Waziri hapa Bungeni kuhusu miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunataka kujua fedha ngapi zimetengwa kwa Lindi, Kilwa na Nachingwea?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo ni Wizara muhimu, kwani zaidi ya nusu ya wakazi wa nchi yetu ni wafugaji na hujipatia maisha yao kutoka katika fani hii. Lakini kwa kiwango kikubwa, wafugaji wengi kama sio wote, hawafaidi ufugaji wao na maisha yao yamekuwa duni na hawajaweza kujiendeleza kwa kutumia rasimali hii kubwa waliyonayo.

Ukosefu wa elimu ya kutosha na wataalam wa kuwaongoza wafugaji, imekuwa kikwazo kikubwa kuendeleza hazina hii kubwa. Ni vyema Serikali ikaweka Mkakati

Maalum wa kuinua sekta hii ili iweze kutoa mchango wake katika Pato la Taifa na kuendeleza maisha ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kuwa kila sehemu ya nchi yetu inafaa kwa ufugaji. Ziko sehemu maalum zinazofaa na Serikali ingetenga sehemu mbalimbali maalumu kwa ajili ya wafugaji. Kama tusipofanya hivyo, mwishoni tutakuta nchi yote imekuwa jangwa. Mfano wa malisho yoyote yale yanayotumiwa na mbuzi, mimea yote hukauka kwani mbuzi akichuna mti na mate yake yakiupata, huathirika na kukauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku wa kutosha hata ku-*export,* lakini cha kushangaza, *super market* karibu zote zinaleta nyama kutoka nje. Hii ni hujuma kwa uchumi wetu. Kwa nini Serikali haizuii uingizaji wa nyama kutoka nje, *unless* kama tuna ugonjwa unaozuia utumiaji wa nyama za hapa au kama hatuna nyama ya kutosha. Kwa kweli sekta ya ufugaji haitakua kama nyama ya ng'ombe, kuku, hata mayai yanatoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali, labda ni kidogo mno kuelimisha Watanzania, kutumia vitu vinavyozalishwa hapa nchini. Kuna kasumba mbaya sana kwenye akili za Watanzania kuwa, kila kitokacho nje ni bora kuliko cha hapa nyumbani. Hii ni hatari kubwa na uchumi wetu hautakua na mwishoni tunakula taka taka toka nje na kuacha chema kilichopo hapa nyumbani. Lazima tuwe na Mikakati Maalum ya kuelimisha watu wetu waelewe sio kila kitokacho nje ni chema, hasa katika dunia ya sasa ya ushindani, lazima tujifunze kujivunia chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaitakia Wizara kila la kheri katika kazi ngumu iliyo mbele yao, kwani Wizara hii ikifanya vizuri, mchango wake utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwakomboa Watanzania kutoka katika lundo la umaskini na afya mbaya, kwani wakijua kunywa maziwa ni hatua moja ya ukombozi.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu wafugaji wetu wa kienyeji. Wafugaji wetu huswaga mifugo yao kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wafugaji hawana elimu yoyote kuhusu malisho kwa mifugo yao. Wanapoamua kulisha wanyama wao wanalisha ovyo ovyo tu. Wafugaji wapewe elimu kuhusu utunzaji mzuri wa sehemu za malisho kwa wanyama wao. Aidha, waelimishwe kulisha mifugo yao sehemu moja kabla ya kuhamia sehemu nyingine, hii itasaidia ukuaji wa majani kadri mzunguko wa malisho utakavyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji pia hawana budi kuwapa chanjo wanyama wao ili kuepusha maradhi mbalimbali. Kuna tatizo linalojitokeza kwa wafugaji wetu. Kuna baadhi ya wafugaji mifugo yao inatoa maziwa vizuri lakini hata siku moja familia yake haipati maziwa. Maziwa yote yanapelekwa kuuzwa, pia hata hiyo mifugo aliyonayo, mfano mbuzi, hata siku moja hawezi kuchinja na watoto wakapata nyama.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa kuwapa elimu wafugaji wetu ili waweze kutumia mifugo yao katika kujenga afya zao. Pia elimu itolewe kwa wafugaji wetu kwani wapo baadhi wanafurahia kuhesabu wingi wa mifugo waliyonayo, badala ya

kupunguza kwa njia ya kuuza na kutumia fedha hizo katika mambo kadhaa mfano, kusomesha watoto wao, kujenga nyumba zenye gharama nafuu na kujipatia lishe bora. Wafugaji wengi wanatumia pesa zao kwa starehe tu ya kunywa pombe lakini hawana hata nyumba bora za kuishi na wala watoto wao hawasomeshwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabucha mengi yanayouza nyama hayapo katika hali nzuri. Ni machache tu ambayo yametengenezwa katika hali nzuri ya kiafya, kwa kuzibwa na vioo kuzuia wadudu kama inzi wasiiguse nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihamasishe wale wenye mabucha, wayaweke mabucha yao katika hali nzuri na ya kuvutia. Pia machinjio yaliyopo mikoani yaboreshwe, kuna baadhi ya machinjio yanakuwa machafu sana, kiasi cha kuweza kumfanya mlaji wa nyama akiona sehemu ile, asiweze kula nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuipongeza Serikali kwa jithada zake za kuweza kutokomeza ugonjwa hatari wa *Rift Valley,* ambao ulileta vifo vya raia kadhaa. Serikali iendelee kuhakikisha kuwa, dawa za kutosha kwa chanjo zipo na wafugaji waendelee kuelimishwa kuhusu athari za ugonjwa huu.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya, ila nasikitika, Serikali imeona ng'ombe kama siyo mali. Ng'ombe ni zao kama mazao mengine. Hata wakati wa njaa, wafugaji hawakuombi msaada wa chakula, badala yake walisaidia watu wengine. Naomba tuwathamini ni muhimu. Ng'ombe waanaweza kutuongezea uchumi kama mipango ikiwa mizuri. Turuhusu viwanda na biashara ya ng'ombe na nchi jirani tupate pesa za kigeni. Ni afadhali wafugaji wenye ng'ombe walipe kodi kwa mifugo yao, badala ya kuwafukuza ovyo ovyo. Wizara imekuwa kama "Futa Mifugo." Wafugaji wamenyanyaswa sana tena sana.

Naomba viongozi waliohusika hasa Wakuu wa Wilaya, ambao wengi wao walitumia nafasi hiyo kujinufaisha, wachukuliwe hatua. Wafugaji wa Karagwe na Biharamulo waliteswa na wengi wao walinyang'anywa ng'ombe wao, wengine walisingiziwa kuwa si raia wa nchi hii ili wachukue mifugo yao. Kwa kweli wafugaji waliteswa na Wapinzani waliwazomea, waliwaambia kuwa waliichagua CCM. Kuna uchonganishi mkubwa sana na Chama. Naomba Serikali ifanye jitihada za makusudi za kujali wafugaji, wapatiwe mabwawa ya kunyweshea mifugo wao.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na wasaidizi wake, kwa hotuba nzuri. Lakini nawapa pole kwa kazi nzito.

Mchango wangu utalenga kwenye eneo moja tu la kuboresha mifugo. Kwenye hotuba zimeelezewa hatua mbalimbali, zinazochukuliwa na Wizara zikiwemo tafiti na mpango au mwongozo wa utoaji huduma za ugani, ambao unasambazwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Kwenye ukanda wa Pwani mwongozo huo haujeonekana. Isitoshe maeneo ya Mkoa wa Pwani, kama wapo Maofisa Ugani ni wachache na hawapo vijijini.

Ingefaa kila kijiji, kata na kadhalika, kiwe na Afisa Mifugo, atakayesaidia kueneza elimu ya mifugo. Vilevile dawa za wanyama licha ya kuwa ghali hazipatikani kwa urahisi. Zipo dawa katika maduka binafsi, lakini hao hao wauzaji, hawana elimu ya kuelezea matumizi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba pia imeelezea uhamishaji wa mifugo kutoka maeneo yenye mifugo mingi kwenda maeneo kusiko na mifugo, hasa kutoka Mkoa wa Mbeya kwenda Mikoa ya Lindi na Pwani. Mlipoanzisha mpango huu mwaka jana, tuliitahadharisha Serikali yafuatayo: Mnahamisha matatizo kutoka eneo moja kwenda lingine; mnaanzisha migogoro baina ya wakulima wa Pwani na wafugaji kwa kugombea ardhi, mazao ya wakulima kuharibiwa na mifugo na kadhalika; na pia Serikali haikufanya maandalizi katika maeneo ya Pwani na Lindi ili mifugo ikifika pawe na malisho ya kutosha, maji na barabara za vijijini.

Kwa kuwa, Serikali haikutusikiliza, sasa matatizo yameanza hasa katika Wilaya yangu ya Kisarawe, kama ifuatavyo: Kwanza, wafugaji wameingia kiholela si kutoka Mbeya tu, hata maeneo mengine ambayo hayakutegemewa kuleta mifugo.

Kwa hiyo, idadi ya mifugo iliyoingia ni kubwa kuliko ilivyotegemewa na sasa tumeleta uharibifu wa ardhi. Tayari migogoro baina ya wafugaji na wakulima, imezuka kwenye Kata yangu ya Mafizi Wilayani Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea jibu jinsi Serikali itakavyochukua hatua za haraka kutatua migogoro hiyo na kuhamisha baadhi ya wafugaji na mifugo yao ili kuepusha madhara katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, sitaunga mkono hoja kama sitaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara kwa hotuba ambayo imegusa karibu sehemu zote za kitengo hiki cha ufugaji. Baada ya hapo napenda sasa kutoa hoja yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ila ninaishauri kupitia Mradi wa *PADEP* kuwa ni wakati muafaka sasa Mradi huu ukashawishiwa kuanza kazi Kanda ya Ziwa kama Mikoa ya Mwanza na Mara, naamini wafugaji wa mikoa hii wamehamasika katika uchangiaji wa Miradi inayowagusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada nzuri kuhusu ugawaji wa ardhi ya malisho ya mifugo, nashauri yafutayo:-

- Itolewe elimu kwa wafugaji jinsi ya kupunguza idadi ya mifugo ikiendana na MKUKUTA, kwake yeye mfugaji hasa. Akilielewa neno MKUKUTA akiwa mfugaji, itapunguza ari ya kutafuta malisho kwa sababu eneo analoishi litamtosha kwa makazi na malisho.

- Kuendelea kuchimba malambo na mabwawa, hasa kwenye maeneo ya wafugaji wakubwa kama Mikoa ya Mwanza, Arusha, Shinyanga, Mara na Singida. Hii ni pamoja na ukame wa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafanya vizuri kujenga au kukarabati majosho katika Wizara hii. Ninaishauri Wizara iweze kuhamasisha wafugaji binafsi, kujenga majosho yao, hasa wafugaji wakubwa. Uwezo huu wanao ila wanahitaji elimu inayogusa gharama na umuhimu wa kuogesha mifugo yao (MKUKUTA).

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kudhibiti Ugonjwa wa Bonde la Ufa. Nashauri vyombo/vifaa vya kupima maradhi yatokanayo na mifugo kwenda binadamu, vinunuliwe na viwe humu nchini. Pia itolewe elimu kwa wafugaji, kuelezea athari za utumiaji wa mizoga ya wanyama wanaokufa na athari hizo.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakupongeza kwa kuliongoza Bunge na usimamizi mzuri. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni moja ya sera na mifugo ina faida kubwa kwetu, faida kwa kilimo, kitoweo (mboga) na kwa utalii na kadhalika. Kwa hiyo, naiomba Serikali, iidhinishe hoja hii, itoe fedha nyingi kwa bajeti hii bila pingamizi, lakini wa usimamizi wa matumizi ya Wizara uwe unaendana na Awamu ya Nne. Ubabaishaji marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya mifugo itolewe, huduma za lazima ziwepo na wataalamu waenziwe na miundombinu yote ya mifugo kwa faida ya nchi yetu. Magonjwa ya mifugo yazidi kudhibitiwa, kuwe na utaratibu mzuri wa kushughulikia magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Wizara kuwe na majosho ya kileo kwa wafugaji wakubwa na wafugaji wadogo pia wawezeshwe kwa mikopo ya fedha ili wafugaji wawe ni wenye kujiajiri na kuajiri wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za mifugo zipatikane kwa urahisi na kwa bei nafuu na kutengewa maeneo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jibo langu la Magogoni, naunga mkono hoja mia kwa mia. Asante.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo katika nchi yetu inakabiliwa na maradhi mbalimbali, hasa yale yanayosambazwa na kupe. Kutokana na uchache wa majosho katika Halmashauri nyingi, kumesababisha kuenea kwa magonjwa hayo, hali inayopelekea kupoteza mifugo mingi.

Kwa kuwa ujenzi wa majosho ni jukumu la Halmashauri wenyewe na kwa kuwa Halmashauri nyingi uwezo wa kukusanya mapato ni mdogo na hivyo, kushindwa kujenga

majosho na malambo ya kutosha; ili azma nzima ya kudhibiti maradhi ya mifugo yanayoenezwa na kupe ni vyema basi Serikali ikachukua juhudi za makusudi, kuzipatia fedha Halmashauri hizo ili ziwezeshwe kujenga majosho na malambo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa dawa za kuogeshea, imetuma Mawakala wa kusambaza dawa hizo. Kadhalika, Serikali inatoa ruzuku katika madawa ya ukogeshaji ili mfugaji aweze kuzipata dawa hizo kwa bei rahisi. Kwa bahati mbaya hali si kama ilivyokusudiwa, dawa za kukogeshea zimekuwa hazipatikani na pale zinapopatikana, zinakuwa za bei ya juu na hivyo, wafugaji kushindwa kuzinunua. Ni vyema basi, Wizara ikaandaa utaratibu mwingine ambao utapelekea wafugaji kupata dawa za kukogeshea pale wanapozihitaji, lakini pia katika bei iliyo nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa kuku na hasa kuku wa nyama, umeshamiri katika miji mbalimbail hapa nchini. Kwa bahati mbaya upatikanaji wa vifaranga umekuwa wa matatizo kutokana na uzalishaji wake kuwa mdogo. Wafugaji wengi wamekuwa wanaagiza vifaranga nje ya nchi ambavyo vinakuwa ghali na mara nyingine vinakufa sana kutokana na maradhi au udhaifu. Kwa kuwa kawaida kifaranga wa nyama anatunzwa kwa wiki sita mpaka nane ili afikie uzito wa kuuzwa, baadhi ya wafugaji kwa kutaka kupunguza gharama za uendeshaji, hutumia homoni *(hormones)* ili kuvikuza vifaranga hivyo kwa muda mfupi zaidi wa wiki mbili mpaka nne. Jambo hili limesababisha madhara kwa walaji wa kuku hao. Miongoni mwa madhara ambayo walaji wamekuwa wanayapata ni pamoja na wanaume kuota matiti, kuota matako makubwa na kutokuota ndevu. Kwa Wanawake mara nyingi madhara yanayoonekana ni kuota ndevu na kuwa na sauti nzito.

Kutokana na madhara haya; je, Serikali inachukua hatua gani kuwadhibiti wafugaji wanaotumia dawa (homoni), kwa kukuzia vifaranga, hali inayosababisha madhara mbalimbali kwa walaji?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara hii, pamoja na Waziri, kwenda Kitengule kule kwenye Ranchi kumaliza ngogoro wa wafugaji. Lakini isiishie hapo, kwa sababu haya matatizo ni ya siku nyingi na matatizo mengi yanasababishwa na ofisi za mifugo mkoa, pamoja na mawilaya.

Serikali iwe mikakati mahususi kwa wananchi wake. Jambo hili la kuwahamisha wakulima na wafugaji liende pamoja kuliko kuchukua maamuzi, kwani kufanya hivyo ni kuwanyanyasa wananchi kwa kuwa Serikali imepata mwekezaji na kuwapa taarifa ya kuwaondoa. Je, mnapowaondoa haraka haraka waende wapi, wakati hakuna maandalizi ya wapi watahamia? Kuanzisha makazi mengine ni jambo baya sana kwa wananchi, si Kitengere peke yake, bali na sehemu nyingine. Naomba nijue kilichosababisha.

Bukoba tulikuwa na Kituo cha Ufugaji na Kilimo, sasa hakipo tena, kilikuwa kinaitwa Makongo. Naiomba Wizara hii ya Mifugo, inipe jibu la kuniridhisha, tuna Kikulula Karagwe, wananchi walikuwa wakipata semina na kukopeshwa ng'ombe,

wananchi walikuwa wanachukua sana lakini sasa wamekata tamaa kwa kukosa sehemu ya kuuza maziwa *fresh* na mgando. Naomba mambo yote niliyoyauliza kwenye mchango wangu huu, nipatiwe majibu ili niweze kujua kama Mkoa wa Kagera hauwezi kufuga. Asante.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake, kwa kuandaa hotuba yenye malengo ya kuboresha huduma za mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rorya ina jumla ya mifugo 418,308. Mifugo inachangia asilimia kubwa ya uchumi wa wananchi. Sekta ya Kilimo hutegemea mifugo, mifugo huchangia lishe bora kwa kulinda, kujenga na kukinga afya za wananchi, vile vile mifugo imewasomesha na inaendelea kuwasomesha wataalamu na viongozi waliopita na waliopo Wilayani Rorya. Kuanzia mwaka 2000 hadi 2004, biashara ya mifugo kupitia minada katika Wilaya ya Rorya, iliwaingizia Wananchi wa Wilaya ya Rorya Sh.3,881,531,400.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Serikali kupitia Mradi wa *DAPS* na *ASDP,* itasimamia mipango ya miradi ya majosho na malambo kwa kuwapeleka wataalamu katika Wizara, kwa kushirikiana na TAMISEMI, katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kuwaelekeza Halmashauri namna ya kuibua miradi ya majosho. Wilaya ya Rorya inayo majosho 28, majosho yanayofanya kazi ni 11 tu. Naomba Wizara itume wataalamu kusaidia kuibua mpango wa mradi wa kufufua majosho 17, ambayo hayafanyi kazi na kusababisha huduma ya tiba kuzorota. Majosho hayo 17 ni Josho la Nyamagara; Josho la Obwere; Josho la Masonga; Josho la Sokorabolo; Josho la Omoche; Josho la Kirogo; Josho la Nyanduga; Josho la Luanda Simbiri; Josho la Panyako; Josho la Ikoma; Josho la Ingri Juu; Josho la Kyabebi; Josho la Ruhu; Josho la Kinesi; Josho la Komuge; Josho la Marasibora; na Josho la Oliyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu yenye matumaini na ninaunga mkono hoja. Asante.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii. Namshukuru Waziri wa Mifugo, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wake wote, kwa hotuba yao nzuri, yenye mwelekeo na kukuza ufugaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo, Serikali itenge maeneo maalumu ya wafugaji ili kuwaondolea usumbufu wa kuhamahama na hivyo kuleta uharibifu wa mazingira na kusambaza magonjwa ya mifugo na kusababisha migogoro na wakulima. Vilevile wajengewe majosho katika maeneo hayo, pamoja na kujengewa mabwawa ya aina mbili; mabwawa na visima na mabwabwa ya kutega au kuvuma maji ya mvua na kuyahifadhi, ili visima au mabwabwa yakikauka, waweze kutumia na kuwapunguzia adha wafugaji ya kwenda maeneo ya mbali kutafuta maji. Pia nashauri wapatiwe dawa, chanjo na madaktari wazuri. Tunaiomba Serikali ijenge viwanda vingi hapa nchini ili wananchi wafaidike na matunda ya nchi yao. Ijenge viwanda vya kusindika nyama na

viwanda vya maziwa, angalau kwa wilaya zenye mifugo mingi nchini, waweze kuajiri. Vilevile wapatiwe masoko ya nje na sisi wenyewe kwanza vijana wetu watapata ajira na wafugaji wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji bora wa kisasa, Serikali ihamasishe ufugaji bora wa kutoa ng'ombe wa kisasa nchini, wafugaji waweze kuzalisha kwa tija, kwa kutoa maziwa mengi na nyama ya kutosha. Ili kufanikisha hayo, wafugaji wapatiwe elimu ya kutosha jinsi ya kufuga ng'ombe hao. Serikali iboreshe miundombinu ili wafugaji waweze kupeleka mifugo yao kwenye masoko kwa ajili ya mauzo na hivyo, kuweza kupata mahitaji yao mbalimbali kama vile chakula, nguo na fedha za kusomesha watoto wao, pamoja na mengineyo.

Natoa shukrani kwa Waziri, pamoja na timu yake, Mungu awape kila la kheri katika utendaji wao wa kazi na awakupe maisha mazuri na bajeti yao mwakani iongezwe ili wafanikiwe vizuri.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara hii na taasisi zake, kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa pongezi za pekee kwa Wizara hii, kwa jinsi ilivyopambana kwa ujasiri na umahiri mkubwa na *Rift Valley Fever*. Aidha, napenda kuipongeza Wizara kwa jitihada zake na mafanikio iliyoyapata katika kupambana na Ugonjwa wa Mafua ya Ndege na maradhi mengine ya mifugo.

Jitihada nyingine za kuboresha mifugo na kuleta mapinduzi kutoka uchungaji wa kuhamahama na kuleta ufugaji wa kisasa na mifugo bora zaidi, zinastahili pongezi. Vile vile jitihada za kuongeza malambo na majosho, pamoja na uzalishaji wa malisho bora, zinastahili pongezi. Hata hivyo ni bahati mbaya, kwani Wizara hii haijatambua na kuupa Mkoa wa Tanga, msukumo kwa kiwango cha kutosha. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Chama cha Ushirika cha Wafugaji wa Mkoa wa Tanga *(TDCU)* na wadau wengine, bado Wizara haioneshi dalili ya kuunga mkono kwa kipaumbele kinachostahili jitihada hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana *TDCU,* imekuwa ikiiomba Wizara iruhusu *TDCU* iendelee kutumia sehemu ya eneo la *LITI Buburi* kwa uzalishaji na uendelezaji wa mitamba na hatimaye kuwa na mifugo bora na mingi zaidi. Wizra imeonesha uzito mkubwa katika kuruhusu *TDCU* iendelee na mipango yake hiyo. Athari ya kutopata kibali hicho ni kukwamisha upanuzi wa uzalishaji na uboreshaji wa mitamba. Aidha, mipango ya upanuzi wa Kiwanda cha Maziwa cha *Tanga Fresh* inakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha wafugaji Mkoani Tanga kimeongeka kutokana na Kiwanda cha Maziwa Tanga *(Tanga Dairy)* kubinafsishwa kwa wawekezaji ambao wamekigeuza kiwanda hicho kuwa karakana ya matrekta. Hili linafahamika kwa Wizara, lakini ahadi yao ya siku nyingi, kuliingilia kati suala hili, hakuna dalili ya hilo kufanyika na hivyo kuendelea kudumaza ufugaji na uzalishaji wa maziwa Mkosni Tanga.

Wilaya ya Mkinga ina nafasi kubwa sana ya kuendeleza sekta ya mifugo na kuchangia zaidi Pato la Taifa. Ili wilaya hii iweze kuitumia fursa hii ipasavyo, kuna umuhimu mkubwa kwa wilaya hii kupewa kipaumbele maalumu, kwa kuipatia kwa kiwango cha kutosha, maafisa ughani, malambo, majosho, malisho, dawa, machinjio ya kisasa, mitambo ya kuhifadhia na kusafirisha maziwa mikoani, mafunzo, taarifa za masoko na ulinzi wa kutosha, dhidi ya waporaji kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, upimaji wa ardhi na utengaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya maendeleo ya mifugo ni muhimu, sio tu kuepusha mapambano kati ya jamii za wafugaji na wakulima, bali pia kuwezesha shamba darasa, kuwezesha ushindani miongoni mwa wakulima na ubora wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa hongera kwa kazi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na mifugo mingi, lakini hakuna viwanda vya nyama:-

(a) Kuna juhudi gani za kuwa na viwanda katika maeneo ya mikoa yenye mifugo wengi mfano, Shinyanga, Mwanza, Mara, Singida na Tabora?

(b) Pamoja na uhaba wa fedha au wahisani, nashauri juhudi zifanywe ili angalau kiwanda kilichoharibika kwa muda mrefu Shinyanga kifanye kazi.

(c) Je, upo mpango wowote wa kuanzisha machinjio ya kisasa hasa katika maeneo ya mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo wengi wanauzwa kwa mnada (bila kupimwa uzito), utaratibu unaompunja sana mfugaji, kwani ni wa kubahatisha. Je, Wizara ina mpango gani wa kubadilisha mfumo huo wa mauzo ili uwe wa kutumia mizani?

Mazao ya chakula hupewa ruzuku kwa pembejeo mfano, mbolea, je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa madawa ya kuoshea mifugo? Je, Wizara inafahamu kuwa Mabwana Shamba (Maafisa Kilimo), ndio wanaofanya kazi kwa niaba ya mabwana mifugo ambao hawapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema Wizara hii muhimu, ingawa bado inaitwa sekta ndogo. Sekta ndogo ambayo ina faida nyingi; maziwa, nyama, ngozi, mbolea na pesa; kwa nini mnaidharau sekta kubwa na kuiita ndogo? Jifunzeni wenzetu wa Botswana walivyoithamini na kufaidika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara iendelee kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima ili kuondoa migongano ambayo mpaka sasa inaleta usumbufu sana, maeneo karibu yote hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi wananchi wetu wanaoishi vijijini, wana shida sana ya kupata dawa za mifugo yao, dawa zinazopatikana bei ni kubwa sana hivyo, kushindwa kulipia au ni dawa ambazo muda wake unakuwa umekwisha. Naomba sana Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, waone uwezekano wa kufikisha dawa karibu na wananchi.

Mpaka leo huko vijijini, vyeo vya Bwana Shamba na Bwana Mifugo, huko nyuma walikuwa pamoja lakini siku hizi wametengana na hata mafunzo wanayochukua ni tofauti. Kwa hiyo, vyeo hivi vitenganishwe kabisa, kwani kutumia vyeo vyote viwili ni kutowatendea haki wananchi. Mpaka sasa tuna upungufu sana wa Maafisa Mifugo, naomba Serikali iajiri wa kutosha na kuwapeleka kila kijiji. Majosho mengi hapa nchini yameharibika, naomba sana Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, wasaidie tatizo hili. Bado wananchi wetu wengi wanafuga na kuwa na ng’ombe wengi kupita kiasi. Naomba elimu itolewe kwao ili wapunguze mifugo yao na kufuga kisasa kupata ng’ombe bora wa nyama na maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana elimu iendelee kutolewa na sheria zirekebishwe ili kukomesha, kwani tatizo hili husababisha kuharibu mazingira sana kwa kufyeka miti ili wapate maeneo ya kuishi na pia kufyeka maeneo makubwa ili kuwafukuza wanyama wakali na ndorobo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache narudia kukupongeza na kuomba mwaka 2007/2008, kuwe na mabadiliko makubwa kwa upande wa wafugaji kwa faida ya Taifa hili.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELE YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Nianze kwanza kwa kutamka kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini, kutoa pole kwa familia ya waliokuwa Wabunge wenzetu ambao kwa mapenzi ya Mola wetu walitutoka mwaka huu. Pia natoa pole kwa familia za wahanga wote wa ajali mbalimbali za barabara zilizotokea Arusha na Singida, zilikuwa kubwa. Vile vile natoa pole kwa Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed - Mbunge wa Donge na Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwa kufiwa na mama yake mpenzi. Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za Marehemu wote. *Amen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Ilemela na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kwa kunishirikisha vilivyo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Namshukuru pia Katibu Mkuu Dr. Charles

Nyamlunda, Naibu Katibu Mkuu Dr. Jonas Nywelewasi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaonipa katika kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba niishukuru sana familia yangu hususan mke wangu Leonsia Mwailwa na watoto wangu ambapo wa mwisho Francis Mlingwa anakaa na mama yake. Kwa kuendelea kunipa moyo katika utendaji wangu wa kulitumikia Taifa. Waliobaki watoto wangu, wako shule za *boarding*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Shinyanga, Mjini kwa ushirikiano wanaonipa kama mwakilishi wao hapa Bungeni. Naendelea kuwaahidi utumishi mwema *inshallah* kwa kipindi chote cha miaka mitano.

Kwa niaba yao, naishukuru sana Serikali kwa kuwezesha kupatikana mwekezaji katika kiwanda cha Nyama cha Shinyanga. Aidha, naishukuru taasisi ya Kalitasi Tanzania hususan Mhashimu Askofu Aloisusi Balina kwa kuanza ujenzi wa Kiwanda cha Maziwa Shinyanga pamoja na vituo vya kukusanyia maziwa kutoka kwa wafugaji, mradi unaosimamiwa vizuri sana na Meneja anaitwa Mikomangwa. Nafahamu pia mamlaka ya mgodi wa almasi wa Mwadui una mpango wa kufufua kiwanda cha maziwa kilichopo Mwadui. Nikiwa mwana Shinyanga naahidi ushirikiano wangu ili azma hii nzuri ya mgodi iwe kweli na Serikali inawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nianze kutoa maelezo ya hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, zilizojitokeza katika hotuba ya bajeti Waziri wangu. Pia nitatoa maelezo kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hotuba za mipango na Bajeti za Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu na kadhalika.

Nasema, baadhi, kwani Mheshimiwa Waziri, atawatambua Waheshimiwa Wabunge wote muda mfupi ujao atakapokuwa anahitimisha hoja yake. Naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Nakuhakikishia kwamba tunathamini sana michango yao na tunawaahidi kuwa itazingatiwa katika utekelezaji wa mipango ya Wizara yetu na watapata majibu mahususi kwa kila mmoja. Hivyo kwa heshima na taathima nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mpitishe bajeti ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa maelezo kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge, nimegawanya katika muundo ufuatao: kwanza hoja kuu, halafu Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja mahususi pale inapowezekana na maelezo mahususi au ya jumla kama pale michango yao ilikuwa inafanana. Nitaanza na wale waliochangia kwenye hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Wale waliozungumza, Mheshimiwa Felister Bura, yeye alizungumzia kuhusu kujenga kiwanda cha kusindika nyama Dodoma. Maelezo ni kuwa machinjio ya Dodoma ambayo imepata mwekezaji itapanuliwa ili kuweza kusindika nyama. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, mfugaji mwenzangu, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Juma Killimbah, wote walizungumzia ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo nchini. Maelezo ni kuwa Serikali imedhamiria kuinua uzalishaji wa nyama nchini na tayari imeitangazia sekta binafsi kujitokeza kushirikiana kujenga machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Mwanza na Pwani.

Mheshimiwa Juma Killimbah alikuwa mahususi katika Mkoa wake wa Singida. Maelezo ni kwamba matangazo kwa ajili ya Mikoa mingine ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Singida, kuhusu viwanda vya kusindika mazao ya Mifugo itatangazwa baadaye. Kwa sasa wafugaji wa Singida wana shughuli ya kutumia kiwanda cha nyama au machinjio ya Dodoma. Waliochangia kwa maandishi ni wafutao:

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Juma Said Omar, Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Mgeni Kadika na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum. Hawa walizungumzia ujenzi wa viwanda ikiwa ni pamoja na viwanda vya kuku. Serikali inakaribisha wawekezaji ili tuweze kushirikiana kama nilivyosema.

Aidha, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Lekule na Mheshimiwa Fuya Kimbita walizungumzia viwanda vya ngozi, Kiwanda cha Ngozi cha Moshi kinachomilikiwa na *IPS* kinafanya kazi kwa sasa na kinasindika ngozi za ng'ombe 12,000, mbuzi na kondoo 48,000 kwa mwezi.

Kuhusu miundombinu ya mifugo, yaani malambo, majosho na minada, Waheshimiwa Wabunge, wengi walizungumzia ujenzi wa Malambo, Majosho na kadhalika. Hawa walikuwa ni Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Capt. John Chiligate, Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Luhaga Mbina, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Diana Chilolo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ephraim Madege, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Fuya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Salim Hemed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kilwa, ningependa kulisema makusudi kwamba malambo mawili ya Malandego na Matandu yamekwishajengwa tayari. Jibu la ujumla la Waheshimiwa Wabunge, waliozungumzia suala la malambo ni kwamba wananchi wanashauri kupitia Halmashauri zao kuibua miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo ikiwa ni pamoja na malambo, majosho, minada kupitia *DADPs*.

Aidha, minada hiyo iwekewe mizani ili kuweza kupima mifugo ili pale mifugo inapouzwa isiuzwe kwa kukadiria bali kwa kupimwa. Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi kwa mahususi alisema, kwa kuwa Wilaya ya Rorya ni Wilaya mpya, sasa inahitaji majosho 17.

Tunapenda kumhakikishia Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi kuwa tutafika Wilaya mpya ya Rorya kushughulikia majosho kupitia *DADPs*.

Waheshimiwa Wabunge, waliozungumza kuhusu ruzuku ya madawa ya mifugo ni Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Kimbita, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Vuai Khamisi, Mheshimiwa Juma Omar, Mheshimiwa Meryce, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Kimwanga, Mheshimiwa Alyoce Kimaro na Mheshimiwa Lucas Selelii.

Maelezo ni kuwa kampuni inayosambaza dawa kwa Mkoa wa Arusha mahususi kwa ajili ya Mheshimiwa Lekule Laizer ni *Mukpa Tanzania Limited* na Msambazi ni *codes* kwa Wilaya ya Longido. Orodha ya kampuni nane zilizoingia mkataba na Serikali kwa kuagiza na kusambaza dawa za ruzuku. Mikoa iliyopokea dawa hizo, aina na kiasi cha dawa na bei zake imefafanuliwa kwa undani katika kiambatanisho cha hotuba ya Maendeleo ya Mifugo, namba 12. Serikali pia imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kama ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, Waheshimiwa Wabunge, pia waliongelea suala la ardhi na malisho kwa ajili ya wafugaji ambao ni Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Lekule Laizer tena na Waheshimiwa Wabunge wengi. Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Mwanawetu Said, Mheshimiwa Mtutura Abdallha Mtutura, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Zaynab Vulu. Hoja ilikuwa ni ardhi na malisho kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwapatia wafugaji maeneo ya kudumu, Serikali kupitia Halmashauri zake ina utaratibu wa kuainisha na kupima maeneo kwa ajili ya ufugaji kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la mbung'o Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda na Mheshimiwa Lekule Laizer, mfugaji mashuhuri. Maelezo ni kuwa Halmashauri zinaomba kuingiza kwenye mipango ya *DADPs* mikakati ya kuzuia na kutokomeza mbung'o. Kuna dawa za kuogesha zinazoua kupe pamoja na mbung'o kwa wakati huo huo. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itatokomeza mbung'o kupitia kampeni ya kutokomeza mbung'o Barani Afrika, kwa kifupi *PATEC* inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za ugani na elimu kwa wafugaji, hoja hii ilizungumziwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Michael Lekule na

Mheshimiwa Felister Bura. Maelezo ni kuwa, mafunzo yanatolewa kuhusu ufugaji bora kupitia vyuo vyetu tulivyonavyo. Aidha, Halmashauri zinashauriwa kutoa mafunzo kwa wafugaji kupitia *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwa namna ya pekee kutambua mchango wa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ambaye pamoja na mambo mengine alimwomba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo au mimi Naibu wake tutembelee Wilaya ya Kilindi. Tunamuahidi Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kwamba tutafika Wilaya ya Kilindi, tunatambua nafasi yake katika suala la wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mheshimiwa Serukamba alizungumzia suala la mikakati ya kuendeleza zao la nyama. Tunakubaliana na ushauri wake na tutazingatia katika kuandaa mikakati na kutekeleza sera ya Taifa ya mifugo. Mheshimiwa Lekule Laizer alizungumzia *ranch* ya *West Kilimanjaro*. Hili Mheshimiwa Waziri atalizungumzia. Mheshimiwa Sevelina Mwijage alizungumzia mgogoro wa mipaka katika *ranch* za Kitengule na Misenyi, hili atalizungumzia Mheshimiwa Waziri wangu. Mheshimiwa Estherina Kilasi alizungumzia utoaji wa hati miliki kwenye *ranch* kwani hata kwenye Wilaya yake ya Mbarali kuna *ranch* ya Usanga. Zoezi la utoaji hatimiliki linaendelea ikiwemo *ranch* ya Usangu.

Kuhusu suala la utafiti wa mifugo na udhibiti wa magonjwa, Mheshimiwa George Lubeleje alizungumzia uboreshaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Felister Bura, alizungumzia suala la homa ya Bonde la Ufa na kusisitiza kuimarisha maabara. Maelezo ni kuwa Serikali imeimarisha taasisi hiyo na kwa sasa ina kasma yake. Mchakato wa sheria wa kuanzisha taasisi umeanza na imeelezwa kwenye hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Maabara ya kuchunguza magonjwa ya mifugo ikiwa ni pamoja na homa ya bonde la ufa imekamilika kule Dar es Saalam.

Kuhusu utambuzi, usajili na ufuatiliaji na ustawi wa wanyama, suala hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina, pamoja na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, ambaye Mheshimiwa Mpina, alisema uandikishwaji na usajili wa mifugo hii, pengine utaleta urasimu kwa wafugaji hasa anapouza mifugo yake na kwamba *register* ya Taifa ya Takwimu inahitaji ushirikishwaji wa ngazi zote kuanzia kijiji, kata, Wilaya na akauliza: Je, Serikali imejipanga vipi? Maelezo ni kuwa utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji utaweka mazingira ya kuhakikisha rasimu wa lazima unaepukwa kwa kushirikisha wadau wakati wa maandalizi yake na kwamba Wizara itatoa mafunzo kwa wagani katika ngazi za Wilaya hadi kata jinsi ya kuweka kumbukumbu za kuwezesha *register* hiyo kufanyakazi katika ngazi za chini. *(Makofi)*

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura, yeye alitaka kujua Serikali itoe tamko la kukomesha ukatili wa kuning'iniza kuku miguu juu kichwa chini. Maelezo ni kuwa uning'inizaji kuku ni mateso kwa wanyama hao na Serikali iko mbioni kuboresha sheria ya ustawi wa wanyama inayotarajiwa kufikishwa kwenye Bunge lako Tukufu hivi

karibuni ambayo itadhibiti vitendo vyote vya ukatili wa wanyama wakiwemo kuku. Sheria itazingatia utoaji wa elimu wa umma kukazia utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwenye hotuba za bajeti zilizotangulia kwanza suala la viwanda vya nyama, machinjio ya kisasa, maziwa na soko la mazao ya mifugo, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq alizungumzia kwamba Serikali iongeze ushuru wa nyama za kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani hususan wawekezaji binafsi yaani wazalendo.

Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa alitaka ushuru katika maziwa kutoka nje uongezwe ili kulinda maziwa ya ndani. Mheshimiwa Lucas Selelii, yeye amezungumzia tena leo hapa kwamba nyama ya kuku kutoka nje ya nchi ipigwe marufuku ili kulinda soko la ndani.

Maelezo ni kuwa, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, kuwa ni vyema kulinda viwanda vya ndani hasa pale vinaposhindana na wazalishaji kutoka kwenye nchi zenyewe uwezo wa kutoa ruzuku. Serikali inatekeleza hili kwa kuzingatia taratibu za mikataba ya kimataifa ikiwemo shirika la biashara duniani, katika biashara mbalimbali ikiwemo biashara ya nyama. Pia, Serikali inatoza ushuru kwa mazao ya mifugo kutoka nje kwa mfano nyama na maziwa yanayoingizwa nchini kama ilivyo kwa bidhaa nyingine.

Aidha, bidhaa za nyama ambazo zimekuwa zikiingizwa hapa nchini ni tani 1000 tu hii ni sawa na asilimia 0.25 ikilinganishwa na uzalishaji na ulaji wa takriban tani 400,000 hapa nchini kwa mwaka 2006/2007. Bidhaa hizo zimekuwa zikilenga masoko yenye mahitaji maalum kama migodi, maduka makubwa *(super markets)* na hoteli za kitalii. Hivi sasa bidhaa za nyama zinazozalishwa hapa nchini zimeanza kupenya katika masoko hayo yaliyoko hapa nchini.

Pia ni mategemeo yetu kwamba kuongezeka kwa viwanda vya kuzalisha nyama kama vya Safi kilichoko Sumbawanga, *Tanzania Pride Meat* kilichoko Morogoro na majichinjio yetu ya Dodoma na vingine vitakavyojengwa kufufuliwa au kupanuliwa kutaongeza uzalishaji na mauzo ya nyama bora katika soko hili maalum hapa nchini na kwa bei ya ushindani. Zaidi ni kuwa katika kulinda soko la ndani la maziwa, Serikali iliondoa kodi ya *VAT* katika vifungashio vya maziwa, iliongeza kodi katika maziwa yanayotoka nje kwa asilimia 20 na ushuru wa forodha kwa asilimia 15 kuanzia mwaka 2001. Ushuru huu umesaidia kwa kiwango kikubwa kufanya bei ya maziwa yanayoingizwa nchini kuwa na ushindani wa haki na bidhaa za maziwa yanayozalishwa hapa nchini. Pia Serikali imezuia uingizwaji wa nyama ya kuku kuja nchini kutoka nje kutokana na tishio la ugonjwa wa mafua makali ya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa James Lembeli na Mheshimiwa Ahmed Salum wote ni Wabunge wa kutoka Mkoa wa Shinyanga walitoa shukrani kwa Serikali kupata wawekezaji wa kukufua Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga na wakatarajia kuwa kiwanda cha nyama cha Mbeya pia kimepata na kwamba itasaidia kuongeza pato la wananchi wa Mikoa hiyo. *(Makofi)*

Pia walizungumzia ukweli kuwa sasa wafugaji wa Shinyanga watapata soko la uhakika la mifugo yao. Maelezo ni kuwa tumepokea shukrani hizo na nimezungumzia hapa mwanzoni kwenye utangulizi. Pia nakubaliana na Mheshimiwa Joyce Machimu kuwa viwanda hivyo na vingine vitakavyojengwa vitasaidia kuongeza thamani ya mifugo yetu, hivyo kuongeza pato la wananchi na ajira hususan kwa wananchi wa mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kimepata mwekezaji ambaye kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo ilivyosema, ni *Tripple 'S' Limited,* kinatarajia kuzalisha tani 6,000 za nyama kwa mwaka. Kiwanda hicho kitaongeza idadi ya ng'ombe watakaochinjwa na ni changamoto kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga wenye mifugo mingi kuongeza uvunaji wa mifugo bora kwa ajili ya kiwanda hicho, ili kuinua kipato chao na kuondoa umaskini. Kiwanda cha Nyama cha Mbeya hakikupata mwekezaji kupitia *PSRC* kwa kushirikiana na Sekta ya binafsi. Serikali itakamilisha ujenzi wa kiwanda hicho kupitia mpango wake wa kujenga viwanda vipya na kufufua vilivyopo.

Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, alisema Serikali iendelee kuwahamasisha wananchi wazalendo kuwekeza katika sekta ya mifugo kama yeye alivyowekeza kwa kuwa na kiwanda cha nyama na machinjio ya kisasa.

Nampongeza Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya - Mbunge wa Kwela na wawekezaji wengine waliojitokeza kuwekeza katika sekta ya mifugo. Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji nchini kupitia dira ya Taifa ya mwaka 2025, MKUKUTA - Sera ya Taifa ya mifugo na Sera mbalimbali ambazo zinatoa fursa kwa wananchi wazalendo kuwekeza hapa nchini, kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, umahasisishaji unafanyika kwa kuwashawishi wananchi kuunda vikundi na Vyama vya Ushirika kushirikisha Sekta binafsi katika kutoa huduma mbalimbali za mifugo na katika viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo. Aidha, Serikali imehamasisha uwekezaji kwa kugawa sehemu za ranchi za *NARCO* kwa wawekezaji wazalendo 125 na kati yao 96 wameanza kuwekeza kwa kufuga, kwa sasa, jumla ya ng'ombe 25,000. Serikali imedhamiria kushirikiana na sekta binafsi katika ujenzi na uendeshaji wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, tayari matangazo yamekwishatolewa magazetini. Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, tena alizungumzia viwanda vya nyama na machinjio ya kisasa pamoja na masoko yajengwe maeneo ya wafugaji kama vile Shinyanga, Singida, Tabora, Mwanza, Mara, Arusha na kadhalika. Serikali inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, ambaye hata leo amezungumzia hapa. Serikali imedhamiria kama nilivyosema kuinua uzalishaji wa nyama nchini. Kama nilivyosema tayari Serikali imekwishatangaza kujenga machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika katika mikoa ya Arusha, Kagera, Mara, Mwanza na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa James Lembeli aliomba viwanda vya ngozi na viwanda vya maziwa vijengwe Kahama. Serikali inahamasisha sekta binafsi ikiwa ni pamoja na wananchi wa Kahama kujitokeza kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya ngozi na vya maziwa. Serikali itakuwa tayari kushirikiana na wawekezaji hao katika Wilaya ya Kahama, Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Michael Lekule Laizer, alisema Serikali iwasaidie wafugaji kupata soko la uhakika la mifugo yao kwa vile soko la nchi jirani lina usumbufu mwingi. Serikali imejenga minada mipakani ili kurahisha biashara ya mifugo na nchi jirani. Minada hiyo ni ya Longido na Wasso iliyoko Loliondo. Magena - Tarime, Lukole - Karagwe, Murusagamba – Ngara, Buhigwe – Kasulu, Kasesya - Sumbawanga Vijijini, Munga – Rombo na Kileo - Mwanga. Serikali inasisitiza matumizi ya minada mipakani.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na *TCIAA* imeanzisha mtandao wa kutoa taarifa za masoko na bei za mazao ya mifugo. Nchi za *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeanza utaratibu wa mashauriano kuhusu biashara za mipakani. Wafugaji wa Arusha hususan kwa Mheshimiwa Lekule, wameanza kuuza mifugo yao katika machinjio ya *Arusha Meat Company* iliyoko Sakina inayomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Arusha na mimi mwenyewe nilikwishaitembelea. Wanauza kwa bei nzuri zaidi kuliko nchi jirani. Mheshimiwa Lekule Laizer na wafugaji wa Mikoa jirani watumie fursa hiyo.

Kuhusu suala la ngozi, Mheshimiwa Kabwe Zitto, alizungumzia kuwa uzalishaji wa vipande vya ngozi ulipungua kwa mwaka 2006/2007 kutokana na ukame wakati nyama iliongezeka zaidi. Zaidi, alisema, uzoefu umeonyesha wakati wa ukame wanyama wanachinjwa zaidi. Sasa iweje vipande vya ngozi vipungue? Maelezo ni kuwa takwimu zilizonukuliwa na Mheshimiwa Mbunge ni sahihi. Ni za mwaka 2006 ambapo ngozi zilipungua kutokana na ubora hafifu uliotokana na ukame wa mwaka 2005/2006 na hivyo kutonunuliwa. Aidha, katika mwaka 2006/2007 uzalishaji wa ngozi uliongezeka ambapo jumla ya vipande 4,796,630 vya ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zilizalishwa ikilinganishwa na vipande 4,010,000 zilizozalishwa mwaka 2005/2006.

Aidha, katika kipindi hicho, kiasi cha tani 370,566 za nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo zilizalishwa ikilinganishwa na tani 88,294 ikiwa imepungua kidogo. Mheshimiwa Waziri alilizungumzia kuwa hili lilitokana na wananchi kuogopa kutokana na homa la bonde la ufa. Kuhusu ufugaji wa kisasa, Mheshimiwa Fuya Kimbita alizungumzia ufugaji wa kisasa utiliwe mkazo hasa Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Sera ya Serikali kuhimiza ufugaji wa kisasa na kwamba Kanda ya Kaskazini kati ya kanda ambazo ufugaji wa kisasa umetiliwa mkazo sana. Katika Kanda hiyo inayojumuisha Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara kuna jumla ya ng'ombe wa maziwa 268,200 sawa na asilimia 52.3 ya ng'ombe wa maziwa nchini na kwamba kwa sasa mbuzi wa kisasa 86,365 sawa na asilimia 29.4 ya mbuzi wa kisasa waliopo nchini wako Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi kuhusu uuzaji wa mazao ya mifugo nje, Mheshimiwa Fuya Kimbita aliendelea kusema mazao ya mifugo hususan nyama ziuzwe nchi za nje ili kuchangia pato la Taifa. Maelezo ni kuwa, nyama ng'ombe, mbuzi,

kondoo imeanza kuuzwa nje kuanzia mwezi Mei, 2006. Katika mwaka 2006/2007 jumla ya tani 92 za nyama zenye thamani ya shilingi milioni 352 ziliuzwa nje. Mauzo mengine nje yanafanywa kupitia mifugo hai ambapo ng'ombe 2,542 na mbuzi 1,852 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.03 waliuzwa. Kutokana na kujengwa kwa machinjio ya kisasa na viwanda vipya inatarajiwa mauzo ya nyama nje yataongezeka.

Kuhusu mchango wa sekta ya mifugo katika uchumi wa nchi, Mheshimiwa Wilson Masilingi alisema, mifugo ipewe kipaumbele ili iweze kuchangia pato la Taifa. Aidha, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii alisema Serikali kwa makusudi iimarishe sekta ya mifugo. Maelezo ni kuwa katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini (MKUKUTA), mifugo imepewa kipaumbele ili iweze kuchangia kikamilifu pato la Taifa na kumwondolea mwananchi umaskini. Katika muundo wa Serikali, Sekta ya Mifugo imepewa kipaumbele kwa kusimamiwa na Wizara kamili ili iweze kupewa raslimali ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamis Kagasheki, alisema Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa wingi wa mifugo. Hata hivyo, Sekta hii haijatumika kikamilifu katika kuinua pato la Taifa. Maelezo ni kuwa, jitihada za Serikali za kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika pato la Taifa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Sera ya Taifa ya mifugo ya mwaka 2006. Kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini, kuweka mazingira mazuri, kutoa fursa na kushirikisha sekta ya binafsi kama nilivyosema na wadau wengine kuwekeza katika sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tafsiri ya sekta ya mifugo, hili limekuwa ni suala la mara kwa mara. Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii analizungumzia kwamba pengine Sekta ya Mifugo imedharauliwa kwa kuitwa sekta ndogo. Hii sio kweli. Mifugo ni sekta kamili inayosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo. Kwa hiyo, huo ni uzito mkubwa. Hata hivyo, kulingana na tafsiri ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Taifa, mifugo ni sehemu ya sekta pana ya kilimo inayojumuisha mazao, mifugo, misitu, nyuki au asali na samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilikuwa ni nyingi za Waheshimiwa Wabunge, lakini kama nilivyoahidi tutahakikisha kuwa kila Mheshimiwa Mbunge anapata majibu yanayostahili na kama nilivyosema, hii ni changamoto kwetu ya kuhakikisha kuwa michango waliyotoa tutaijumuisha katika mipango ya kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa kumalizia, napenda kusema tena kuwa, kwa asilimia 100, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba nimwite mtoa hoja, atakayetumia kama dakika 20. Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda pia kusema kwamba Wabunge wote

waliochangia hoja hii ni 58 na kati yao 45 wamechangia kwa maandishi na 13 wamechangia kwa kuzungumza.

Lakini pia wapo kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, Wabunge 28 ambao walichangia kupitia Bajeti za Wizara mbalimbali hasa ya Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uendeshaji, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Cheyo - Mbunge wa Ileje na Wajumbe wote. Taarifa yao ya Kamati iliyosomwa kwa niaba yao na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe. Ni wazi kwamba hotuba yao imetusaidia sana na itatusaidia sana mbele ya safari katika kutekeleza yale ambayo tunatakiwa kuyafanya kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda moja kwa moja kuwatambua wote wale waliochangia katika hotuba yangu leo hii. Kwanza kabisa nianze na waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ambao ni Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Felista Aloyce Bura, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Khalifa Khalifa na Mheshimiwa Naibu Waziri na Dr. Charles Ogesta Mlingwa - Mbunge wa Shinyanga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliochangia kwa maandishi, ningependa pia niwataje haraka haraka. Ni Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Kabuzi Faustin Rwilomba, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Ahmed Ali Salim, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Zainab Vulu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Juma Said Omar. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mheshimiwa Hemed Mohammed

Hemed, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Philemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunashukuru sana kwa michango na ushauri na kwa njia moja au njia nyingine tunaweza kusema ushauri fasaha sana uliotolewa na baadhi ya wachangiaji ambao wanaifahamu vizuri sekta ya mifugo. Mengi ya maswali na hoja zao zimejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ni vyema pia kutambua kwamba hoja nyingi ambazo zimejenga *foundation* ya mazungumzo ya leo zilitolewa na Kamati ya Kilimo na Ardhi ambazo nyingi tumezijibu, lakini nitapenda kurudia maeneo machache ambayo yamekuwa yakijirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kujua kwamba baada ya Serikali kujitoa kwenye shughuli za biashara, tulijitoa pia kwenye maeneo mengi. Mfano, maeneo ya kujenga na kuendesha majosho, shughuli hiyo ilihamishiwa kwenye Halmashauri ambazo nazo zingesimamia wafugaji ili wajiunge kwenye vikundi na kuendesha majosho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majosho hayo wakati sera hii tunaianza yalikuwa kwenye hali nzuri sana, lakini tukafika mahali usimamizi na yale ambayo tuliyategemea kutoka kwa wananchi na wafugaji hayakufanyika. Sasa kidogo utaona kwamba mambo mengi sana yanayotukwaza kwenye magonjwa ya mifugo yanatokana na ukosefu wa kinga kwa wanyama hawa na ukosefu wa pembejeo ambazo zinatakiwa kusambazwa na sekta binafsi.

Lakini hata pale ambapo Serikali za Mitaa au Halmashauri zilipoweza kusaidia matunzo ya majosho hayo imekuwa matatizo sana. Kwenye sehemu ambayo ni malambo, matengenezo yake yamekuwa mabovu, malambo mengi sana yameharibika na maeneo mengi sana ambayo tulitarajia kwamba mambo yangekwenda vizuri hayakwenda kama yalivyotarajiwa. Kwa hiyo, ni changamoto, sisi ndiyo tunaangalia sekta hii. Ni jukumu letu kuangalia mbinu ambazo zinaweza kusababisha kuibua ari na kuinua ubora wa mifugo yetu ili iweze kupata soko nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi nyingi watu wanaofanya *export* ya nyama ya mazao ya mifugo. Kawaida ni *private sector* na *private sector,* usitegemee kwamba yule mfugaji aliyeko Singida kwa Mheshimiwa Killimbah, ndiyo yatakayopeleka nyama Uarabuni.

Ni kawaida kabisa kwamba hili tabaka la kati la wananchi ambao Waheshimiwa Wabunge tuko kwenye hiyo *middle class* ndiyo wanatakiwa kufanya hizi biashara za kunenepesha mifugo, unapeleka kwenye machinjio kama alivyoshauri Mheshimiwa mchangiaji hapa, nadhani alikuwa Mheshimiwa Bura. Unanenepesha, halafu unapeleka kwenye mnada au kwenye kiwanda cha machinjio au kwenye kiwanda cha nyama, wananunua mifugo na kuchinja kwa ubora unaotakiwa na kuuza nchi za nje.

Tusitarajie kabisa kwamba mfugaji yule mdogo akafanye hii biashara ya kuuza nje, ni lazima tuendeleze hii *middle class* na kila siku nadhani kuanzia mwaka jana tunashauriwa Waheshimiwa Wabunge tuingie kwenye hii biashara. Napenda niwashukuru sana baadhi ya Wabunge waliomo humu ndani ya Ukumbi huu, wameingia kwenye hiyo biashara na nina hakika kwamba watafanya kweli badala ya kufanya kitu ambacho ungetegemea kwamba mfugaji anayetembea na mifugo angekifanya kwa sababu soko la nje linajali sana ubora. Soko la nje linajali sana kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, kujua hii nyama inatokana na ng'ombe alizaliwa wapi. Wanataka wafahamu kwamba hii nyama imechinjwa tarehe ngapi na kiwanda kipi?

Sasa takwimu hizo zote za utunzaji wa takwimu za namna hiyo, hauwezi kufanywa na mkulima yule mdogo na ndio maana Serikali yetu kwa ujumla tumekubaliana kama Sera turudishe kwa ku-*support private sector* ili tuanze kujenga tena viwanda ambavyo ndiyo itakuwa soko la kudumu la wananchi. *(Makofi)*

Ni kweli leo mkulima au mfugaji aliyeko Kilosa ukimwambia apunguze mifugo, atakwambia niuze wapi? Nionyeshe soko liko wapi? Unakuta ng'ombe wake anauzwa kwa Sh. 60,000/=, hawezi kukubali! Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wametushauri na nina hakika utaratibu wetu wa kuanzisha ranchi ndogo ndogo na kuanzisha viwanda vya nyama, maana kuna *category* karibu tatu. Kuna machinjio ya kawaida ya Miji na Manispaa. Hao nao wanatakiwa kufuata taratibu ambazo zinaleta ubora wa nyama inayouzwa kwa walazi wa maeneo yale.

Lakini pia kuna machinjio ambayo yanachinja na kuuza nyama kwenye vipande vikubwa kama hii ya Dodoma. Hii unachinja kwa utaratibu unaokubalika na unaweza kuuza nyama kwa mapande kama ni mguu, kama ni mbavu zikiwa pamoja unaweza kuuza pia kwenye soko la kimataifa. Lakini kuna viwanda vya nyama ambavyo mpaka vina majiko ambayo yanapika, kuweka kwenye makopo au kuweka kwenye kontena ambazo zinaweza kutumika kwenye maduka moja kwa moja au kukata nyama kama tunazozikuta kwenye *super market.* Kwa hiyo, aina zote hizo tatu za *process* ya nyama nina hakika kwamba tutazifikia. Lakini tuanze angalau *abettor* zetu za mijini zinazotarajiwa kuuza nyama nchi za nje zifikie ubora na ndiyo jukumu letu la kwanza.

Nakubaliana sana na Mheshimiwa Laizer. Ni kweli tumeanza mkakati wa kuibadilisha *NARCO,* ni kweli ulikuta na wao wanajaza ng'ombe, mfano kama Kongwa wana ng'ombe 9,000. Ukiwauliza, ng'ombe 9,000 unaweka wa nini? Tulitegemea, na ni matarajio yetu kwamba *NARCO* au ranchi kama Kongwa wanachukua ng'ombe kama watakavyochukua kwenye ranchi ndogo ndogo wananenepesha, baada ya kunenepesha wanapeleka kwenye machinjio kama ya Dodoma wanauza. Halafu wananunua ng'ombe wale ambao hawana ubora unaotakiwa, wanawanenepesha kwenye maeneo yao na wanauza. *NARCO* na ranchi zetu siyo za kufuga kama wanavyofanya ndugu zetu wa Kisukuma, Wamasai na kadhalika. Hilo nimeliona na ninakushukuru sana Mheshimiwa Laizer na ndiyo tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Serukamba kwa mchango wake ambao alifanya utafiti. Lakini napenda pia nimtaarifu kwamba Bodi ya

Maziwa tayari tumeshaanzisha. Hivi karibu tutaanzisha Bodi ya Nyama. Kwa hiyo, tuko kwenye *direction* au kwenye mwelekeo ambao Mheshimiwa Serukamba alikuwa akiuelezea hapa. Tunapenda sana tukushukuru kwa kutukumbusha na ndiyo kilichotakiwa kifanyike muda mrefu. Lakini unajua matatizo ya kiuchumi nayo yanatuweka nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa matatizo aliyoyasema ya *Tanganyika Packers* lakini sasa hivi wala hatuyazungumzii tena. Kwa sababu tumeweza kutengeneza *Tanganyika Packers* nyingine nyingi tu na siyo lazima ziwe za Serikali, tatizo tulilonalo Watanzania ambalo nadhani ni kwa sababu biashara huko nyuma tulikuwa hatuzichangamkii sana, tumekuja kuchangamkia biashara za kununua na kuuza. Biashara ya nyama inahitaji usubiri. Lakini biashara ya kuuza sukari, khanga, vitenge, unanunua asubuhi, saa 4.00 unauza, unapata fedha. Lakini hiyo biashara haitatupeleka sehemu ambayo tunarajia. Ni vyema tujifunze biashara za kusubiri na ndiyo zinaweza kutusaidia sana katika kuiendeleza nchi yetu.

Napenda nimshukuru Mheshimiwa Killimbah, nadhani amepata majibu mazuri tu ya kuhusu machinjio Singida. Tuanze na hii kwanza, sasa hivi ina-*operate* kwa *capacity* ndogo sana. Baada ya *RVF* kwisha sasa ndiyo wanakaribia ng'ombe 80, 90 kwa siku. Hii machinjio ina uwezo wa kwenda mpaka ng'ombe 200 kwa siku. Sasa barabara ya lami inawekwa mnaiona, itakuwa ni rahisi sana kusafirisha mifugo kutoka Itigi, kutoka Manyoni, kutoka Iramba kuleta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tu-*utilize* hiki kiwanda kwanza. Tukiona *capacity* yake imeshafikiwa, tunaweza kuangalia na *private sector* kwa sababu inakimbilia mahali ambapo kuna faida. Huenda wakaanzisha kiwanda bila hata ya kuambiwa na mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa wafugaji nadhani tumejitahidi sana na programu nyingi sana tumefanya kwa ajili ya kuwafundisha Mpwapwa kwa Mheshimiwa Lubeleje. Ameona makundi ya wafugaji wengi sana wakipelekwa pale kupata mafunzo. Tunafanya hivyo hivyo kwenye vituo vyetu vingi. Vituo vingi tungependa sasa hivi tuvianzishe kwenye Wilaya kule kule na ndiyo maana tunapenda kuajiri watalaam wengi kwa ajili ya kuwapeleka kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutenganisha Wilayani kule kwenye Halmashauri, kilimo na mifugo. Serikali tumelipokea na nina hakika kwamba wahusika wanalifanyia kazi. Ni kweli ni fani mbili tofauti. Ni mchango mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambaye ametueleza mambo mengi sana. Lakini dogo ambalo nataka kulizungumzia ni maandalizi ya matumizi ya teknolojia ya viini tete. Teknolojia inatumika kama njia ya ushindani. Teknolojia inavyozidi kuwa ya hali ya juu inakuwa gharama. Sasa tunasema, sisi tuanze hata hii ya bei rahisi ya kununua mbegu, au kuchukua mitamba na kupeleka sehemu ambako hawana.

Tutakapokua kiuchumi, hizi teknolojia mpya tutaweza kuzifanya bila kuwa na matatizo makubwa kwa sababu tutakuwa tayari tuko kwenye ushindani mkubwa.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la udhibiti wa magonjwa, unatukwaza sana. Magonjwa haya yanatukuzwa, lakini kama unavyofahamu, baada ya utaratibu wa kuruhusu sekta binafsi uhusike kwenye kuuza madawa, chanjo na mafanikio yake hayakuwa mazuri, tulirudi nyuma. Tulifika mahali kama mtakumbuka, hata ruzuku tulikuwa hatutoi, lakini kuanzia mwaka huu tumeanza kutoa ruzuku kwa pembejeo na madawa. Hata chanjo za *RVF* tulitoa bure. Sasa ni mwanzo mzuri uchumi utakavyozidi kuwa na nguvu, nina hakika tutairudisha sekta kwenye barabara yake na nina hakika mauzo nchi za nje hatutakuwa *black listed* kwenye baadhi ya maeneo.

Kwa kweli napenda nichukue fursa kusema kwamba soko la Uarabuni wanatusaidia tu, lakini *strictly* leo ukitaka kuuza nyama kwenye *European Union* bado huwezi uka-*qualify*, na hauwezi uka-*qualify* kwa sababu matakwa yao ya *Sanitary* na *Saito Sanitary* huwezi kukidhi hata kidogo. Sasa hili soko linalopatikana Comoro, wapi; ni vyema tukalitumia ipasavyo. Kama mlivyoona kwenye takwimu zetu, tumeanza kuuza nyama kwa wingi sasa hivi. Tunaomba mtuunge mkono kwa sababu hata unapoiambia Serikali mkatafute soko ni kama tunarudi nyuma tulikotoka. Soko linatafutwa, yule mfanyabiashara ndiye aliye na *interest* kwenye biashara yake. Sisi tunaweza ku-*support* tu mahali ambapo kuna nchi nyingine zinataka *protocol* ya nchi na nchi, pale tunaweza kusaidia na nina hakika kwamba tutafika wote kwenye malengo tuliyoyaweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nataka kuzungumzia shamba la *West Kilimanjaro*. Shamba la *West* Kilimanjaro wakati tunatangaza kutoa *lease, sub-lease* kwa wafugaji wadogo wadogo kutoa *runch* ndogo ndogo wananchi waliokuwa wamevamia *West Kilimanjaro,* walikwenda Mahakamani na mnajua kesi zikienda Mahakamani hazimaliziki upesi. Sasa juzi tukaanzisha tena jitihada za kumaliza hii kesi, vijiji viwili vikakubali, sasa bado vijiji viwili.

Naomba sana Waheshimiwa Wabunge wanaotoka sehemu hizo watusaidie, kwa sababu ikimalizika tu, hiyo tutatangaza hatutakuwa na pingamizi na wataleta maombi yao lakini tunachosisitiza ni kwamba shughuli zao kwenye maeneo yale zilingane na madhumuni yaliyowekwa kwa ajili ya maeneo yale, yaani ufugaji. Tumefanya hivyo, juzi nilikuwa Misenye, tumewapa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Nina hakika wengi wenu tumeshawapa majibu asubuhi karibu Wabunge 27 ambao walichangia kwenye Wizara tofauti zilizopita. Majibu yasipokidhi, tupo tayari kwa ajili ya kuwapa maelezo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa usikivu. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono, lakini ili tuweze kufikia utaratibu mzuri, basi tunaingia hatua nyingine.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo

Kifungu 1001 – *Administration and General* … … Sh. 1,901,641,100/=

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 292 *vote* 99 *sub-vote* 1001 kifungu Na. 250100. Wakati nimechangia kwa maandishi nilielezea tatizo la wafugaji waliotoka bonde la Ihefu, kuleta kwenye Wilaya za Mkoa wa Pwani, nikatoa mfano wa Wilaya ya Kisarawe ambako wafugaji hao wamepelekwa eneo ambalo ni vyanzo vya maji ya mto Ruvu. Sasa niliomba Wizara husika itueleze imeweka mkakati gani wa kuondoa tatizo la ng'ombe kwenda kwenye vyanzo vya maji ambayo athari yake itakuwa ni ya kitaifa kwa maana Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani inategemea maji kutoka Ruvu.

Sasa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri mwenyewe, sikusikia ni mkakati ngani umewekwa na Serikali kutengeneza malambo ya maji na majosho na kutenga maeneo ili pia kuondoa migogoro iliyoko baina ya wafugaji na wakulima.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Vulu alileta hilo kwa maandishi, lakini kimoja ambacho tulielekeza kwenye uhamishaji wa mifugo kutoka Ihefu, ni kupelekwa kwenye maeneo ambayo yalianishwa na Wilaya zenyewe na Mikoa ikisimamia. Sasa kama Mheshimiwa anavyosema kwamba ile mifugo imepelekwa sehemu nyingine, kwa kweli labda atuachie muda tucheki, lakini ni wajibu wa Wilaya husika kusimamia na kwa vile yale maeneo yalipimwa kwa usimamizi wao wenyewe inakuwa ni vigumu sana sisi Wizara kujua maeneo yote yale. Lakini tuna hakika kwamba kuna utawala kamili kwenye wilaya na nina hakika kwamba watakuwa walifuata maelekezo. Kama hawakufuata tutachukua kumbukumbu ili tuweze kufuatilia.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo hayo, kwenye hotuba imezungumziwa kuna Kamati iliundwa ya kwenda kufanya utafiti katika maeneo ambayo ng'ombe hawa walipelekwa. Sasa naomba kama hiyo Kamati haikupeleka maelezo sahihi, naomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mifugo, pamoja na Wizara ya mazingira waweze kufanya utaratibu wa kwenda kuangalia tatizo hili haraka sana kabla hatujaleta tatizo kubwa zaidi.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa bahati nzuri moja ya sehemu ambayo nilitaka kuzungumzia ameizungumzia Mheshimiwa Vulu, lakini kwa taarifa ya Waziri tu ni kwamba ingawa maeneo yalitengwa na Halmashauri, lakini kule walikopelekwa wafugaji wameondoka wameingia katika

maeneo ya wakulima na kuharibu vyakula vya wakulima. Kwa hiyo, Serikali inachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba wale waliopelekwa kule wanakwenda kwenye maeneo ambayo wamepangiwa.

Mwaka jana wakati suala hili linaanza, tuliishauri Serikali kwamba ni vizuri wangeanza kuweka miundombinu kabla hawajawapeleka wafugaji kule ili kwa sababu kutakuwa na matatizo hakuna maji sioni hatua gani Serikali imechukua ya kuhakikisha kwamba kulikuwa na matayarisho mazuri ambayo yangezuia haya yote yaliyotokea. Nimeangalia katika hotuba ni kweli wanasema pale kwenye mpango wa mwaka huu watashughulikia lakini Serikali itachukua hatua gani ya haraka ili kusudi kuweza kuhakikisha kwamba tatizo lililojitokeza halitoendelea, nataka majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumkumbusha Mheshimiwa Janguo kwamba *operation* ya kuwahamisha wafugaji kutoka eneo la Ihefu ilifanyika kwa sababu nchi ilikuwa katika giza wakati ule na kilicholaumiwa kikubwa ni uharibifu wa vyanzo vya maji vya eneo hilo ambalo ndilo linaleta maji kwenye bwawa la Mtera. Kwa hiyo, hapakuwepo na muda tena wa kusubiri hili.

Katika swali la pili hili na la kwanza napenda nimweleze au nimkumbushie tu Mheshimiwa Janguo, ni mzoefu sana kwamba kwenye Serikali ziko Serikali tatu. Kuna Serikali za vijiji ni Serikali kamili halafu kuna Serikali za Mitaa ambazo ni Halmashauri. Sasa maelekezo yanaweza kupelekwa na ninavyoona maelezo ya Mheshimiwa Janguo na maelezo ya Mheshimiwa Vulu, ni kwamba, kuna tatizo kule, watu wameanza kuhama kwenda sehemu nyingine na uhamaji huo unatakiwa wapewe vibali. Sasa huyo anayewapa vibali ni nani? Wanakokwenda, nani anayewapokea?

Kwa hiyo, kuna tatizo na ndiyo maana nikasema tutajaribu tena kulifuatilia kwenye maeneo ambayo yanaleta matatizo na ni kweli hakuna anayependa tena mto Ruvu na mito ambayo chanzo chake ni sehemu za Uluguru na sehemu nyingine iingie kwenye matatizo kama tuliyoyapata.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote* 99 *program* ya 10 *sub-vote* 1001 *item* 250100. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimezungumzia kuhusu asilimia kubwa ya wazungumzaji walikuwa wanazungumzia athari za wale wafugaji na sio za wale ambao wamepelekewa hii mifugo. Mimi kama mmojawapo ambaye niko tumepelekewa mifugo, nina maelezo kwamba kuna tatizo la hawa wafugaji kutokaa kwenye maeneo ambayo wamepangiwa na hii imekuwa ni migogoro katika maeneo ya wakulima wengi.

Naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri iwapo wafugaji hawa watakaa maeneo ambayo hawakupangiwa kwa kipindi hicho na kwa madai ya kwamba miundombinu haipo pale na hawana shule na wana watoto hawana zahanati kwenye maeneo ambayo wamepagiwa. Ni hatua gani Serikali itachukua ili kuwasaidia wananchi wa maeneo yale ili kusiwe na migogoro?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyoeleza hapo awali, mambo mengi sana yanatakiwa yashughulikiwe kwenye Serikali za Vijiji na Serikali za Wilaya, mfano ni kweli fedha zinatakiwa zitoke Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa. Mwaka huu wa Fedha kuna fedha zimetoka *Central Government* karibu shilingi bilioni mia mbili, zimekwenda kwenye Halmashauri za Wilaya, ni mategemeo yetu ni kwamba, chini ya programu za *DADPS*, Halmashauri za Wilaya zitaibua miradi hii ambayo sasa ndiyo inahitajika haraka. Mfano, majosho, malambo na kadhalika. Kwa hiyo, hii hatuwezi, la sivyo tukianza tukiingilia moja kwa moja kwenda kwenye wilaya ile *D by D* itakuwa haipo tena, tutakuwa tunarudi nyuma.

Kwa hiyo, ni vizuri sisi kama wajumbe wa Halmashauri za Wilaya zetu, kuwaambia kwamba fedha zimekuja, sasa miradi ya kupendekeza tufanye mradi huu ili tuombe fedha kutoka kwenye mfuko wa chini ya *ASDP*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge ajaribu kuwakumbusha wenzake wilayani kwamba fedha zimepelekwa na *Central Government,* tutapeleka fedha zinapopatikana kwa programu kama hii ya kusaidia maeneo ambayo yana matatizo kwa sababu wafugaji wengi wamekwenda kwa mara moja. Lakini wafugaji tuliwa-*distribute* vizuri sana, hakuna mahali ambapo kuna *pressure* kubwa, ni usimamizi unapolegalega kunakuwepo na matatizo hayo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza vizuri sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyojibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini nimesimama kwa sababu ya suala hili la wafugaji na Serikali za Wilaya na za Mitaa kutotekeleza wajibu wake. Kwanza kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, tulifanya uamuzi ule kuokoa hali ya mazingira ilivyokuwa katika nchi yetu, hatukuwa na njia. Lakini kwa kuchukua hatua hiyo, wafugaji wasionekane kama ni raia wasio na haki katika nchi yao, ni lazima na wenyewe wapewe heshima, waheshimiwe kama binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, Viongozi wa Wilaya wanajua tulikubaliana washughulike na mambo haya. Tunaposikia Mheshimiwa Janguo anasema wanahama, wanapohama viogozi wa wilaya wako wapi? Kwa suala la miradi kama alivyoeleza vizuri sana Mheshimiwa Waziri tunategemea kwamba wataibua miradi ili wasaidie wafugaji katika maeneo yale, tafadhali wafugaji wasionekane kama ni raia ambao hawana haki katika katika nchi yao. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru *vote 99 program 10 sub-vote 1001 item 250100.* Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka ufafanuzi wa mambo mawili, lakini sikuyasikia na nianze kusema kwamba maeneo kame ambayo yana wafugaji wengi kama Dodoma na Shinyanga ambayo yana upugufu mkubwa wa malisho na inapelekea wafugaji wengi kuhamahama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kutafuta malisho pamoja na maji. Sasa nilitaka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kutayarisha mashamba makubwa zaidi ya malisho sambamba ya kujenga mabwawa na malambo ili kunusuru ule utaratibu ulioko sasa wa wafugaji hawa kuhamahama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine?

Lakini la pili kama taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tuliyoipata hapa hivi karibuni, hadi Juni 16, 2007 watu 139 walikufa na mifugo 50,000 ilikufa kutokana na homa ya bonde la ufa.

Sasa nilitaka kujua tu kwamba zile familia ambazo walikufa ng'ombe wengi zaidi ambao ni wachungaji wadogo wadogo, Serikali ina mpango gani wa kuziwezesha zile familia ili angalau ziweze kujiendesha tena katika hali ile ile ya zamani kuboresha maisha katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali la mashamba ya malisho, huu utaratibu wa kuwaelekeza watu kwamba malisho yanaweza kuwa chanzo kimojawapo cha kipato, ndio programu sasa hivi iko kwenye *stage* ambayo ni nzuri. Watu wengi wanaanza kuelewa na lazima tuelewe kwamba wananchi huwezi ukawapeleka kasi. *Process* ya *learning* lazima i-*take place*, la sivyo itakuwa ni mapinduzi na kama kweli utaweza kufanya mapinduzi wakati wa matatizo haya mengine kwanza ya kupunguza mifugo itakuwa ni tatizo sana.

Kwa hiyo tumeanza watu watachukua muda wataelewa tunaweka mashamba ya mfano watu wataitwa wataona, na kuna wengine wameshaingia tayari kama ukisoma taarifa yangu wameshaanza kuingia kwenye hiyo biashara. Mfano kuna mtu mmoja pale tumesema Dr. Rashid nadhani mnafahamu, *Managing Director* wa *TANESCO* amezalisha marobota zaidi ya 25,000 ya hei, sasa ni biashara kama unavyolima pamba, mahindi na kadhalika.

Sasa katika maeneo haya tunategemea kwamba wananchi wakishaelewa na hakika kwamba mambo ya malisho ya kutegemea kuhamahama kwa sababu malisho yamekwisha, itapungua. Lakini tuache wananchi waelewe *concept* yenyewe, waelewe umuhimu ulivyo na faida zake.

Kuhusu *RVF* nadhani lazima nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendeshwa kwa kodi. Sasa kama tunapata majanga ambayo ni ya asili, ambayo hutukutegemea, halafu tuanze wote kulipa fidia, ina maana tutoze kodi zaidi.

Juzi tu humu tulikuwa tunalalamika juu ya bei ya mafuta imepanda, lakini tutalipa vingapi? Kwa sababu siku hizi hata paa la nyumba ya mtu likiezuliwa na upepo mnachukua ile familia mnawapeleka wanakwenda kukaa kwenye darasa. Zamani ilikuwa siku ya pili au usiku huo huo wananchi au majirani wanakuja na fito na kadhalika kusaidia. Sasa ukitaka Serikali itusaidie, ina maana itabidi tutoze kodi zaidi. Kwa hiyo, sitegemei kwamba tutapata fedha za kuweza kufidia kwenye matatizo ambayo ni *natural calamities.*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* 99 *program 10 sub-vote 1001 item 250100.* Nakubaliana na alivyosema Mheshimiwa Waziri kuhusu shamba la *NARCO* na naipongeza Serikali kwa sababu mashamba mengine wamekwishagawia wananchi.

Hofu ya wananchi walioko katika shamba hilo, wanadhani kwamba watatolewa kwenye hilo shamba wapewe wawekezaji. Je, Waziri atakubali twende katika hilo shamba tukutane na hao wananchi tuwahamasishe ili jambo hili liishe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni biashara ya mifugo. Mifugo ni benki hai. Sasa tunataka tujue namna ya kupata masoko haya ya nje kama masoko ya Uarabuni ili uwaunganishe na hao wafanyabiashara wakubwa nao waweze wakafaidika na hayo masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la …..

**NAIBU SPIKA:** Mawili tayari. Kwanza ujibiwe hayo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *West Kilimanjaro* sina tatizo, ni vyema tukalizungumza nje ya taratibu zetu, nadhani unaelewa, kitu kikiwa Mahakamani hatuwezi kuleta mjadala hapa.

Kwa hiyo, ushauri wake ni mzuri lakini siasa inabidi kama navyopendekeza kwamba itumike zaidi ili watoe hiyo kesi Mahakamani.

La kuhusu benki hai, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge vizuri sana. Lakini kama nilivyosema, atakayebadilisha sekta hii ni pamoja na sisi tulioko humu. Kama ulivyojitahidi sana Mheshimiwa Mbunge ukafanya, waliokuwa wanauza mifugo upande wa Kajiado ukawabadilisha wakaleta mifugo, sasa wanauza kwenye *meat plant* ya Arusha. Jitihada hizo tungependa zitumike kwa maeneo makubwa zaidi na hivyo tutabadilisha sekta hii kwa sisi wenyewe kuwa katika mstari wa mbele.

Kwa hiyo, nina hakika kwamba Serikali inachoweza kukifanya ni kusaidia pale ambapo jitihada tayari zimeshaanzishwa na walio katika sekta yenyewe. Napenda sana nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada ambazo amezionyesha.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimalizie hilo moja iliyonikatiza. Nilisimama hapa nikazungumzia wafugaji waliohamishwa kwenye bonde la Ihefu. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lekule, naomba ukae. Kanuni zetu zinasema, kama swali linalofanana limeulizwa katika kifungu kile kile haliwezi kuulizwa na mwingine. Kwa hiyo, hili la Ihefu limezungumzwa tena, nimenyamaza Mheshimiwa Mwanawetu amezungumzia, akazungumza na Mheshimiwa Janguo, akazungumza nani, kwa hiyo, tumejibiwa. Hili hutaruhusiwa kwa sababu tayari limezungumzwa na wenzio.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 99 programu 10 sub-vote 1001 item 250100 basic salary*, wakati nachangia asubuhi, kuna jambo moja ambalo naona Mheshimiwa Waziri hakulijibu wala Naibu Waziri. Nilisema, ili kuweza ku-*improve livestock production,* inabidi kuweza kui-*map* Tanzania kwa

kutumia *JS geographical information survey*. Sasa naona wakati Waziri anasema, hajalisema ili tuweze kujua *suitabla area* kwa ajili ya mifugo.

Lakini jambo la pili, Mheshimiwa Waziri wakati anajibu amesema wakati tunapeleka mifugo yetu/*products* zetu hasa Uarabuni, Warabu ni kama wanatupa hisani hivi. Mimi likanishitua kidogo kwa sababu anasema *products* zetu hazija-*meet sanitary measures, so* nilitarajia sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri atuambie anafanya nini sasa, anaweka lini programu tuweze ku-*meet* hizo *sanitary measure* ili tuweze ku-*access* iwe *European Market* lakini pia ili hao Waarabu wasitufanyie hisani wanunue kwa sababu ni biashara?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimsahihishe Mheshimiwa Mbunge kwamba wanaonunua nyama zetu Uarabuni, nimesema Uarabuni maana yake ni geografia…

**NAIBU SPIKA:** Nyama ya ng'ombe bwana!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Tunauza nyama ya ng'ombe Uarabuni. Hilo nimeona nilisahihishe tusionekane Waarabu tu ndiyo wanaonunua tu, wananunua Waswahili wako kule pia. La kwanza, swali lake la *maping* tayari linafanywa. Tunaposema chini ya sheria ya vijiji, kwa mwaka 1999, tayari ilielekeza kwamba yatengwe maeneo ya malisho na maeneo ya wakulima na matumizi mengine. Sasa hiyo unayosema *geographical image* hizo *tool* wanazozitumia *surveyor's* wanatumia *GPS, theodorate* tulisema chochote kile, lakini *already* maeneo yameaishwa yanajulikana.

Sasa kinachofanyika sasa hivi ni kuweka kwenye *documents* ili mtu akitaka ufugaji, akienda kijiji fulani anaambiwa maeneo ya ufugaji bwana ni haya hapa. Kwa hiyo, uende huku, kama unataka ukulima ni haya hapa na kama ukitaka ukulima mkubwa nenda *land bank* kaulize wapi unaweza kupata eka mia tano au eka elfu tano unazozitaka. Hizo ni taratibu ambazo tayari zinafanyika. Nina hakika kwamba isingekuwa *constress* ya fedha maeneo mengi sana yangeshakuwa *maped*.

Swali la pili, ku-*meet standards SPS,* nasema tayari tumeanza. Tunapoleta madawa ya ruzuku maeneo ambayo ni *disease free* mfano hizi *runch* ndogo ndogo tunazoziweka sasa hivi, *eventually* sheria inaniruhusu nitazitangaza kuwa ni *disease free* kwa sababu wana *extension services* zote. Sasa nyama kutoka maeneo au kutoka kama *NARCO* alivyotueleza Mheshimiwa Lekule Laizer usitegemee kwamba nyama hiyo tutazidi kuiuza kwa bei ambayo tunaipata sasa hivi. Tunaweza kuuza maeneo mengi zaidi ili mradi yanatimiza masharti ambayo tumewekeana ya viwango vya kimataifa. Sasa nadhani tuko njiani sasa hivi kutekeleza na ku-*meet* hizo *standards* kwa kutoa ruzuku ya madawa, pembejeo, kutaka wananchi waogeshe, kupeleka wataalam wa *extension services* ili ku-*improve quality* ya mifugo na kadhalika.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *centre measure* ni pamoja na juhudi hizo ambazo zinafanyika za kutoa ruzuku na kutoa madawa.

Mimi nadhani bado, unapoongelea *centre measure* tuangalie tunachofanya kwenye samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mwanza vile viwanda vya samaki ukiingia ndani hata wewe mwenyewe uliyeingia unaweza ukajiona ni mchafu kwa sababu unakuta kuna *hygiene,* ni *the highest order*! Kwa hiyo, nilidhani kwenye nyama ile *hygiene* tuiweke na nyama yetu ndio itapata *product* au ukiniambia kwamba kwa kuwapa ruzuku peke yake tuna-*meet standard*, mimi naomba nieleweshwe vizuri hapo.

**WAZIRI WA MAENDELEO WA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Peter Serukamba tuko pamoja tu. Nadhani tunatumia lugha tofauti. Ukienda machinjio ya Dodoma ukafananisha na viwanda vya samaki ni kwamba kimoja kina-*handle* vitu vidogo na ni vingi. Hiki kimoja kina-*handle* miguu mikubwa ya nyama na kadhalika lakini usafi, *precautions*, kuoga, kuosha, ku-*scrub* sijui kufanya nini vyote vinafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa ni kuwa, tuwe na maabara na nadhani kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba Maabara ya *Central Veterinary Laboratory* na Maabara hizi ndogo *VIC Veterinary Investigation Center* zote sasa ziko *equipped* kuweza ku-*handle* maeneo ambayo yatatufikisha kwenye *standards* zinazoweza kuuza bila kupigiwa kelele sehemu nyingine. Nakubali samaki wako mbali zaidi kuliko sisi, lakini sasa na sisi tunakwenda kwenye *standard* hiyo hiyo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 99 program* ya *10 sub-vote 1001 item 250100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo imekuwa ikitoa takwimu za mifugo takriban zile zile. Kila mwaka kwa mfano ng'ombe milioni 18, mbuzi milioni 13, kondoo milioni 400, kuku na kadhalika. Takwimu hizi zimekuwa zikilalamikiwa sana hata na Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba ni *misleading*. Zikiwa *misleading,* maana yake ni kwamba, zinapoelekezwa katika mipango ya maendeleo zinakuwa sio sahihi.

Kambi ya Upinzani katika Bajeti iliyopita mwaka 2006/2007 ilitaka Wizara ifanye sensa ya mifugo, lakini Mheshimiwa Waziri katika Bunge hili akaahidi kwamba hayo yataangaliwa katika mwaka huu na vile vile mwaka huu hatujapata maelezo yoyote kuhusu sensa ya mifugo. Nataka Mheshimiwa Waziri atoe maelezo, hatua hii imefikia wapi hadi sasa? Kwa sababu kuendelea katika hali hii na takwimu hizi maana yake tunaeleza mambo ambayo sio sahihi na mipango yetu yote itakuwa siyo sahihi. Ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: Sensa ya mifugo ni ghali sana kama ilivyo sensa ya binadamu, tutahitaji karibu shilingi bilioni 60 kufanya sensa ambayo ni *one to one,* yaani *100 percent*. Sasa sisi tunachofanya ni kutumia *statistical procedures* za ku-*index* kulingana na *sample* ambazo tunachukua kwenye maeneo ambayo *scientifically* pia inakubalika.

Lakini kitu ambacho tunatakiwa kukifanya ni ku-*merge* kwenye sensa ya binadamu itakayofuata. Ingekuwa vizuri tukafanya *complete package,* yaani tuna-*indicate* sensa ya vitu vingi ambayo itaweza kuhesabu mifugo na kadhalika na kuanzia pale unakuwa na *basic* takwimu ambazo zinaweza zikatufikisha pazuri. Lakini kwa sasa hivi hatuna fedha za kuweza kufanya sensa ya mifugo tu, halafu kesho kutwa mnaanza sensa ya binadamu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... Shs.584,903,500/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … ... Shs.622,584,200/=
Kif. 1004 - *Livestock Research and Training Institute*… … ... ... ... Shs.1,782,363,000/=
Kif. 1005 - *Information, Communication and Edu. Techn.*… … ... .... ... Shs. 92,246,600/=
Kif. 1006 - *National Livestock Institute* - Mpwapwa … … ... .... ... Shs.566,043,000/=
Kif. 7001 - *Veterinary Services* … … Shs.3,258,373,600/=
Kif. 7002 - *Livestock Identif. Regist. Traceab. Unit*… … ... ... ... .... Shs.244,633,800/=
Kif. 7003 - *Pastoral System Development*…… Shs.389,991,100/=
Kif. 7004 - *Central Veterinary Laboratories* … ...Shs.871,630,700/=
Kif. 8001 - *Anima Production* … … ... Shs.2,307,105,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA IV**

**MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO**

**FUNGU 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Shs.114,000,600/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning...* ... ... .... Shs.9,661,400,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2007/2008 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 25 Julai, 2001 Saa Tatu Asubuhi)*